

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Sita – Tarehe 18 Mei, 2015**

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kutohaka na maagizo yaliyotolewa humu wiki iliyopita kuhusu Hati za kuwasilisha Mezani. Kama kuna kundi lolote, Kamati, Serikali au Upinzani hawajaleta Hati hazisomwi. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais! Mheshimiwa Naibu Waziri!

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):**

Randama za Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) pamoja na (Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):**

Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MHE. JASSON S. RWEKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu) kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**MHE. ESTHER N. MATIKO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, UTAWALA BORA NA MAHUSIANO NA URATIBU:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza maswali Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Engineer Athumanji Mfutakamba.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 34

**Malengo ya Milenia Kushirikisha Wananchi  
Katika Kuondoa Umaskini**

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA)** aliuliza:-

Malengo ya Milenia (MDGs) likiwemo la kuondoa umaskini uliokithiri na njaa yatafikia ukomo ifikapo mwaka 2015.

Je, Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs) kuanzia 2015 yatashirikishaje wananchi hasa wa vijiji kama Jimboni Igalula ili umaskini wa chakula vijiji na mijini na wastani wa Taifa upungue au utoweke kabisa tutakapofika Malengo ya Dira ya Taifa 2025, MKUKUTA na changamoto nydingine za maendeleo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Engineer Athumanji Rashid Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli malengo la ya Milenia, likiwemo la kuondoa umaskini ulikothiri na njaa yatafikia ukomo mwaka huu wa 2015. Hata hivyo, malengo ya kuondoa umaskini uliokithiri na njaa hayakukamilika na hivyo kutambuliwa na kuendelezwa katika kitu kinaitwa STG.

Mheshimiwa Spika, lengo la kwanza la mapendekezo ya malengo ya maendeleo endelevu au STGs ni kuondoa umaskini wa aina zote kila mahali na la pili ni kuondoa tatizo la njaa, kujenga usalama wa chakula, kuboresha lishe na kuhamasisha kilimo endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu kubwa malengo ya maendeleo endelevu yanatekelezwa kutumia Sera, Mipango na Mikakati ya Maendeleo katika ngazi zote kuanzia ile ya Kitaifa hadi Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji. Kila nchi itakuwa na wajibu wa kutathmini katika hatua ambayo imefikia katika maeneo yaliyoainishwa katika STGs na kubuni mipango, mbinu na mikakati ya kuendeleza maeneo husika ili kufikia malengo yaliyowekwa na

kuhakikisha mikakati hiyo inajumuishwa katika mipango na sera za maendeleo katika ngazi mbalimbali za kiutawala katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, wananchi wote wa Tanzania waishio mijini na wale waishio vijiji ikiwemo wananchi wa Jimbo la Igala watashirikishwa wakiwa ndiyo walengwa watakaonufaika katika matokeo ya utekelezaji wa malengo husika.

Aidha, wananchi watahusika katika kuchangia nguvukazi yao, muda wao, utaalam na ujuzi wao na hata rasilimali fedha pale inapowezekana katika kupanga na kutekeleza mikakati ya maendeleo kufikia malengo ya STGs.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, ajenda hiyo mpya ya Maendeleo ya Kimataifa imekuja wakati muafaka ambapo Serikali iko katika mchakato wa kutengeneza mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano utakaoanza kutekelezwa mwaka 2016. Katika ngazi ya Taifa malengo stahiki yatakayoainishwa katika STGs yatajumuishwa katika mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano na hivyo kuiwezesha nchi kuanza utekelezaji wa ajenda sambamba na utekelezaji wa mpango huu wa maendeleo.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali haikutumia Mfuko wa TASAF ili kuondoa umaskini kuliko kugawa pesa za kula siku hadi siku. Ni sawa na kumpa mvuvi samaki kuliko kumpa mvuvi nyavy na ndoano. Je, Serikali inaonaje, kila siku mwananchi unampa hela ya kula, kwa nini msiwape pesa, mitaji zile sehemu maskini kabisa kama kule Igala watu wasiojiweza, mitaji ya kuweza kuondoa umaskini kuliko kuwapa pesa, kumfanya mtu awe masikini siku hadi siku?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kaya maskini sana zinapewa fedha kwa ajili ya kujikimu. Sasa kama hawatafika kwenye mitaji wakafa hapo tutakuwa tumefanya nini. Kwa hivyo, TASAF III inawapa watu fedha za kujikimu, inawapa fedha za kuweza kupeleka watoto kliniki, inawapa fedha za kupeleka watoto shuleni na baadaye inawapa ajira ili wapate fedha kidogo za kuanzia mitaji yao.

Kwa hiyo, TASAF III imeangalia kila hatua. Nataka Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu lijue kwamba TASAF III imeaangalia mambo *in totality*, haiangalii moja tu na hilo la kuwapa nyavy na ndoano nalo lipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mfutakamba, ni swali moja tu kwa sababu swali lako limeshachukuliwa na aliyeuliza. Mfutakamba!

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kusherehesha swali langu nililouliza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu toshelezi, lakini yako matatizo wakati mwingine kwenye familia maskini. Kijana anaweza kwa sababu ya hali ya umaskini na ambaye ana nafasi ya kifedha anamfanya matatizo lakini pale Tabora hapelekwi Mahakamani. Mwenyekiti wetu wa CCM Uyui.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili litazamwe watu wasinyanyaswe kwa sababu ni maskini kwa wale ambao ni matajiri na kuchukua nafasi zao, ile kesi ya RPC haipeleki Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**WAZIRI WA NCHI OFISI, YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa taarifa yake, tunachukua ushauri wake na tutaufanya kazi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri kwamba lengo kuu la SDG ni kuondoa umaskini na umaskini kwetu hapa Tanzania maana yake ni kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania tuna hekta zaidi ya milioni 29 zinazofaa kwa umwagiliaji, hasa ukizingatia sasa hivi tuna janga kubwa sana la ukosefu wa mvua. Sasa nataka kujua, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba tunakuwa na kilimo cha umwagiliaji, kwa sababu hata hatujafika heka 700,000. Naomba kujua sasa, tutaondoje umaskini kama hatuwekezi kwenye umwagiliaji huku tukijua zaidi ya asilimia ya Watanzania wako katka sekta ya kilimo? (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali hili ambalo limekuwa linaulizwa sana humu ndani na Wabunge wengi.

Mheshimiwa Spika, wiki iliypita nilijibu swali hili humu ndani Bungeni ambalo pia lilitaka kujua mikakati ya Serikali kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Nilisema kwamba tunao mpango madhubuti na mkubwa kabisa ambao utahakikisha kwamba asilimia 25 ya chakula kinachozaishwa nchini kinatokana na kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, malengo tuliyojiwekea katika kipindi ambacho kinakwisha, sasa hivi tuko asilimia 24, kwa maana ya kwamba chakula kilichozaishwa hapa nchini karibu tani milioni 16, asilimia karibu 17 yake imetokana na kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, tunao mpango mkubwa, tunaomba tu Waheshimiwa Wabunge tutakapoleta bajeti ya kipindi hiki muis-support ili mipango hii ya umwagiliaji iweze kwenda vizuri zaidi.

**SPIKA:** Tunafanya ngonjera swali moja. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh.

Na. 35

#### **Idadi ya Magereza na Wafungwa**

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Nchi yetu inaendeshwa kwa msingi wa utawala wa sheria na kuheshimu haki za binadamu, lakini kama mtu yeyote akivunja sheria au kufanya uhalifu wa aina yoyote huhukumiwa kulingana na sheria za nchi zinavyoelekeza kulingana na aina ya kosa:-

(a) Je, hadi sasa ndani ya nchi yetu kuna Magereza mangapi na wafungwa wangapi kwa ujumla?

(b) Je, ni wafungwa wangapi wamefungwa kwa makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa watoto na wanawake?

**NAIBU WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu A na B kama ifuatavyo:-

(a) Katika nchi yetu tuna jumla ya Magereza 126 ambayo yana uwezo wa kulaza jumla ya wafungwa na mahabusu 38,000 kwa siku na yamegawika katika mchanganuo ufuatao:-

- (i) Magereza makubwa (*Central prisons*) yako 12;
- (ii) Magereza ya Wilaya (*District Prisons*) yako 68; na
- (iii) Magereza ya kilimo (*open farm prisons*) yako 46.

(b) Wafungwa wanaotumikia vifungo mbalimbali katika Magereza kote nchini kwa makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa watoto na wanawake ni 1,067.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, katika nchi yetu kuna Majiji Makuu mbalimbali, ningetaka kujua labda ni Jiji gani linaongoza kwa uhalifu huu wa ubakaji na udhalilishaji na mikakati gani Serikali imeweka ili kupambana na kuzuia uhalifu huu katika Jiji hilo linaloongoza na Majiji mengine?

Swali la pili ni kwamba kuna taarifa kwamba baadhi ya Magereza yamekosa nguo za wafungwa, hali inayosababisha wafungwa wanakuwa na nguo mbovu zinazoonesha miili yao ambayo haistahiki kuonekana na watu wengine, hivyo kushindwa kupangiwa kazi za nje kama vile mashambani. Nataka kujua, Serikali ina mkakati gani wa kuondokana na tatizo hili? Ahsante.

**NAIBU WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza Jiji ambalo linaongoza katika masuala ya unyanyasaji kwa mujibu wa wahalifu ambao wako Magerezani la kwanza ni Tabora, wahalifu wako 307 kwenye Gereza la Uyui, la pili ni Tanga ambalo lina wahalifu 110 na likifuatiwa na Arusha ambako wako 85.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu nguo za wafungwa. Mahitaji halisi ya wafungwa kwa maana ya nguo pamoja na askari angalau wapate jozи mbili kila mfungwa kila mwaka. Ni kweli kwamba kuna tatizo la kufikia hatua hii kwa sababu hasa ya ufinyu wa bajeti, lakini tatizo la kuwa kuna baadhi ya wafungwa wanavaa nguo ambazo zinachanika ni sawa, lakini wafungwa hakuna ambaye anakwenda uchi au kushindwa kufanya kazi kwa sababu hana nguo ya kuvaa.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa vile katika kuzingatia haki za binadamu na utawala bora ni pamoja na kuhakikisha Magereza yanakuwa na nafasi ya kutosha kuwahifadhi watu bila kurundikana. Gereza la Mbarali ni mionganoni mwa Magereza ambayo yalifunguliwa ikiwa bado hayajakamilika, hata hivyo kwa sasa hivi linahifadhi watu tofauti na uwezo wake na hivyo kufanya uwezekano wa kuwatenganisha wakubwa na wadogo kuwa ni mgumu. Namwomba Mheshimiwa Waziri aseme ni lini Gereza la Mbarali litatengewa bajeti ili kusudi liweze kulingana na hadhi ya gereza?

**NAIBU WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mbarali kuna msongamano mkubwa wa mahabusu na wafungwa hali ambayo takribani iko kwenye magereza mengi sana. Hali ya Gereza la Mbarali haitoshelezi kama ilivyo katika Magereza mengi nchini. Jitihada za Serikali zinaendelea kujenga Magereza mapya pale ambapo inawezekana, lakini misongamano hii pia inasababishwa na kukosekana kwa Magereza katika

baadhi ya Wilaya za karibu na hivyo baadhi ya wafungwa hulazimika kwenda kwenye magereza ya karibu au ya Wilaya ambayo ipo pale karibu.

Mheshimiwa Spika, katika hili mkakati wetu mkubwa ni kuhakikisha kwamba Wilaya 42 ambazo hazina Magereza ya Wilaya yanajengwa ili kupunguza hii. Pia jitihada zipo nydingi sana kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu lakini pia na taratibu za kupunguza wafungwa na mahabusu Magerezani ili kupunguza msongamano zinaendelea.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hapa nchini imejengeka tabia ya watu amba wanachukua hatua mkononi na kuwaua kwa kuwachoma moto vijana amba wamefanya udokozi.

Napenda kujua je, kuna hatua gani ambazo zimebekwa na Serikali ili kudhibiti hatua hiyo ya watu amba wanajichukulia sheria mkononi na kuwahukumu wengine kwa kuwachoma moto?

**SPIKA:** Hii ilikuwa Magereza, tena mnachoma moto! Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo yanasisitisha sana na ambayo Serikali haipendi kuyaona yanatokea ni wananchi kujichukulia sheria mikononi. Nchi hii inaendeshwa kwa sheria na ni vema kila ambaye anaonekana anafanya udokozi afikishwe kwenye vyombo vyia sheria na apate hukumu ambayo ndiyo inatakiwa isimamiwe.

Suala la utii wa sheria bila shuruti siyo tu kwamba unaanzia kwa mdokozi, lakini pia kwa sisi amba tumemwona. Tunatakiwa sote tuendelee kuamini kwamba sheria za nchi zitachukua hatua na mtu ambaye amefanya kosa ataadhibiwa ipasavyo. Kitendo cha kuchukua sheria mkononi ni jambo ambalo tunaweza kuelimishana, lakini na watu amba tunawakamata wamefanya hivyo, nao tunachukua hatua, lakini tuendelee kuelimishana wale amba wako karibu ya matukio wasimame wima kuhakikisha kwamba vitendo hivyo havifanyiki.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Khatib Said Haji, kwa niaba yake Mheshimiwa Mkiwa!

Na. 36

#### **Makosa ya Uzembe na Uzururaji**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA (K.n.y. MHE. KHATIB SAID HAJI)** aliuliza:-

Kumekuwa na matuko ya vijana kukamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya uzembe na uzururaji katika nchi yetu:-

Je, ni mazingira yapi yanayowafanya Polisi kujiridhisha ni vijana wangapi ni wazembe na wazururaji na kustahili kukamatwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 176 na 177 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, mtu yejote anaweza kukamatwa kwa kosa la uzembe na uzururaji iwapo ataonekana

katika maeneo na mazingira ambayo yanapelekea kuonekana kwamba mtu huyo yupo hapo kwa jambo lisilo halali.

Aidha, iwapo itabainika kuwa mtu huyo anajihuisha na vitendo kwa mfano vya ukahaba, uvunji fu wa amani au vitendo vya aibu kama vile kuvua nguo hadharani anaweza kukamatwa kwa kosa la uzembe na uzururaji na akafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, ni dhana ya kisheria iliyo dhahiri kuwa kila mtu anawajibika kufanya kazi halali ili kujipatia kipato cha kujikimu na hivyo mtu yeyote mwenye uwezo wa kufanya kazi anapoamua kwa makusudi kuishi maisha ya kutangatanga na kwa kuombaomba mitaani anaweza kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri yasiyokuwa na afya, napenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa riziki ya mbwa ipo miguuni mwake, kwa kuwa Serikali haina ajira za kuwapa wananchi wala pesa za kuwapa mikopo vijana na vijana wanapoamua kujiajiri, mfano, vijana wanaokamatwa sana ni vijana wa bodaboda, wapiga debe wa kwenye vituo vya basi kukamatwa na kuambiwa wazururaji na kunyimwa haki zao za msingi.

Sasa napenda kujua, je, ni kwa nini wanakamata watu amba hawana vigezo alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba ni makahaba na wengineo na kukamatwa watu amba wanaweza kujishughulisha kutafuta riziki na kuwatia hatiani kwamba ni wazembe na wazururaji na nafahamu kabisa kwamba Serikali haina uwezo wa kuwaajiri na wala haina pesa za kuwapa ili wajiajiri?

Kwa kuwa, wanaokamatwa wakikamatwa vijana 20 wanaofikishwa Polisi ni vijana watano au sita amba hawana pesa. Napenda kujua, Polisi wanawachujaje vijana barabarani kwa kupewa pesa kidogo wakawaachia baadhi ya vijana amba hawawafikishi Polisi na wanaofikishwa Polisi ni wale tu amba hawana pesa mfukoni na kulichafua Jeshi la Polisi. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze kwa kuwa na uchungu sana na suala la ajira na kusimamia haja ya vijana hawa kupewa mikopo badala ya kukamatwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inasimamia jambo hilo hilo ambalo kwa maneno umelisema unalismamia, lakini vijana wapo wengi, sensa inasema na haiwezekani ikawa Serikali inakumbakumba tu vijana wengi bila sababu. Mara zote anayekamatwa kama hashukiwi kuwa amekosa, basi atakuwa na kosa. Pia Serikali kwa kweli haijafikia hatua ya kuwa ikamate vijana wake wa bodaboda amba hawana makosa.

Mheshimiwa Spika, lazima nikwambie kama una ujuzi mzuri au unafuatilia vijana wako wa bodaboda, vijana wa bodaboda ni vijana wetu amba tumewawezesha ili wajiwezeshe, bodaboda maana yake ni hiyo. Mara nyingi wanashabikia kwenye uvunji fu wa amani iwe au mmojawapo kafanya au vinginevyo, lakini haitoshi kuwa wengi hawakufanya isitokee vurumai na kama ilivyo kazi ya Jeshi la Polisi ni kusimamia amani na ambaye ataonekana anaichezea lazima akamatwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pesa kidogo, wanafikishwa wachache, hili ni jambo zuri, lakini ni taarifa muhimu katika kuhakikisha kwamba ulinzi unafanyika vizuri na tumeirahisisha

hii kwa watu kama hao ambao wanakamatwa kwenye makosa haya madogo, kwamba kila OCS anakuwa na uwezo wa kuwapa dhamana pale ambapo inatokea.

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo linafanyika baina ya walipokamatwa na Kituo cha Polisi hili ni lazima nilikeme na nalikeme na nishirikiane na wewe kulikemea, lisimame mara moja, askari wahakikishe kwamba aliyekamatwa anafika kituoni na lolote litakalofanyika kituoni ndiyo la halali lakini siyo la barabarani.

**SPIKA:** Maswali mengi na muda hautoshi, twende Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, kwa niaba yake Mheshimiwa Christowaja Mtinda!

Na. 37

**Vikundi Haramu vya Vijana Vinavyohatarisha  
Maisha ya Raia**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. MHE. MARYAM SALUM MSABAHA)** aliuliza:-

Kumezuka vikundi haramu vya vijana vinavyohatarisha maisha ya raia na mali zao hasa kwenye sehemu za miji mikubwa.

Je, Serikali imechukua hatua gani za kuwawezesha vijana hao kujajiri wenyewe huko vijijini?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ukosefu wa ajira kwa vijana ni moja ya changamoto ambazo zinalikabili Taifa. Serikali katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 kwa kushirikiana na wadau wengine imechukua hatua mbalimbali za kuwawezesha vijana huko vijijini kujajiri wenyewe na mfano mdogo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa miaka mitano wa kuwawezesha vijana unaolenga kukuza uzalishaji katika kilimo na kuongeza kipato cha vijana waishio vijijini. Mradi unajulikana kama *Empowering Youth in Agricultural Investment Through Establishment of Village Agricultural Youth Clubs (A pathway towards Economic Liberalization for rural Youth in Tanzania)*.

Mradi unatarajiwa kuunganisha vijana na mabenki ili waweze kukopeshwa kwa urahisi na kuimarisha usindikaji mazao ili kuongeza thamani ya mazao.

Pili, Serikali Kuu kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa inatenga bajeti maalum kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya vijana. Programu hii imesaidia vijana wengi kupata mikopo ya kuanzisha miradi ya kujajiri katika maeneo mbalimbali ya vijijini na mijini kupitia SACCO\$ zilizoanzishwa na vijana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira kwa vijana ni suala mtambuka ambapo wadau mbalimbali tunahitajika kushirikiana kwa pamoja katika kutatua changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kubuni miradi mbalimbali ya kuwasaidia vijana huko huko vijijini.

Aidha, nitoe wito kwa vijana kutokimbilia mijjini bila kuwa na uhakika wa ajira, badala yake wabuni miradi ya kilimo huko vijjini na Serikali itakuwa tayari kuwasaidia kupitia mipango niliyoitaja au mipango mingineyo.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, majibu ya msingi yameonesha kwamba Serikali imeanzisha huo mradi tajwa.

Swali langu ni kwamba, je, ni kwa namna gani huu mradi ambaa Serikali inaanza kuutekeleza utakwenda sambamba na uanzishwaji wa viwanda vikubwa kwa sababu vijana waliopo vijjini watajihusisha na kilimo cha mazao kwa aina ya ufugaji na uvuvi na hivyo watahitajita mazao yao yapelekwe kwenye viwanda ili waweze kujitegemea vizuri. Ni kwa namna gani Serikali imejiandaa kuanzisha viwanda hivyo?

Pili, kwa kuwa katika kipengele cha pili Waziri amejibu kwamba kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa vijana wameendelea kupata mikopo kupitia SACCOS zao. Sina tatizo na hili pamoja na mgogoro uliopo wa kupatikana kwa pesa hizi kutoka Halmashauri zetu.

Swali langu ni kwamba, je, ni kwa namna gani sasa Serikali itajikita zaidi kutoa elimu ya biashara kwa vijana maana ni wengi ambaa hawajui wafanye nini, wanaweza kupata fedha, lakini wasijue wanazifanyaje. Ni kwa namna gani Serikali imejiandaa sasa kutoa elimu ya biashara kwa vijana waishio vijjini ili pesa zao zifanye kazi sawasawa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo haitolewi bila kutoa elimu kwa vikundi ambavyo vinaomba mikopo hiyo. Wataalam wa Wizara yetu wamesambaa nchi nzima kutoa mafunzo kwenye Halmashauri, kwa hiyo vikundi ambavyo vimeomba fedha iwe ni miradi ya kibiashara na mingi ni miradi ya kibiashara, kwa hiyo bila kupata elimu hatutoi mikopo ile.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatoa elimu ya kibiashara kabla ya kutoa mikopo hiyo na vijana hawa wanaelewa vizuri sana na fedha ile wanaitumia vizuri sana katika kuijendeleza kiuchumi. Ahsante.

**SPIKA:** Na sehemu ya viwanda vikubwa tena, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa majibu kuhusiana na elimu.

Pia hata sisi Wizara ya Kazi na Ajira tulioomba shilingi bilioni tatu kwa ajili ya vijana. Katika hizo shilingi bilioni moja ilikuwa itumike katika kutoa elimu na shilingi bilioni mbili zilikuwa zikae kama dhamana kule CRDB kwa ajili ya kuwakopesha. Kwa hiyo, kama Wizara ya Fedha itatupa hizo fedha kabla ya mwezi Juni/Julai, basi tutafanya hivyo.

Swali la kwanza alilouliza Mheshimiwa Mbunge ni kuhusiana na viwanda vidogo vidogo na katika jibu langu la msingi nimegesia kwamba mojawapo ya shughuli ambazo vijana wanafanya katika ile programu yenye ya kilimo niliyoitaja ni kuhakikisha kwamba katika hiyo programu pia kuna kuweka thamani ya mazao kwa kutumia viwanda vidogo vidogo ambavyo wanavitengeneza na SIDO wana utaalam mkubwa sana katika hilo.

Mheshimiwa Spika, tulipoahimisha SIDO Kitaifa mwaka 2014 Musoma, vijana wengi walionesha jinsi ya kuongeza thamani ya mazao kwa kutumia hivi viwanda vidogovidogo. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo pia ni muhimu na namshukuru Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tukizungumzia suala zima la vijana na ajira ni jambo la msingi, lakini hivi sasa dunia inajiaandaa katika Beyond 2015 Millennium Development Goals na ajenda hii sasa inakwenda kwa upana wake. Sasa nataka nijue Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba inatoa elimu ya vijana kwa mapema zaidi, sasa ni jinsi gani watafanya katika hayo malengo yatakapangwa Beyond 2015 ili na wao wawe mionganoni mwa watu ambao wameshiriki ipasavyo ili mradi katika agenda ya maendeleo waweze kushiriki vizuri? Ahsante.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema suala hili ni mtambuka na katika sera yetu ya ajira tunasema Wizara ya Kazi na Ajira, kazi yake ni kuratibu fursa za ajira zilizopo na kutokana na hiyo hali ya kwamba ni sera mtambuka, naomba hili suala tushirikiane.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza tushirikiane katika kuwabadiishia vijana wetu ile attitude ya kuajiriwa, hiyo ndiyo inayotupa shida kwa sababu vijana wengi na hasa wanaomaliza elimu ya juu, wanajua kwamba wanapomaliza tu ni lazima wapate ajira Serikalini. Kwa hiyo, kwa kushirikiana hivyo tutawapa vijana elimu pale tulipo kwa sababu vijana hawapo Wizarani bali wapo katika maeneo yetu, kwa hiyo, tushirikiane katika hili na Serikali itatumia wakati wake katika kutoa elimu hii.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar.

Na. 38

#### **Unyanyasaji kwa Wafanyakazi wa Ndani**

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR** aliuliza:

Ingawa ziko sheria za kuzuia unyanyasaji wa wafanyakazi wa ndani, lakini bado wafanyakazi hao wanaendelea kunyanyaswa na kupata matatizo mengi katika maeneo ya kazi:-

(a) Je, kwa nini Serikali haizitumii sheria hizi zilizopo kudhibiti matatizo hayo?

(b) Je, kuna ukaguzi wowote unaofanyika katika majumba ili kugundua matatizo na mazingira wanayofanyia kazi watu hawa?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imeendelia kuzitumia sheria zilizopo hususani Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2014 ambayo inakataza aina yoyote ya ubaguzi na unyanyasaji wa mfanyakazi sehemu za kazi. Aidha, Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004 imeweka Bodi za Kisika ambazo zinaainisha kima cha chini cha mshahara anaopaswa kulipwa mfanyakazi katika sekta husika ikiwemo mahotelii na majumbani.

Serikali kwa kutambua mchango mkubwa unaofanywa na wafanyakazi wa majumbani imejenga uelewa wa wadau kuhusu haki za wafanyakazi wa majumbani na kujenga uwezo wa Maafisa Kazi juu ya mbinu za ukaguzi na usimamizi wa haki za haki kwa wafanyakazi wa majumbani.

(b) Katika kipindi cha mwaka 2014 hadi Machi, 2015, Wizara yangu imefanya kagazi za kazi 1,843 katika sekta mbalimbali ikiwemo ya Huduma ya Mahoteli na Majumbani. Changamoto kubwa iliyopo katika kukagua wafanyakazi wa majumbani ni namna ya kuwatambua.

Hata hivyo, mara wanapopata matatizo na waajiri wao ndipo hapo hukimbilia kwenye Chama cha Wafanyakazi wa Mahoteli na Majumbani (*CHODAWU*) ambapo mashtaka hayo hupelekwa katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Serikali inakamilisha utaratibu wa kuridhia Mkataba Na. 189 wa Shirika la Kimataifa (*ILO*) ambao utaweka mfumo mzuri wa ukagazi wa wafanyakazi wa majumbani na ndani.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Wafanyakazi wengi wa ndani hawajui haki zao na vile vile hawajui kama kuna chombo ambacho kinaweza kuwatetea. Je, Wizara imechukua hatua gani kuitangaza taasisi hii ili hawa wafanyakazi wakimbilie?

Pili, kuanzishwa kwa mikataba baina ya waajiri na waajiriwa katika sekta ya wafanyakazi wa ndani itasaidia sana kuondoa madhira ambayo wafanyakazi hawa wanayapata. Je, ni lini Serikali itaanzisha mikataba hii? Ahsante.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Nassib kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimshukuru sana kwa kufuatilia masuala ya haki za wafanyakazi katika sekta zote, lakini naomba pia nimtaarifu kwamba wafanyakazi wa majumbani wanakifahamu hiki chama cha *CHODAWI* na wanafahamu haki zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kumhakikishia hilo, miaka miwili au mitatu iliyopita tulikuwa na wafanyakazi wa majumbani kupitia chama chao ambao walialikwa kwenye Mkutano wa Kimataifa wa *ILO*, Geneva na wakaja kutoka dukuduku zao na matatizo yao katika suala zima la kazi yao katika maeneo wanayofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tatizo kubwa ni kuwatambua. Kuwatambua kwa namna kwamba, Wakagazi wetu wanapokwenda, wanaambiwa mimi siyo mfanyakazi wa nyumbani, ni mdogo wa mwenye nyumba na kwa hali hiyo huwezi kuchukua hatua hata kama ukiona kuna tatizo ambalo linahusiana na mgogoro kati ya mwajiriwa na mfanyakazi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa niulize swali la nyongeza.

Wafanyakazi wa majumbani ni wengi sana. Humu Bungeni kila mmoja ana mfanyakazi, asilimia 80 ya watu wanaokaa mijini wana wafanyakazi wa majumbani.

Sasa maswali; moja kuna mtu mmoja anajiita Nabii Tito, huyu anapita kwenye mabaa kuhamasisha watu watembee na wafanyakazi wa majumbani kwamba ni halali na Wizara hii haijachukua hatua yoyote.

Mheshimiwa Spika, pili, swali limeuliza huu Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Majumbani ni lini Serikali itausaini?

**SPIKA:** Ngoja kwanza.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Hilo hajajibu ni lini!

**SPIKA:** Ngoja kwanza, wewe ni swali la nyongeza, lile la kwanza linatosha. Mheshimiwa Waziri naomba ujibu.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mkosamali kwamba nimesahau kujibu sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Nassib kuhusiana na Mkataba wa 189 ambao tulikwishausaini, tatizo ni kwamba, hatujaleta Bungeni kuja kuridhia. Sababu ni kwamba, Mkataba ule kuna mambo mengine ambayo hayahusiani na maisha na mila na desturi za Kitanzania. Kwa hiyo, tunaufanya kazi ili tuchukue maeneo yale tu ambayo tunaweza kuyaridhia na mnaweza mkayakubali kama Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuulete katika Bunge lililopita, lakini naahidi kwamba utakuja katika Serikali ijayo na uko karibu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba, huyo Nabii Tito sisi hatujamsikia na naomba tupate taarifa zaidi na nafikiri hilo ni suala la kijinai.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mbali ya manyanyaso na matatizo ambayo wanayapata wafanyakazi wa majumbani, kuna kundi lingine la vijana ambao wanafanya kazi katika viwanda. Kamati yetu ya Mazingira tuliweza kutembelea kwenye Viwanda vya Mkoa wa Dar es Salaam, hali inatisha, kuna vijana wamekatwa mikono, hawana vifaa, wanakwenda kwenye mashine ambazo zinaleta athari za kiafya pamoja na kupoteza viungo vyao na baadaye huwa wanafukuzwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kwa namna gani chombo cha OSHA kimekuwa kikifanya kazi ipasavyo ili kuhakikisha vijana hawa wanafanya kazi katika mazingira bora kama Mikataba inavyosema, siyo wanakatwa mikono na miguu halafu baadaye wanafukuzwa?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuna manyanyaso katika sehemu kadhaa katika maeneo ya kazi. Kama nilivyosema Wizara yangu kupitia Maafisa Kazi tumefanya kaguzi 1,800 na zaidi katika kipindi hiki cha kuanzia Machi, 2014 hadi sasa hivi. Katika kaguzi hizo kuna watu ambao tumewapeleka Mahakamani, wengine imebidi walipe fedha na wengine wamepewa compliance order na adhabu nyininge.

Mheshimiwa Spika, tusipopata taarifa wakati ambapo labda hatujakwenda kukagua, kwa sababu siyo kila siku tutakwenda kukagua, kwa hiyo, mambo ambayo yanatokea katika maeneo ya kazi kila siku siyo rahisi Wizara na Maafisa Kazi kuyafahamu, tunachohitaji ni taarifa kwa wale ambao wametendewa makosa. Wafanyakazi wengi wanafikiri Waziri anaweza kumwamuru mwajiri kwenda Mahakamani, sheria hainiruhusu mpaka tukague na OSHA wakague wapate taarifa. Sasa pale ambapo hatupati taarifa kwa kukagua, tunaomba wafanyakazi watupe ushirikiano kwa kupeleka taarifa hizo OSHA au CMA.

**SPIKA:** Muda hautoshi. Twende Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa John Lwanji!

Na. 39

#### **Mpango wa Kufikisha Umeme Vijijini Manyoni**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Serikali ilishatoa ahadi ya kupeleka umeme kwenye Vijiji vya Aghondi, Mabondeni na Kitopeni na kushusha umeme Kijiji cha Gurungu Wilayani Manyoni kupitia REA/TANESCO.

Je, mpango huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (MHE. STEPHEN J. MASELE K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, TANESCO imetenga shilingi milioni 43.46 kwa ajili ya kuunganisha umeme katika Kijiji cha Gurungu ambapo mradi umekamilika mwezi Machi, 2015. Kazi zilizofanyika zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 0.5; ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa kilomita moja na kufunga transfoma moja ya kVA 50. Mpaka sasa wateja watatu wamefanya malipo kwa ajili ya kuunganishiwa umeme. TANESCO inaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajitokeze kulipia na kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Aghondi kimeingizwa katika mpango wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa MCC Awamu ya II. Tunachosubiria ni hatua ya upembizi na athari za kimazingira kufanyika na wataalam wa MCC ili mradi uingizwe katika utekelezaji. Mradi wa kupeleka umeme Kijiji cha Aghondi unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 33 umbali wa kilomita 14; ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 0.4 umbali wa kilomita mbili; ufungaji wa transfoma moja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapataao 20.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Mabondeni na Kitopeni vinatarajiwa kuingizwa katika mpango wa REA awamu ya III. Gharama zinazohitajika kuvipatia umeme vijiji hivi ni shilingi milioni 752.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Ni kweli huo mradi wa Gurungu umekamilika na sisi kama viongozi tutaendelea kuwahimiza wananchi wa Gurungu waweze kuchangamkia uunganishaji wa umeme. Pamoja na pongezi hizo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, jirani na maeneo hayo ninayoyazungumza kuna mradi ambao uliidhinishwa na Serikali huu wa kutoka Kata ya Mitundu kwenda Kata ya Mwamagambe kupitia vijiji vya Kalangali, Kiyombo, Kirumbi kwenda Mwamagambe, uliishaidhinishwa na iliahidiwa kwamba mpaka tarehe 30 Juni mwaka huu mradi huo ungekamilika.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kwamba, huo mradi mpaka leo haujaanza. Pamoja na jitihada zetu nyingi za kumhimiza huyo Mkandarasi aliyepewa hiyo kazi lakini hajaanza hiyo kazi na inaonekana anakaidi. Ningependa kujua Serikali inachukua hatua gani juu ya Mkandarasi huyu ili kazi hiyo iweze kufanyika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna ahadi kama hiyo katika swali langu la msingi iliyowahi kutolewa kuhusu kupeleka umeme Kata ya Kitaraka kutoka Itigi, Kitaraka, Kazikazi kwenda mpaka Igombega na eneo lile ni njia kuu ya lami inayotoka Itigi kwenda Tabora. Sasa tuna lami lakini hatuna umeme. Ningependa kujua ahadi hiyo imefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (MHE. STEPHEN J. MASELE K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwanza tunashukuru kwa pongezi hizo. Kata

alizozieleza Mheshimiwa Mbunge; Kata ya Mitundu, Mwamagembe na vijiji vya Kalangali, Kiyombo na Kilumbi zipo katika mradi wa REA ambao unatekelezwa hivi sasa Awamu ya II, Mradi Kabambe.

Mheshimiwa Spika, kilichopo sasa hivi ni utekelezaji ambapo Mkandarasi Kampuni ya SPECON ambayo imepewa Mkoa mzima wa Singida na maeneo mengine ya Mkoa wa Tabora, wanaendelea na kazi za ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo mengine na kwenye maeneo haya bado hawajafika. Hivyo Serikali itamhimiza Mkandarasi kuhakikisha kwamba, anaongeza speed ya utekelezaji wa mradi huu kama ilivyopangwa kufikia Juni 30 uweze kukamilika na hususan katika maeneo haya ya Mitundu na Mwamagembe.

Mheshimiwa Spika, dhamira na malengo ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wote waishio vijiji wanapata nishati ya umeme na kazi hii inaendelea kwani ni endelevu. Kwa hivyo, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi vijiji vya Kitara, Kazikazi na vingine vyote alivyovitaja katika awamu zinazofuata REA Awamu ya III vitazingatiwa ili wananchi wanaoishi maeneo hayo waweze kupata umeme.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni dhahiri kwamba, nishati ya umeme ni kiashiria mojawapo na kichochezi cha maendeleo sehemu yoyote ile. Maeneo mengi ya Mkoa wa Mara hususan Tarime, wametandaza nguzo za umeme ziko chini zinakaribia kuharibika na wakati Mheshimiwa Muhongo aliyejewa Waziri wa Nishati na Madini, alifanya ziara mwanzoni mwa mwaka huu aliwaahidi wana Mara kwamba kuitia umeme wa REA wanakwenda kupata umeme kwa zaidi ya asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua imebaki miezi miwili tu Serikali inakwenda kutekeleza vipi hiyo ahadi ya aliyejewa Waziri wa Nishati na Madini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (MHE. STEPHEN J. MASELE K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupongeza jitihada zinazofanywa na Wakandarasi kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yanahitaji kupelekewa umeme katika awamu hii ya II ya REA angalau nguzo kama kifaa muhimu zaidi katika kazi hizo zimeweza kufika kwenye maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, kazi hii inahusisha ukusanyaji wa vitendea kazi mbalimbali vikiwemo nguzo, waya na vifaa vingine ambavyo Wakandarasi wameendelea kufanya kazi hizo kwa bidii kubwa na maeneo mengi ya nchi ambayo yanapaswa kuwa na umeme katika miradi hii ya REA tayari angalau nguzo zimefika. Kwa hivyo, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zilitengwa, zikapitishwa kwenye Bunge hili na Wakandarasi walishapatikana na wako site wanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hivyo Serikali itahimiza uharakishaji wa miradi hii ili ahadi ya aliyejewa Waziri wa Nishati na Madini na ahadi ya Serikali ya kufikisha umeme kwenye maeneo mbalimbali inafikiwa ifikapo mwezi Juni kama ambavyo ilikuwa imepangwa kwenye mikataba.

**SPIKA:** Hizo zinakuwa ahadi za Serikali, siyo za mtu. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Gosbert Blandes.

Na. 40

**Kusambaza Umeme kwenye Vijiji na Maeneo Muhimu**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Mradi wa umeme unaotoka Nyakahanga kwenda vijiji vya Bisheshe, Rwandaro, Nyakayanja, Nyaishozi, Ihembe I na Ihembe II umekamilika lakini wananchi zaidi ya asilimia tisini (90%) hawajapewa umeme:-

(a) Je, ni lini wananchi wa vijiji hivyo watapewa umeme huo?

(b) Je, taasisi mbalimbali kama vile shule, zahanati, makanisa na viwanda zitapewa lini umeme huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (MHE. STEPHEN J. MASELE K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme vijiji vya Bisheshe, Rwandaro, Nyakayanja, Nyaishozi, Ihembe I, Ihembe II, Kasheshe, Rugu, Bujara na Kahanga kutoka Nyakahanga ulitekezwa chini ya Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Kwanza.

Katika mradi huo ujenzi wa uti wa mgongo (*backbone*) wa miundombinu ya usambazaji umeme umekamilika. TANESCO inaendelea kusambaza umeme kwenye maeneo ya jirani na njia kuu iliyojengwa kuititia uwekezaji wa ndani (*Capital Investment Programmes*).

Mheshimiwa Spika, hivi sasa utekelezaji wa Mradi Kabambe wa kusambaza Umeme Vijijini awamu ya pili unaendelea ambapo njia za umeme zilizopo sasa zitarefushwa ili kuwafikia wananchi wengi zaidi hususan kwenye maeneo ya vijiji vya Kamuli, Rwandaro, Nyakayanja, Ruhinda Sekondari, Nyaishozi, Kigando, Ihembe I na Ihembe II.

Mradi unatekelezwa na Wakandarasi wawili; M/S Urban na Rural Engineering Services kwa pamoja. Kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 33 yenye umbali wa kilomita 320; ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 0.4, umbali wa kilomita 460; ufungaji wa transforma 53 na kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 6,000. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 22.34 na mradi umekamilika kwa asilimia 47.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa wananchi wa kawaida, taasisi mbalimbali zinatakiwa kuwasilisha maombi katika ofisi za TANESCO zilizopo karibu na maeneo yao ili kupatiwa huduma ya umeme ambapo daima taasisi hizo hupewa kipaumbele.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Blandes, swali la nyongeza!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla. Pia nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kupeleka umeme katika maeneo hayo, lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, haya maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyataja ni kweli nguzo kubwa zimekwenda, swali langu ni kwamba, wananchi wa vijiji hivyo zaidi ya asilimia 90 wanaona nguzo kubwa zinapita, lakini umeme haujaingia majumbani kwao. Hata ukienda sasa hivi utakuta vitongoji vingi vya Kikanzi, Rwandaro, Kitumbi, Bisheshe, Nyakayanja, Kigando, Kasheshe, Katebuka, Bushonga, hawana umeme, ni nguzo kubwa zimepita. Ni lini hii asilimia 90

ya wananchi ambao hawajapewa umeme na wanauhitaji watapewa? Hilo ndiyo swali langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba sasa hivi kuna Mkandarasi anaendelea kusambaza umeme katika Wilaya ya Karagwe na hasa katika maeneo ya Tarafa ya Nyabionza kwa maana ya Bushanga, lakini hivi ninavyozungumza Mkandarasi huyo amesimama kwa sababu vibarua wote wamegoma na dalili za kwamba mradi huu utakwisha kama ulivyopangwa hazipo.

Nataka kujua, je, Serikali inalijua hili na kama inalijua, inafanya juhudi gani za haraka kuhakikisha kwamba mradi huu unasonga mbele?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi kwani bado Wizara itakuja kuwasilisha mambo yake.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) (MHE. STEPHEN J. MASELE K.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, Serikali iliwaagiza Wakandarasi wote maeneo yote ambayo wanapitisha nguzo zenyé umeme mkubwa kuweka vipozeo vya umeme (transfoma) kwa ajili ya kuhudumia wananchi walioko kwenye maeneo hayo. Zoezi kama hilo limefanyika pia kwenye maeneo ya Nkasi ambapo umeme umepita kwenye baadhi ya vijiji na wameweka transfoma ya kuushusha kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hili ni agizo la Serikali, nina imani Wakandarasi wote wanazingatia kufanya hivyo akiwemo anayefanya kazi katika eneo hili la Karagwe. *It doesn't make sense unajenga umeme unapeleka mbele na unaacha wananchi kwenye vijiji njiani ambao wanastahili pia kupata umeme. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuwaagiza Wakandarasi wote kuhakikisha kwamba wanazingatia kuwaunganishia umeme wananchi wote walioko kwenye maeneo ambako wanapitiwa na njia za umeme.*

Mheshimiwa Spika, hili la pili, Serikali haina taarifa kama wafanyakazi wa kampuni hiyo wamegoma na hivyo tutalifuatilia kujua tatizo ni nini ili tuweze kushirikiana nao kulitatua. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante. Tunakwenda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany!

Na. 41

#### **Malipo ya Wastaafu wa Jumuia ya Afrika Mashariki**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Kwa miaka mingi sasa kumekuwa na kilio cha wastaafu wa Jumuia ya Afrika Mashariki ambapo baadhi yao hawajalipwa kabisa huku baadhi yao wakilipwa kiwango cha chini sana bila kuzingatia hali halisi ya uchumi:

(a) Je, Serikali inatoa taarifa gani kwa Wazee hao?

(b) Je, Wazee hao watalipwa malipo yao au ndiyo funika kombe mwanaharamu apite?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mawaziri kuitia Waraka Na. 39/2005 liliagiza Wizara ya Fedha kulipa mafao hayo yanayodaiwa na wastaifu wa Afrika Mashariki kwa kuzingatia hati ya makubaliano iliyosainiwa tarehe 21 Septemba, 2005 kwa sheria za iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Sheria za Fedha na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hati ya makubaliano hayo, Serikali ilikubali kuwalipa wastaifu 31,831 waliofanya katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hadi tarehe 30 Juni, 1977 kwa kufuata kumbukumbu za kila mmoja na baada ya malipo hayo Serikali itakuwa haidaiwi tena.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha shilingi bilioni 117.0 kilitolewa ili kutumika kulipa stahili ya kila mmoja. Serikali ilitekeleza makubaliano hayo kwa kuwalipa wastaifu 31,792 waliojitokeza kati ya Julai, 2005 na Desemba 2013 kati ya wastaifu 31,831, walokubalika katika hati ya makubaliano (*Deed of Settlement*). Katika malipo hayo ilikubalika pia kuwa kila mstaifu aongezewe riba ya asilimia kumi na saba na nusu ili kufidia kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo ya Baraza la Mawaziri kwa kuzingatia hati ya makubaliano, *Deed of Settlement* na wazee hao walilipwa mafao yao kwa mujibu wa hati ya makubaliano na hakuna madai mengine ambayo Serikali inadaiwa kisheria.

Hivyo basi, pamoja na maelezo hayo, naomba kuhitimisha majibu haya kwa kueleza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Desemba, 2013 Serikali imewalipa wastaifu 31,792 wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa kuzingatia hati ya makubaliano ilyoafikiwa kwa pamoja.

(b) Mheshimiwa Spika, Wazee hao wamelipwa mafao yao na kwa mujibu wa hati ya makubalianoy hakuna madai mengine ambayo Serikali inadaiwa.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini maelezo yake yametawaliwa zaidi na hati ya makubaliano, ni nini hasa maana ya hati ya makubaliano? Makubaliano hayo yalikuwa ni yapi? Swalii la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba kwa muda mrefu hii hoja ya wastaifu wa Afrika ya Mashariki ni ya muda mrefu na Serikali inasema kwamba imeshawalipa wote. Sisi kama Wabunge bado tunaletewa malalamiko mengi ya wastaifu hao kwamba bado wengi wao hawajalipwa mafao yao, pamoja na thamani ya fedha kuanguka.

Je, Mheshimiwa Waziri mlifanya rejea tena kwa Wastaifu wote na ninyi mkajiridhisha pamoja na hiyo hati ya makubaliano?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba ile Hati ya Makubaliano (*Deed of Settlement*) inatokana na kesi ilioyofunguliwa na wastaifu mwaka 2003. Kwa hiyo, baada ya miaka miwili ya majadiliano, mahakama ikaamua kwamba nendeni mkaafikiane huko huko nje.

Sasa walipokwenda nje kuafikiana, wakaja na kitu kinaitwa *Deed of Settlement* iliyorudishwa mahakamani ikaridhiwa na mahakama kwamba sawa, sasa ninyi watu 31,831 nendeni mkalipwe bilioni 117. Wao katika ile *Deed of Settlement* walikuwa wameandikiana pale, basi iliporudi Serikalini, Baraza la Mawaziri likasema tunalipa kitu hiki tumemalizana na hii kesi.

Mheshimiwa Spika, iliporudi nje, katika wale waliosaini ile *Deed of Settlement* wengine walisema hapana twende tukadai zingine na wengine wakasema hapana hizi pesa ni ndogo. Kwa hiyo, baada ya pale mionganoni mwao wenye ikatokea ubishi. Kwa hiyo, toka mwaka 2005 mpaka 2010 ambapo malipo hayo yamefanywa kuna watu kama 40 ambao wao walihakikiwa lakini hawakwenda kuchukua hizo hela.

Mheshimiwa Spika, baada ya pale wakajitokeza na wengine tena, kwa mfano wa Shirika la Reli ambako kulikuwa na watu 242 ambapo 42 walihakikiwa, lakini wakasema na wale 200 wengine na ugumu wake unatoka na nini, kwamba kuna mashirika pale kama manne *East African Airways, East African Harbours, Post And Telecommunications*.

Mheshimiwa Spika, sasa yale wote yana watendaji na tatizo hili siyo la Tanzania peke yake, kote ni tatizo. Kwa hiyo, naomba kusema kwamba, Mahakama kwa busara yake iliamua kwamba *out of court settlement* baada ya kuafikiana na kujadiliana wingi wa wazee na kadhalika, ndio ilikuwa njia bora na ndoyo ikaamuliwa kulipa wale wazee 31,831.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niseme kwamba kwa kuwa ule ulikuwa ni uamuzi wa Kimahakama, Serikali baada ya kulipa dhamana yake au *obligation* yake kwenye jambo lile haikuwa na *obligation* nydingine tena, lakini nakubaliana na Mheshimiwa Barwany kwamba muda ukipita sana thamani ya pesa na kadhalika inafanya kwamba hata haki uliyopewa mwaka 2005 kwa mwaka 2015 inaonekana ni ndogo.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Cecilia Paresso atauliza swali.

Na. 42

### **Mgogoro wa Wananchi na TANAPA**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Kumekuwepo na mgogoro wa muda mrefu kati ya wananchi wa Kata ya Buger Wilayani Karatu na TANAPA wanaohifadhi Msitu wa Maranq uliopo katika Kata hiyo:-

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huo ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi kwa utulivu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la msitu wa Maranq lilikuwa ni Msitu wa Hifadhi toka mwaka 1957. Msitu huu ulipandishwa hadhi na kujumuishwa kwenye sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kwa Tangazo la Serikali Namba 105 la mwaka 2009.

**SPIKA:** Naomba uongeze sauti.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, eneo la msitu wa Maranq lilikuwa ni Msitu wa Hifadhi toka mwaka 1957. Msitu huu ulipandishwa hadhi na kujumuishwa kwenye sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kwa Tangazo la Serikali Namba 105 la mwaka 2009. Kabla ya kupandishwa hadhi na kujumuishwa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, Msitu huu haukuwahi kuwa chini ya Kijiji chochote hata hivyo wananchi walikuwa wanaruhusiwa kuingia na kuokota kuni.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Taifa ya Tanzania Sura Namba 282, baada ya Msitu wa Maranq kupandishwa hadhi, wananchi hawaruhusiwi kuingia na kufanya shughuli yoyote ikiwemo kuokota kuni.

Mheshimiwa Spika, endapo kuna mgogoro wowote kati ya wananchi wa Kata ya Bugeri na TANAPA kuhusu eneo la Msitu wa Maranq, Wizara yangu iko tayari kushughulikia mara moja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Katika jambo lolote suala la ushirikishwaji wa wananchi ni jambo la msingi sana na mmechukua eneo hili nyie TANAPA bila ya kukaa na wananchi na kuwashirikisha. Ni kwa nini mmefanya hivyo bila ya kuwashirikisha wananchi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, mnasema kwamba endapo kuna mgogoro, ni kama vile hamjui wakati muda wote wa miaka mitano hapa Bungeni tumewaeleza na kuwaambia kuwa kuna mgogoro katika eneo hilo kati ya wananchi na TANAPA, askari wa TANAPA wanawapiga wananchi, wanawavunja miguu, wananchi ni walemaru, wanatozwa faini mbalimbali ambazo hatujui zinakwenda wapi, tumewaambia halafu mnasema kwamba endapo. Sasa ni lini mtakuja kukaa na hawa wananchi ili haya matatizo yaondoke?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, siku za nyuma kulikuwa kuna mgogoro katika eneo hilo, ni kweli na kilifanyika kikao kati ya wataalam wa Halmashauri ya Wilaya, wananchi pamoja na TANAPA. Tiliuangalia kwa makini mgogoro huo na kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi walikuwa wanalima kwenye yale mashamba tuliamua kuyatoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anasema lakini tulishakaa kikao kati ya wananchi, TANAPA pamoja na Halmashauri ya Wilaya na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ndiyo wameweka beacon kwenye hayo maeneo ambapo kwa sasa kwenye mgogoro kwa maana ya mipaka, sisi hatuna.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna mgogoro ambaa umejitokeza sasa hivi, wananchi wameamua kuchungia ng'ombe kwenye eneo la hifadhi. Kwa mujibu wa sheria hilo ni kosa na kama mtu ataingia kwenda kuchunga ng'ombe tutamchukulia hatua za kisheria. Hapa katikati lilijitokeza tatizo na askari wetu mmoja wa wanyamapori alinyang'anywa bunduki.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu iko tayari kukaa na kama kuna kitu kimejitokeza, sisi tutakaa pamoja na tutazungumza pamoja. Leo hii nimezungumza na Mkurugenzi pamoja na Mkurugenzi wa Hifadhi ya Manyara amesema hakuna mgogoro wowote.

**SPIKA:** Kusema sema hovyo! Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, naomba kuwatambua baadhi ya wageni tulionao.

Tunao wageni 28 wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi ambaa ni Maafisa kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ikulu, Ndugu Peter Ilomo naomba asimame alipo, ahsante na karibu. (Makofii)

Naibu Katibu Mkuu wa Utumishi Ndugu Hab Mkwizu; Naibu Katibu Mkuu Ikulu, Ndugu Suzan Mlawi; Karani wa Baraza la Mawaziri, Ndugu Gerson Mdemu; kuna Katibu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ndugu Tixson Nzunda; halafu kuna Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Dkt. Edward Hosea. Ahsanteni sana. (Makofii)

Wageni wa Mheshimiwa Job Ndugai Mheshimiwa Naibu Spika amba ni wanafunzi kutoka shule ya Sekondari ya Saint John, Manyoni. Hawa wanafunzi wasimame walipo kama wameingia. Ahsanteni, tumefurahi kuwaona na tunawatakieni kusoma kwema. (Makofii)

Tuna viongozi nane kutoka Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango wakiongozwa na Dkt. Philip Mpango, Katibu Mtendaji, ye ye mwenyewe yupo. Nashukuru. (Makofii)

Kuna watumishi 20 kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka na wao wasimame sijui wako wapi. Ahsanteni sana, tumefurahi kuwaona. (Makofii)

Tuna wageni nane wa Mheshimiwa Sophia Simba Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutoka Chuo Kikuu Huria wakiongozwa na Dkt. George Nyaronga, Dkt. George uko wapi na wanafunzi wenye wapi. Ahsanteni sana na karibuni. (Makofii)

Tuna wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe, ni Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Ndugu Jumanne Kpollo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Serengeti. Makamu huyo asimame na wenzake. Ahsante sana na karibuni. (Makofii)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Philipo Mulugo, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kutoka Chunya wakiongozwa na Ndugu Kapala Makelele, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mwenyekiti wa CCM. Naomba wageni hawa wasimame. Ahsanteni sana na karibuni sana. (Makofii)

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye ni Ndugu Ahmed Kiobya, Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Ibwera. Huyu siyo ndugu, anaitwa Mheshimiwa. Ahsante na karibu sana. (Makofii)

Pia tunawakaribisha wageni wengine wote.

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa nane watakuwa na Kikao chao katika ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, naye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao leo saa nane, lakini katika ukumbi namba 231.

Halafu nawatangazia Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi, maana yake Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kuwa tutakuwa na kikao cha majumuisho saa tano asubuhi katika Ukumbi wa Spika. Jana tulisema Jumapili hatukufanikiwa kwa sababu viongozi wengine hawakuwepo. Kwa hiyo, ni Wenyeviti wote pamoja na Kamati ya Bajeti, tutakuwa nao katika Ukumbi wa Spika, saa tano.

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka  
wa Fedha 2015/2016 - Ofisi ya Rais, Utumishi**

**SPIKA:** Ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Mtoa Hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi atachangia dakika 40 na yule wa Mahusiano na Uratibu dakika 20. Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, MHE. CELINA  
OMPESHI KOMBANI (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI  
YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA  
ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu Fungu 20 na 30; Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32; Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, Fungu 33; Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 67; Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94; Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, Fungu Tisa (9); Ufutiliaji na Utekelezaji wa Miradi, Fungu namba Sita (6) na Idara za Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Fungu namba Nne (4), Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha mpango wa utekelezaji wa makadirio ya fedha katika Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake kwa mwaka wa 2015/2016.

Awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Jasson Rweikiza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na pia nampongeza Mheshimiwa Gosbert Blandes kwa kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Wenyeviti wote na Makamu Wenyeviti...

**SPIKA:** Wale wanaotoka tunataka amani humu ndani, muondoke kimya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** ...katika Kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Sheria, Katiba na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti wa mwaka 2014/2015 na mapendekezo ya utekelezaji wa Makadirio ya Mpango na Matumizi wa mwaka 2015/2016.

Maoni na ushauri wa Kamati umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa jinsi inavyokidhi matarajio ya wadau wetu pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati.

Naomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake katika kuingoza nchi yetu kwa amani na utulivu na chini ya uongozi wake Serikali imeendelea kutekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi katika kipindi cha uongozi wake.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbalimbali za umma. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kusimamia vyema shughuli za kila siku za Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima, nampongeza Naibu wako pia na Makamishna wote ambao wanakusaidia wewe.

Namshukuru sana Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu; Mheshimiwa Kapteni Mstaafu Mheshimiwa George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora pamoja na Profesa Mark Mwandomsya, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Peter Ilomo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu; Bwana Hab Mkwizu, Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bibi Suzan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu, Makamisha, Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zote zilizo chini ya Rais.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki pamoja na familia yangu kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipatia na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika kipindi hiki cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko natoa pole kwa Watanzania waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo ajali, mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpa pole Mama Maria Nyerere kwa kufiwa na mwanawe mpendwa John Nyerere ambaye amefariki wiki moja iliyopita na mazishi kufanyika kule Butiama.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nachukua nafasi hii pia kuzishukuru nchi wahisani wa maendeleo ambao wanatusaidia katika maendeleo mbalimbali katika nchi yetu. Nchi hizo ni pamoja na Australia, China, Indonesia, Finland, Brazil, India, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujeruman, Uswiss, Marekani, Ireland, Israel, Canada, Denmark, Norway, Sweden, Jumuiya ya Madola, Umoja wa Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ya Japan, UNDP, Bill and Melinda Gates Foundation, Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na OPEC.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa fedha 2014/2015, pamoja na mpango wa maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti. Utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2014/15 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano yaani 2011 - 2016, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) Awamu ya Pili na llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kazi ambazo zimefanyika katika Ofisi ya Rais, Ikulu pamoja na Taasisi zake ni kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 9.4 katika Fungu 20 na shilingi bilioni 275.0 kwa Fungu 30, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 159.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 shilingi bilioni 6.5 katika Fungu 20 na shilingi bilioni 218.5 katika Fungu 30 za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa fedha za maendeleo jumla shilingi bilioni 113.1 ziliwa zimepokelewa, sawa na asilimia 71 ya bajeti iliyoidhinishwa ya fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ikulu. Ofisi ya Rais ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi mwezi Machi, 2015 kazi zifuatazo zimefanyika:-

(i) Huduma za Rais na familia yake;

(ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma;

(iii) Mikutano 33 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri imefanyika; na

(iv) Juhudi za kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea na mukutano wa ushirikiano katika masuala ya utawala bora ulifanyika mwezi Januari mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, maeleo zaidi ya utekelezaji katika Ofisi ya Rais, Ikulu yapo katika hotuba yangu ambayo Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329, jukumu kubwa la TAKUKURU ni kuelimisha umma juu ya rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani na kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwezi Julai, 2014 hadi mwezi Machi, 2015 kazi zifuatazo zimetekelizwa:-

(i) Tuhuma 3,383 zikiwemo tuhuma mpya 615 za mwaka 2014/2015 zilichunguzwa ambapo uchunguzi wa tuhuma 607 umekamilika.

(ii) Kesi mpya 192 zilifunguliwa Mahakamani zikiwemo kesi 11 zilizotokana na uchunguzi maalum wa vocha za pembejeo za kilimo; kesi nne zinazohusu maliasili ya nchi na kesi 11 zinazotokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(iii) Majadala 50 yanayohusu tuhuma za rushwa yaani *grand corruption* yalifikisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na kati ya majalada hayo 27 yamepata kibali cha watuhumiwa kufikishwa Mahakamani.

(iv) Kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika jitihada za kupambana na rushwa, watusika waliopatikana na hatia walirejesha jumla ya shilingi 623,943,408/= na takwimu zaidi za mwenendo wa uchunguzi wa tuhuma za rushwa zinaonyeshwa katika kiambatanisho namba moja cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, maeleo ya kina ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais TAKUKURU yapo katika kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la mpango huu ni kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini, unaotambulika na kukubalika kisheria. Mfumo huu umelenga kufanya urasimishaji wa rasilimali na biashara kuwa ni wa haraka, rahisi na ni wa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, utekelezaji wa mfumo huu unakusudiwa kuwawezesha Watanzania kushiriki kwa ukamilifu katika uchumi wa soko unaotambulika kisheria. Katika kipindi cha mwaka 2014/2015 kazi zifuatazo zimeteklezwa:-

(i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makazi, Nishati na Maji ya Zanzibar urasimishaji wa ardhi umeendelea kutekelezwa katika sehemu za Nungwi na Chokocho na wananchi wamepewa usajili;

(ii) Utaratibu wa kutayarisha na kutoa hati za hati miliki za kimila umefanyika jumla ya hati 9,754 zimetayarishwa katika Halmashauri nane; na

(iii) Mashamba ya wakulima wa chai yamerasimishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa katika Wilaya ya Misenye, Kilombero na Kilosa nao pia umefanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa rejea zaidi, maelezo zaidi yapo kwenye hotuba yangu ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo TASAF. TASAF ipo katika utekelezaji wa awamu ya tatu inayohusu mpango wa kunusuru kaya maskini uliozinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Agosti, 2012. Na utekelezaji wa mpango huu unafanyika katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/2015 TASAF imetekleza mambo yafuatayo:-

(i) Utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini umefikiwa katika Halmashauri 159 Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Jumla ya kaya maskini 945,293 zenye watu milioni 4.8 kutoka katika Vijiji 7,808 Mitaa 1,952 na Shehia 40 zimetambulika na kaya 932,301 zimeandikishwa. Lengo ni kuandikisha kaya zaidi ya milioni moja, ifikapo mwezi Juni mwaka huu; na

(ii) Kaya maskini 266,601 zililipwa jumla ya shilingi bilioni 42.6 katika vipindi vya mizunguko nane ya malipo kama ruzuku ya kunusuru katika maeneo ya utekelezaji zikiwemo Halmashauri 38 Tanzania Bara, pamoja na Unguja, Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwa rejea zaidi tuangalie kiambatanisho namba mbili na maelezo zaidi yapo katika hotuba yangu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wayapitie na kuyaangalia.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa kujitegemea. Majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibashara ili kuongeza ufanisi katika biashara.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kazi zifuatazo zimefanyika:-

- (i) Vijana wajasiriamali 50 ambaao ni wahitimu wa Chuo cha VETA Dar es Salaam walijunga katika vikundi kumi na walipewa mikopo;
- (ii) Mafunzo ya awali yalifanyika kwa vijana 324 wahitimu wa VETA Dar es Salaam kuhusu uchanganuaji wa miradi ya biashara; na

(iii) Utafiti juu ya mahitaji ya kibiashara ya vijana waliohitumu vyuo vya ufundi umefanyika na utafiti huo umebaini kuwa vijana wamependelea kufanya shughuli za kiufundi zinazotegemeana katika eneo moja na wengi wanahitaji mikopo ya zana za ufundi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina yapo katika kitabu ambacho Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; katika mwaka 2014/2015 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 36.4 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 29.1 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.2 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 jumla ya shilingi bilioni 25.8 zilipokelewa na kutumika kama matumizi ya kawaida na kwa upande wa miradi ya maendeleo jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na weledi. Aidha, watumishi wa umma wanawajibika kwa usikivu kwa wananchi pale wanapotoa huduma mbalimbali kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Julai, 2014 hadi Machi, 2015, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake zimetekeliza kazi zifuatazo:-

(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma:-

(i) Imetoa vibali vya ajira mpya katika nafasi 58,483 kati ya nafasi 68,133 zilizoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2014/2015 na vibali vingine vinaendelea kutolewa;

(ii) Watumishi wa Umma 15,992 wa kada mbalimbali walipandishwa vyeo katika nafasi za vyeo 49,000 zilizoidhinishwa. Kwa hiyo, wengine watapandisha vyeo mwezi huu na mwezi ujao; na

(iii) Kima cha chini cha mshahara kilipandishwa kutoka 240,000 kwenda 265,000.

Mheshimiwa Spika, maelezo zaidi ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yapo katika kitabu ambacho Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC). Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala na kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo mbalimbali ya utumishi wa umma. Pia ni jukumu la chuo kutoa machapisho mbalimbali ya kitaalamu katika utumishi wa umma.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 kazi zifuatazo zimetekeliza na Chuo cha Utumishi wa Umma:-

(i) Mafunzo ya kuijandaa kufanya mitihani yalitolewa kwa watumishi 692;

(ii) Ushauri wa kitaalam ulitolewa kwa Taasisi 21 katika fani ya mafunzo ya kimenejimenti na usimamizi katika utumishi wa umma;

- (iii) Machapisho tisa ya kitaaluma yalitolewa;
- (iv) Tawi la Chuo cha utumishi wa Umma la Mbeya lilifunguliwa; na
- (v) Aidha, awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo lenye ghorofa tatu limeanza kwa ajili ya madarasa na ofisi katika campus ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtando (TaGLA). Wakala ina jukumu la kuwajengea uwezo watumishi wa umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano, kwa lengo la kuwawezesha kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wakala imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa washiriki 585;
- (ii) Huduma za maunganisho (*bridging service*) na msaada wa kiufundi kwa wadau 18 nchini, kwa kuwawezesha kufanya mikutano na mafunzo kwa njia ya mitando ilitolewa; na
- (iii) Baada ya wakala kuunganishwa kwa mkongo wa Taifa imeongeza uwezo wa kuunganisha vituo 20 kufanya mikutano na mafunzo kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Serikali Mtando (*E-Government*); Wakala ina jukumu na mamlaka ya kuratibu kusimamia na kukuza jitihada za Serikali mtando katika utumishi wa umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Wakala ina wajibu wa kuweka na kusimamia mifumo ya mawasiliano iliyo salama Serikalini, inayowezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wakala imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Taasisi za Serikali 67 zimeunganishwa kwenye mtando wa mawasiliano Serikalini yaani *Government Network*;
- (ii) Uboreshaji wa mfumo wa barua pepe wa Serikali kwa kuunganisha Taasisi za Serikali 35 kwa lengo la kutumia mfumo huu limekamilishwa;
- (iii) Tovuti Kuu ya Serikali yaani *Government Portal* imeboreshwa kwa kuweka nyaraka na taarifa muhimu kwa matumizi ya wananchi wote;
- (iv) Tovuti za Taasisi 30 za Serikali zimetengenezwa, zimebekwa na kuhifadhiwa;
- (v) Tovuti ya takwimu huru imeanzishwa na inapatikana kwa kupitia anuani ya open data portal; na
- (vi) Mfumo wa kuomba ajira kwa njia ya ki-elektroniki umekamilishwa na umeunganishwa.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya Serikali mtando yapo katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 33 lilitengewa jumla ya shilingi bilioni 8.7. Kati ya hizo bilioni 6.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida; bilioni 2.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hadi kufikia mwezi Machi, 2015 shilingi bilioni 3.2 za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kutumika na jumla ya shilingi milioni 489.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilipokelewa.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398 ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za viongozi wa umma waliotajwa katika kifungu cha 4(1) cha sheria hiyo kinazingatia misingi ya maadili kwa lengo la kukuza imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa viongozi wa umma.

Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi imefanya kazi zifuatazo:-

- (i) Viongozi wa umma 13,193 walitumiwa fomu ya tamko la rasilimali na madeni;
- (ii) Vikao viwili vya Baraza la Maadili vimefanyika Jijini Dar es Salaam;
- (iii) Viongozi wa umma 3,980 wamepata elimu kuhusu Sheria ya Maadili; na
- (iv) Ujenzi wa mfumo wa kielektroniki unaotumika kukusanya na kuchakata taarifa mbalimbali zinazohusu viongozi wa umma umeandaliwa na upo katika hatua za majaribio.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya kina yapo katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira. katika mwaka wa fedha 2014/2015, Fungu 67 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya fedha za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya shilingi bilioni 2.2 zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Sekretarieti ya Ajira ni kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa kanzidata wa wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira, kuandaa orodha ya wahitimu wa Vyuo Vikuu na wataalam wenye weledi kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika utumishi wa umma, kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika utumishi wa umma, kufanya usaili na kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mchakato wa ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/2015 Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imetekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye hotuba yangu ambayo Waheshimiwa Wabunge wamepatiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 13.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2015, jumla ya fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 2.7 ambazo zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma ni Tume rekebu na inayo wajibu wa kuhakikisha kwamba masuala ya rasilimali watu katika utumishi wa umma yanaendeshwa kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na taratibu kwa lengo la kuimarisha utendaji unaozingatia

malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ina mamlaka ya rufaa kwa watumishi wa umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume imetekeleza kazi ambazo nimeziainisha katika hotuba yangu, naomba Waheshimiwa Wabunge wasome yapo maelezo ambayo yametoa ufanuzi kwa kina.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, Fungu namba Tisa (9), iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mpaka kufikia mwezi Machi, 2015 jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoanzishwa kwa tamko la Rais kuititia Tangazo la Serikali Na. 162 la tarehe 3 Juni, 2011. Uanzishwaji wa Bodi ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume mbalimbali zilizoishauri Serikali namna ya kuboresha mishahara katika utumishi wa umma, pamoja na utekelezaji wa sera ya mishahara na motisha katika utumishi wa umma ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Bodi hii ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza kwa Rais kuhusu viwango vya mishahara, posho na mafao katika utumishi wa umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kazi mbalimbali zimetekelizwa na naomba Waheshimiwa Wabunge wasome katika kitabu ambacho tumewagawia cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi, Fungu Namba sita (6) lilitengewa jumla ya shilingi bilioni 34.2 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 28 ni kwa ajili ya fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 shilingi bilioni 17.7 zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo, Serikali ilianzisha mpango wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Kitaifa. Mfumo huu wa Telekeza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ulilenga kurahisisha kufikishwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia 2025.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa BRN umekuwa katika mikondo miwili mikubwa yaani ujenzi wa mfumo na taasisi za kusimamia na kuhakikisha kuwa matokeo tarajiwa yanapatikana, pamoja na usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mikakati inayoainishwa katika maeneo makuu sita ya matokeo Kitaifa yanayojumuishwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mfumo huu. Maeneo haya sita ni Elimu, Kilimo, Maji, Nishati, Rasilimali Fedha pamoja na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya ziada katika kasma hii yapo katika kitabu changu ambacho Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na sasa naomba kutoa mapendekezo ya mpango wa bajeti wa 2015/2016 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa bajeti kwa mwaka 2015/2016 kwa Mafungu ya 20, 30, 32, 33, 67, 94, (9), (6) na (4) umeandalowi kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoidhinishwa katika Mwongozo wa Taifa wa kuandaa mpango wa bajeti kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu; Ofisi hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo ambazo zimeainishwa katika hotuba yangu pamoja na taasisi zake kama ifuatavyo:-

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa mwaka 2015/2016 nayo imepanga kutekeleza kazi ambazo zimeainishwa katika hotuba yangu.

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kwa mwaka 2015/2016 nazo kazi ambazo zimepangwa kutekelezwa ziko katika hotuba yangu, naomba Waheshimiwa Wabunge wazipitie.

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa mwaka 2015/2016, imepanga kutekeleza kazi ambazo zimeainishwa kwa kina katika hotuba yangu.

Taasisi ya Uongozi nayo kwa mwaka 2015/2016 imepanga kutekeleza kazi mbalimbali ambazo zimeainishwa katika hotuba yangu.

Mfuko wa Rais wa Kujitegemea kwa mwaka 2015/2016 umepanga kutelekeza kazi mbalimbali ambazo pia zimeainishwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kutekeleza mpango wa mwaka 2015/2016, Fungu 20, Ofisi ya Rais, Ikulu, linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 20.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Fungu 30, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 322.5 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 145.5 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake maelezo ya kina yapo katika kitabu changu ambacho nimekigawa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016 itatekeleza kazi mbalimbali zikiwemo taasisi zake ambazo ni pamoja na Chuo cha Utumishi wa Umma, Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtando (TaGLA), Wakala wa Serikali Mtando (e-Government).

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mpango wa mwaka 2015/2016 Fungu 32, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 46.6 na kati ya fedha hizo bilioni 37.7 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 8.9 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Maelezo ya kina yapo katika kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi itatekeleza kazi mbalimbali ambazo zimeainishwa katika kitabu changu. Ili kutekeleza mpango wa mwaka 2015/2016, Fungu 33 yaani Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeomba jumla ya shilingi ya shilingi bilioni 7.7 na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 6.2 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 1.4 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Maelezo ya kina yapo katika kitabu ambacho Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi mbalimbali na ili kutekeleza mpango huu Fungu 67, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Rais Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi mbalimbali ambazo zimeainishwa katika kitabu changu na ili kutekeleza mpango wa mwaka 2015/2016 Fungu 94 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma imeomba kutumia jumla ya shilingi bilioni 14.0 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Maelezo ya kina yapo katika kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa Fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi mbalimbali ambazo zimeainishwa katika kitabu changu. Ili kutekeleza mpango huu Fungu Tisa (9) yaani Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maelezo ya kina yapo katika kitabu ambacho Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ufutiliaji na Utekelezaji wa Miradi. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Rais Ufutiliaji na Utekelezaji wa Miradi utatekeleza kazi mbalimbali ambazo zimeainishwa katika kitabu changu na ili kutekeleza mpango wa mwaka wa fedha 2015/2016 Fungu Na. (6) Ofisi ya Rais, Ufutiliaji na Utekelezaji wa Miradi imeomba jumla ya shilingi bilioni 20.2 na kati ya fedha hizo, bilioni tano ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 14 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kumbukumbu za Nyaraka. Idara ya Kumbukumbu za Nyaraka hiyo ni Idara mpya na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Fungu Na. (4) Idara ya Kumbukumbu za Nyaraka imeomba shilingi bilioni 1.4 na kati ya hizo, bilioni 1.2 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi milioni 250 ni kwa ajili ya fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, majumuisho. Ofisi ya Rais Ikulu, Menajimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, Ufutiliaji na Utekelezaji wa Miradi na Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa kisheria ndizo zenye kuhakikisha kuwa majukumu hayo muhimu yanatekelezwa katika mipango na bajeti za mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, hayo yanawezekana yakienda sambamba na uimarishaji wa usimamizi bora wa shughuli za Serikali ili kupata Matokeo Makubwa Sasa kwa lengo la kufikia malengo ya mipango ya Kitaifa ya muda wa kati na ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2014/2015, na mipango yetu kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Rais Ikulu - Fungu 20, Matumizi ya kawaida jumla ya shilingi 20,575,672,000/=.

Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Matumizi ya Kawaida shilingi 322,593,728,000/= na matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 145,503,265,000/. Jumla shilingi bilioni 468,096,993,000/=.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Fungu 32; Matumizi ya Kawaida, shilingi 37,717,620,000/=, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi 8,959,944,000/. Jumla shilingi 46,677,564,000/=.

Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Matumizi ya Kawaida shilingi 6,216,691,000/=; na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi 1,485,897,000/. Jumla ni shilingi 7,702,588,000/=.

Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Matumizi ya kawaida shilingi 5,427,839,000/=.

Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi ya Umma, Matumizi ya Kawaida shilingi 14,070,255,000/=.

Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma; Matumizi ya Kawaida shilingi 3,262,452,000/=.

Fungu Na. 6 - Ofisi ya Rais, Ufutiliaji na Utekelezaji wa Miradi; Matumizi ya Kawaida shilingi 5,958,004,000/= na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo shilingi 14,276,934,000/=.

Fungu Na. 4 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; Matumizi ya Kawaida shilingi 1,236,324,000/= na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo jumla ya shilingi 250,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, MHE. CELINA  
OMPESHI KOMBANI (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI  
YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochangua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya

Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09), Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (Fungu 06) na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04), Bunge lako sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2014/15. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2015/16.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala; pia nampongeza Mhe. Gosbert Begumisa Blandes (Mb) kwa kuendelea kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe walioteuliwa katika Kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu katika kipindi hiki.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2014/15 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/16. Maoni na ushauri wa Kamati umetuwezesha kutekeleza majukumu kwa jinsi inavyokidhi matarajio ya wadau wetu pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati.

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake katika kuiongoza nchi yetu. Chini ya uongozi wake Serikali imeendelea kutekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi katika kipindi cha Uongozi wake.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbalimbali za Umma. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) kwa kusimamia vyema shughuli za kila siku za Serikali na ndani ya Bunge lako Tukufu.

6. **Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nampongeza pia Naibu Spika Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) kwa kuendesha vyema shughuli za Bunge. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu (Mb), Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o (Mb) na Mheshimiwa Kidawa Hamis Salehe (Mb) kwa umahiri wao wa kuliongoza Bunge lako Tukufu.

7. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu; Mheshimiwa Kapt. (Mst.) George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandsoya (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum kwa ushirikiano wao mkubwa katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii. Aidha, nawashukuru Balozi Ombeni Yohana Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Peter Alanambula Ilomo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Bwana HAB Mkwizu, Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bibi Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Makamishna na Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais na Taasisi zake kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki na familia yangu kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu katika nafasi niliyo nayo.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako binafsi, Bunge lako pamoja na jamaa na familia ya Mbunge aliyeaga dunia katika mwaka huu wa fedha, Marehemu Kapt. John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi.

Aidha, natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo ajali na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi. Amina.

9. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao ni Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja na Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika jithada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Hivyo, nachukua nafasi hii kuzishukuru Nchi hizo na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambazo ni: Australia, China, Indonesia, Finland, Brazil, India, Italia, Japan (JICA), Korea ya Kusini (KOICA), Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Uhlanzi, Uingereza (DfID), Ujerumani (GIZ), Uswisi, Marekani (USAID), Ireland, Israel, Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), Norway (NORAD), Sweden (SIDA), Jumuiya ya Madola, Umoja wa Ulaya, Benki ya Dunia, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), UNDP, Bill and Melinda Gates Foundation, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na OPEC.

11. **Mheshimiwa Spika**, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili (2) ambayo ni; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa mwaka wa fedha 2014/15 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2015/16.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2014/15

12. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/15 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II) na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Kazi zilizotekelawa kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:

### OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

13. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha, 2014/15, Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilitengewa jumla ya **Shilingi 9,446,179,000** (Fungu 20) na **Shilingi 275,038,880,000** (Fungu 30) kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 159,214,964,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2015 **Shilingi 6,515,034,086** (Fungu 20) na **Shilingi 218,588,296,756** (Fungu 30) za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 113,156,143,316** zilipokelewa na kutumika, kiasi hicho ni wastani wa asilimia 71 ya bajeti iliyoishinishwa ya fedha za maendeleo.

#### (a) Ikulu

14. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2014 hadi Machi, 2015, kazi zifuatazo zilitekelezwa:

- (i) Huduma kwa Rais na familia yake zimeendelea kutolewa;

- (ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa na ushauri wenyewe lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi zilitolewa;
- (iii) Mikutano 33 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo Nyaraka 70 zilichambuliwa, Mikutano 16 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na Nyaraka 38 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano tisa (9) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na Nyaraka 39 zilifanyiwa uamuzi. Aidha, Mikutano minane (8) ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 18 zilijadiliwa;
- (iv) Mikutano 11 ya Kamati ya Katiba, Sheria na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na kujadili miswada 15 ya Sheria, mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Uchumi na Fedha ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo mada na Hati tisa (9) zilijadiliwa na kutolewa uamuzi. Aidha, mikutano wa Kamati ya Mazingira ya Baraza la Mawaziri ulifanyika ambapo Hati mbili (2) zilijadiliwa;
- (v) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) umeandaliwa na umewasilishwa Serikalini kwa uamuzi. Mkakati huu utatekelezwa kwa miaka mitano (2015/16 hadi 2019/20);
- (vi) Juhudi za kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zinaendelea na Mkutano wa ushirikiano katika masuala ya utawala bora ulifanyika mwezi Januari, 2015;
- (vii) Utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership) umeendelea kuratibiwa. Mpango kazi wa Awamu ya pili 2014/15 - 2015/16 umeandaliwa na kuanza kutekelezwa. Maeneo ya kipaumbele katika Mpango huo ni pamoja na kuweka wazi maeneo ya ardhi yaliyopimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali; kutungwa kwa Sheria ya Haki ya Kupata Habari; kuanzishwa tovuti ya takwimu huria (Open Data) na kuweka kwenye tovuti nyaraka mbalimbali za fedha na bajeti. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa mpango huo hadi Desemba, 2014 imekamilika;
- (viii) Rufaa 72 za Watumishi wa Umma zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa Rais kwa uamuzi. Aidha, malalamiko 168 ya watumishi wa umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo na Rais au Katibu Mkuu Kiongozi;
- (ix) Kamati Maalum inayoratibu utekelezaji wa Mpango wa Mapambano Dhidi ya Rushwa ulioko chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa imefanya vikao vitano (5) vya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango katika kupunguza rushwa na urasimu katika ufanyaji wa biashara nchini;
- (x) Taarifa ya Mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne kwa mwaka 2005-2014 iliandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu;
- (xi) Taarifa za utekelezaji wa Programu nane za Maboresho kwa mwaka 2014/15 zilichambuliwa kila robo mwaka na kubainika utekelezaji wake ni wa wastani;
- (xii) Ufuatiliaji wa Programu za Maboresho ngazi ya utekelezaji umefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Kituo cha Kutolea Huduma za Biashara kwa Pamoja – Horohoro na Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga ambapo ilibainika kwamba mifumo ya upimaji utendaji kazi inatekelezwa;

- (xiii) Mikutano sita (6) baina ya Serikali na viongozi wa dini mbalimbali na vyama vya siasa ilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mara na Tanga kwa lengo la kusisitiza amani, utulivu na upendo mionganoni mwa Watanzania;
- (xiv) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano, Ikulu umekamilika kwa asilimia 98 na ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 8 Desemba, 2014;
- (xv) Ukarabati wa Jengo la Wageni katika Ikulu Ndogo ya Chamwino unaendelea; na
- (xvi) Ukarabati wa kawaida wa Jengo la Ikulu, Ikulu Ndogo ya Dodoma Mjini na Mwanza pamoja na nyumba za wafanyakazi wa Ikulu umefanyika.

**(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

15. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329, jukumu kubwa la TAKUKURU ni kuelimisha umma juu ya rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mahakamani na kuishauri Serikali namna ya kuziba mianya ya rushwa.

16. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2014 hadi Machi, 2015 kazi zifuatazo zilitekelezwa:

- (i) Tuhuma 3,383 zikiwemo tuhuma mpya 615 za mwaka 2014/15 zilichunguzwa ambapo tuhuma 607 uchunguzi ulikamilika. Kati ya tuhuma ambazo uchunguzi umekamilika, majalada 207 yaliombewa kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo majalada 133 yaliopata kibali kwa kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Kati ya majalada 133 yaliopata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani, majalada 14 yalihusu uchunguzi maalum wa vocha za pembejeo na majalada sita (6) yalihusu uchunguzi wa maliasili ya nchi;
- (ii) Majalada 187 ambayo yametokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yalichunguzwa ambapo majalada 38 yalikamilika na kuombewa kibali kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Kati ya hayo majalada 13 yaliopata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani;
- (iii) Kesi mpya 192 zilifunguliwa mahakamani zikiwemo kesi 11 zilizotokana na uchunguzi maalum wa Vocha za Pembejeo za Kilimo, kesi nne (4) zinazohusu maliasili ya nchi na kesi 11 zilizotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
- (iv) Majalada 50 yaliyohusu tuhuma za rushwa kubwa (Grand Corruption) yalifikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Kati ya hayo majalada 27 yamepata kibali na watuhumiwa wamefikishwa Mahakamani;
- (v) Kesi 856 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 192. Kati ya kesi hizo, kesi 664 zinaendelea mahakamani na kesi 196 zilitolewa uamuvi. Kesi 73 watuhumiwa walipatikana na hatia na kuadhibiwa, kesi 24 ziliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali na kesi 123 watuhumiwa wake waliachiliwa huru;

- (vi) Kutokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika jitihada za kupambana na rushwa, wahusika waliopatikana na hatia walirejesha Shilingi 623,941,408. (Takwimu na mwenendo wa uchunguzi wa tuhuma za rushwa zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na.1**);
- (vii) Utafiti katika maeneo sita (6) wenyе lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti umefanyika katika maeneo ya vipimo, miundombinu ya barabara, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, misamaha ya kodi, maji na sekta zinazolalamikiwa zaidi kwa vitendo vya rushwa;
- (viii) Udhibiti wa haraka wa malalamiko ya wananchi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maaazimio yatokanayo na mapendekezo ya udhibiti huo ulifanyika katika maeneo ya Elimu, Kilimo, Ardhi, Afya, Misitu, Mahakama, Uhamiaji, Vizazi na Vifo, Polisi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) na Sekta Binafsi;
- (ix) Warsha 101 za wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na ufuatiliaji wa haraka kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa zimefanyika katika maeneo ya Ardhi, Afya, Kilimo, Mifugo, Ushirika, Gesi, Barabara, Polisi na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);
- (x) Kwa kutumia taarifa za ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa 'Public Expenditure Tracking System' (PETS), Miradi ya Maendeleo 1,069 yenye thamani ya Shilingi bilioni 156.8 ilikaguliwa. Miradi 169 yenye thamani ya Shilingi bilioni 23.4 ilibainika kuwa na kasoro zilizoashiria kuwepo kwa rushwa au ubadhirifu ambapo miradi 87 kati ya iliyobainika kuwa na kasoro wahusika walishauriwa namna ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza wakati miradi 82 uchunguzi wa kina umeanzishwa ili wahusika wachukuliwe hatua;
- (xi) Elimu kuhusu rushwa na athari zake ilitolewa kuptitia njia mbalimbali za uelimishaji umma zikiwemo semina 2,125, mikutano ya hadhara 938, habari na nakala 159, maonesho 111, vipindi vya radio 130, vipindi vya runinga 11, machapisho makala 129,972, taarifa kwa vyombo vya habari 70 na shughuli mbalimbali za kijamii. Aidha, elimu kuhusu athari za rushwa ilitolewa kwa makundi maalum ya wakulima na wafugaji ambapo semina 22 na mikutano ya hadhara 12 ilifanyika;
- (xii) Mwongozo wa kuzuia na kuchunguza vitendo vya rushwa katika ununuzi wa umma umeandalowi;
- (xiii) Viashiria vya kupima kiwango cha rushwa na mafanikio ya mapambano dhidi ya rushwa nchini vimeandalowi na kukamilika;
- (xiv) Elimu ya athari za rushwa katika uchaguzi ilitolewa nchini kote wakati wa Uchaguzi wa Viongozi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Desemba 14, 2014 ili kuwashamasisha wananchi kutumia kura zao kupata viongozi waadilifu. Njia zilizotumika katika uelimishaji ni pamoja na semina 85, mikutano ya hadhara 299, vipindi vitano (5) vya radio na kurusha matangazo matano (5) ya runinga;
- (xv) Watumishi wapya 394 walioajiriwa walipatiwa mafunzo ya awali ya uchunguzi. Aidha, watumishi wengine 40 walipatiwa mafunzo nje ya nchi na watumishi 119 walipatiwa mafunzo ndani ya nchi;
- (xvi) Ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Mkinga umekamilika. Aidha, ujenzi wa ofisi katika Mkoa wa Mbeya unaendelea;

- (xvii) Ushirikishwaji wa kundi la vijana kwenye mapambano dhidi ya rushwa uliendelea kuzingatiwa ambapo vijana walio shulenii, vyuoni na wasio kwenye mfumo rasmi wa elimu walipatiwa elimu ya masuala mbalimbali ya rushwa na kuwasisitiza kuijunga na klabu za wapinga rushwa kwa lengo la kuwajenga kimaadili. Klabu 517 mpya za wapinga rushwa zilifunguliwa na 1,542 kuimarishwa; na
- (xviii) Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Ushauri ya Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika amepatikana. Michoro na makadirio ya gharama za ujenzi imeandaliwa.

**(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za (MKURABITA)**

**Wanyonge Tanzania**

17. **Mheshimiwa Spika**, jukumu kubwa la Mpango huu ni kuandaa na kusimamia Mfumo wa Kitaifa wa Umiliki wa Rasilimali na Uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Mfumo huu unalenga kufanya urasimishaji wa rasilimali na biashara kuwa wa haraka, rahisi na wa gharama nafuu. Aidha, utekelezaji wa mfumo huu unakusudiwa kuwawezesha Watanzania kushiriki kwa ukamilifu katika Uchumi wa soko unaotambulika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makazi, Nishati na Maji ya Zanzibar urasimishaji wa ardhi umeendelea kutekelezwa ambapo viwanja 1,230 vya Nungwi na Chokochi vimepimwa na kutangazwa kwa wananchi kwa ajili ya uhakiki wa umiliki kabla ya usajili;
- (ii) Uratibu wa kutayarisha na kutoa Hati za Haki Miliki za Kimila umeendelea kufanyika kwa wamiliki wa mashamba katika Halmashauri za Wilaya 20 ambazo upimaji umekamilika. Jumla ya hati 9,754 zimetayarishwa katika Halmashauri za Wilaya nane (8) za Mwanga, Muleba, Mbinga, Mkuranga, Rufiji, Manyoni, Kilombero na Mbarali;
- (iii) Mashamba ya wakulima wa chai yameendelea kurasimishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ambapo mashamba 506 yamepimwa na Hati za Haki Miliki za Kimila kutayarishwa;
- (iv) Urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa umefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ambapo Hati za Haki Miliki za Kimila 566 zimetayarishwa katika Vijiji 11. Aidha, urasimishaji wa mashamba ya wakulima wa miwa katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero na Kilosa unaendelea ambapo Hati za Haki Miliki za Kimila zilizoandaliwa ni 1,105; na
- (v) Urasimishaji wa biashara umefanyika katika Manispaa ya Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ambapo mafunzo yametolewa kwa wafanyabiashara 250 na kati ya hao, wafanyabiashara 140 walisajiri majina ya biashara BRELA na wafanyabiashara 100 walifungua akaunti za benki. Aidha, wafanyabiashara 120 wamejiunga na Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPF).

**(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

18. **Mheshimiwa Spika**, TASAF ipo katika utekelezaji wa Awamu ya Tatu inayohusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini uliozinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Agosti 2012. Utekelezaji wa Mpango huu unafanyika katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar.

19. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelawa katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015 ni kama ifuatavyo:

- (i) Utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini umefikia Halmashauri 159 Tanzania Bara na Unguja na Pemba. Jumla ya kaya maskini 945,263 zenyé watu milioni 4.8 kutoka katika jumla ya Vijiji 7,808, Mitaa 1,952 na Shehia 40 zimetambuliwa na Kaya 932,301 zimeandikishwa. Lengo ni kuandikisha Kaya zaidi ya milioni moja ifikapo Juni, 2015;
- (ii) Jumla ya Shilingi bilioni 42.6 zimelipwa kama ruzuku ya kunusuru kaya maskini zipatazo 266,601 katika vipindi vya mizunguko 8 ya malipo katika Mamlaka za Maeneo ya Utekelezaji 40 zikiwemo Halmashauri 38 Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba (**Kiambatisho Na. 2**);
- (iii) Viongozi wa Serikali 24,743 na Wataalam 5,437 kutoka katika maeneo ya utekelezaji wa Mpango walijengewa uelewa. Aidha, Wawezeshaji wa kitaifa wa Mpango 5,600 walijengewa uwezo ili kuweza kuwaelimisha wananchi kuhusu Mpango na uwekaji vigezo vya umaskini. Pia Kamati za Usimamizi za Jamii 2,833 na Timu za Jamii zipatazo 35,508 zilizohusika na ukusanyaji takwimu pia zilifundishwa kuhusu Mpango;
- (iv) Mifumo ya utekelezaji na uendeshaji wa shughuli za TASAF Awamu ya Tatumeendelea kukamilishwa na kutumika. Wadau mbalimbali wamepata mafunzo ya jinsi ya kutumia mifumo hiyo. Hadi kufikia Machi, 2015 waingiza takwimu wapatao 310 wamefanya kazi ya kuingiza takwimu kwenye Masjala ya Kitaifa ya Kaya Maskini;
- (v) Vipindi vya radio 14 na vya runinga 14 viliandaliwa na kutangazwa kwa nia ya kukuza uelewa wa wananchi kuhusu TASAF Awamu ya Tatumeendelea kanuni na taratibu za utekelezaji wa Mpango na majukumu ya wadau mbalimbali wa Mpango. Aidha, machapisho mbalimbali yaliandaliwa na kusambazwa kwa wadau na wananchi katika maeneo yote 161 ya utekelezaji;
- (vi) Ukaguzi wa fedha za utekelezaji na uhakiki wa kaya maskini zilizotambuliwa ulifanyika katika maeneo ya utekelezaji 40 ili kujiridhisha na matumizi ya fedha. Matokeo ya ukaguzi yamebaini matumizi sahihi ya fedha zilizotumika katika utekelezaji na kaya chache ambazo zilibainika hazikustahili kuingia katika Mpango ziliondoleta kabla ya malipo kufanyika;
- (vii) Ufuutiliaji wa karibu katika utekelezaji wa Mpango wa TASAF Awamu ya Tatumeendelea katika maeneo yote 161 ya utekelezaji kwa kupitia maafisa wa ufuutiliaji. Aidha maeneo yaliyokuwa na matatizo ya utekelezaji yaliweza kurekebishwa;
- (viii) Miradi ya ujenzi ya kutoa ajira za muda 544 yenyé thamani ya Shilingi bilioni 10.6 iliibuliwa na kutekelezwa katika mamlaka ya maeneo ya utekelezaji manane (8) ambayo ni Halmashauri za Chamwino, Kibaha, Bagamoyo, Lindi, Manispaa za Mtwara na Lindi na Unguja na Pemba. Aidha, miradi hiyo iliwafikia walengwa 58,336 walioko kwenye Vijiji/Mitaa/Shehia 355. Aina ya miradi iliyoibuliwa ni pamoja na ukarabati wa barabara za vijiji, viwanja vya michezo, malambo, upandaji miti, vitalu vya michezo, usafi wa mazingira, kuotesha mikoko, kutengeneza makingamaji, visima vya kuchimba kwa mikono, kusafisha mifereji ya maji taka, kuzoa takataka, kukarabati miundo mbinu ya umwagiliaji maji nk. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015, jumla ya Shilingi bilioni 2.5 zililipwa kwa walengwa 50,926; na

(ix) Taarifa zimekusanya katika Vijiji na Shehia zote zenye walengwa walioandikishwa ili kujua maeneo yenyepungufu wa huduma za jamii (elimu, afya na maji) zitakazowafanya walengwa kushindwa kutimiza masharti ya Mpango.

**(e) Taasisi ya Uongozi**

20. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya UONGOZI ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 274 la mwaka 2010 kwa lengo la kuwa Kituo cha Utaalam wa Hali ya Juu (Centre of Excellence) cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza (Emerging Leaders) wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015, kazi zifuatazo zimetekelizwa:

- (i) Kozi 11 kwenye maeneo ya Ufanisi katika Sekta ya Umma na Maeneo mengine zimeandaliwa. Kozi hizo ni Uhusiano wa Kisiasa na Kiutawala, Uboreshaji na utoaji wa Huduma za Umma, Menejimenti wakati wa dharura, Mambo mtambuka yanayoathiri Huduma za Umma, Matumizi ya TEHAMA kutoa huduma za kielektroniki, Msingi wa Mawasiliano, Ufanisi katika Uandishi, Usanifu wa Kuzungumza Mbele ya Hadhara, Mawasiliano Wakati wa Dharura, Matumizi Mazuri ya Muda na Ufundishaji na Ushauri;
- (ii) Kozi 10 za muda mfupi ziliendeshwa kwa viongozi 281 ili kuwajengea uwezo na weledi katika utendaji wao. Kozi hizo ziliikuwa katika maeneo ya Uhusiano wa Kisiasa na Kiutawala, Ushirikiano Serikalini, Matumizi ya TEHAMA katika kutoa Huduma za Kielektroniki, Usimamizi wa Mchakato wa Sera Tanzania, Misingi ya Ufanisi katika Sekta ya Umma, Mawasiliano Fanisi, Ufundishaji na Ushauri, Matumizi Mazuri ya Muda, Semina Elekezi kwa Wakuu wa Wilaya wapya na Usimamizi wa Mashirika ya Umma;
- (iii) Vipindi saba (7) vya mahojiano viliandaliwa na kutangazwa kwenye runinga kwa nia ya kuimarisha na kujenga uwezo wa viongozi wa sasa na wanaochipukia. Baadhi ya viongozi waliohojiwa ni Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Museveni, Waheshimiwa Marais wastaafu Benjamin Mkapa wa Tanzania, Olusegun Obasanjo wa Nigeria, Thabo Mbeki wa Afrika ya Kusini na Festus Mogae wa Bostwana. Aidha, baadhi ya wataalamu waliohojiwa ni Dkt. Frannie Leauter – Mwenyekiti wa Mfuko wa MKOBA, Dkt. Wendy Luhabe – Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Mfuko wa Wanawake, Afrika Kusini na Carlos Lopez - Katibu Mkuu wa "United Nations Economic Commission for Africa" (UNECA);
- (iv) Mikutano miwili (2) ya majadiliano ilifanyika, mmoja kuhusu Changamoto za Mageuzi Afrika na wa pili ulihusu Ukuaji wa Miji Afrika Mashariki na Jinsi tunavyotaka iwe kufikia mwaka 2050;
- (v) Upembusi yakinifu kuhusu Kituo cha Kutathmini Viongozi na Maendeleo ya Kazi kwa Viongozi ulifanyika na matokeo kutolewa kwenye Mkutano wa Faragha wa Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa huko Dodoma;
- (vi) Mkutano wa Kimataifa ulifanyika kama sehemu ya maadhisho ya Wiki ya UONGOZI mwezi Julai, 2014. Mada ililenga kutambua changamoto za mageuzi Afrika. Mkutano ulishirikisha viongozi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Aidha, mashindano ya uandishi wa Insha yalifanyika kwa vijana wa umri wa miaka kati ya 18 na 25 katika Afrika Mashariki kuhusu Jambo ambalo wangebadilisha kama wangepata nafasi ya kuwa viongozi katika Bara la Afrika;

- (viii) Mkutano wa kutafakari utendaji kazi ulifanyika mwezi Septemba, 2014 kwa Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na viongozi wakuu wa baadhi ya Mashirika ya Umma. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadiliana na kuainisha changamoto mbalimbali za Uongozi katika Sekta ya Umma;
- (ix) Semina kuhusu Uchukuaji wa hatua za Kupunguza Ukataji Miti ovyo ikiwa na mpango wa kutekeleza Jukwaa la Uchumi wa Kijani na lengo la kuongeza uelewa kwa watunga sera, watoa maamuzi na watu wenye ushawishi katika jamii kuhusu masuala yanayohusu uchumi wa kijani ilifanyika; na
- (x) Taasisi imeendelea kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya UONGOZI katika Kijiji cha Kondo, Bagamoyo.

**(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)**

22. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea ni pamoja na kutoa huduma za mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na kutoa huduma za ushauri na mafunzo ya kibiashara ili kuongeza ufanisi katika biashara.

23. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya kazi zilizotekelawa katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015 ni kama ifuatavyo:

- (i) Vijana wajasiriamali 50 ambao ni wahitimu wa Chuo cha Ufundı Stadi (VETA) Dar es Salaam waliojiunga katika vikundi 10 walipewa mikopo;
- (ii) Mafunzo ya awali kwa vijana 324 wahitimu wa VETA Dar es Salaam kuhusu uchanganuaji wa miradi ya biashara, kutafuta masoko ya bidhaa, ufungaji wa bidhaa, namna ya kutangaza bidhaa, utunzaji wa kumbukumbu za biashara, kijana kujitambua na taratibu za mikopo inayotolewa na Mfuko yalifanyika; na
- (iii) Utafiti juu ya mahitaji ya kibiashara ya vijana wahitimu wa Vyuo vya Ufundı Stadi umefanyika. Utafiti huo umebaini kuwa vijana wanapendelea kufanya shughuli za kiufundi zinazotegemeana katika eneo moja na wengi wanahitaji mikopo ya zana za ufundı. Matokeo haya yatasaidia kupanga namna bora ya kuwafikia walengwa wa Mfuko.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZAKE**

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungi 32) iliidhinishiwa **Shilingi 36,406,348,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 29,127,598,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,278,750,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 **Shilingi 25,817,546,085** zilipokelewa na kutumika kwa matumizi ya kawaida. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 2,192,532,500** zilipokelewa na kutumika.

25. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na weledi. Aidha, Watumishi wa

Umma wanawajibika kuwa wasikivu kwa wananchi pale wanapotoa huduma mbalimbali kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

26. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi Machi, 2015 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza kazi zifuatazo:

**(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

- (i) Vibali vya ajira mpya kwa nafasi 58,483 kati ya nafasi 68,138 zilizoidhinishwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2014/15 vilitolewa. Mgawanyo wa nafasi mpya zilizotolewa kisekta ni kama ifuatavyo: Walimu 31,056; Wataalam wa Afya 8,345 na watumishi wengineo 19,082. Kulingana na makisio ya Ikama na bajeti iliyoidhinishwa, vibali viliviyotolewa kwa nafasi mpya vilikuwa kwa kada zote;
- (ii) Watumishi wa Umma 15,992 wa Kada mbalimbali walipandishwa vyeo kati ya nafasi za vyeo 49,003 zilizoidhinishwa;
- (iii) Kima cha chini cha mshahara kilipandishwa kutoka Shilingi 240,000 hadi Shilingi 265,000 kwa mwezi;
- (iv) Madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma yalifanyiwa kazi. Hadi kufikia Machi, 2015 madai ya watumishi 68,945 ya Shilingi bilioni 76.95 yalipokelewa. Watumishi 44,477 wamelipwa malimbikizo ya Mishahara ya Shilingi bilioni 46.57. Aidha, madai ya watumishi 18,070 waliosalia ya Shilingi bilioni 25.17 yapo kwenye hatua ya uhakiki na kusubiri malipo kufanyika;
- (v) Uwezo wa watumiaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umejengwa na kuimashwa kwa kutoa miongozo, ushauri na mafunzo sehemu za kazi kwa Wizara 26; Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Umma na Wakala za Serikali 126; Sekretarieti za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 143;
- (vi) Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Tuli kilichopo Dodoma ulikamilishwa na Kituo kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 18 Machi, 2015. Kituo hiki kimeongeza uwezo wa Serikali wa kutunza kumbukumbu na nyaraka kutoka makasha 200,000 hadi makasha 700,000;
- (vii) Mfumo wa utunzaji kumbukumbu umewekwa katika Ofisi 30 za Wakuu wa Wilaya zilizopo katika Mikoa ya Simiyu, Katavi, Njombe na Geita na hivyo kufanya Ofisi 103 za Wakuu wa Wilaya kati ya 135 kuwa na mfumo huo;
- (viii) Ufuatiliaji na tathmini ya utunzaji wa kumbukumbu ulifanyika katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya 27 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Katavi na Mara. Tathmini imeonesha kuwa wastani wa muda wa kutafuta jalada katika ofisi hizo umepungua kutoka dakika 10 ilivyokuwa mwaka 2013/14 hadi dakika tano (5) mwaka 2014/15;
- (ix) Uhamasishaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma ulifanyika kwa kutumia mbinu za Kimasoko (Social Marketing Approach) kwa watumishi 701 wa Sekta ya Afya katika Hospitali tatu (3) za Mkoa wa Tanga. Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga – Bombo, Hospitali ya Wilaya ya Muheza na Hospitali ya Wilaya ya Lushoto;

- (x) Utafiti kuhusu Hali ya Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma ulifanyika kwa kutumia Mshauri Mwelekezi. Matokeo yalionesha kuwa kiwango cha uzingatiaji wa maadili mionganoni mwa watumishi wa umma kimeongezeka kutoka asilimia 56.9 mwaka 2006 hadi asilimia 66.1 kwa mwaka 2014;
- (xi) Mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma yalitolewa kwa watumishi wa umma 1,097 kutoka Taasisi za Umma 10. Taasisi hizo ni Ofisi ya Makamu wa Rais; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Kazi na Ajira; Wizara ya Uchukuzi; na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Taasisi nyingine ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mamlaka ya Chakula na Dawa; Bodi ya Wataalam wa Ununuza na Ugavi; Shirika la Utangazaji Tanzania na Chuo cha Taifa cha Utalii;
- (xii) Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili ulifanyika katika Taasisi za Umma 15 kwa lengo la kupunguza ukiukwaji wa maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma na kuongeza viwango vya uzingatiaji wa Maadili;
- (xiii) Nakala za machapisho 5,205 ya miongozo mbalimbali kuhusu Maadili ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma zimesambazwa katika Tasasi za Umma 65 zikiwemo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Machapisho hayo ni "Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma"; "Waraka wa Mavazi Na.3 Mwaka 2007"; "Mwongozo wa Namna ya Kushughulikia Malalamiko ya Wananchi"; "Kufanya Kilicho Sahihi" na "Kijitabu cha Hoja zetu kuhusu Maadili";
- (xiv) Taasisi sita (6) za Serikali zimewezeshwa kuainisha mahitaji na kubuni mifumo ya Serikali Mtando ya kurahisisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi;
- (xv) Mwongozo wa kusimamia matumizi ya Mawasiliano kwa Njia ya Video na Mwongozo wa Kusimamia na Kuendesha Tovuti za Serikali imeandaliwa na kusambazwa katika Taasisi za Serikali kwa utekelezaji;
- (xvi) Rasimu ya Sera ya Serikali Mtando na Mkakati wa Utekelezaji wake imeandaliwa;
- (xvii) Tathmini ya mahitaji ya Idara za Elimu, Afya, Kilimo na Mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara imekamilika;
- (xviii) Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umeboreshwa kulingana na mahitaji ya watumiaji wa mfumo hasa katika maeneo ya Maandalizi ya Bajeti na Ikama na uandaaji wa ripoti mbalimbali za usimamiaji wa rasilimaliwatu na mishahara;
- (xix) Watumishi wa Umma 802 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja mbalimbali nje ya nchi kwa lengo la kuboresha utendaji wao wa kazi kama ifuatavyo: Jamhuri ya Korea 107, Australia 58, India 227, China 123, Uhlanzi 142 na Japan 145;
- (xx) Viongozi na Watumishi wa Umma 16 wamewezeshwa kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kikanda yenye lengo la kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu

changamoto zinazoukabili utumishi wa umma na kuweka mikakati ya jinsi ya kuzitatua;

- (xxi) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtando Tanzania (TaGLA) imewezeshwa kwa kulipiwa masafa ya Intaneti (Bandwidth) kwa ajili ya kuwezesha maunganisho ya mtando;
- (xxii) Wakala ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania na Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtando zimejengewa uwezo na kuimarishta ili ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo;
- (xxiii) Vikao vya kazi nane (8) kwa njia ya video (Video Conference) vimefanyika katika Sekretarieti za Mikoa yote. Walengwa wakuu wa Vikao hivyo ni Maafisa na Watendaji katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vikao hivyo vimetumika kutoa maelekezo ya utekelezaji wa masuala mbalimbali. Aidha, vimetoa fursa kwa washiriki kubadilishana uzoefu katika utendaji kazi na namna ya kutatua changamoto zinazojiteza. Mada mbalimbali kuhusu usimamizi wa utumishi wa umma zilizowasilishwa;
- (xxiv) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara na Idara Zinazojitegemea nane (8) ilihuisha ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; OWM-TAMISEMI; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji; Tume ya Maendeleo ya Ushirika; na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa;
- (xxv) Tathmini ya utendaji kazi wa Wakala zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilifanyika. Wakala hizo ni Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), Wakala ya Serikali Mtando (eGA) na Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtando (TaGLA). Matokeo ya tathmini yameonesha kuna mafanikio mbalimbali yamepatikana pamoja na uwepo wa changamoto zinazoathiri utendaji kazi wa Wakala hizo na zimeshaanza kufaniwa kazi;
- (xxvi) Mwongozo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini utakaotumika katika Taasisi za Umma umeandaliwa;
- (xxvii) Mwongozo wa utekelezaji wa Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi katika Taasisi za Umma umeandaliwa;
- (xxviii) Matumizi ya Mifumo na Viwango vya Utendaji Kazi yaliimarishta kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali kutumia Mifumo ya Utendaji Kazi kama ifuatavyo:
  - Mipango Mkakati ya Taasisi tano (5) ilihuisha. Taasisi hizo ni Wizara ya Maji; Wizara ya Kazi na Ajira; Hospitali ya Mirembe; Bodi ya Mfuko wa Barabara; na Bodi ya Usajili wa Wabunifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi;
  - Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi uliwekwa katika Taasisi sita (6) ambazo ni Wizara ya Fedha, Idara ya Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi; Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam; Mamlaka ya

- Usalama wa Anga Tanzania; Shirika la Viwango Tanzania; Wakala ya Mafunzo ya Uvubi; Chuo cha Usimamizi wa Fedha;
- Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ziliwezesewa kuhuiswa Mikataba yao ya Huduma kwa Mteja. Aidha, Sekretarieti za Mikoa 12 zilielimishwa juu ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja;
  - Tathmini ya ndani (self assessment) ya Taasisi ilifanywa kwa Wakala tano (5) ambazo ni Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao, Wakala ya Serikali Mtandao, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo, Wakala ya Mafunzo ya Uvubi na Wakala ya Maabara ya Vetenari Tanzania;
  - Mpango wa Utekelezaji (Operational Plan) wa OWM-TAMISEMI Kitengo cha Miundombinu uliandaliwa; na
- (xxix) Huduma kwa Viongozi Wastaafu wa Kitaifa tisa (9) na wajane wa viongozi wanne (4) zimetolewa kwa mujibu wa Sheria.

**(b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

27. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo mbalimbali ya Utumishi wa Umma. Pia, ni jukumu la Chuo kutoa machapisho mbalimbali ya kitalaamu katika Utumishi wa Umma.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015 kazi zifuatazo zilitekeleza:

- (i) Mafunzo ya kujandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma yalitolewa kwa Watumishi 692 ikilinganishwa na lengo la watumishi 900;
- (ii) Mitihani ya Utumishi wa Umma iliandaliwa na kutolewa kwa Watumishi 494 ikilinganishwa na lengo la watumishi 692;
- (iii) Mafunzo ya awali yalitolewa kwa watumishi wa umma 290;
- (iv) Mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) yalitolewa kwa watumishi wa umma 110;
- (v) Mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa Serikali za Mitaa, mafunzo ya Menejimenti, Usimamizi wa ofisi na Utunzaji wa fedha za umma yalitolewa kwa Watumishi wa Umma 980 ikilinganishwa na lengo la watumishi 1,580;
- (vi) Washiriki 15,832 kati ya 21,380 walidahiliwa katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya Rasilimaliwateru, usimamizi wa ununuzi na ugavi katika utumishi wa umma, uongozi na utawala bora yalitolewa;
- (vii) Ushauri wa Kitaalamu ultolewa kwa Taasisi 21 katika fani za mifumo ya kimenejimenti na usimamizi katika Utumishi wa Umma;
- (viii) Utafiti wa Kitaalamu kwa maeneo tofauti saba (7) ya lengo la maeneo ya utafiti tisa (9) ulifanyika. Utafiti huo ulihusu maeneo ya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo

wa Wazi wa Mapitio, Tathmini ya Utendaji Kazi na Utoaji Huduma kwa Mteja, Utunzaji kumbukumbu na Uhazili;

- (ix) Machapisho tisa (9) ya lengo la machapisho 17 ya kitaalamu katika utumishi wa umma katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala yalitolewa;
- (x) Watumishi 84 walijengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao, Shahada ya Uzamivu (10); Shahada ya Uzamili (5); Shahada ya Kwanza (10); Stashahada (6); na watumishi 53 walihuduria mafunzo ya muda mfupi na warsha mbalimbali;
- (xi) Tawi la Chuo cha Utumishi wa Umma la Mbeya lilifunguliwa na kufanya Chuo kuwa na matawi sita (6); na
- (xii) Ujenzi wa jengo lenye ghorofa tatu (3) kwa ajili ya madarasa na ofisi katika Kampasi ya Tabora, kwa awamu ya kwanza umeanzishwa.

**(c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtando Tanzania (TaGLA)**

29. **Mheshimiwa Spika**, Wakala ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa lengo la kuwawezesha kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

30. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2014/15 Wakala ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa washiriki 585. Kati ya hao, 450 walitoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na 135 walikuwa Washiriki binafsi na mashirika yasiyo ya Kiserikali;
- (ii) Kutoa huduma ya Maunganisho (Bridging Services) na msaada wa kiufundi kwa wadau 18 nchini kwa kuwawezesha kufanya mikutano na mafunzo kwa njia ya mtando;
- (iii) Watumishi watatu (3) wa Wakala walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia; na
- (iv) Wakala imeongeza uwezo wa kuunganisha vituo 20 kufanya mikutano au mafunzo kwa wakati mmoja baada ya kuunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa.

**(d) Wakala ya Serikali Mtando (eGA)**

31. **Mheshimiwa Spika**, Wakala ina jukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtando katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kutekeleza majukumu yake, Wakala ina wajibu wa kuweka na kusimamia mifumo ya mawasiliano iliyo salama Serikalini inayowezesha utoaji huduma bora kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

32. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Wakala imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i) Taasisi za Serikali 67 kati ya 72 zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network). Mtandao huu unaziwezesha Taasisi za Serikali kuwasiliana kwa urahisi na usalama zaidi pamoja na kuipunguzia Serikali na Taasisi zake gharama za mawasiliano ya simu, video na intaneti;
- (ii) Ugawaji wa huduma za masafa ya intaneti (Government bandwidth) kwenye Taasisi za Serikali 116 umesimamiwa na kuratibiwa;
- (iii) Uboreshaji wa Mfumo wa Barua Pepe wa Serikali kwa kuunganisha Taasisi za Serikali 35 kwa lengo la kutumia mfumo huu umekamilishwa;
- (iv) Tovuti Kuu ya Serikali (**Government Portal-[www.tanzania.go.tz](http://www.tanzania.go.tz)**) imeboreshwa kwa kuweka nyaraka na taarifa muhimu ikiwa ni pamoja na Sheria 1,427; fomu mbalimbali 640; Kanuni na Taratibu 153; matoleo 136 ya Gazeti la Serikali; Sera 94; Hotuba za Viongozi wa Kitaifa 356; Miundo ya Utumishi 25; Hotuba za Bajeti 104 na Mikataba ya Kimataifa 63;
- (v) Tovuti za Taasisi 30 za Serikali zimetengenezwa (developed), zimewekwa (installed) na kuhifadhiwa (hosted);
- (vi) Tovuti ya Takwimu Huru imeanzhishwa na inapatikana kupitia anuani hii (**Open Data Portal-[www.opendata.go.tz](http://www.opendata.go.tz)**);
- (vii) Mfumo wa Kuomba Ajira kwa Njia ya Kielektroniki (e-Recruitment Portal) umekamilishwa na kuunganishwa na Mfumo wa Simu za Mikononi (Government Mobile Platform);
- (viii) Mafunzo kuhusu Serikali Mtandao yalitolewa kwa watumishi wa Wakala na Taasisi nyingine za Serikali katika maeneo ya usimamizi wa Mtandao wa Mawasiliano (Government Network Professional Skills); utumiaji wa Mfumo wa Barua Pepe wa Serikali (Government Mailing System (GMS) kwa watumishi 125 kutoka Taasisi 79 za Serikali; utengenezaji wa mifumo tumikishi ya simu za mikononi (mobile applications development); usimamizi na uvezeshaji wa mifumo na miundo ya TEHAMA katika sekta maalum za umma kwa watumishi 15; na usalama wa taarifa za Serikali kwenye mitandao na miundombinu ya TEHAMA (Government Network Security Skills) kwa watumishi wa TEHAMA kutoka katika Taasisi 75 za Serikali; na
- (ix) Ushauri wa kitaalam na kiufundi umetolewa kwa Taasisi za Serikali 32 kwenye maeneo ya utengenezaji na uboreshaji wa mtandao wa ndani wa Taasisi (Local Area Network); utengenezaji wa Mipango ya kujikinga na majanga (Disaster Recovery Plans); utengenezaji wa mikakati ya utekelezaji wa TEHAMA (ICT Strategic Plans), kupitia maandiko ya miradi mbalimbali ya TEHAMA ya Taasisi za Serikali (ICT Project Write up Review) pamoja na uvezeshaji na upatikanaji wa Tovuti katika Mtandao wa Intaneti (Search Engine Optimization).

#### OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

33. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33) ilitengewa **Shilingi 8,795,396,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 6,339,538,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,455,858,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2015, **Shilingi 3,291,350,377.52** za Matumizi ya Kawaida

ziliwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, jumla ya **Shilingi 489,657,979** zilipokelewa na kutumika.

34. **Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura ya 398, ili kuhakikisha kwamba mienendo na tabia za Viongozi wa Umma waliotajwa katika Kifungu cha 4(1) cha Sheria hiyo kinazingatia misingi ya maadili kwa lengo la kukuza imani ya wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma.

35. **Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelwa katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Machi, 2015 ni kama ifuatavyo:

- (i) Viongozi wa Umma 13,167 wa kada mbalimbali walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2014. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2014 jumla ya Viongozi wa Umma 9,596 walirejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni;
- (ii) Matamko 300 kati ya Matamko 9,596 ya Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma yaliyopokelewa, yameandaliwa kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki;
- (iii) Malalamiko 77 yalipokelewa na kuchambuliwa, kati ya malalamiko hayo, malalamiko 41 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo malalamiko 29 yalisikilizwa uchunguzi wa awali na 12 taratibu za uchunguzi zinaendelea. Malalamiko 36 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yalielekezwa kwenye Mamlaka zinazohusika;
- (iv) Vikao viwili (2) vya Baraza la Maadili vilifanyika Jijini Dar es Salaam ambapo mashauri 27 yaliwasilishwa mbele ya Baraza la Maadili. Kati ya mashauri hayo, mashauri 18 yalisikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri tisa (9) yaliahirishwa kutohana na sababu mbalimbali;
- (v) Viongozi wa Umma 3,980 walipatiwa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuitia Vikao vya Kamati ya Ushauri vya Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Arusha, Tabora, Kigoma, Njombe, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mwanza, Katavi, Kilimanjaro, Lindi na Manyara. Aidha, elimu hiyo imetolewa kwa Watumishi wa Umma 1,000;
- (vi) Ukusanyaji maoni ya Wadau mbalimbali kwa nia ya kuifanya marekebisho Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma umekamilika. Muswada wa Sheria umeandaliwa na kuwasilishwa Bungeni tayari kwa kusomwa mara ya kwanza;
- (vii) Rasimu ya Mwongozo wa Maadili ya Viongozi wa Umma imeandaliwa na kujadiliwa na kikao cha Wadau. Mwongozo huo unatarajiwa kuanza kutumika mwezi Julai, 2015;
- (viii) Rasimu ya mfumo utakaotumika kupokea na kushughulikia malalamiko mbalimbali ya Wananchi na Viongozi imeandaliwa;
- (ix) Hadidu za Rejea kwa ajili ya kufanya Utafiti kuhusu hali ya maadili na ufahamu wa Viongozi na Wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma

- zimeandaliwa. Aidha, taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri wa kufanya Utafiti huo zinaendelea;
- (x) Mwongozo utakaotumika katika kufanya uchunguzi wa ukiukwaji wa Maadili ya Viongozi wa Umma umeandaliwa;
- (xi) Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano umeandaliwa na umeanza kutumika ili kuboresha mawasiliano na Wadau;
- (xii) Mkakati wa TEHAMA umeandaliwa na unatarajiwa kuanza kutumika mwezi Julai, 2015;
- (xiii) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Kanda ya Kusini, Mtwara Awamu ya tatu unaendelea na umefikia asilimia 80 ya ujenzi;
- (xiv) Mchakato wa ujenzi wa Jengo la Maadili Makao Makuu unaendelea ambapo taratibu za kumpata Mzabuni wa ujenzi wa Jengo hilo unaendelea. Aidha, upembuzi yakinifu umefanyika na kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha;
- (xv) Rasimu ya Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma na wa Sekta Binafsi imeandaliwa na kujadiliwa na Wadau. Ahadi za uadilifu zitaanza kutumika Julai, 2015; na
- (xvi) Ujenzi wa Mfumo wa kielektroniki utakaotumika kukusanya na kuchakata taarifa mbalimbali zinazohusu Viongozi wa Umma umeandaliwa na uko katika hatua ya majaribio.

#### **OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

36. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67) iliidhinishiwa **Shilingi 5,683,371,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Mwaka. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 4,930,675,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 752,696,000** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 **Shilingi 2,282,667,502** zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

37. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Sekretarieti ya Ajira ni: Kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa kanzidata za wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira; kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam wenye weledi kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma; kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika Utumishi wa Umma na kufanya usaili; na kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira.

38. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:

- (i) Usaili kwa nafasi wazi za kazi 6,362 katika Utumishi wa Umma uliendeshwa, nafasi mpya zikiwa 4,772 na mbadala 1,590;

- (ii) Wasailiwa 4,953 walipangiwa vituo vya kazi. Kati ya nafasi hizo, Wizara 684; Sekretarieti za Mikoa 577; Mamlaka ya Serikali za Mitaa 1,607; Taasisi, Idara na Wakala za Serikali 2,085. Aidha, ajira mpya zilikuwa 3,467 na mbadala 1,486; Usaili kwa ajili ya kujaza nafasi za Wakurugenzi/Wakuu wa Idara 21 na Wakuu wa Vitengo 15 wa Wakala na Taasisi za Umma 16 ulifanyika;
- (iv) Katika kutekeleza marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 ambayo imekasimu madaraka ya kuendesha mchakato wa ajira kwa baadhi ya kada za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sekretarieti ya Ajira imeweza kusimamia mchakato kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa 34;
- (v) Waajiriwa wapya 1,274 waliokuwepo kwenye Kanzidata (Database) wamepangwa kwa waajiri 146;
- (vi) Orodha ya wahitimu toka Vyuo Vikuu mbalimbali imeboreshwa baada ya Vyuo Vikuu 23 kuwasilisha orodha zao za wahitimu 47,073;
- (vii) Kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtando mfumo mpya wa maombi ya kazi kwa njia ya kielektroniki umeanzishwa na kutumika kwa baadhi ya kada;
- (viii) Vipindi vinne (4) kwenye runinga vinavyohusu ukasimishwaji wa ajira ya kada 22 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa viliandaliwa na kurushwa. Aidha, vipindi vinavyohusu uanzishwaji wa utumaji na upokeaji wa maombi ya kazi kwa njia ya mtando navyo viliandaliwa na kurushwa;
- (ix) Mikutano mitano (5) na Waandishi wa Habari imefanyika kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa mchakato wa ajira Serikalini ili kuendelea kukuza uelewa juu ya mambo mbalimbali yanayohusu ajira Serikalini; na
- (x) Watumishi watano (5) wamepatiwa mafunzo ya shahada ya uzamili na mmoja katika stashahada ya utunzaji wa kumbukumbu.

#### **OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

39. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94) iliidhinishiwa **Shilingi 13,270,160,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 5,711,339,000** zilikuwa za mishahara na **Shilingi 7,558,821,000** za Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2015 **Shilingi 7,290,230,320.75** zilipokelewa na kutumika.

40. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Umma ni Tume rekebu na inao wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwater katika Utumishi wa Umma yanaendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu kwa lengo la kuimarisha utendaji unaozingatia malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ni Mamlaka ya Rufaa kwa watumishi wa Umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za Nidhamu.

41. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Tume ya Utumishi wa Umma ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Rufaa **78** na malalamiko **151** yalichambuliwa kwa ajili ya uamuza;
- (ii) Mfumo wa ukaguzi wa rasilimaliwater ulihuishwa;

- (iii) Watumishi 60 wa Tume walipata mafunzo ya kuongeza ujuzi;
- (iv) Wadau walielimishwa kuhusu utekelezaji sahihi wa Sheria ya Utumishi wa Umma kwa kufanya mikutano mitatu (3) na waandishi wa habari, kutangaza kipindi cha radio na runinga;
- (v) Walimu 10,916 walisajiliwa, 3,374 walithibitishwa kazini, 3,332 walipandishwa vyeo, 339 walibadilishwa kazi na vibali vya kustaafu 1,655 vilitolewa; na
- (vi) Mashauri ya Nidhamu ya Walimu 142 yalitolewa uamuzi ambapo 100 walifukuzwa kazi, 10 walirudishwa kazini na mashauri 32 yalirudishwa kwenye Kamati za Walimu za Wilaya.

#### **OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILABI KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

42. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Bodi ya Mishahara na Masilabi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09) iliidhinishiwa **Shilingi 3,326,931,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,981,000,000** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 345,931,000** kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 **Shilingi 1,596,827,149** zilipokelewa na kutumika.

43. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Masilabi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 162 la tarehe 3 Juni, 2011. Uanzishwaji wa Bodi ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume mbalimbali ziliizoishauri Serikali namna ya kuboresha Mishahara katika Utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma (2010). Bodi hii ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendeleza kwa Rais kuhusu viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa ujumla.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15 kazi zifuatazo zilitekelezwa:

- (i) Maandalizi ya Tathmini ya Kazi katika Utumishi wa Umma ambayo itakuwa msingi wa kuoanisha na kuwianisha mishahara na masilabi yamekamilika. Majadiliano na Mtaalam Mwelekezi kwa ajili ya kazi hiyo yanaendelea;
- (ii) Utafiti wa kubaini sababu zinazowafanya watumishi wasivutiwe na kubaki katika Utumishi wa Umma umefanyika. Matokeo ya Utafiti huu yametumika wakati wa kuandaa Mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kupanga mishahara na masilabi;
- (iii) Utafiti wa tatizo la uhaba wa watumishi wa umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, hususan kwenye maeneo yenye mazingira magumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 116 (zikiwemo Manispaa 3 na Halmashauri za Wilaya 113); Wizara 9; na Taasisi za Umma 10 ulifanyika. Aidha, mapendekezo ya vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kutoa motisha kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu yatawasilishwa Serikalini baada ya uchambuzi wa taarifa ya utafiti huu kukamilika;
- (iv) Taarifa za Mishahara na Masilabi katika Utumishi wa Umma zilikusanywa na kuzihifadhi katika Kanzidata ya Bodi;

- (v) Rasimu ya Mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kupendekeza na kupanga mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma iliandaliwa na iko kwenye hatua ya kujadiliwa na wadau ili kupata maoni yao; na
- (vi) Uwezo wa kiutendaji wa wajumbe wa Bodi na watumishi ulijengwa kuitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuongeza ufanisi.

**OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI**

45. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (Fungu 06) iliidhinishiwa **Shilingi 34,299,579,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 6,137,964,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 28,161,615,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 **Shilingi 17,792,464,097** zimepokelewa na kutumika.

46. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi na udhibiti katika utekelezaji wa miradi na mipango ya maendeleo, Serikali ilianzisha mfumo wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Kitaifa. **Mfumo huu wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)** unalenga kuharakisha kufikiwa kwa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa kufikia mwaka 2025 (*Tanzania Development Vision 2025*). Utekelezaji wa Mfumo BRN umekuwa katika mikondo mikuu miwili, yaani: ujenzi wa mfumo na taasisi za kusimamia na kuhakikisha kuwa matokeo tarajiwa yanapatikana, pamoja na usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa katika Maeneo Makuu sita ya Matokeo Kitaifa yaliyojumuishwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mfumo huu. Maeneo hayo sita yалиhusu sekta za Elimu, Kilimo, Maji, Nishati, Rasilimalifedha na Uchukuzi.

47. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ufanisi ulioanza kujitokeza katika utekelezaji wa sekta sita za kipaumbele, sekta nyingine saba zimeongezwa katika mfumo wa BRN mwaka 2014/15. Ongezeko hili limetokana na Serikali kutambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya biashara kama hatua muhimu katika kujenga uchumi imara vilevile umuhimu wa kuboresha sekta ya afya. Kwa maana hiyo maeneo sita yameongezwa chini ya eneo la uboreshaji wa mazingira ya kibiashara ni, Kuoanisha taratibu na Miundo ya Taasisi, Upatikanaji wa Ardhi na Utoaji wa Hati Miliki, Sheria na Stadi za Kazi, Mifumo na Viwango vya Kodi, Tozo na Ada, Udhibiti wa Rushwa, Utekelezaji wa Mikataba, Sheria na Haki.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi Machi, 2015, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Watumishi 98 wameajiriwa. Kati ya hao, watumishi 51 wapo Makao Makuu ya PDB na watumishi 47 wapo katika Wizara zinazotekeliza vipaumbele vya BRN. Aidha, Ofisi za kudumu za Taasisi zimepatikana;
- (ii) Miradi ya kipaumbele inayotekeliza katika sekta zote imeendelea kusimamiwa chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa. Kazi hii inaambatana na ushiriki wa Taasisi katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazokabili miradi hiyo;
- (iii) Ukaguzi huru wa matokeo ya utekelezaji wa miradi ya Matokeo Makubwa Sasa imeratibiwa na kampuni ya Pricewaterhouse Coopers. Katika taarifa yao, wakaguzi hao wamethibitisha kuwepo kwa mabadiliko katika fikra za watumishi Serikalini na kuzingatia uwekaji wa vipaumbele katika kupanga matumizi ya rasilimali, na kutekeleza majukumu kwa kulenga matokeo na muda uliopangwa;

- (iv) Tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa kwa kipindi cha mwaka 2013/14 ilifanyika na jopo huru Januari 2015. Taarifa hiyo lilionyesha kuridhika kwake na hatua iliyofikiwa katika kutekeleza mfumo huu. Jopo hilo lilioongozwa na Mheshimiwa Festus Mogae, Rais Mstaafu wa Botswana na mshindi wa zawadi ya Uongozi Uliotukuka Barani Afrika ya Mo Ibrahim;
- (v) Upembuzi yakinifu kupitia maabara za BRN wa mahitaji ya mageuzi ya sekta ya afya umefanyika Oktoba, 2014;
- (vi) Ushirikiano na Sekretarieti za Mikoa umeanza kutekelezwa ili kujenga uwezo kwa kuanzisha Vitengo vya Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Miradi katika ngazi za Mikoa. Hatua hii imeongeza msukumo katika ushiriki wa Viongozi wa Mikoa na Wilaya kufutilia utekelezaji wa miradi husika. Kwa kuanzia mafunzo yametolewa kwa Sekretariati za Mikoa ya Mtwara, Mbeya, na Kigoma; na
- (vii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa kwa Mwaka 2013/2014 imetolewa Machi 5, 2015, ili kuwafahamisha wananchi maendeleo ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa kwa kipindi cha mwaka mmoja wa utekelezaji.

### C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/16

49. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2014/15, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2015/16.

50. **Mheshimiwa Spika**, Mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 67, 94, 09, 06 na 04 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16 kama ifuatavyo:

#### OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

##### (a) Ikulu

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuendelea kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kimataifa na kazi nyingine zinazohusu kumshauri Rais;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Awamu ya Tatu wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirkisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (iv) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership);
- (v) Kuendelea kuelimisha watumishi juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na UKIMWI mahali pa kazi na namna ya kujikinga na UKIMWI;

- (vi) Kuratibu na kuandaa Mikutano 50 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambapo Nyaraka 100 zitachambuliwa. Mikutano 25 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) itafanyika, ambapo Nyaraka 70 zitatolewa ushauri. Mikutano 20 vya Baraza la Mawaziri itafanyika ambapo Nyaraka 60 zitatolewa uamuzi;
- (vii) Kuandaa na kufanikisha mukutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri Wizarani, wadau wengine na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- (viii) Kutoa mafunzo muhimu kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Maofisa wengine wa Serikali;
- (ix) Kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri kwa mwaka 2014/15 na Taarifa ya Utekelezaji wa Maamuzi ya Baraza la Mawaziri kwa Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kipindi cha Julai, 2005 hadi Desemba, 2015;
- (x) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi. Vilevile, mikutano miwili (2) ya kueleweshana na Watendaji na Maafisa wa Serikali 100 kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi itafanyika;
- (xi) Kupanga na kuendesha mikutano minane (8) ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika sekta ya umma nchini;
- (xii) Kuendelea kuratibu masuala ya siasa na mahusiano ya jamii;
- (xiii) Kuendelea kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;
- (xiv) Kukarabati nyumba kumi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino;
- (xv) Kukamilisha ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano Ikulu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la Mapokezi upande wa baharini; na
- (xvi) Ukarabati wa Ikulu Ndogo Mbeya na maandalizi ya ujenzi wa Ikulu Ndogo Zanzibar.

**(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

52. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuendelea kuchunguza tuhuma 2,776 zilizopo na mpya zitakazojitokeza;

- (ii) Kukamilisha uchunguzi maalum unaoendelea katika vocha za pembejeo za kilimo, maliasili na tuhuma zilizobainishwa na taarifa ya Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
  - (iii) Kukamilisha uchunguzi wa tuhuma 10 za rushwa kubwa (*Grand corruption*) kama ilivyopangwa katika Mpango Mkakati wa Taasisi;
  - (iv) Kuendelea kuendesha kesi 664 zilizopo mahakamani na zitakazoendelea kufunguliwa kutokana na kukamilika kwa chunguzi mbalimbali;
  - (v) Kufuatilia na kudhibiti vitendo vya rushwa katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi;
  - (vi) Kuendelea kutoa elimu kuhusu athari za rushwa kwa wananchi, watumishi wa Serikali na makampuni binafsi na kuendeleza ushirikiano na Asasi za Kiraia katika mapambano dhidi ya rushwa;
  - (vii) Kuendelea kutoa Elimu kwa wananchi kuhusu athari za rushwa katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2015;
  - (viii) Ufunguzi na uimarishaji wa Klabu za Wapinga Rushwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa;
  - (ix) Kuwajengea uelewa wa masuala ya rushwa Asasi za Kiraia na wanahabari ili washiriki kikamilifu kuwajengea uwezo wananchi wa kudhibiti rushwa;
  - (x) Kuendelea kuimarishe mifumo ya utendaji dhidi ya mianya ya rushwa kwa kufanya utafiti na udhibiti katika sekta za nishati na mazingira;
  - (xi) Kushirikisha wadau kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;
  - (xii) Kuendelea kufuatilia miradi ya maendeleo katika Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha thamani halisi ya fedha;
  - (xiii) Kuimarishe kitengo cha Ufuatiliaji na Urejeshaji wa Mali za Umma (*Asset Tracing and Asset Recovery*); Maabara ya Uchunguzi na Ofisi za Waratibu wa Kanda wa Ufuatiliaji wa Matumizi ya fedha za umma (*PETS*) katika miradi ya maendeleo kwenye Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo kwa watumishi;
  - (xiv) Kufanya mafunzo maalum ya weledi kwa watumishi;
  - (xv) Kuandaa mafunzo maalum kwa waheshimiwa Majaji na Mahakimu kuhusu Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329; na Sheria Na.6 ya 2010 ya Gharama za Uchaguzi na vitendo vya rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu mwaka 2015; na
  - (xvi) Kuanza ujenzi wa jengo la ofisi la Makao Makuu ya Bodi ya ushauri wa masuala ya rushwa ya Umoja wa Afrika baada ya kukamilika kwa mchakato wa umiliki wa kiwanja na kumpata Mkandarasi wa ujenzi.
- (c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

53. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuendelea na uratibu wa marekebisho ya Sheria za Ardhi, Biashara na ya Kitaasisi kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta Tanzania Bara na Zanzibar;
- (ii) Kujenga uwezo kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi Vijiji katika Halmashauri za Wilaya nne (4) ambazo ni Urambo, Iramba, Kilwa na Biharlamulo (Tanzania Bara). Aidha, Urasimishaji wa ardhi Vijiji utafanyika katika Wilaya za Chake chake Pemba na Wilaya ya Magharibi Unguja;
- (iii) Kukamilisha ujenzi wa masjala za Vijiji 16 na kuanza ujenzi mpya wa Masjala 13 katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali Nchini;
- (iv) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati Miliki za Kimila kwa wakulima 900 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 225 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya tisa (9) ambazo ni Mbarali, Mbinga, Sumbawanga, Kasulu, Kigoma, Muleba, Meru, Geita na Moshi;
- (v) Kuendelea na uratibu wa zoezi la kumalizia kutayarisha na kutoa Hati za Haki Miliki za Kimila katika Halmashauri za Wilaya saba (7) ambazo tayari zimerasimishwa. Halmashauri hizo ni Rufiji, Kasulu, Musoma, Misungwi, Sikonge, Kigoma na Chamwino;
- (vi) Kujenga uwezo kwa ajili ya urasimishaji wa ardhi mijini katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Manispaa za Musoma, Moshi, Tabora na Sumbawanga;
- (vii) Kuendelea na uratibu wa utayarishaji na utoaji wa Hati Miliki katika maeneo ya Tunduma - Mbeya, Kimara Baruti - Dar es Salaam na Mwangata - Iringa;
- (viii) Kujenga uwezo kwa ajili ya urasimishaji wa biashara katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Halmashauri za Jiji la Mwanza na Mbeya, Manispaa za Iringa na Mtwara na Halmashauri ya Mji wa Njombe. Aidha, wananchi waliorasimisha ardhi zao katika Halmashauri hizi watajengewa uwezo ili waweze kutumia hati zao kupata mitaji kutoka Taasisi za fedha;
- (ix) Kuanza urasimishaji wa biashara katika Wilaya za Kusini Unguja na Micheweni, Pemba;
- (x) Kuendelea na mchakato wa uanzishwaji wa Chombo cha Kitaifa chenye nguvu ya kisheria kitakachosimamia Urasimishaji wa Rasilimali na Biashara pamoja na ukujji wa sekta rasmi ya uchumi wa nchi; na
- (xi) Kuendelea na mchakato wa uanzishwaji wa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya nchini.

**(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

54. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 TASAF imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo milioni moja katika vipindi vya mizunguko 6 ya malipo katika Halmashauri 159 Tanzania Bara pamoja na Wilaya zote za Unguja na Pemba, Tanzania Zanzibar. Aidha, uhawilishaji wa fedha utafanywa kwa kufuata Kalenda ya Malipo ya kila baada ya miezi miwili;
- (ii) Kutekeleza miradi ya kutoa ajira ya muda kwa walengwa ambapo jumla ya miradi 3,500 ya kutoa ajira za muda inatarajiwa kuibuliwa na wananchi katika Vijiji/Mitaa/Shehia hizo;
- (iii) Kuhamasisha na kuanzisha vikundi 668 vya kuweka akiba na kuwekeza kwenye shughuli za kilimo, ufugaji na biashara ili kuziweshesha kaya za walengwa kuondokana na umaskini;
- (iv) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji taarifa za utekelezaji (Management Information System) katika maeneo yote ya utekelezaji. Mifumo hiyo ambayo itajikita katika matumizi ya kompyuta kwa njia ya mtando, itawezesha maeneo ya utekelezaji yote 161 kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mpango kabla ya taarifa hizo kuunganishwa katika ngazi ya Taifa. Jambo hili litaboresha zaidi ukusanyaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango;
- (v) Kutekeleza miradi ya huduma za jamii ya sekta za elimu, afya na maji kwa kujenga na kuboresha miundombinu inayolenga katika maeneo ya Mpango yenye upungufu wa huduma hizo. Lengo likiwa ni kuziwezesha kaya za walengwa katika maeneo hayo kuweza kukidhi masharti ya kupata ruzuku yanayohusiana na elimu na afya. Jumla ya miradi 330 itatekelezwa katika mamlaka 161 za maeneo ya utekelezaji wa Mpango ikiwa ni maeneo ya Halmashauri 159 za Tanzania Bara pamoja na Wilaya zote za Unguja na Pemba;
- (vi) Kujenga uwezo wa Halmashauri na jamii katika kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango ili kuongeza maarifa na ufahamu wa kusimamia, kufuatilia na kutekeleza shughuli za Mpango; kufanya tafiti shirikishi za kijamii na kiuchumi ili kubaini fursa na vikwazo katika kujiletea maendeleo; na pia kukusanya na kutunza takwimu na kumbukumbu mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Jamii na Halmashauri husika;
- (vii) Kuimarisha Mfumo wa Masjala ya Walengwa wa Mpango wa kaya zote maskini zilizotambuliwa na kuandikishwa. Masjala hii itatunza taarifa zote za walengwa, yaani kaya zaidi ya milioni moja (yenye takriban watu milioni 7.5) ambazo zimetambuliwa na kuandikishwa; na
- (viii) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini za shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji. Shughuli hii pia itahusisha ukusanyaji wa takwimu za awali za walengwa wa Mpango ili baadaye kuweza kupima Mpango ulivyoweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**(e) Taasisi ya UONGOZI**

55. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Uongozi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuendelea kuandaa kozi kwenye maeneo ya Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya Umma na maeneo mengine yatakayotokana na maombi kutoka kwa wadau;

- (ii) Kuandaa na kuendesha kozi 12 katika fani mbalimbali zitakazohusu Mkakati wa Uongozi kwa ajili ya maendeleo endelevu, Menejimenti inayozingatia matokeo, Ufanisi katika Usimamizi wa Sekta ya Umma na Kutafakari matokeo ya Uongozi na kuchukua hatua;
- (iii) Kufanya mahojiano 12 na wakuu wa nchi waliopo madarakani na waliostaafu, ndani na nje na nchi, na Wataalam mbalimbali kuhusu uongozi na maendeleo endelevu ili kukuza uelewa na kupata uzoefu kwao na kurusha mahojiano hayo katika runinga;
- (iv) Kuandaa mikutano mitatu (3) ya majadiliano itakayowahusisha viongozi na wataalamu kuzungumzia masuala mbalimbali ya Uongozi na maendeleo endelevu;
- (v) Kuandaa mkutano wa Jukwaa la Viongozi wa Afrika na mikutano miwili (2) ya jukwaa la viongozi wanaochipukia;
- (vi) Kuanda semina mbili (2) zikiwa ni mpango wa kutekeleza Jukwaa la Uchumi wa Kijani zikiwa na lengo la kuongeza uelewa kwa watunga sera, watoa maamuzi na watu wenye ushawishi katika jamii kuhusu masuala yanayohusu uchumi wa kijani;
- (vii) Kufanya utafiti kuhusu Tathmini ya Utawala kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;
- (viii) Kutekeleza mradi wa usimamiaji wa rasilimali asili ambao unahu kutathmini masuala mbalimbali katika sekta ya gesi asilia na madini;
- (ix) Kufanya mkutano na waandishi wa habari kuhusu Uongozi na Jukwaa la Viongozi la Afrika; na
- (x) Kuendelea kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme na kuanza ujenzi wa Taasisi ya UONGOZI, Kijiji cha Kondo, Bagamoyo.

**(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)**

56. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kutoa mikopo kwa walengwa amba ni vijana wajasiriamali waliohitimu vyuo vya ufundi stadi (VETA) katika maeneo ya Dar es Salaam na Morogoro katika programu ya majaribio;
- (ii) Kufanya utafiti ili kubaini huduma wanazostahili vijana hasa waliomaliza mafunzo kwenye vyuo vya ufundi stadi katika mikoa ya Tanga, Lindi na Mtwara kwa nia ya kuwaendeleza na kuwaweka pamoja;
- (iii) Kuendelea kujenga uwezo wa watendaji kuhusu utoaji huduma bora; na
- (iv) Kujenga uwezo wa walengwa katika kukuza mitaji yao na ushirikishaji wa wajasiriamali wanaowazunguka.

57. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2015/16, Fungu 20; Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba **Shilingi 20,575,672,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fungu 30;

Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba **Shilingi 322,593,728,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 145,503,265,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

### **OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZAKE**

#### **(a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa.

59. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itahakikisha kuwa Watumishi wa Umma wanawajibika kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali. Majukumu haya yatafikiwa kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji wa Utumishi wa Umma;
- (ii) Kuandaa na kuhuisha mapendekezo ya Miundo na Mgawanyo wa Majukumu kwa Wizara na Idara Zinazojitegemea baada ya kuundwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano;
- (iii) Kuendelea kuzisimamia Wakala za Serikali zilizoanzishwa na kujenga uwezo kwa Wizara mama wa kuzisimamia Wakala zilizo chini yake;
- (iv) Kuandaa na kuendesha Semina Elekezi kwa Viongozi watakaochaguliwa/ kuteuliwa kuunda Serikali ya Awamu ya Tano;
- (v) Kuboresha masilahi ya Watumishi wa Umma kwa kuendelea kutekeleza Sera ya Malipo ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010;
- (vi) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika mwaka wa fedha 2015/16 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 71,496. Kipaumbele kitakuwa katika Sekta za Elimu 28,957; Afya 10,870; Kilimo 1,791; Mifugo 1,130 na watumishi wengineo 28,748. Aidha, watumishi 113,520 wa kada mbalimbali watapandishwa vyeo;
- (vii) Kukamilisha Sera ya Serikali Mtando pamoja na Mkakati wake wa Utekelezaji;
- (viii) Kukamilisha uandaaji wa Viwango na Miongozo ya kuweka na kusimamia Mifumo ya Serikali Mtando (e-Government Standards and Guidelines);
- (ix) Kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa masuala ya TEHAMA katika Taasisi za Serikali (ICT Governance Framework);
- (x) Kuratibu Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika 'Regional Communication Infrastructure Programme' (RCIP) katika eneo la Serikali Mtando;
- (xi) Kuziwezesha Idara za Elimu, Afya, Kilimo, Maji na Mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara, ili

- kuwafikia watendaji katika sehemu zao za kutoa huduma (Service Delivery Points);
- (xii) Kukamilisha utengenezaji na uwekaji mfumo wa Kieletroniki wa Uendeshaji wa Masuala ya Kiofisi (e-Office) kulingana na tathmini ya mahitaji ya wadau;
- (xiii) Kuboresha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kulingana na mahitaji ya watumiaji na mabadiliko ya Teknolojia;
- (xiv) Kuweka na kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ki-elektroniki wa kuhifadhi Taarifa za Maadili na Malalamiko katika Taasisi za Umma 34;
- (xv) Kuendelea kufuutilia uzingatiaji wa maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma;
- (xvi) Kuendelea kufanya vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuitia huduma ya "Video Conference" pamoja na kusambaza mwongozo wa matumizi ya huduma hiyo katika Taasisi za Serikali;
- (xvii) Kusimamia utekelezaji wa mifumo ya utendaji kazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma;
- (xviii) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma na kuchukua hatua ipasavyo;
- (xix) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Serikali;
- (xx) Kusimamia utekelezaji wa masuala ya Anuai za Jamii kwa kuendeleza Stadi za Uongozi kwa makundi maalum katika Utumishi wa Umma;
- (xxi) Kuandaa na kuendesha Mikutano miwili (2) ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma na mikutano miwili ya Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma;
- (xxii) Kuandaa na kuendesha Mikutano miwili (2) ya Baraza la Wafanyakazi mahali pa kazi, Mikutano miwili (2) ya Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Sekta za Afya, Elimu, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;
- (xxiii) Kukarabati miundombinu na majengo ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; na
- (xxiv) Kuwahudumia Viongozi Wastaifu wa Kitaifa kwa mujibu wa Sheria.
- (b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

60. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania katika mwaka wa fedha 2015/16 kimepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kutoa mafunzo ya kujandaa kufanya Mitihani kwa Watumishi 730; ya Utumishi wa Umma

- (ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi, Menejimenti, wa ofisi kwa watumishi wa umma 3,000; Utawala na Usimamizi
- (iii) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wapya wa umma;
- (iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa fedha za umma, Menejimenti ya Rasilimaliwateru, wa umma, Uongozi na Utawala Bora; 20,560 katika fani za utunzaji Usimamizi wa ununuzi
- (v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Taasisi za Umma;
- (vi) Kufanya utafiti kwa maeneo 10 katika yanayolenga kuboresha utoaji wa masuala huduma katika utumishi wa umma; mbalimbali
- (vii) Kuandaa machapisho mbalimbali kama vile majarida, vitabu na makala ya kitaalamu katika utumishi wa umma katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala;
- (viii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi 150 Uzamivu; sita (6) Shahada ya Uzamili; 11 Shahada ya Kwanza na Stashahada; na 120 mafunzo ya muda mfupi; na
- (ix) Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) litakalotumika kwa ajili ya madarasa na ofisi katika tawi la Tabora.

**(c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtando (TaGLA)**

61. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, Wakala inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Wadau 1,500 katika kozi za nje na ndani kwa kutumia mtando na njia zingine;
- (ii) Kuanzisha vituo shirikishi vya mafunzo kwa njia ya mtando mikoani;
- (iii) Kuongeza ushirikiano na asasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kutoa mafunzo kwa kutumia mtando na njia ya kawaida;
- (iv) Kutoa maunganisho (Bridging Services) na huduma za kitaalamu kuwezesha kufanyika kwa mikutano na mafunzo kwa njia ya video;
- (v) Kukamilisha ujenzi wa lifti (elevator) kwa matumizi ya watumishi na wateja wa Wakala;
- (vi) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wakala kwa kuwapa mafunzo kukidhi ongezeko la wateja na mabadiliko ya haraka ya teknolojia.

**(d) Wakala ya Serikali Mtando (eGA)**

62. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, Wakala ya Serikali Mtando inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuziunganisha Mamlaka za Serikali za Mitaa 77 kwenye mfumo wa mawasiliano salama Serikalini (Government Secured Network);
- (ii) Kujenga uwezo na kuimarisha usalama wa miundombinu na mifumo ya TEHAMA pamoja na taarifa za Serikali;
- (iii) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na viwango vyta matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (iv) Kuweka na kuunganisha Taasisi 100 za Serikali kwenye Mfumo wa Pamoja na Salama wa Barua Pepe wa Serikali (Secure Government-Wide Mailing System) kwa lengo la kurahisisha mawasiliano salama ya barua pepe katika Taasisi za Serikali;
- (v) Kusimamia ugawaji wa huduma za kiasi cha masafa ya intaneti (Government bandwidth) kwenye Taasisi za Serikali;
- (vi) Kuandaa michoro ya awali na kufanya upimaji wa eneo mahususi litakalotumika kujenga ofisi za kudumu za Wakala;
- (vii) Kutoa ushauri na utaalam elekezi kwa Taasisi za Serikali (ICT Consultancy and Advisory);
- (viii) Kusimamia na kuboresha Tovuti Kuu ya Serikali na Tovuti nyingine za Taasisi za Umma;
- (ix) Kutoa mafunzo maalum ya TEHAMA kwa watumishi 600 kutoka katika Taasisi 150 za Umma;
- (x) Kuwawezesha watumishi 40 wa Wakala kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi na watumishi wawili (2) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu;
- (xi) Kutoa taarifa na kuhamasisha matumizi ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma, na
- (xii) Kufanya utafiti unaohusu matumizi ya Serikali Mtandao.

63. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2015/16, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba **Shilingi 46,677,564,000**. Kati ya fedha hizi **Shilingi 37,717,620,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 8,959,944,000** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

#### **OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

64. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itaendelea na jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sura 398 kwa lengo la kukuza na kuimarisha maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kupokea, kuchambua na kufanya uchunguzi wa awali na wa kina wa malalamiko ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kuchapisha na kusambaza Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma;
- (iii) Kufanya uhakiki wa Matamko ya Rasilimali na Madeni ya Viongozi wa Umma;
- (iv) Kuwaelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa njia ya semina, mafunzo, maonesho ya wasanii, vipindi vya radio na runinga;
- (v) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Ahadi ya Uadilifu kwa Viongozi wa Umma, Watumishi wa Umma na wa Sekta Binafsi ikiwa ni sehemu ya Mkakati mahsus wa kuanza Kampeni ya Maadili ya Kitaifa;
- (vi) Kutoa elimu kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa Asasi Zisizo za Kiserikali kwa lengo la kuzijengea uwezo na kuziwezesha kusaidia kutoa elimu ya Maadili kwa Umma;
- (vii) Kujengea Ofisi uwezo kwa kuwapatia Watumishi mafunzo kulingana na fani zao na kuwapatia vitendea kazi;
- (viii) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Kusini – Mtwara kwa awamu ya tatu na kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu (Maadili House);
- (ix) Kufanya utaratibu wa kupata viwanja kwa ajili ya Ofisi za Kanda ya Kaskazini – Arusha na Kanda ya Ziwa – Mwanza pamoja na kutafuta wafadhili kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Kanda;
- (x) Kuanzisha mfumo wa Kisheria utakaosaidia kusimamia na kudhibiti Mgongano wa Masilahi; na
- (xi) Kufanya Utafiti juu ya hali ya maadili na ufahamu wa Viongozi na Wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

65. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2015/16, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba **Shilingi 7,702,588,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,216,691,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,485,897,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

66. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka cha fedha wa 2015/16, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kutekeleza majukumu ya msingi yaani kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira ili kuwezesha waajiri kupata wafanyakazi wenyewe sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;
- (ii) Kuendesha mchakato wa kujaza nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali;
- (iii) Kuimarisha Kanzidata na kutunza Takwimu za wahitimu kutoka kwenye Vyuo mbalimbali kwa urahisi wa Rejea;
- (iv) Kutembelea waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa shughuli zake; na
- (v) Kuboresha na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mchakato wa ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na Wataalamu mbalimbali kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtando.

67. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2015/16, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba **Shilingi 5,427,839,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

68. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuratibu mikutano ya kila robo mwaka ya Tume kutolea uamuji Rufaa na Malalamiko kadri yatakavyopokelewa;
- (ii) Kufanya ukaguzi wa rasilimaliwatu kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;
- (iii) Kushughulikia mashauri ya ajira na nidhamu ya walimu;
- (iv) Kuelimisha wadau kuhusu majukumu ya Tume kuititia njia mbalimbali kama ziara za viongozi na watendaji wa Tume, vyombo vya habari, Mikutano ya kazi na Wadau na maonyesho;
- (v) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu maadili ya kazi na kujiepusha na mazingira hatarishi kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI na Mapambano dhidi ya rushwa;
- (vi) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuongeza vitendea kazi vikiwemo vifaa vya ofisi; na
- (vii) Kuwajengea uwezo watumishi 60 kwa kuwapatia mafunzo.

69. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2015/16, Fungu 94; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kutumia **Shilingi 14,070,255,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**OFISI YA RAIS, BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

70. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kufanya tathmini ya kazi kwa watumishi wa umma;
- (ii) Kuandaa vigezo vya kuzingatiwa wakati wa kutoa motisha kwa watumishi wa umma wanaofanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu;
- (iii) Kufanya utafiti juu ya malipo ya masilahi ya watumishi wa umma kwa kuzingatia utendaji;
- (iv) Kukamilisha na kusambaza Mwongozo wa kupendekeza na kupanga mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma;
- (v) Kuandaa sheria ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na
- (vi) Kujenga uwezo wa kiutendaji wa Wajumbe wa Bodi na Watumishi.

71. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2015/16, Fungu 09; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kutumia **Shilingi 3,262,452,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

**OFISI YA RAIS, UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI**

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kukamilisha utekelezaji wa mipango iliyodhamirwa katika sekta sita (6) za kipaumbele katika Awamu ya Kwanza ya BRN. Malengo yalikuwa ni kwa miaka mitatu (3) na mwaka 2015/16 utakuwa ndio mwaka wa mwisho wa utekelezaji;
- (ii) Kufanya uchambuzi wa kimaabara wa matokeo yaliyopatikana katika sekta sita (6) za Awamu ya Kwanza, na kupendekeza hatua zinazostahili kufuata katika maeneo yote ya kipaumbele;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa programu iliyoidhinishwa katika sekta ya afya pamoja na maeneo sita ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa;
- (iv) Kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo watendaji katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Wilaya na Taasisi nyingine za Umma;
- (v) Kuandaa ukaguzi na tathmini huru kwa mfumo na matokeo yaliyopatikana; na
- (vi) Kuendelea kutoa elimu kwa washirika na wananchi ili kuelewa zaidi mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa.

73. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha 2015/16, Fungu 06: Ofisi ya Rais, Ufuatilaji wa Utekelezaji wa Miradi inaomba Jumla ya **Shilingi 20,234,938,000**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 5,958,004,000** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 14,276,934,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### **IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

74. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilianzishwa mwaka 1963 kwa Waraka wa Rais, Namba 7. Aidha, mwaka 1965 Sheria ya Nyaraka za Taifa Namba 33 na marekebisho yake kwa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Namba 3 ya mwaka 2002 ilitungwa. Kimsingi Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilianzishwa mwaka 1999 baada ya kuunganisha Idara ya Nyaraka za Taifa na Kitengo cha Kusimamia Mifumo Serikalini. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, jukumu la Idara ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zote za utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Taifa. Vilevile, Idara inasimamia utekelezaji wa Sheria ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu Namba 18 ya mwaka 2004, ambao ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Aman Karume.

75. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imekuwa Idara inayojitegemea kuanzia mwezi Februari, 2015 baada ya kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

76. **Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, Idara mpya inayojitegemea ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kuandaa Mpango Mkakati wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa;
- (ii) Kuanza ujenzi wa kituo cha kuwaenzi Waasisi wa Taifa (Mwalimu. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume);
- (iii) Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka cha Kanda ya Ziwa (Mwanza);
- (iv) Kutoa ushauri kwa Taasisi za Umma kuhusu utunzaji bora wa kumbukumbu na nyaraka na kuweka Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu katika ofisi 32 za Wakuu wa Wilaya;
- (v) Kuweka na kusimamia viwango vya utunzaji wa kumbukumbu na Nyaraka katika Taasisi za Umma;
- (vi) Kutunza na kuhifadhi Nyaraka za Taifa zitakazopokelewa kutoka kwenye Taasisi za Umma na kuhakikisha zinapatikana zinapohitajika;
- (vii) Kuratibu uandaaji wa miongozo ya kutunza na kuteketeza kumbukumbu katika Taasisi za Umma;
- (viii) Kuratibu mipango ya kutunza na kuhifadhi kumbukumbu muhimu (vital records) katika Taasisi za Umma;

- (ix) Kuandaa na kuratibu mipango ya hadhari ya kudhibiti na kukabili majanga yanayoweza kuharibu kumbukumbu na nyaraka za taifa;
- (x) Kuratibu uhamishaji wa majalada yaliyofungwa kwa kuyapeleka katika vituo vya kuhifadhi kumbukumbu tuli;
- (xi) Kuhifadhi nyaraka kwa kutumia teknolojia za kisasa ili kulinda urithi andishi wa Taifa;
- (xii) Kuratibu Mfuko wa Udhamsini wa Kuwaenzi Waasisi kwa ajili ya kuendeleza uhifadhi wa nyaraka na vitu vya Waasisi wa Taifa vyenye umuhimu wa kihistoria, na
- (xiii) Kusimamia matumizi sahihi ya nyaraka na majina ya Waasisi wa Taifa.

77. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2015/16, Fungu 04: Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba **Shilingi 1,486,324,000**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 1,236,324,000** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 250,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### **MAJUMUISHO**

78. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma, Ufuatiliaji wa Utekelezaji Miradi na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, kisheria ndizo zenye kuhakikisha kuwa majukumu hayo muhimu yanatekelezwa katika Mipango na Bajeti za mwaka 2015/16. Hayo yanawezekana yakienda sambamba na uimarishwaji wa Usimamizi bora wa shughuli za Serikali ili kupata Matokeo Makubwa Sasa kwa lengo la kufikia Malengo ya Mipango ya Kitaifa ya muda wa kati na muda mrefu.

79. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2014/15 na mipango yetu kwa mwaka wa fedha 2015/16, naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2015/16 kwa muhtasari kama ifuatavyo:

80. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Sasa nimwite Waziri wa Nchi, Uratibu na Mahusiano dakika 20!

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU, MHESHIMIWA DKT. MARY  
M. NAGU (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI  
YA FEDHA ZA OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO  
(FUNGU 66) KWA MWAKA 2015/2016  
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango Fungu 66, Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/2015 na likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya fedha ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, mapitio ya utekelezaji wa

majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Tume ya Mipango kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini na Makamu wake Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili, makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/2016 hatua ambayo ilitusaidia kuanda na kuwasilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kunithea kuwa Waziri katika Ofisi yake. Hii inaonesha jinsi anavyoendelea kuniamini. Napenda kuwapongeza na kuwashukuru Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa maelekezo na ushirikiano wao kwangu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote Ofisi ya Rais na Mawaziri wote kwa ushirikiano na upendo ambao wanaunesha katika kufanya kazi. Nawapongeza Wabunge wote kwa kazi nzuri ya kufuatilia shughuli za Serikali. Bila ushirikiano wa Watendaji wote wa Ofisi ya Rais wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Bwana Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Ikulu Bwana Peter Ilomo na Katibu Mkuu Mtendaji Tume ya Mipango na Wakuu wote wa Taasisi chini ya Ofisi ya Rais, tusingekuwa na hotuba hii, kwa hivyo nawapongeza na kuwashukuru.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais Tume ya Mipango ni kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa na pili kubuni sera za uchumi, mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa na pia usimamizi wa uchumi na kuendesha tafiti za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu haya ya msingi, naomba sasa niwasilishe kwa muhtasari utekelezaji kwanza wa bajeti kwa mwaka 2014/2015; pili, ahadi za Serikali Bungeni; tatu Miradi ya Maendeleo inayotekelizwa na Tume ya Mipango na nne utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yako. Aidha, taarifa ya utekelezaji itafuatiwa na mapendekezo ya Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/2015 ni shilingi bilioni 13.04; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.5 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 6.6 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Miradi ya Maendeleo ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 4.9 ambapo shilingi bilioni 3.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni moja ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 30 Aprili, 2015 Tume ya Mipango ilikuwa imepokea shilingi bilioni 4.9 sawa na asilimia 37.4 ya bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa mishahara ni shilingi bilioni 1.5, sawa na asilimia 97.1 ya bajeti ya mishahara. Matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 3.3, sawa na asilimia 49.1 ya bajeti ya matumizi mengineyo na matumizi ya maendeleo ni shilingi milioni 146.4 sawa na asilimia tatu ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mtiririko huu wa fedha umeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango hususan miradi ya maendeleo na kuendesha tafiti za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, ahadi zilizotolewa Bungeni chini ya Fungu 66 kwa mwaka 2014 ni kama ifuatavyo:

- (i) Kufuatilia utekelezaji wa mpango wa maendeleo 2014/2015;

- (ii) Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2015/2016;
- (iii) Kuanza maandalizi ya Mpango wa pili wa Maendeleo wa miaka mitano ya mwaka 2016/2017 mpaka 2020/2021;
- (iv) Kuendesha tafiti za kiuchumi na kijamii; na
- (v) Kujenga uwezo wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango ilifuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kitaifa na ya kimkakati 52 katika mikoa na sekta mbalimbali kama ilivyoordheshwa katika ukurasa wa tano wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu lilikuwa ni kuhakiki utekelezaji wa miradi husika ikiwa ni pamoja na kuainisha mafanikio na changamoto za utekelezaji ili kushauri ipasavyo. Aidha, kwa miradi ya sekta binafsi, lengo pia lilikuwa ni kupata taarifa za miradi, ajira na mipango ya baadaye ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto kuu zilizoonekana katika miradi iliyofuatiliwa ni pamoja na miradi mingi ya maendeleo kutopata fedha za kutosha na kwa wakati hali iliyosababisha utekelezaji kuwa nyuma ya ratiba. Vilevile utekelezaji wa baadhi ya miradi unasuasua au kusimama kabisa kutokana na malimbikizo ya madeni ya Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, aidha, ilionekana kuwa maeneo mengi ya miradi ya maendeleo hayana hatimiliki hususan miradi ya bandari na viwanja vya ndege. Hali hiyo inasababisha uvamizi wa maeneo hayo na migogoro na wananchi, hivyo kuathiri uwekezaji. Hata hivyo, Serikali inafanya kila kinachowezekana kutatua migogoro hiyo inapojitokeza na kulipa fidia pale inapolazimu ili kutowakatisha tamaa wawekezaji na kuepusha usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, Serikali inakusudia kuimarisha vyanzo vya mapato vya kodi na visivyo vya kodi. Vilevile Serikali imehakiki madai ya Wakandarasi ili kuweka utaratibu wa kulipa malimbikizo husika moja kwa moja kutoka Hazina. Aidha, Serikali imeelekeza Wizara, Idara, Taasisi, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kupata hatimiliki ili kudhibiti uvamizi na gherama za ulipaji fidia usio wa lazima.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango iliandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/2016 ambayo yalijadiliwa na kuriadihiwa na Bunge, Novemba 2014. Mapendekezo hayo yalizingatia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016), MKUKUTA II (2011 - 2015), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010 na Sera na Mikakati ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, aidha, Tume ya Mipango imekamilisha Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/2016 kwa kuzingatia Mapendekezo ya Mpango yaliyordhiwa na Bunge, Novemba 2014. Rasimu hiyo iliwasilishwa kwa Wabunge wote tarehe 29 Aprili, 2015 katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere – Dar es Salaam. Aidha, rasimu ya Mpango ilijadiliwa katika Kamati ya Bunge ya Bajeti tarehe 5 Mei, 2015, Dar es Salaam.

Maoni ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi, yatazingatiwa katika Rasimu ya Mpango itakayowasilishwa Bungeni Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango imeanza maandalizi ya kutayarisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utakaoongoza usimamizi wa

uchumi na mipango ya maendeleo kwa kipindi cha 2016/2017 – 2020/2021. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utalenga katika kujenga uchumi wa viwanda kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango Elekezi wa Maendeleo (2011/2012 – 2025/2026) ya kujenga uchumi ambaa una maendeleo ya viwanda yaliyo karibu sawa na nchi zenyne hadhi ya kipato cha kati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kulenga viwanda vinavyotumia utajiri mkubwa wa rasilimali zilizopo nchini, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utajielekeza katika kujenga viwanda vitakavyotuwezesha kutumia vizuri fursa za nchi, hususan nafasi ya kipekee ya Tanzania kijigrafia inayotuwezesha kuwa lango kuu la biashara na huduma kwa nchi za Afrika, hususan eneo la maziwa makuu na kuuza bidhaa zetu katika soko kubwa la kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC.

Mheshimiwa Spika, vile vile, MKURABITA itapewa nafasi kubwa katika kurasimisha biashara na mali za wananchi pamoja na kuimarisha vikundi vyta kiuchumi hususan SACCO\$ na VICOBA. Vilevile tutahakikisha viwanda mama vyta chuma vyta Liganga na Mchuchuma vinapewa nafasi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango iliendelea kutekeleza tafiti ambazo hazikukamilika mwaka 2013/2014, ambazo ni Maendeleo ya ujuzi utakaoiwezesha Tanzania kuwa na uchumi imara ifikapo mwaka 2025 na Muundo Taasisi (*Institutional Framework*) kuchochea uwekezaji na maendeleo ya teknolojia viwandani. Tafiti hizi zimekamilika na zinajumuisha mapendekezo ya kisera kwa ajili ya kujadiliwa na wadau kabla ya kuwasilishwa kwenye mamlaka za maamuzi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Tume ya Mipango imeanza maandalizi ya awali kwa ajili ya kuendesha tafiti hususan katika eneo la maendeleo ya viwanda na ukuaji wa miji. Lengo la tafiti hizo ni kupata taarifa muhimu zitakazosaidia katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021).

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2011/2012 – 2015/2016 kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2011 hadi Disemba, 2013. Mapitio hayo yalifanyika ili kupima mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji; kubainisha maeneo ambayo yanahitaji msukumo zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kupata taarifa zitakazosaidia katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji, Tume ya Mipango iliajiri watumishi wapya 26 ambapo Wachambuzi Sera walipangiwa kazi katika Klasta za Tume ya Mipango ni 18 na watumishi wengine nane walipangiwa katika Idara na Vitengo Saidizi. Aidha, watumishi saba walihamia katika Idara za Utawala kwa utaratibu wa kawaida wa utumishi wa umma. Hadi sasa, Tume ina jumla ya watumishi 149, ambapo wanaume ni 91 na wanawake ni 58.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuimarisha weledi, Tume ya Mipango imewevezesha watumishi nane kushiriki katika mafunzo ya muda mrefu katika maeneo ya shahada ya uzamivu katika uchumi na shahada ya uzamili katika uchumi, sera na mipango; menejimenti ya fedha, uhasibu, utawala, sheria na teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha, watumishi wawili waliwezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango imekamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji katika Sekta ya Umma ambaa umeanza kutumika

katika mwaka 2014/2015. Mwongozo huu unataka maelekezo ya utaratibu na hatua zinazohitajika katika kuandaa andiko la mradi na kutekeleza miradi yote inayotumia fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zilizotekelawa katika Mwaka 2014/2015, ni pamoja na Kuratibu Mazungumzo ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Serikali ya Japan, Kuratibu Maandalizi ya Mchango wa Tanzania katika Malengo Endelevu ya Maendeleo kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Fedha, kuandaa Mpango Mkakati wa TEHAMA wa Tume ya Mipango na Mwongozo wa Kudhibiti Vihatarishi. Maelezo ya shughuli hizo yapo katika ukurasa wa 12 – 15 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo 2014/2015. Katika mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango ilitekeleza miradi mitatu ya maendeleo; Mradi wa Kujenga uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Mradi wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu na Mradi wa Kuhamasisha Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umaskini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira (*Pro-Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development*).

Mheshimiwa Spika, kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili 30, 2015, Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ule wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu haikupata fedha. Hata hivyo, Tume ya Mipango ilifanya kazi za kuchambua maandiko ya miradi ya maendeleo ya baadhi ya Wizara, Idara na Wakala za Serikali na kutoa ushauri na maelekezo ya kuboresha maandiko hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili 30, 2015, shughuli zilizotekelawa katika mradi wa Kuhamasisha Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umaskini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira ni pamoja na kuendesha utafiti ili kubaini mafanikio katika juhudzi za kupunguza umaskini na kuongeza kipato kwa namna ambayo haitaathiri mazingira katika wilaya mbalimbali za Tanzania. Kwa ujumla kuna mafanikio dhahiri ya kupungua kwa umaskini kutokana na kuinuka kwa kipato na kuongezeka kwa tija na kuimarika kwa bei katika shughuli msingi za wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya maeneo ilibainika kuwa wananchi wamejitalidi sana kuboresha nyumba na makazi na pia kuongeza umiliki wa vyombo na zana za kudumu. Familia nyingi pia zimedhihirika kubadili au kuchanganya shughuli za kiuchumi kama vyanzo msingi vya kuongeza mapato yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, katika sehemu nyingi ilibainika kuwa ongezeko la kipato limeendana na matokeo hasi ya utunzaji wa mazingira, hususan, uvunaji holela wa misitu, kilimo kuendeshwa katika maeneo oevu na vyanzo vya maji, uharibifu wa mazalia ya samaki na ukuaji wa miji midogo kiholela.

Mheshimiwa Spika, maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Katika Bunge la Bajeti la mwaka 2014/2015, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilihoji na kushauri yafuatayo:-

(i) Sualia la kutolipwa kwa muda mrefu posho maalum kwa watumishi wa Tume ya Mipango litafutiwe ufumbuzi wa haraka.

(ii) Tume ya Mipango iongezewe wataalam.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba hatua zimechukuliwa na zimeelezwaga katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2015/2016. Katika mwaka 2015/2016, shughuli za kipaumbele zitakazotekelawa na Tume ya Mipango ni pamoja na:-

- (i) Kukamilisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- (ii) Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa;
- (iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/2016;
- (iv) Kuendesha tafiti za kiuchumi na kijamii; na
- (v) Kujenga uwezo wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, maeleo ya shughuli za kipaumbele kwa mwaka 2015/2016 yapo ukurasa wa 19 – 22 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itatekeleza miradi ifuatayo:-

- (i) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Bajeti na Miradi ya Maendeleo;
- (ii) Mradi wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma;
- (iii) Mradi wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu; na
- (iv) Mradi wa Kuhamasisha Ukuaji wa Uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kujenga uwezo wa kuratibu, utekelezaji wa miradi ya maendeleo utakuwa umeelezwa kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, shughuli zitakazotekelawa katika Mradi wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma vilevile ziko katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, shughuli zitakazotekelawa katika Mradi wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu iko katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2015/2016. Katika mwaka 2015/2016, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, inaomba kutengewa shilingi 11,588,052,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 7,871,896,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 3,716,156,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa maombi hayo ya fedha yapo katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/2015 na Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (Makofii)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Hoja hiyo pia, imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU, MHESHIMIWA DKT. MARY M. NAGU (MB.) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO (FUNGU 66) KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

#### **UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango (Fungu 66), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/15 na likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya fedha ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2015/2016.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote ninapenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/15 na makadirio ya matumizi ya fedha za Tume ya Mipango kwa mwaka 2015/16. Aidha, naomba kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2015/16, hatua ambayo ilitusaidia kuandaa na kuwasilisha hotuba hii.
3. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ni: (i) Kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa; na (ii) Kubuni sera za uchumi, Mikakati na Mipango ya Maendeleo ya Taifa, na pia usimamizi wa uchumi na kuendesha tafiti za kiuchumi na kijamii.
4. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majukumu hayo ya msingi, naomba sasa niwasilishe kwa muhtasari utekelezaji wa: (i) bajeti kwa mwaka 2014/15; (ii) ahadi za Serikali Bungeni; (iii) miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Tume ya Mipango; na (iv) utekelezaji wa maagizo ya Kamati yako. Aidha, taarifa ya utekelezaji itafuatiwa na mapendekezo ya mpango na makadirio ya matumizi kwa mwaka 2015/16.

#### **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA ORTM, 2014/15**

5. **Mheshimiwa Spika**, bajeti ya Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/15 ni shilingi 13,042,514,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,518,726,500 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 6,633,898,500 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Miradi ya maendeleo ilitengewa shilingi 4,889,889,000 ambapo shilingi 3,814,670,000 ni fedha za ndani na shilingi 1,075,219,000 ni fedha za nje.
6. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 30, 2015, Tume ya Mipango ilikuwa imepokea shilingi 4,878,520,955 sawa na asilimia 37.4 ya bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa: mishahara ni

shilingi 1,474,306,480 sawa na asilimia 97.1 ya bajeti ya Mishahara; Matumizi Mengineyo (OC) ni shilingi 3,257,844,475 sawa na asilimia 49.1 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo, na Matumizi ya Maendeleo ni shilingi milioni 146,370,000 sawa na asilimia 3.0 ya Matumizi ya miradi ya maendeleo. Mtiririko huu wa fedha umeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli za Tume ya Mipango, hususan miradi ya maendeleo na kuendesha tafiti za kiucumi na kijamii.

## UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SERIKALI BUNGENI

7. **Mheshimiwa Spika**, ahadi zilizotolewa Bungeni chini ya Fungu 66 kwa mwaka 2014/15 ni:-

- i. Kufuatilia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2014/15;
- ii. Kuanda Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16;
- iii. Kuanza maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21);
- iv. Kuendesha tafiti za kiuchumi na kijamii; na
- v. Kujenga Uwezo wa Tume ya Mipango.

- **Kufuatilia Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo**

8. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango ilifuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo 52 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Morogoro, Mbeya, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Dar es Salaam na Pwani. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha ile ya Umma na Sekta Binafsi katika maeneo ya barabara, madaraja na vivuko, bandari, nishati, maji, kilimo, umwagiliaji, viwanda, utalii, elimu, afya, viwanja vya ndege, mifugo na madini. Lengo kuu lilikuwa ni kujiona maendeleo ya utekelezaji wa miradi husika pamoja na kuainisha mafanikio na changamoto za utekelezaji ili kuishauri Serikali ipasavyo. Aidha, kwa miradi ya sekta binafsi, lengo pia lilikuwa ni kupata taarifa za uwekezaji, ajira na mipango ya baadaye ya mradi husika.

9. **Mheshimiwa Spika**, Changamoto kuu zilizoonekana katika miradi iliyofuatiliwa ni pamoja na miradi mingi ya maendeleo kutopata fedha za kutosha na kwa wakati, hali iliyosababisha utekelezaji kuwa nyuma ya ratiba. Vilevile, utekelezaji wa baadhi ya miradi unasuasua au kusimama kabisa kutokana na malimbikizo ya madeni ya wakandarasi. Aidha, ilioneekana kuwa maeneo mengi ya miradi ya maendeleo hayana hatimiliki hususan miradi ya bandari na viwanja vya ndege. Hali hiyo inasababisha uvamizi wa maeneo hayo na migogoro na wananchi, hivyo kuathiri uwekezaji. Hata hivyo, Serikali inafanya kila kinachowezekana kutatua migogoro hiyo inapojitokeza na kulipa fidia pale inapolazimu ili kutowakatisha tamaa wawekezaji, na kuepusha usumbufo kwa wananchi.

10. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, Serikali inakusudia kuimarisha vyanzo vya mapato vya kodi na visivyo vya kodi. Vilevile, Serikali imehakiki madai ya wakandarasi ili kuweka utaratibu wa kulipa malimbikizo husika moja kwa moja kutoka Hazina. Aidha, Wizara, Idara, Taasisi, Wakala za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Halmashauri zimeelekezwa kupata hatimiliki ili kudhibiti uvamizi na gharama za ulipaji fidia usio wa lazima.

- **Kuanda Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16**

**11. Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango iliandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 ambayo yalijadiliwa na kuridhiwa na Bunge, Novemba 2014. Mapendekezo hayo yalizingatia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16), MKUKUTA II (2011 - 2015), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010, na sera na mikakati ya kisekta. Aidha, Tume ya Mipango imekamilisha rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 kwa kuzingatia Mapendekezo ya Mpango yaliyordhiwa na Bunge, Novemba 2014. Rasimu hiyo iliwasilishwa kwa Wabunge wote tarehe 29/4/2015 katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere – Dar es Salaam. Aidha, rasimu ya Mpango ilijadiliwa katika Kamati ya Bunge ya Bajeti tarehe 5 Mei 2015. Maoni ya wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti hivi sasa yanafanyiwa kazi ili kuboresha rasimu ya Mpango itakayowasilishwa Bungeni Juni 2015.

- **Maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)**

**12. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango imeanza maandalizi ya kutayarisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utakaoongoza usimamizi wa uchumi na mipango ya maendeleo kwa kipindi cha 2016/17 – 2020/21. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utalenga katika kujenga uchumi wa viwanda kwa kuzingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango Elekezi wa Maendeleo (2011/12 – 2025/26) ya kujenga uchumi ambao una maendeleo ya viwanda yaliyo karibu sawa na nchi zenyet hadhi ya kipato cha kati. Mpango huu utajielekeza kuendeleza viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi na viwanda vyenye kutumia teknolojia ya kati, hasa viwanda mama kama vya chuma na vile vinavyotumia makaa ya mawe na magadi soda. Aidha, viwanda vyenye kutumia gesi asilia na mafuta navyo vitapewa msukumo.

**13. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kulenga viwanda vinavyotumia utajiri mkubwa wa rasilimali zilizopo nchini, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utajielekeza katika kujenga viwanda vitakavyotuwezesha kutumia vizuri fursa za nchi, hususan nafasi ya kipekee ya Tanzania kijigrafia inayotuwezesha kuwa lango kuu la biashara na huduma kwa nchi za maziwa makuu, na kuuza bidhaa zetu katika soko kubwa la kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC.

- **Tafiti za Kiuchumi na Kijamii**

**14. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango iliendelea kutekeleza tafiti ambazo hazikukamilika mwaka 2013/14, ambazo ni:- Maendeleo ya ujuzi utakaoiwezesha Tanzania kuwa na uchumi imara ifikapo mwaka 2025; na Muundo taasisi (institutional Framework) kuchochea uwekezaji na maendeleo ya teknolojia viwandani. Tafiti hizi zimekamilika na zinajumuisha mapendekezo ya kisera kwa ajili ya kujadiliwa na wadau kabla ya kuwasilishwa kwenye mamlaka za maamuzi Serikalini.

**15. Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, Tume ya Mipango imeanza maandalizi ya awali kwa ajili ya kuendesha tafiti hususan katika eneo la maendeleo ya viwanda na ukujji wa miji. Lengo la tafiti hizo ni kupata taarifa muhimu zitakazosaidia katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

**16. Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) kwa kipindi cha kuanzia Julai 2011 hadi Desemba 2013. Mapitio hayo yalifanyika ili kupima mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji; kubainisha maeneo ambayo yanahitaji msukumo zaidi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa; na kupata taarifa zitakazosaidia katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 – 2020/21) ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Kazi ya kuboresha mapitio hayo inaendelea ili kujumuisha kipindi chote cha

Mpango na taarifa kamili itawalishwa kwa wadau Novemba, 2015 sambamba na Mapendeleko ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

- **Kujenga Uwezo wa Tume ya Mipango**

**17. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji, Tume ya Mipango iliajiri watumishi wapya 26 ambapo Wachambuzi Sera waliopangiwa kazi katika Klasta za Tume ya Mipango ni 18, na watumishi wengine 8 walipangiwa katika Idara na Vitengo Saidizi. Aidha, watumishi 7 walihamia katika idara za utawala kwa utaratibu wa kawaida wa utumishi wa umma. Hadi sasa, Tume ina jumla ya watumishi 149, ambapo wanaume ni 91 na wanawake ni 58.

**18. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuimarisha weledi, Tume ya Mipango imeweza watumishi 8 kushiriki katika mafunzo ya muda mrefu katika maeneo yafuatayo:- shahada ya uzamivu katika uchumi; na shahada ya uzamili katika: uchumi; sera na mipango; menejimenti ya fedha; uhasibu; utawala; sheria; na teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha, watumishi wawili waliwezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, kwa upande wa mazingira mazuri ya kazi, Tume ya Mipango imeweza kuongeza vitendea kazi na kukarabati vilivyopo kadri upatikanaji wa fedha ulivyoruhusu.

#### **Shughuli Nyingine Zilizotekeliza katika Mwaka 2014/15**

**19. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango imekamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji katika Sekta ya Umma (*Public Investment Management Operational Manual*) ambao umeanza kutumika katika mwaka 2014/15. Mwongozo huu unatoa maelekezo ya utaratibu na hatua zinazohitajika katika kuandaa andiko la mradi na kutekeleza miradi yote inayotumia fedha za umma. Mwongozo huo pia unatoa maelezo na ufanuzi juu ya vigezo mbalimbali vinavyotumika katika uchambuzi wa miradi ya maendeleo kiuchumi, kifedha na kijamii.

- **Kuratibu Mazungumzo ya Ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan**

**20. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango iliendelea kuratibu uchambuzi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Japan. Shughuli zilizotekeliza ni pamoja na kubainisha maeneo ya kipaumbele ya ushirikiano kati ya Tanzania na Japan na kuainisha miradi itakayoombewa ufadhilli kutoka Serikali ya Japan kwa mwaka 2015/16. Miradi iliyowasilishwa kwa Serikali ya Japan kupata ufadhilli kwa mwaka 2015/16 ipo katika sekta za kilimo, viwanda, usafirishaji, ujenzi, nishati, maji, afya na fedha.

- **Kuratibu Maandalizi ya Mchango wa Tanzania katika Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs)**

**21. Mheshimiwa Spika,** Tanzania imepata mafanikio mbalimbali katika kufikia Malengo ya Milenia, hususan katika maeneo ya elimu na afya. Pamoja na mafanikio hayo, changamoto za umaskini, vifo vyta mama wajawazito na upatikanaji wa chakula na lishe zimeendelea kuzikabili nchi zinazoendelea. Changamoto hizo na nyingine zimepelekea Umoja wa Mataifa kuandaa malengo mengine ya maendeleo baada ya mwaka 2015 ambapo Tanzania ni mionganii mwa nchi washiriki. Katika kutimiza adhama hiyo, Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Fedha imekuwa ikitabu na kushiriki katika majadiliano kuhusu Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals). Mapendeleko yaliyowasilishwa na Tanzania kuingia katika SDGs ni pamoja na: kuondokana na umaskini uliokithiri; kuwa na elimu bora na afya nzuri hasa kwa kina mama na watoto; kuwa na

uchumi imara na maendeleo endelevu; kulinda mazingira; kuwa na uwiano sawa wa kijinsia; utawala bora; na kuongeza kasi ya ushirikiano endelevu na nchi mbalimbali.

- **Mpango Mkakati wa TEHAMA wa Tume ya Mipango na Mwongozo wa Kudhibiti Vihatarishi**

**22. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa TEHAMA wa Tume ya Mipango utakaoongoza namna bora ya kujenga uwezo wa wataalam wa Tume ya Mipango katika matumizi ya TEHAMA na ununuzi wa vifaa na mifumo ya kielektroniki. Mkakati huo utasaidia kuipunguzia Tume ya Mipango gharama za ununuzi na kuendesha mifumo hiyo. Aidha, Tume ya Mipango imeandaa mwongozo wa kudhibiti vihatarishi kwa lengo la kuweka viwango na namna Tume ya Mipango itakavyodhibiti vihatarishi ili visiikwaze kufikia malengo yake ya kila mwaka. Vilevile, Tume ya Mipango imeandaa daftari la mali za kudumu pamoja na kuzifanya tathmini yake kwa lengo la kuja thamani na kuweka kumbukumbu ya mali za Serikali zilizopo Tume ya Mipango.

#### **MIRADI YA MAENDELEO 2014/15**

**23. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2014/15, Tume ya Mipango ilitekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni: (i) Mradi wa Kujenga uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; (ii) Mradi wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu (*Population Planning Project*); na (iii) Mradi wa Kuhamasisha Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umaskini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira (*Pro-Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development*).

**24. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2014 hadi Aprili 30, 2015, mradi wa Kujenga uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ule wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu haikupata fedha. Hata hivyo, Tume ya Mipango ilifanya kazi za kuchambua maandiko ya miradi ya maendeleo ya baadhi ya Wizara, Idara, na Wakala za Serikali na kutoa ushauri na maelekezo ya kuboresha maandiko hayo.

**25. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2014 hadi Aprili 30, 2015, shughuli zilizotekelawa katika mradi wa Kuhamasisha Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umaskini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira ni pamoja na kuendesha utafiti ili kubaini mafanikio katika juhudzi za kupunguza umaskini na kuongeza kipato kwa namna ambayo haita athiri mazingira katika wilaya za Nyasa, Bunda, Sengerema, Bukoba na Ikungi. Kwa ujumla, kuna mafanikio dhahiri ya kupungua kwa umaskini kutokana na kuinuka kwa kipato na kuongezeka kwa tija na kuimarka kwa bei katika shughuli msingi za wananchi. Aidha, hili pia limechangiwa na kuimarka kwa upatikanaji wa huduma kama vile elimu, afya, maji, na usafiri.

**26. *Mheshimiwa Spika*,** katika baadhi ya maeneo ilibainika kuwa wananchi wamejitahidi sana kuboresha nyumba na makazi na pia kuongeza umilliki wa vyombo na zana za kudumu. Familia nyingi pia zimedhihirika kubadili au kuchanganya shughuli za kiuchumi kama vyanzo msingi vya kuongeza mapato yao. Pamoja na Mafanikio haya, katika sehemu nyingi ilibainika kuwa ongezeko la kipato limeendana na matokeo hasi ya utenzaji wa mazingira, hususan, uvunaji holela wa misitu, kilimo kuendeshwa katika maeneo oevu na vyanzo vya maji, uharibifu wa mazalia ya samaki, na ukuaji wa miji midogo kiholela. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, viongozi na wananchi wanahimizwa kuongeza jitihada katika kutunza mazingira na kusimamia matumizi ya ardhi ili kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi.

#### **MAAGIZO YA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA**

**27.** **Mheshimiwa Spika**, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2014/15, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilihoji na kushauri yafuatayo:-

- i. Suala la kutolipwa kwa muda mrefu posho maalum (*top-up allowance*) kwa watumishi wa Tume ya Mipango litafutiwe ufumbuzi wa haraka; na
- ii. Tume ya Mipango iongezewe wataalam.

**28.** **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa kwamba hatua zifuatazo zimechukuliwa na Serikali katika mwaka 2014/15:-

- i. Wizara ya Fedha imeendelea kutoa fedha za posho maalum (*top – up allowance*) kwa watumishi wa Tume ya Mipango wanaostahili kulipwa posho hizo na kuwezesha malipo hayo. Aidha, madeni ya nyuma yanayofikia shilingi 916,579,200 yamekaguliwa na yanaendelea kupunguzwa katika bajeti ya 2014/15 kulingana na upatikanaji wa fedha. Pia uchambuzi wa kuwezesha wachambuzi sera wote kulipwa posho ya ziada na malimbikizo umekamilika kwa ajili ya utekelezaji kwa awamu; na
- ii. Kuajiri watumishi wapya 26, na kupata watumishi wengine 7 waliohamia katika utaratibu wa kawaida ndani ya utumishi wa umma.

## **MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/16**

### **A. Shughuli za Kipaumbele, 2015/16**

**29.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, shughuli za kipaumbele zitakazo tekelezwa na Tume ya Mipango ni:-

- i. Kukamilisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21);
- ii. Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17;
- iii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16;
- iv. Kuendesha tafiti za Kiuchumi na Kijamii; na
- v. Kujenga Uwezo wa Tume ya Mipango.

#### **Kukamilisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)**

**30.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Tume ya Mipango inatarajia kukamilisha utayarishaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21). Kama nilivyoeleza awali, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utalenga katika kujenga uchumi wa viwanda. Serikali itahakikisha kwamba Mpango huo unaoandaliwa unatoa matumaini kwa Watanzania hasa katika kukabiliana na umaskini, kuongeza ukuaji shirikishi wa uchumi na kupanua fursa za ajira hasa kwa vijana.

#### **Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17**

**31.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itaandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/17. Mpango huo utakuwa wa kwanza katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21).

### Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**32. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Mipango itaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyobainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Shughuli zitakazotekelawa ni pamoja na kuchambua maandiko ya miradi na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kila robo mwaka; na kufuatilia utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Kitaifa ya kimkakati.

### Tafiti za Kiuchumi na Maendeleo ya Kijamii

**33. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Mipango itaendelea kukamilisha tafiti kuhusu maendeleo ya viwanda, hususan, viwanda gani vipewe kipaumbele kwa kuzingatia fursa za Tanzania, kubaini malengo ya maendeleo ya viwanda kwa miaka 5 (2016/17 – 2020/21); uhusiano kati ya ukuaji wa miji na maendeleo ya viwanda; maendeleo ya sayansi na teknolojia; na kubaini vyanzo vya kugharamia utekelezaji wa Mpango huo. Kama nilivyosema awali, lengo la tafiti hizo ni kusaidia maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

### Kujenga Uwezo wa Tume ya Mipango

**34. Mheshimiwa Spika,** Tume ya Mipango itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake na kuboresha vitendea kazi vya ofisi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Maeneo yatakayopewa umuhimu mkubwa ni pamoja na mafunzo kwa wataalam wa kada zote na ununuzi wa vitendea kazi.

### B. Miradi ya Maendeleo Itakayotekelawa 2015/16

**35. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itatekeleza miradi ifuatayo: (i) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Bajeti na Miradi ya Maendeleo; (ii) Mradi wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma; (iii) Mradi wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu; na (iv) Mradi wa Kuhamasisha Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umaskini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira.

**36. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuratibu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo shughuli zilizopangwa ni:-

- i. Kujenga uwezo wa watumishi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika kuandaa, kusimamia, na kutekeleza mipango ya maendeleo;
- ii. Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo; na
- iii. Maandalizi ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Dodoma.

**37. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2015/16, shughuli zitakazo tekelawa katika mradi wa Maboresho katika Usimamizi wa Fedha za Umma ni kuwezesha uchapaji, usambazaji na kuendesha mafunzo kuhusu Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji katika Sekta ya Umma kwa Maafisa Mipango Serikalini katika ngazi za wizara na mikoa. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa na ujuzi katika kuandaa maandiko ya miradi na uchambuzi wa miradi ya maendeleo.

**38.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, shughuli zitakazotekelawa katika mradi wa Kupanga Masuala ya Idadi ya Watu ni:-

- i. Kuratibu mapitio ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu (2006);
- ii. Kuendesha utafiti kuhusu hali ya Nguvukazi Nchini ikiwa ni moja ya makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- iii. Kujenga uwezo wa watumishi katika uchambuzi wa masuala ya Idadi ya watu na Maendeleo.

**39.** **Mheshimiwa Spika**, shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mradi wa Kuhamasisha Ukuaji Uchumi ili Kupunguza Umaskini bila Kuathiri Maendeleo Endelevu ya Mazingira kwa mwaka 2015/16 ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi na mafunzo kuhusu nyenzo mbalimbali za utayarishaji mipango na uchambuzi wa sera na taarifa za kiuchumi.

#### C. Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2015/16

**40.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango inaomba kutengewa shilingi **11,588,052,000**. Kati ya fedha hizo, shilingi **7,871,896,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na shilingi **3,716,156,000** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa maombi hayo ya fedha ni kama ifuatavyo:-

Maelezo	Kiasi (Shilingi)
• Mishahara (PE)	2,500,007,000
• Matumizi Mengineyo (OC)	5,371,889,000
	<b>7,871,896,000</b>
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	
• Matumizi ya Maendeleo Fedha za Ndani	3,000,000,000
• Matumizi ya Maendeleo Fedha za Nje	716,156,000
• Jumla Matumizi ya Maendeleo	<b>3,716,156,000</b>
<b>Jumla Fungu 66</b>	<b>11,588,052,000</b>

#### HITIMISHO

**41.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa mwaka 2014/15 na Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2015/16.

**42.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Sasa atakuja Msemaji wa Kamati, yeye atawasilisha peke yake Mafungu yote, atatumia dakika zake 30. Halafu Kambi ya Upinzani watatumia dakika 30 kwa mgawanyo wa

dakika 10 kati ya Mheshimiwa Cecilia Paresso dakika 10, Mheshimiwa Profesa Kahigi dakika 10 na Mheshimiwa Esther Matiko dakika 10.

Sasa kwa sababu, ya kazi niliyoitangaza hapa nitamwita Mwenyekiti, aje anisaidie wakati naondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti!

*Mwenyekiti (Mhe. Lediana M. Mng'ong'o) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Rweikiza!

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) na (9) na Kanuni ya 117(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais na Ofisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais inajumuisha Mafungu 10 ambayo ni Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu, Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Fungu 32 – Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 – Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 67 – Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma na Fungu 99 – Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, Fungu 6 – Ofisi ya Rais Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi, Fungu 4 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa na Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ilionesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Taasisi za Ofisi hii zilizoidhinishiwa bajeti kwa ajili hiyo.

Pamoja na kufuatilia namna Serikali ilivyotekeleza miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1), Kamati pia ilichambua Taarifa hiyo kwa kulinganisha kiasi cha fedha zilizoidhinishiwa na Kamati na fedha zilizopatikana kwa lengo la kubaini kiwango cha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kulinganisha upatikanaji wa fedha katika mafungu yaliyotengewa fedha za miradi ya maendeleo. Mafungu hayo ni Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huo Kamati ilibaini kuwa, hadi kufikia Machi, 31 mwaka huu, ikiwa ni mwisho wa robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji wa bajeti, upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ulikuwa mzuri kwa kiasi katika Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambako 71.07% ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa iliweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, hali haikuwa hivyo kwa Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango ambayo, ilipata 2.99% tu ya fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge. Hali hiyo ya upatikanaji wa fedha katika Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais haiakisi uwezekano wa mafanikio katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ni wa mashaka makubwa katika kufanikisha malengo mazuri yaliyopangwa. Si vizuri kwa miradi muhimu kama ya Tume ya Mipango kutopewa uzito unaofaa na kupatiwa fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati imebaini kuwa licha ya miradi ya maendeleo kutengewa fedha kidogo, upatikanaji wa fedha umekuwa ni tatizo wakati wa utekelezaji wa miradi husika na kusababisha utekelezaji hafifu wa malengo ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mifano michache inayoonesha udhaifu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi chini ya Fungu 66 – Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ilitengewa jumla ya shilingi bilioni nne na milioni mia nane themanini na tisa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2015 Tume hii ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 146,370,000 zote zikiwa ni fedha za nje. Kiasi hicho ni sawa na 2.69% cha fedha iliyoidhinishwa kutumika kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF, ulitengewa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 18.5, lakini hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 TASAF ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni tatu tu ya fedha za ndani, sawa na 16.6% ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa, pamoja na malengo mazuri ya Mfuko huo na umuhimu wake katika ustawi wa maendeleo ya jamii, si rahisi kufanikisha dira, dhamira na malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikazingatia kuwa, mipango mizuri haina maana pasipo kutekelezwa na utekelezaji wa mipango unategemea upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika jumla ya mambo 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huo ambao pia uliridhiwa na Bunge lako Tukufu ulilenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu katika Ofisi hii. Kamati ilitaka kujiridhisha ni kwa kiasi gani maoni na ushauri wake ulizingatiwa na Serikali kwa kufanya uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na Serikali ambapo kati ya mambo 35 yaliyopendekezwa, mambo 19 sawa na asilimia 54.3 yamezingatiwa na Serikali. Aidha, maoni 8 kati ya 35 sawa na 22.8% yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na maoni 8 sawa na 22.8 % hayakuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliozingatiwa na Serikali ni kuhusu mikutano baina ya viongozi wa dini mbalimbali na vyama vyaa siasa yenye lengo la kudumisha mshikamano, umoja, amani, utulivu, upendo na uzalendo wetu kama Watanzania katika Mikoa na Wilaya zote nchini. Kamati ilioa ushauri huo kutokana na kuwepo kwa viashiria vyaa kutoweka kwa amani na utulivu nchini. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maelezo ya Serikali yanaonesha kwamba Serikali ilifanya mikutano sita (6) iliyohusisha viongozi wa dini na vyama vyaa siasa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mara na Tanga kwa lengo la kusitiza zaidi amani, utulivu na upendo mionganii mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mfano mwagine ni ushauri wa Kamati kuhusu Sekretarieti ya Ajira nchini kuandaa orodha ya wahitimoo wa vyuo vikuu na wataalam weledi na kuwapa orodha hiyo waajiri. Taarifa ya Serikali imeonesha kuwa Sekretarieti ya Ajira nchini imeimarisha kanzidata (*database*) ya waombaji kazi wenye ujuzi wanaotakiwa na waajiri mbalimbali. Aidha, kuanzia Julai 2014 hadi Machi, 2015, Sekretarieti imewapangia waajiriwa wapya 1,274 waliokuwepo kwenye kanzidata (*database*) kwa waajiri 146.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya ushauri uliozingatiwa, upo ushauri ambaa haukuzingatiwa. Kwa mfano, Kamati ilishauri kwamba Serikali itenye fedha za kutosha na kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kujenga Ofisi za Bodii ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika ili kulinda heshima ya nchi yetu kwa kutimiza ahadi tunazozitoa kama nchi mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Maelezo ya Serikali yanaonesha kuwa ushauri huu haukuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwagine wa kutozingatiwa kwa ushauri wa Kamati ni pale iliposhauri kuhusu kuujengea uwezo Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kwa kuutengea fedha za kutosha ili uweze kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi katika Wilaya zote nchini hususan Wilaya za mpakani. Maelezo ya mtoa hoja hayaoneshi jinsi gani Serikali ilivyozingatia ipasavyo zaidi ya kutambua umuhimu wa MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ushauri unaoendelea kuzingatiwa, Kamati ilishauri kuhusu kufufuliwa kwa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) kwa kuongezewa fedha. Taarifa ya mtoa hoja ilionesha kuwa ushauri huu umezingatiwa katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano na kwamba Serikali imekusudia kuongeza fedha na kuzitoa kwa wakati ili kuwanufaisha walengwa wa Mfuko. Kamati ina maoni kuwa azma hii ya Serikali inapaswa kusimamiwa ipasavyo na kutekelezwa bila kusita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015. Katika utekelezaji wa bajeti na majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa pamoja na Kanuni ya 6(2) ya Nyongeza ya Nane, Kamati ilifuatilia kwa karibu utendaji wa shughuli mbalimbali zilizotekelizwa na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa sehemu kubwa ya majukumu ya kawaida yaliyopangwa kutekelezwa imeweza kufikia kiwango kilichotarajiwa katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano na majukumu yaliyopangwa na kutekelezwa hadi tarehe 31 Machi, 2015 ipo ya kutosha. Nitataja baadhi, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu

kuwa Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi imeweza kufanikisha upembuzi wa mahitaji ya mageuzi ili kuboresha huduma za afya kupitia Maabara Maalum ya Huduma za Afya. Aidha, Maelezo ya Mheshiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yameonesha kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika mwaka wa fedha 2014/2015 imeweza kufungua kesi mpya 161 zikiwemo kesi nane (8) zilizotokana na uchunguzi maalum wa vocha za pembejeo za kilimo, kesi tatu (3) zinazohusu maliasili ya nchi na kesi tisa (9) zilizotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine muhimu wa malengo ya bajeti kwa mwaka 2014/2015 yaliyotekelawa ni kuhusu malengo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), iliyo katika Awamu ya Tatu inayohusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini sana. Kamati ilijulishwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 42 zimelipwa kama ruzuku ya kunusuru kaya maskini zipatazo 266,601 katika vipindi vya mizunguko nane ya malipo katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji 40, zikiwemo Halmashauri 38 Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Malengo yaliyowekwa; wakati wa kupitia malengo ya Bajeti kwa Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii, Kamati ilizingatia uwepo wa Fungu (Vote) jipya, Fungu 04 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa na kupitia malengo yake pamoja na malengo ya mafungu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla katika ulinganishaji Kamati ilibaini kuwa bajeti za mafungu matano zitaongezeka ambapo bajeti katika Fungu 20 – Ikulu itaongoza kwa ongezeko la asilimia 117.82 ikifuatiwa na Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ongezeko la asilimia 25.94. Wakati mafungu hayo yakiwa na ongezeko, bajeti ya mafungu matano itapungua kwa asilima 41.01. Bajeti itakayopungua zaidi ni ya Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi, Fungu 6 kwa silimia 41.01.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Serikali kuhusu makadirio ya matumizi kwa ajili ya Ofisi ya Rais na taasisi zilizo chini yake yanaonesha kuwa mafungu manne hayakukadiriwa kuwa na bajeti ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mafungu hayo ni Fungu 20 - Ofisi ya Rais Ikulu; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma na Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mafungu sita yamekadirira kuwa na matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo. Mafungu hayo ni Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango; Fungu 06 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi na Fungu 04 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa mwelekeo wa makadirio ya matumizi katika taasisi zilizo chini ya ofisi ya Rais umezingatia uzoefu wa uwezekano wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Aidha, si lazima kwa kila taasisi ya Serikali kuwa na mradi wa kutekeleza. Kamati inatambua kuwa makadirio haya yamezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayotekelizwa na Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake. Hata hivyo, ili kuboresha utekelezaji wa majukumu hayo katika Ofisi hii, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla, katika uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015, inaonesha dhahiri kuwa kumekuwa na utekelezaji hafifu wa bajeti kwani utoaji wa fedha kutoka Hazina kwenda katika Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais

umekuwa siyo wa kuridhisha hali iliyosababisha baadhi ya majukumu yaliyopangwa kutotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri mahsus. Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Fungu 20 na 30. Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri pamoja na mambo mengine inalo jukumu kubwa la kumsaidia na kumwezesha Rais kuongoza nchi vizuri kwa ufanisi na ustawi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya ofisi hiyo ambayo ni dira na taswira ya Taifa na ili kuboresha utekelezaji na utendaji wa ofisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kuwajenye uwezo Wajumbe na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa kuwapatia mafunzo stahiki ili waweze kutekeleza majukumu yao ikiwemo kutoa ushauri kwa Rais ili kumwezesha kuongoza nchi vizuri na kwa ufanisi.

(ii) Kwa kuwa Mkakati wa Pili wa Taifa dhidi ya Rushwa umekamilika na kwamba unashubiri uamuzi ya Serikali, ni vema uamuzi huo uharakishwe ili mkakati huo uanze kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016.

(iii) Kwa kuwa majengo ya Ikulu ndogo ya Chamwino na nyumba kumi za watumishi wa Ikulu hiyo yako katika hali mbaya kama ilivyobainika katika ziara ya Kamati ilipotembelea Ikulu ndogo ya Chamwino mwezi Julai, 2014. Kamati inashauri kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati zipatikane kwa wakati kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

(iv) Aidha, Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu ndogo za Mbeya na Zanzibar ili kuhakikisha kuwa Ikulu hizo zinakarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imeanzishwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007. Taasisi hii ni muhimu katika kuimariswa utawala bora nchini unaofuata misingi ya usawa na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu ambapo uzoefu unaonesha kuwa vitendo vya rushwa huongezeka kwa kasi katika kipindi hicho, ni dhahiri kuwa taasisi hii itakuwa na kazi kubwa ya kudhibiti vitendo hivyo na kuhakikisha kuwa mchakato wa uchaguzi unafanyika kwa haki, amani na utulivu. Ili kuimariswa ufanisi wa taasisi hii katika kukabiliana na vitendo vya rushwa, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) TAKUKURU iwezeshe kikamilifu kwa kupatiwa nyenzo, rasilimali watu wenye weledi na kuitenyege bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleza jukumu lake kwa ufanisi Katika kudhibiti vitendo vya rushwa kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu.

(ii) TAKUKURU iongeze nguvu katika kufanya Uchunguzi Maalum wa tuhuma za rushwa katika vocha za pembejeo za kilimo, maliasili pamoja na kukamilisha uchunguzi kuhusu Sakata la Akaunti ya TEGETA ESCROW ili watakaobainika wafkishwe Mahakamani mapema iwezekanavyo kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka. (Makofii)

(iii) TAKUKURU ishirikiana na vyombo vingine vya dola kama Polisi na Mahakama kuwachunguza, kuwakamata, kuwashtaki, kuwahukumu, kuwafunga na kuwafilisi watoaji na walaji rushwa ili haki itendeke na ioneckane inatendeka hapa nchini.

Narudia, TAKUKURU ishirikiana na vyombo vingine vya dola kama Polisi na Mahakama kuwachunguza, kuwakamata, kuwashtaki, kuwahukumu, kuwafunga na kuwafilisi watoaji na walaji rushwa ili haki itendeke na ioneckane inatendeka hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uongozi (*Uongozi Institute*), ilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali wa Kiafrika ili kuimarisha utawala bora katika nchi zao na kusaidia kuleta maendeleo endelevu katika nchi zao. Taasisi hii katika mwaka wa fedha 2015/2016, imepanga kuendelea kutoa kozi mbalimbali za uongozi zitakazohusu mkakati wa uongozi kwa maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Taasisi ya Uongozi inatimiza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na umuhimu wa taasisi hii katika kuwaandaa viongozi kwa kuwapa mafunzo na ujuzi katika kusimamia sekta ya umma na binafsi, Serikali ihakikishe inaiwezesha taasisi hii kwa kuipatia rasilimali watu na kutenga fedha za kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(ii) Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na changamoto kubwa ya kuporomoka kwa maadili ya viongozi wa umma ni vyema chuo hiki kikaingiza mitaala ya maadili ya viongozi ili kuwezesha viongozi wanaopitia katika chuo hicho kuzingatia maadili katika nafasi zao watakazokuwa wakizitumikia.

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulianzishwa mwaka 2004 ili kuwezesha urasimishaji wa mali na biashara za wanyonge kwa lengo la kuwainua kiuchumi na kuwaondoa katika dimbwi la umaskini. Pamoja na kwamba mpango umetimiza miaka 11 tokea kuanzhishwa kwake, bado malengo yake hayajafanyiwa kazi kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mpango huu muhimu uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa Mpango huu unawezeshwa kikamilifu kifedha kwa kutengewa bajeti ya kutosha.

(ii) MKURABITA iongeze kasi ya upimaji wa ardhi katika maeneo mbalimbali vijijini na mijini na kutoa hati miliki ili kuongeza thamani ya ardhi, kuepusha migogoro ya ardhi na kuwawezesha wananchi kukopa katika taasisi mbalimbali za kifedha kwa kutumia dhamana ya hati miliki hizo kwa lengo la kuwawezesha kujikwamua na umasikini kwa kutumia hati za kimila. (Makofi)

(iii) Kwa kuwa benki nyingi nchini zinasita kupokea hati za kimila kama dhamana ya mikopo, ni vyema Serikali ikachukua hatua madhubuti ya kuzielimisha taasisi za kibenki nchini kuhusu uhalali wa hati za kimila kutumika katika dhamana ya mikopo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepewa jukumu kubwa la kuimarisha utawala bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Hivyo basi, Kamati yangu inashauri ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ijengewe uwezo wa kifedha kwa utengewa bajeti ya kutosha pamoja na kupewa rasilimali watu wa kutosha na wenyewe weledi unaostahili.

(ii) Serikali iongeze jitihada za kuimarisha wakala wa mafunzo kwa njia ya mtando ili kutekeleze jukumu lake la kuwajengea uwezo watumishi wa umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kwa lengo la kuwawezesha kuhimili kasi ya mabadilio ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Umma, ina mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa rasilimali watu katika utumishi wa umma kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Ili kuboresha utekelezaji wa Tume hii na kuiwezesha kufikia azma ya dira yake ambayo ni kuwa mfano wa kuigwa, Kamati inashauri Tume iendelee kutoa elimu kwa watumishi wa umma kuhusu maadili ya utumishi wa umma ili kuepuka kutumia madaraka yao vibaya katika kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kuititia Tangazo la Serikali Na.162 la tarehe 3 Juni, 2011. Uanzishwaji wa Bodi ni utekelezaji wa mapendeleko yaliyotolewa na Tume mbalimbali zilizoishauri Serikali namna ya kuboresha mishahara katika Utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Sera ya Mishahara na motisha katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi hii imepewa jukumu mahsusil la kufanya mapitio ya mishahara pamoja na miundo ya mishahara, viwango vya posho na mafao katika utumishi wa umma na kumshauri Rais kuhusiana na mapitio hayo. Kamati inashauri iendelee kuiwezesha Bodi ya Mishahara kifedha ili iweze kukamilisha Mwongozo wa kuzingatia wakati wa kupanga mishahara na maslahi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, ilianzishwa ili kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Viongozi wa Umma Na.13 ya mwaka 1995 kwa kuhakikisha kuwa tabia na mienendo ya viongozi wa umma inazingatia misingi ya maadili ilioanishwa katika sheria. Pamoja na kazi hizo, Kamati inatoa ushauri ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu katika Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, sanjari na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, inaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Taasisi ilitengewa fedha za ndani kwa ajili ya miradi kiasi cha shilingi 1,500,000,000/= lakini hadi kufikia Machi, 2015 hakuna kiasi chochote cha fedha za ndani kilichotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inashauri kuwa Serikali itenye bajeti ya kutosha na kutoa fedha zilizotengwa kwa wakati ili kuiwezesha Taasisi hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango - Fungu 66. Tume ya Mipango ilianzishwa katika Ofisi ya Rais ikiwa na majukumu ya msingi ya kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa, kubuni sera za uchumi, mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa, kusimamia uchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii. Tume ya mipango ndiyo nguzo kuu ya ustawi wa Taifa lolote kwani hakuna nchi yoyote iliyoendelea duniani bila kuwa na mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume ya Mipango ilikabiliwa na changamoto ya kutopata fedha ya kutosha na kwa wakati hali iliyoathiri mipango ya utekelezaji. Ili kuimarisha utendaji kazi wa Tume ya Mipango, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa mipango yote ya maendeleo inapangwa na kusimamiwa na Tume ya Mipango, ni vyema Tume hii ijengewe uwezo kwa kutengewa fedha na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo jumla ya shilingi 3,814,670,000/= zitolewe zote kabla ya mwaka wa fedha 2014/2015 kuisha ili Tume iweze kutekeleza miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imepangwa.

(ii) Kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano wa 2011/2012 - 2015/2016 unakamilika na Serikali kupitia Tume ya Mipango inaandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa 2016/2017- 2020/2021, Kamati inashauri Serikali ifanyie tathmini ya Mpango wa Miaka Mitano unaoisha ili kubaini upungufu uliojitekeza katika mpango huo na kuyafanya kazi kikamilifu katika mpango wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (*President's Delivery Bureau*) ni taasisi iliyoanzishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kupitia Tangazo la Serikali Namba 152 la mwaka 2013 liliotolewa chini ya Sheria ya Mawaziri, Sura ya 299 ya Sheria za Tanzania kwa lengo la kuhakikisha miradi ya kipaumbele chini ya mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa inatekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kuiimarisha Idara ya Ufuatiliaji wa Miradi kifedha na kirasilimali watu ili iweze kufuatilia kwa karibu miradi ya kipaumbele na kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua za haraka za kimaendeleo, kijamii, kiuchumi na kisiasa.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ipanue wigo wa maeneo ya vipaumbele kwa kuingiza suala la ardhi kwani ardhi ni rasilimali muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu.

(iii) Idara iiisimamie kwa karibu Wizara ya Fedha ili kuisukuma kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili kuiwezesha taasisi husika kutekeleza miradi hiyo kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Jukumu kubwa la Idara hii ni kusimamia na kuratibu sera, sheria, kanuni na taratibu zote za utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhifadhi kumbukumbu ni suala muhimu kwa Taifa lolote duniani. Kumbukumbu husaidia Taifa liweze kuendelea kwa kujitathmini kupitia historia

yake mahali lilipotoka na kusahihisha makosa liliyofanya, mahali lilipo na mahali linakotarajia kwenda. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali iijengee uwezo wa kifedha na kirasilimali watu na nyenzo za kisasa ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa.

(ii) Serikali kupitia Idara hii iweke mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa nyaraka zote muhimu za Taifa kutoka katika taasisi mbalimbali na kuzitunza kwa namna ambayo hazitawenza kuharibiwa wala kutumiwa vibaya.

(iii) Serikali itoe fedha zitakazotengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha kuwaenzi waasisi wa Taifa kwa wakati ili kuwezesha ujenzi wa kituo hicho kuanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, kwanza, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa katika kipindi chote cha awamu mbili mfululizo kwa mafanikio makubwa na kwa ustawi wa Taifa hili adhimu. Ni dhahiri kuwa nchi yetu imepiga hatua kubwa katika sekta zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa na kiutamaduni. (Makofi)

Pia, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu.

Tatu, napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Celina Kombani - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Mheshimiwa Mary Nagu - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa ushirikiano mzuri walioipatia Kamati katika utekelezaji wa m Majukumu yake. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kipekee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya 2015/2016.

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dokta Thomas Kashihilah - Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee nawashukuru Ndugu Charles Mloka - Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Athumani Hussein - Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Matamus Fungo na Ndugu Maria Mdulugu - Makatibu wa Kamati na Ndugu Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hii na kuiwezesha kukamilisha majukumu yake kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Mahusiano na Uratibu kama yaliviyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI  
WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, KWA MWAKA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/2016 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(5) na (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata nafasi ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 siku ya tarehe 2 Mei, 2015 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Celina O. Kombani, (MB), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Mary Michael Nagu (MB), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu pamoja na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, (MB), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais inajumuisha mafungu kumi ambayo ni:

- i) Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu);
- ii) Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii) Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- iv) Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v) Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
- vi) Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,
- vii) Fungu 09-Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma,
- viii) Fungu 06-Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi; na
- ix) Fungu 04 Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

## 2.0 YALIYOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na mwenendo wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Taarifa iliowasilishwa kwenye Kamati tarehe 02 Mei, 2015 ilionesha mwenendo wa

upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa taasisi za Ofisi hii zilizoidhinishiwa bajeti kwa ajili hiyo. Pamoja na kufuatilia namna serikali inavyotekeliza Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1), Kamati pia ilichambua taarifa hiyo kwa kulinganisha fedha zilizopatikana na kiasi cha fedha zilizoidhinishiwa kwa lengo la kubaini kiwango cha utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulionesha kuwa kiwango cha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kinatofautiana baina ya taasisi moja na nyingine mionganoni mwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais. Hali hii, pamoja na mambo mengine, ilisababishwa na tofauti ya upatikanaji wa fedha katika taasisi hizo. Kamati ilichambua na kulinganisha upatikanaji wa fedha katika Mafungu yaliyotengewa fedha za miradi ya maendeleo. Mafungu hayo ni:-

- |      |                                                                    |               |
|------|--------------------------------------------------------------------|---------------|
| i)   | Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza<br>Ofisi ya Rais; | la Mawazirina |
| ii)  | Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi                  | wa Umma;      |
| iii) | Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili<br>wa Umma;      | ya Viongozi   |
| iv)  | Fungu 06 - Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji               | wa Miradi; na |
| v)   | Fungu 66 – Ofisi ya Rais Tume ya Mipango.                          |               |

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ulikuwa mzuri kwa kiasi katika Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambapo asilimia 71.07 ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa iliweza kupatikana. Hali haikuwa hivyo kwa Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipangoambayo ilipata asilimia 2.99 tu ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge. Aidha, Ofisi ya Rais – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma - Fungu 33 walipata asilimia 19.94 ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo ya upatikanajiwa fedha katika taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais haiakisi uwezekeno wa mafanikio katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwamfano, Tume ya Mipango iliyotekeliza miradi mitatu (3)muhimu ilipata asilimia 2.99 tu za bajetiyake ya kugharamia miradi hiyoiliyoidhinishwa na Bunge. Miradi hiyo ni;-

- i) *Pro - Poor Economic Growth and Environmentally Sustainable Development, Miradi Namba 4940*
- ii) Kujenga uwezo wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo **Miradi Namba 4941**
- iii) *Population Planning (Masuala ya Idadi ya watu, Miradi Namba 6526*

**Mheshimiwa Spika**, Mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo ni wa mashaka makubwa katika kufanikisha malengo mazuri yaliyopangwa. Si vizuri kwa miradi muhimu kama hiyo ya Tume ya Mipango kutopewa uzito unaofaa na kupatiwa fedha kama inavyoidhinishwa na Bunge. Aidha, ingawa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri imeongoza katika kufanikiwa kupata kiasi kikubwa cha fedha zilizoidhinishwa, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilikuwa ya pili katika taasisi za Ofisi hii kwa kupata kiasi kidogo cha fedha za miradi ya Maendeleo kutokana na kupata asilimia 19.94 ya bajeti yake iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kufanya ulinganifu wa namna taasisi chini ya Ofisi hii zilivyowezeshwa kupata fedha za miradi ya maendeleo, Kamati inabainisha ulinganifu huo katika chati Namba 01 ya Taarifa hii.

**Chati Namba 01: Mtirisko wa Kiwango cha fedha zilizopatikana ikilinganishwa na Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**

**Chanzo: Ukokotozi kutoka Maelezo yaliyowasilishwa kwenye kikao cha Kamati cha tarehe 02 Mei, 2015**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati imebaini kuwa licha ya miradi ya maendeleo kutengewa fedha kidogo upatikanaji wa fedha umekuwa ni tatizo kubwa wakati wa utekelezaji na kusababisha utekelezaji hafifu wa malengo ya Miradi ya Maendeleo.Naomba nitoe mifano michache inayoonesha udhaifu mkubwa wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**i) Utekelezaji wa Miradi chini ya Fungu Fungu 66: Tume ya Mipango**

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Mipango ilitengewa Jumla ya shilingi **4,889,889,000/=** Kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2015, Tume hii ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **146,370,000/-** zote zikiwa nifedha za nje. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 2.99 ya fedha ilizoidhinishiwa kutumika kwa Miradi ya maendeleo. Hali hii imeikumba Taasisi muhimu katika Mipango na utekelezaji wa mambo mbalimbali kwa maendeleo ya nchi hii.

**ii) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ulitengewa jumla ya kiasi cha Shilingi bilioni**18.5**, lakini hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2015, TASAFilikuwa imepokea Jumla ya Shilingi **Bilioni 3** tu ya fedha za ndani sawa na asilimia **16.6** ya fedha zilizoidhinishwa. Ni wazi kuwa pamoja na malengo mazuri ya mfuko huo na umuhimu wake katika ustawi na maendeleo ya jamii, si rahisi kufanikisha dira, dhamira na malengo yake. Ni vema serikali ikazingatia kuwa mipango mizuri haina maana pasipo kutekelezwa, na utekelezaji wa mipango unategemea upatikanaji wa fedha.

**3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015Kamati yangu ilitoamaoni na

ushauri katika jumla ya mambo thelathini na tano. Ushauri huoulilenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa Majukumu katika Ofisi hii. Kamati ilitaka kujiridhisha ni kwa kiasi gani maoni na ushauri wake ulizingatiwa na Serikali kwa kufanya uchambuzi wa Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na serikali ambapo kati ya mambo 35 yaliyopendekezwa, 19 sawa na asilimia 54.3% yamezingatiwa na Serikali. Aidha maoni 8 kati ya 35 sawa na 22.8% yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na maoni 8 sawa na 22.8 % hayakizingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba uniruhusu kutoa mifano ya baadhi ya maoni yaliyotekelvezwa, yaliyo katika hatua ya utekelezaji na ambayo hayakutekelezwa. Mfano wa ushauri uliozingatiwa na serikali ni kuhusumikutano baina ya viongozi wa dinimbalimbali na vyama vya siasa yenye lengo la kudumisha mshikamano, umoja, amani, utulivu, upendo na uzalendo wetu kama watanzania katika mikoa na wilaya zote nchini. Kamati ilitoa ushauri huo kutokana na kuwepo kwa viashiria vya kutoweza kwa amani na utulivu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Maelezo ya serikali yanaonesha kwamba Serikali ilifanyamikutano sita (6) iliyohusisha Viongozi wa dini na vyama vya siasa katika mikoa ya Dares salaam, Mara na Tanga kwa lengo la kusisitiza zaidi amani, utulivu naupendo miongoni mwa watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano mwagine ni ushauri wa Kamati kuhusu Sekretarieti ya Ajira nchini kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam weledi na kuwapa orodha hiyo waajiri. Taarifa ya serikali imeonesha kuwa Sekretarieti ya Ajira nchini imeimarisha kanzidata (Database) ya waombaji kazi wenye ujuzi wanaotakiwa na waajiri mbalimbali. Aidha, kuanzia Mwezi Julai 2014 hadi Mwezi Machi, 2015 Sekretarieti imewapangia waajiriwa wapya 1,274 waliokuwepo kwenye kanzidata(database) kwa waajiri 146 sanjari na kuboresha orodha ya wahitimu wapatao 47,073 toka vyuo 23 vilivyowasilisha orodha hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Mbali ya Ushauri uliozingatiwa, upo ushauri ambaa haukizingatiwa. Kwa mfano, Kamati ilishauri kwamba Serikali itenge fedha za kutosha na kutoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya kujenga jengo la Ofisi za Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika ili kulinda heshima ya nchi yetu kwa kutimiza ahadi tunazozitoa kama nchi mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Maelezo ya serikali yanaonesha kuwa ushauri huu haukizingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano mwagine wa kutozingatiwa kwa ushauri ni Kamati iliposhauri kuhusu kujengeauwezo Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania(MKURABITA) kwa kuutengea fedha za kutosha ili uweze kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi katika wilaya zote nchini hususan wilaya za mpakani. Maelezo ya mtoa hoja hayaoneshi jinsi Serikali ilivyozingatia ipasavyo zaidi ya kutambua umuhimu wa MKURABITA.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ushauri unaoendelea kuzingatiwa, Kamati ilishauri kuhusu kufufuliwa kwa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) kwa kuongezewa fedha. Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kuwa ushauri huu umezingatiwa katika mpango mkakati wa miaka mitano na kwamba Serikali imekusudia kuongeza fedha na kuzitoa kwa wakati ili kunwanufaisha walenga wa Mfuko. Kamati ina maoni kuwa azma hii ya Serikali inapaswa kusimamiwa ipasavyo na kutekelezwa bila kusita.

#### **4.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jukumu lake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane, Kamati ilifuatilia kwa karibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizotekelvezwa na taasisi za Ofisi

ya Rais kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa sehemu kubwa ya majukumu ya kawaida yaliyopangwa kutekelezwa imeweza kufikia kiwango kilichotarajiwa kwa kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika**, mifano ya majukumu yaliyopangwa na kutekelezwa hadi tarehe 30 Machi, 2015 ipo ya kutosha. Kutaja baadhi, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Ofisi ya Rais, Ufuatilaji wa Utekelezaji wa Miradi imeweza kufanikisha upembuzi wa mahitaji ya mageuzi ili kuboresha huduma za afya kuitia Maabara Maalum ya Huduma za Afya. Aidha, Maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yameonesha kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika mwaka wa fedha 2014/2015 imeweza kufungua kesi mpya 161 zikiwemo kesi nane (8) zilizotokana na uchunguzi maalum wa vocha za Pembejeo za kilimo, kesi tatu (3) zinazohusu maliasili ya nchi na kesi tisa (9) zilizotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwingine muhimu wa malengo ya bajeti kwa mwaka 2014/2015 yaliyotekelzeza ni kuhusu malengo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), iliyo katika Awamu ya Tatu inayohusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Kamati ilijulishwa kuwa jumla ya shilingi Bilioni 42 zimelipwa kama ruzuku ya kunusuru kaya maskini zipatazo 266,601 katika vipindi vya mizunguko 8 ya malipo katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji 40, zikiwemo Halmashauri 38 Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba.

## 5.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 5.1 Malengo yaliyowekwa

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kuitia malengo ya Bajeti kwa Ofisi ya Rais na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii, Kamati ilizingatia uwepo wa Fungu (Vote) jipya, Fungu 04 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa na kuitia malengo yake pamoja na malengo ya mafungu mengine. Kilichojoitokeza katika mapitio hayo, ni ukweli kuwa sehemu kubwa ya malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 inahusu majukumu ya kawaida kamailivyo kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Kwa mfano, mpango wa kuendelea na mchakato wa uanzishwaji wa Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya nchini si mpya katika mwaka wa fedha 2015/2016. Kamati inaafiki mipango iliyowekwa na kusitiza kuwa utekelezaji wake unapaswa kusimamiwa na kuhakikisha kuwa bajeti kwa ajili ya shughuli hizo inazingatiwa kwa kuwezesha uhakika wa upatikanaji wa fedha.

### 5.2 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa yanawiana na Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo katika bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, ili kubaini mwenendo wa kibajeti kwa miaka miwili kuanziamwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2015/2016, Kamati ilitumia ulinganishaji wa makadirio hayo kwa kila fungu mionganoni mwa mafungu kumi ya Taasisi zilizochini ya Ofisi ya Rais.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla katika ulinganishaji huo, Kamati ilibaini kuwabajeti za Mafungu matano zitaongezeka ambapo bajeti katika Fungu 20 – Ikulu itaongoza kwa

ongezeko la asilimia 117.82 ikifuatiwa na Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ongezeko la asilimia 25.94. Wakati mafungu hayo yakiwa na ongezeko, bajeti ya mafungu matano itapungua kwaasilima 41.01. Bajeti itakayopungua zaidi ni Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Miradi, Fungu 06 inayopungua kwa silimia 41.01. Muonekano wa mwelekeo huo unaoneshwa katika chati Na. 02 ya Taarifa hii.

**Chati Na. 02: Muonekano wa tofauti ya Ongezeko la Bajeti kwa kila fungu ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015**

**Chanzo: Kutokana na Maelezo ya Serikali yaliyotolewa kwenye Kikao cha Kamati cha tarehe 02 Mei, 2015**

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya matumizi kwa ajili ya Ofisi ya Rais na taasisi zilizo chini yake yanaonesha kuwa mafungu manne hayakukadiriwa kuwa bajeti ya kugharamia miradi ya maendeneo. Mafungu hayo ni:

Fungu 20 - Ofisi ya Rais Ikulu; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma na Fungu 09 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

Aidha, Mafungu sita yamekadiriwa kuwa na matumizi ya kugharamia miradi ya Maendeleo. Mafungu hayo ni: Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; Fungu 32- Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Fungu 33- Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Fungu66- Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango; Fungu 06 - Ofisi ya Rais, Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Miradi na Fungu 04- Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ililinganisha kiasi cha Makadirio ya kugharamia miradi ya Maendeleo na jumla ya bajeti kwa kila fungu ili kuwianisha shughuli za kawaida na miradi iliyopangwa.Uchambuzi wa Kamati umebainishakuwa kuna tofauti kubwa ya uwiano huo katika Mafungu ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais. Kwa mfano, wakati Ofisi ya Rais, Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Miradi,Fungu 06 ukiwa na Bajeti ya Maendeleo ambayo ni asilimia 70.5 ya Bajeti yake, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Fungu 04, imekadiria bajeti ya miradi ya Maendeleo ambayo ni asilimia 16.82 ya Bajeti yake.

**Mheshimiwa Spika**, ili kudhihirisha uwiano huo na tofauti yake kwa kila Fungu, Chati Na. 03 ya taarifa hii inaonesha sura nzima ya uwiano huo.

**Chati Na. 03: Muonekano wa uwiano kati ya bajeti ya miradi ya maendeleo na Bajeti nzima ya kila Fungu liliopangiwa fedha za miradi hiyo.**

**Chanzo:Ukokotozi kutokana naTaarifa ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rasi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliyowasilishwa kwenye Kamati tarehe 02 Mei, 2015**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa mwelekeo wa makadirio ya Matumizi katika taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais umezingatia uzoefu wa uwezekano wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, si lazima kwa kila taasisi ya serikali kuwa na Mradi wa kutekeleza. Kamati inatambua kuwa makadirio haya yamezingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika mwongozo wa taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

#### **6.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**,Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayotekelizwa na Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake.Hata hivyo ili kuboresha utekelezaji wa majukumu katika Ofisi hii, Kamati inaushauri kama ifuatavyo:

## 6.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2014/2015 inaonesha dhahiri kuwa kumekuwa na utekelezaji hafifu wa bajeti kwani utoaji wa fedha kutoka Hazina kwenda katika idara na taasisi zilizochini ya Ofisi ya Rais umekuwa si wa kuridhisha hali iliyosababisha baadhi ya majukumu yaliyopangwa kutotekelizwa. Kamati inashauri Serikali kuongeza juhudzi za kubuni vyanzo vipyta vya mapato na kusimamia kikamilifu vyanzo vya mapato vilivyopo ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuepuka kutegemea kutekeleza mipango ya bajeti yake kwa kutumia fedha za wahisani ambazo hazina uhakika.

## 6.2 Maoni Mahsus

### 6.2.1 Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri:Fungu 20 na 30

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri pamoja na mambo mengine inalo jukumu kubwa la kumsaidia na kumwezesha Rais kuweza kuongoza nchi vizuri kwa ufanisi na ustawi mkubwa. Ofisi hii ndiyo inayosimamia upatikanaji wa huduma kwa Rais na familia yake, kushughulikia ratiba ya kazi za Rais, na kutoa ushauri kwa Rais kuhusu masuala mbalimbali kama vile uchumi, sheria, jamii na siasa, kusimamia na kuimarisha utawala bora, uaadilifu na uwajibikaji pamoja na masuala ya utumishi, tuzo zataifa, ajira, rufaa za watumishi wa Umma zinazowasilishwa kwa Rais na kwa Katibu Mkuu kiongozi, kuchambua na kushauri kuhusu rasimu za miswada mbalimbali ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu ya ofisi hiyo ambayo ni dira na taswira ya nchi, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo ili kuboresha utekelezaji na utendaji wa ofisi hii; -

(i) Serikali iendelee kuwajengea uwezo Wajumbe na Sekretarieti ya Baraza la Mawazirika kuwapatia mafunzo stahiki ili waweze kutekeleza majukumu yao ikiwemo kutoa ushauri kwa Rais ili kumwezesha kuongoza nchi vizuri na kwa ufanisi.

(ii) Kwa kuwa Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa wa awamu ya Tatu umekamilika na unashubiri Maamuzi ya Serikali, ni vema Serikali ikaharakisha kutoa maamuzi hayo ili uanze kutekelezwa katika kipindi cha kuanzia Mwaka wa fedha 2015/2016. Aidhakatika kuutekeleza Mkakati huo, Serikali ishirikishe kikamilifu wadau kutoka katika Sekta ya Umma na Sekta binafsi ili kuhakikisha kuwa jamii kwa ujumla inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maudhui na dhima ya mkakati huo katika mapambano dhidi ya Rushwa.

(iii) Kufuatia ziara ya Kamati iliyofanyika Mwezi Julai, 2014 katika Ikulu ndogo ya Chamwino na kujionea hali mbaya ya majengo ya pamoja na Nyumba kumi za Watumisi wa Ofisi hiyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zote zitakazotengwa kwa ajili ya ukarabati zinatolewa kama iliyopangwa na kwa wakati ili majengo hayo yakarabatiwe. Aidha, Serikali ihakikishe inatoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa Ikulu ndogo za Mbeya na Zanzibar ili kuhakikisha kuwa Ikulu hizo zinakarabatiwa.

### 6.2.2 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeanzishwa na kupewa majukumu kwa Mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007. Taasisi hii ni muhimu katika kuimarisha utawala bora nchini unaofuata misingi ya usawa na utawala wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majukumu makubwa ya Taasisi hii na ikitiliwa maanani kuwa katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia vitendo vya rushwa vimekuwa vikiongezeka na watusika kutumia mbinu mbalimbali na za kisasa zaidi na hivyo kuathiri utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuimarisha utawala bora unaofuata misingi ya sheria.

Aidha, kwa kuwa Mwaka huu ni Mwaka wa Uchaguzi Mkuu ambapo uzoefu unaonesha kuwa vitendo vya rushwa huongezeka kwa kasikatika kipindi hicho, ni dhahir kuwataasisi hii itakuwa na kazi kubwa ya kudhibiti vitendo hivyo na kuhakikisha kuwa mchakato wa uchaguzi unafanyikakwa haki, amani na utulivu. Ili kuimarisha ufanisi wa taasisi hii katika kukabiliana na vitendo vya rushwa, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kamati inashauri kuwa TAKUKURU iwezeshe kikamilifu kwa kuipatia nyenzo, rasilimali watu wenye weledi na kuitengea bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleza jukumu lake kwa ufanisi. Katika kudhibiti vitendo vya Rushwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi Mkuu.

(ii) TAKUKURU ichukue hatua madhubuti za kupambana na rushwa ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu athari za rushwa kwa jamii na hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi Mkuu.

(iii) TAKUKURU itoe mafunzo maalum mapema kwa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu kuhusu Sheria Na. 11 ya 2007 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa pamoja na Sheria Na. 6 ya 2010 ya Gharamaza Uchaguzi ili kuhakikisha kuwa Mhimili wa Mahakama unaimarishwa kikamilifu kuhusiana utoaji haki katika masuala yanayohusu Sheria ya Uchaguzi na Sheria ya garama za uchaguzi.

(iv) TAKUKURU iongeze nguvu katika kufanya uchunguzi Maalum wa tuhuma za rushwa katika vocha za pembejeo za kilimo, maliasili pamoja na kukamilisha uchunguzi kuhusu Sakata la Akaanti ya TEGETA ESCROW ili watakaobainika wafkishwe Mahakamani mapema iwezekanavyo kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki inatendeka.

#### **6.2.3 Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute)**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) ilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali wa Kiafrika ili kuimarisha utawala bora katika nchi zao na kusaidia kuleta maendeleo endelevu katika nchi zao. Chuo hiki kilianzishwa baada ya kutambua kuwa uongozi bora ndiyo chachu ya maendeleo katika nchi yoyote duniani. Aidha, taasisi hii inatambua kuwa viongozi wazuri wanatakiwa kuandaliwa na kulelewa ili waweze kutoa uongozi mzuri katika nchi au taasisi zozote watakazoziongoza.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi hii katika mwaka wa fedha 2015/2016 imepanga kuendelea kutoa kozi mbalimbali za uongozi zitakazohusu mkakati wa uongozi kwa maendeleo endelevu, ufanisi katika usimamizi wa sekta ya Umma, kutafakari matokeo ya Uongozi na kuchukua hatua na stadi za majadiliano na kufanya mahojiano na Wakuu wa Nchi walioko, madarakani na wastaa fu ili kukuza uelewa na kupata uzoefu kutoka kwa viongozi hao.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kuwa Taasisi ya Uongozi inatimizamajukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo:

(i) Kutohakikisha kuwa Taasisi ya Uongozi inatimizamajukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kutohakikisha kuwa Taasisi ya Uongozi inatimizamajukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo:-

majengo yake ya utawala, hotel na viwanja vya michezo katika kijiji cha Kondo katika wilaya ya Bagamoyo.

(ii) Serikali ihamasishhe Wizara, Idara na Wakala mbalimbali wa Serikali kutenga bajeti ili kupeleka Watendaji wake walioko katika ngazi za maamuzi kwenye chuo cha uongozi kwa lengo la kuwapatia mafunzo yanayoandalishi na taasisi hii ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma.

(iii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kikitangaza chuo cha Uongozi ili kifahamike ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu ili Viongozi mbalimbali na viongozi watarajiwa waweze kujunga na chuo na kunufaika na mafunzo yanayotolewa na chuo hicho.

(iv) Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na changamoto kubwa ya kuporomoka kwa maadili ya viongozi wa Umma, ni vyema chuo hiki kikaingiza mtaala wa maadili ya viongozi ili kuwezesha viongozi wanaopitia katika chuo hicho kuzingatia maadili katika nafasi zozote watakazokuwa wakizitumikia.

#### **6.2.4 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (Mkurabita)**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania ulianzishwa Mwaka 2004 ili kuwezesha urasimishaji wa mali na biashara za wanyonge kwa lengo la kuwainua kiuchumi na kuwaondoa katika dimbwi la umasikini. Pamoja na kwamba mpango umetimiza miaka kumi na moja tokea kuanzishwa kwake, bado malengo yake hayajafanyiwa kazi kiasi cha kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Ili Mpango huu muhimu uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati yangu iona maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa Mpango huu unawezeshwa kikamilifu kifedha kwa kutengewa bajeti ya kutosha ili kutekeleza jukumu liliokusudiwa katika uanzishwaji wake na kuwanufaisha wananchi wa Tanzania.

(ii) MKURABITA iongeze kasi ya upimaji wa ardhi katika maeneo mbalimbali vijijini na mijini na kutoa hati miliki ili kuongeza thamani ya ardhi ,kuepusha migogoro ya ardhi na kuwawezesha wananchi kukopa katika taasisi mbalimbali za kifedha kwa kutumia dhamana ya hati miliki hizo kwa lengo la kuwawezesha kujikwamua na umasikini kwa kutumia hati za kimila.

(iii) Kwa kuwa benki nyingi nchini zinasita kupokea hati za kimila kama dhamana ya mikopo, ni vyema Serikali ikachukua hatua madhubuti ya kuzielimishataasisi zakibenki nchini kuhusu uhalali wa hati za kimila kutumika katika dhamana ya mikopo.

#### **6.2.5 Ofisi Ya Rais, Menejimenti Ya Utumishi Wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepewa jukumu kubwa la kuimarishautawala bora katika uendeshaji wa shughuli za serikali kwa kubuni sera, sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za utumishi wa umma na kujenga uwezo wa watumishi wa umma iliwaweze kutoa huduma bora kwa wadau wake.

**Mheshimiwa Spika**, watumishi wa umma ambao wanasimamiwa na Ofisi hii ndio wanaofanya kazi ya kuutumikia umma siku hadi siku. Kwa msingi huo Ofisi hii inahitaji kuimarishwa kikamilifu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa lengo la kuwezesha Utumishi wa

umma kutoa huduma bora zitakazochangia kuleta mafanikio kwa Taifa. Hivyo basi, Kamati yangu inashauri ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ijengewe uwezo wa kifedha kwa utengewa bajeti ya kutosha pamoja na kupewa Rasilimaliwatu wa kutosha na wenyewe weledi unaostahili.

(ii) Kamati inashauri Serikali iongeze jitihada za kuimarisha wakala wa mafunzo kwa njia ya mtando ili utekeleze jukumu lake la kuwajengea uwezo watumishi wa umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kwa lengo la kuwawezesha kuhimili kasi ya mabadilio ya sayansi na teknolojia.

(iii) Kamati inatambua umuhimu wa wakala wa serikali mtando wenyewe mamlaka ya kuratibu,kusimamia na kukuza jitihada za Serikali mtando katika utumishi wa umma kwa kusimamia mifumo ya mawasiliano iliyo salama serikalini. Hivyo basi Kamati inashauri watendaji wa wakala huu wapewe mafunzo stahikiili waweze kuongeza kasi ya utoaji elimu kuhusu Serikali mtando kwa lengo la kudhibiti matumizi mabaya ya mawasiliano.

#### 6.2.6 Tume ya Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Umma ina mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.Katika kutekeleza jukumu hili Tume ina wajibu wa kuhakikisha waajiri,waajiriwa,mamlaka za ajira na nidhamu zinazingatia sheria,kanuni na taratibu katika kusimamia masuala yanayohusu Rasilimaliwatu pamoja na kushugulikia kwa wakati rufaa na malalamiko.ili kuboresha utekelezaji wa Tume hii na kuiweshera kufikia azma ya Dira yake ambayo ni kuwa mfano wa kuigwa,Kamati inashauri yafutayo:-

i) Tume ya utumishi wa Umma iendelee kutoa elimu kwa watumishi wa Umma kuhusu maadili ya utumishi wa Umma ili kuepuka kutumia madaraka yao vibaya katika kuwatumikia wananchi.

ii) Tume inapopokea rufaa kutoka kwa Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika kutohakana nahatua zilizochukuliwa na mamlaka za nidhamu iharakishe kusikiliza rufaa hizo ili kuhakikisha haki inatendeka kwa wakati.

#### 6.2.7 Bodi ya Mishahara na Maslahi Katika Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma ni chombo kiilichoanzishwa kwa Tamko la Rais kuitia Tangazo la Serikali Na.162 la tarehe 3 Juni,2011.Uanzishwaji wa Bodi ni utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume mbalimbali zilizoishauri Serikali namna ya kuboresha mishahara katika Utumishi wa Umma pamoja na utekelezaji wa Sera ya Mishahara na motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010.

**Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma imepewa jukumu mahsusila kufanya mapitio ya Mishahara pamoja na miundo ya Mishahara, viwango vya posho na mafao katika utumishi wa Umma na kumshauri Rais kuhusiana na mapitio hayo.Kamati inatambua na kuthamini kazi nzuri inayofanywa na Bodi hii katika kuboresha maslahi ya watumishi wa umma nchini kwa kadri uchumi wan chi unavyoruhusu,hata hivyo Kamati yangu inashauri kuwa Serikali iendelee kuiweshera Bodi ya mishahara kifedha ili iweze

kukamilisha Mwongozo wa kuzingatia wakati wa kupanga mishahara na maslahi katika utumishi wa umma na kuusambaza kwa lengo la kuwezesha taasisi za Umma kuutumia na kuwianishamishaharakatika Utumishi wa Umma na kuondoa tofauti isiyi ya lazima ya viwango vya mishahara katika utumishi wa umma.

#### **6.2.8 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Fungu 33**

**Mheshimiwa Spika,** Sekretarieti ya maadili ya viongozi wa Umma ilianzishwa ili kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Viongozi wa Umma Na.13 ya mwaka 1995 kwa kuhakikisha kuwa tabia na mienendo ya Viongozi wa Umma inazingatia misingi ya maadili iliyooanishwa katika Sheria.Aidha Sekretarieti ina jukumu la kukuza na kusimamia misingi ya maadili Uongoziwa Umma nchini kwa kutoa elimu,kufanya uchunguzi na kuhakiki wa mali na madeni ya Viongozi wa Umma ili kukidhi dhima ya Utawala Bora kwa Maendeleo ya Taifa.Kamati inatambua kazi nzuri zinazofanywa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Pamoja na kazi hizo Kamati inashauri kama ifuatavyo:

- i) Taarifa ya Taasisi hii iliyotolewa mbele ya Kamati yangu wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu katika Ofisi ya Rais pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015,sanjari na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, inaonesha kuwa kwa Mwaka wa fedha 2014/2015 Taasisi ilitengewa fedha za ndani kwa ajili ya miradi kiasi cha Shilingi 1,500,000,000.lakini hadi kufikia Machi 2015 hakuna kiasi chochote cha Fedha za ndani. Hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali itenge bajeti ya kutosha na kutoa fedha zinazotengwa kwa wakati ili kuiwezesha Taasisi hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hasa fedha za miradi ya maendeleo.
- ii) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma iharakishe kukamilisha Mwongozo wa maadili ya Viongozi wa Umma ili kuwezesha viongozi Viongozi wa Umma wa ngazi mbalimbali waweze kuufuata ili kuepuka ukikwaji wa maadili ya viongozi wa Umma.
- iii) Serikali ihakikishe fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za makao makuu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ili kupunguza gharama za pango la Ofisi.

#### **6.2.9 Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango: Fungu 66**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Mipango ilianzishwa katika Ofisi ya Rais ikiwa na majukumu ya msingi ya kutoa dira na mwongozo wa uchumi wa Taifa,kubuni sera za uchumi,mikakati na mipango ya maendeleo ya Taifa, kusimamia uchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii.Tume ya mipango ndio nguzo kuu ya ustawi wa taifa lolote kwani hakuna nchi yoyote ilioendelea duniani bila kuwa na mipango ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**Katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume ya Mipango ilikabiliwa na Changamoto ya kutopata fedha ya kutosha na kwa wakati hali ilioathiri mipango ya utekelezaji.Aidha Maendeo mengi ya miradi ya maendeleo haina hati miliki hususani viwanja vya bandari na viwanja vya ndege ambapo wananchi huvamia maeneo hayo na kusababasha migogoro hivyo kuathiri uwekezaji.Ili kuimarisha utendaji kazi wa Tume ya Mipango, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- (i) Kwa kuwa mipango yote ya maendeleo inapangwa na kusimamiwa na Tume ya mipango, ni vyema tume hii ijengewe uwezo kwa kutengewa fedha na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha Kamati inashauri fedha zilizotengea kwa ajili ya

miradi ya maendeleo jumla ya shilingi 3,814,670,000/= zitolewe zote kabla ya mwaka wa fedha 2014/2015 kuisha ili Tume iweze kutekeleza miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imepanga.

(ii) Kwa kuwa Tume ya Mipango ndiyo kituo mahsusini cha fikra rejea na ushauri kwa Serikali kuhusu mikakati ya maendeleo ya Taifa, Kamati inashauri Serikali itilie maanani suala la kuwajengea uwezo kielimu watumishi wa Taasisi hii ili waweze kutumia weledi huo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa ustawi na ushamiri wa maendeleo ya Taifa letu.

(iii) Kwa kuwa mpango wa maendeleo ya Taifa wa miaka mitano wa 2011/2012-2015/2016 una kamiliika na Serikali kupitia Tume ya Mipango inaandaa Mpango wa pili wa maendeleo ya Taifa wa 2016/2017-2020/2021, Kamati inashauri Serikali ifanyie tathimini ya mpango wa miaka mitano unaoisha ili kubaini mapungufu yaliyojitekeza katika mpango huo na kuyafanya kazi kikamilifu katika mpango wa pili. Aidha katika mpango wa maendeleo ya Taifa wa 2016/2017-2020/2021 Serikali izingatie katika kukuza uchumi wa wananchi wa kawaida ili kuhakikisha kuwa wananaufaika ipasavyo na rasilimali za nchi yao.

#### **6.2.10 Ofisi ya Rais-Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi: Fungu 6**

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (President's Delivery Bureau) ni taasisi ilioanzishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kupitia Tangazo la Serikali Namba 152 la Mwaka 2013 liilotolewa chini ya Sheria ya Mawaziri (Utekelezaji wa Majukumu ya Mawaziri) Sura ya 299 ya Sheria za Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la kuanzishwa kwa taasisi hii ni kuhakikisha miradi ya kipaumbele chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now) inatekelezwa kwa ufanisi na matokeo tarajiwa yanapatikana. Ili kuimarisha utendaji wa taasisi hii, Kamati yangu inashauri kama ifuatavyo;

(i) Serikali iendelee Kuiimarisha Idara ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi kifedha na kirasilimaliwatu ili iweze kufuatilia kwa karibu Miradi ya Kipaumbele na kuiwezesha Nchi yetu kupiga hatua za haraka za kimaendeleo kijamii, kiuchumi na kisiasa.

(ii) Idara ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi izijengee uwezo kwa kutoa elimu kwa Wizara, Mikoa na Idara mbalimbali za Serikali ili ziweze kuelewa kwa ufasaha maeneo ya kipaumbele na kuzisaidia kubainisha mikakati mahsusini ya kutekeleza kwa lengo la kupata Matokeo Makubwa kwa haraka zaidi.

(iii) Serikali kwa Kushirikiana na Idara ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi ipanue wigo wa maeneo ya Vipaumbele kwa kuingiza suala la Ardhi kwani Ardhi ni rarilimali muhimu sana katika maendeleo na ustawi wa taifa. Ni dhahiri kuwa hakuna maendeleo yoyote yanayoweza kufanyika bila kuwepo kwa ardhi.

(iv) Idara ii simamie kwa karibu Wizara ya Fedha ili kuisukuma katika kuoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ili kuwezesha taasisi husika kutekeleza miradi hiyo kama inavyopangwa.

(v) Serikali kupitia taasisi hii iimarishe Mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za miradi ya maendeleo iliyo katika maeneo ya Vipaumbele ili kuwa na takwimu sahihi zitakazowesha Serikali kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazoikabili miradi hiyo.

(vi) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wadau kuhusu mfumo wa utekelezaji wa miradi ya vipaumbele ili kwawezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi husika na kuepuka migogoro kati ya Serikali na wadau katika utekelezaji wake.

#### **6.2.11 Ofisi ya Rais:Idara ya Kumbukumbu na nyaraka za Taifa: Fungu 4**

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nyaraka za Taifa 3 ya Mwaka 2002 iliyotungwa ili kufuta Sheria Na. 33 pamoja na marekebisho yake. Jukumu kubwa la Idara hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Kanuni na taratibu zote za utunzaji wa Kumbukumbu na nyaraka za Taifa. Vile vile Idara hii imeundwa ili kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 18 ya Mwaka 2004 ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la kuhifadhi kumbukumbu muhimu ni ni suala muhimu kwa taifa lolote duniani.Kumbukumbu husaidia taifa liweze kuendeleakwa kujitathmini kupitia historia yake mahali lilikutoka na kusahihisha makosa lililowahi kuyafanya, mahali lilipo na mahali linakotarajia kwendalli kuboresha uanzishwaji na utendaji wa Idara hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo;

(i) Serikali iijengee uwezo wa kifedha na kirasilimaliwatu na nyenzo za kisasa ili kuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa.

(ii) Serikali kupitia idara hii iweke mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa nyaraka zote muhimu za taifa kutoka katika taasisi mbalimbali na kuzitunza kwa namna ambayo hazitaweza kuharibiwa wala kutumiwa vibaya.

(iii) Serikali kupitia idara hii na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iandae mfumo mzuri wa kuwaenzi waasisi wa taifa letu kupita usomaji wa nyaraka mbalimbali walizowahi kuziandika wakati wa uhai wao.

(iv) Serikali itoe fedha zitakazotengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa kituo cha kuwaenzi waasisi wa taifa kwa wakati ili kuwezesha ujenzi wa kituo hicho kuanza mapema iwezekanavyo.

#### **7.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**,kwa kuhitimisha, kwanza, napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa katika kipindi chote cha awamu mbili mfululizo kwa mafanikio makubwa na ustawi wa Taifa hili adhimu. Ni dhahiri kuwa nchi yetu imepiga hatua kubwa katika sekta zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa na kiutamaduni.

Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, tunakupongeza kwa busara zako katika kuliongoza Bunge letu Tukufu lenye changamoto nyingi hasa katika kipindi hiki.

**Mheshimiwa Spika**, tatu, napenda kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Celina O. Kombani (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, na Mheshimiwa Marry Michael Nagu (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu kwa Ushirikiano Mzuri walioipatia Kamati katika utekelezaji wa Majukumu yake. Aidha Nawashukuru Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano waliooutoa wakati Kamati ilipochambua makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru kipekee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka 2015/2016.

Napenda kuwashukuru pia ushirikiano wa dhati walionipa katika kipindi chote ambacho nimekuwa kiongozi wao. Kutohana na ushirikiano na umoja uliokuwepo mionganini mwa wanakamati umeiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake kwa mafanikio makubwa nay a kujivunia. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1)	Mhe.Jasson Samson Rweikiza	-	Mwenyekiti
2)	Mhe. Gosbert Begumisa Blandes	-	M/Mwenyekiti
3)	Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb	-	Mjumbe
4)	Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	-	Mjumbe
5)	Mhe.William Mganga Ngeleja	-	Mjumbe
6)	Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb	-	Mjumbe
7)	Mhe. Halima J. Mdee, Mb	-	Mjumbe
8)	Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb	-	Mjumbe
9)	Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb	-	Mjumbe
10)	Mhe. Ali Hamis Seif, Mb	-	Mjumbe
11)	Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb	-	Mjumbe
12)	Mh. Abdallah Sharia Ameir, Mb	-	Mjumbe
13)	Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb	-	Mjumbe
14)	Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb	-	Mjumbe
15)	Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb	-	Mjumbe
16)	Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb	-	Mjumbe
17)	Mhe.Nyambari C.M.Nyangwine,Mb	-	Mjumbe
18)	Mhe. Ramadhan Haji Saleh, Mb	-	Mjumbe
19)	Mhe. Zahra Ali Hamad ,Mb	-	Mjumbe
20)	Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb	-	Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Ndg. Charles J. Mloka, mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Athumanji Hussein,Mkurugenzi msaidizi katika Idara ya Kamati,Ndugu Matamus Fungo na Maria Mdulugu, Makatibu wa Kamati na Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Mahusiano na Uratibu kama yalivowasilishwa na Mto Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA  
Mei, 2015**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS –  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, MHE. VINCENT JOSEPHAT NYERERE (MB), AKIWASILISHA  
BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
FEDHA KATIKA OFISI YA RAIS – MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA  
2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y MHE. VINCENT JOSEPHAT NYERERE – MSEMAJI MKUU WA  
KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kada ya utumishi wa umma hapa nchini ina changamoto nydingi, changamoto kubwa ni ile ya kufanya kazi kwa mazoea jambo ambalo limejirudisha nyuma sana maendeleo ya Taifa kutokana na tija ndogo katika utendaji. Kufanya kazi kwa mazoea kunaondoa ile dhana ya utendaji wa kitaalam na kutokana na hali hiyo Tanzania imeendelea kushuhudia majanga na maafa makubwa kutokana na utendaji usiozingatia utaaliam.

Watanzania wameshuhudia Watanzania wengi wakifariki katika hospitali za umma kutokana na kukata tamaa kwa wauguzi na madaktari, tumeona maghorofa yakiporomoka na barabara kuharibika kutokana na wakandarasi wazembe wanaopata zabuni kwa njia za kifisadi na rushwa, tumeshuhudia elimu yetu ikiporomoka kutokana na walimu na watumishi wengine wa umma wenye dhamana ya kusimamia elimu kukata tamaa na kutozingatia kanuni za utumishi wao. Jambo hili limechangiwa sana na Serikali iliyopewa dhamana ya kusimamia masuala haya kutojali umuhimu na mazingira ya kazi kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi na mazingira ya kazi kwa watumishi wa umma. Kwa miaka yote ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiwatetea watumishi wa umma katika nyanja mbalimbali lakini cha kusikitisha ni kwamba Serikali hii ya CCM inayojiiita siku mara zote imekuwa ikipuuza na kubeza mapendekezo haya mazuri yanayotolewa na Kambi ya Upinzani Bungeni. Miiongoni mwa masuala muhimu tuliyopendekeza na Serikali kuyapuuza ni kama ifuatavyo:-

Moja, kima cha chini cha mshahara. Kambi Rasmi ya Upinzani ilipiga kelele sana kuitaka Serikali kupandisha kima cha chini cha mshahara kufikia shilingi 315,000/= kwa mwezi lakini

Serikali imeamua kuziba masikio na mpaka sasa hajijatekeleza pendekezo hilo. Inashangaza kuona Serikali ikijigamba kuwa imepandisha kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 240,000/= hadi shilingi 265,000/= sawa na ongezeko la shilingi 25,000 tu.

Mheshimiwa Spika, hebu tuvae viatu vya hao watumishi wanaolipwa shilingi 265,000/- kwa mwezi tuone kama wanaweza kuishi kwa wiki moja tu na fedha kama hiyo. Tukumbuke watumishi hao wana familia, wanatakiwa kulipa kodi za nyumba, ada za shule kwa watoto wao na maisha mengine yanatakiwa kuendelea vilevile. Hivyo, kutopandisha kima cha chini cha mshahara wa watumishi kama tunavyopendekeza ni kutokuwa na utu. Sasa Kambi ya Upinzani Bungeni haishauri tena Serikali bali inawaahidi watumishi wote wa umma kwamba iwapo Upinzani utashika madaraka ya dola kupitia UKAWA katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2015, kima cha chini cha mshahara kitapandishwa na ngazi nyingine za mishahara kwa watumishi wa umma zitaboreshwana sana ili watumishi wawewe kukabiliana na changamoto za maisha, hivyo watumishi wa umma wakae mkao wa kula. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaraja na mishahara ya watumishi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitaka Serikali kushughulikia malalamiko ya watumishi wa umma ambao wanapandishwa madaraja bila mishahara yao kuboreshwa. Wengine hurekebishiwa mishahara lakini mishahara mipya hailipwi mpaka miaka miwili hadi mitatu ipite ndipo walipwe mishahara mipya. Watumishi wanaojiendeleza kielimu wanacheleweshwa kupandishwa madaraja hadi muda wa miaka mitatu na wakati mwininge hushushwa madaraja. Mpaka sasa malalamiko haya bado yapo na Serikali inaonekeana kushindwa kuyashughulikia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahidi watumishi wote wa umma kwamba iwapo Upinzani utachukuwa dola katika uchaguzi huu matatizo ya kutopandishwa madaraja na mishahara kwa wakati yatakuwa historia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao ya watumishi wa umma wanapostaifu. Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea malalamiko mengi ya watumishi wanaosumbuliwa sana katika kupata mafao yao. Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani kitendo cha Serikali kuwatumikisha watumishi na wanapostaifu inawanyanyapaa. Suala la kustaifu si jambo la ghafla au la dharura, hivyo kunatakiwa kuwe na utaratibu mzuri wa mafao kwa wakati ambapo mtumishi akistaifu apate mafao yake haraka iwezekanavyo. Kwa kuwa Serikali hii inafanya mzaha na maisha ya watumishi wake, Kambi ya Upinzani inawaahidi watumishi wote kwamba tukichukua madaraka, mambo haya yote yataweza kufanyiwa kazi ndani ya muda mfupi iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu. Walimu ni sehemu ya watumishi wa umma. Serikali hii ya CCM imekuwa ikiwatumia sana walimu katika shughuli zake mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia sensa za watu na makazi, uandikishaji wapiga kura, isipokuwa mwaka huu Serikali imewatosa walimu kuandikisha wapiga kura kwa kigezo kwamba hawana elimu ya kompyuta lakini baada ya kazi zote hizo, Serikali huwasahau Walimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitetea maslahi ya walimu hasa madai yao ya malimbikizo ya mishahara, posho za uhamisho na posho za mazingira magumu ya kazi lakini Serikali mara zote imekuwa ikitoa ahadi hewa za kulipa madai ya walimu. Mbaya zaidi kuna Walimu wanapata ajira lakini wanafanya kazi mpaka miezi sita hawajalipwa mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahidi walimu na watumishi wote kwamba tukichukua madaraka madai yote ya Walimu yatalipwa mara moja na huo utakuwa ndio mwisho wa kulimbikiza madeni kwa Walimu na watumishi wa umma wa kada zingine zote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma kushiriki katika masuala ya kisiasa. Serikali hii ya CCM imekuwa ikiwakataza na mara nyingine kuwatisha na kuwaadhibu watumishi wa umma wanaoshiriki katika mikutano ya kisiasa.

Kambi Rasmi ya Upinzani inawajulisha watumishi wa umma kwamba Sheria ya Utumishi wa Umma haikatazi watumishi kuhudhuria mikutano ya siasa isipokuwa kwa muda wa saa za kazi. Ni muhimu pia Serikali hii ya CCM ikatambua kwamba imeridhia Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika wa mwaka 2011 ambapo pamoja na mambo mengine mkataba huo unazisitiza nchi zilizoridhia mkataba huo kuwapa watumishi wake uhuru wa kujinga na vyama vya siasa na kushiriki katika shughuli za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili ya utumishi wa umma. Kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi ya Upinzani imelipigia kelele sana suala la ujisadi uliokithiri na matumizi mabaya ya madaraka miongoni mwa watumishi wa umma Serikalini. Wananchi watakumbuka ujisadi mkubwa na matumizi mabaya ya madaraka ya viongozi wa umma katika sakata la EPA, Richmond, wizi wa mabilioni ya fedha za umma katika Akaunti ya Tegeta Escrow na mengine yanayofanana na hayo. Katika matukio haya, Serikali hii ya CCM imeanguka mara nne kwa kwa kuvunjwa kwa Baraza la Mawaziri kutockana na ujisadi na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kelele zote za Kambi ya Upinzani na licha ya Maazimio ya Bunge lako katika masakata yote hayo kuelekeza hatua za kisheria na kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya waliohusika na masakata hayo, bado Serikali hii ya CCM imeendelea kuwa na shingo ngumu kutekeleza maazimio ya Bunge ya kuwachukulia hatua mafisadi na badala yake inajitahidi kuwakingia kifua mafisadi hawa.

Itakumbukwa kwamba hivi karibuni ikulu ya Rais imewasafisha baadhi ya watumishi wa sakata la Escrow kuwa hawatusiki na ujisadi huo. Ni vema pia wananchi wakatambua kwamba wakati Serikali inawatetea wezi wa fedha za umma ambazo zingeweza kutumika katika kusambaza huduma za maji, afya na elimu wakati huo inawakaba wananchi kuwachangisha fedha za maabara na fedha za matembezi ya Mwenge wa Uhuru na wananchi wanaoshindwa kutoa michango hiyo, wananyang'anywa mali zao na wengine kukamatwa na Polisi.

Kambi ya Upinzani inapenda kuwahakikishia umma wa Watanzania kwamba endapo Upinzani utaingia madarakani kupitia UKAWA katika uchuguzi mkuu wa Oktoba, 2015 utakuwa ndiyo ukomo wa rushwa na ujisadi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwatambua Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kama watumishi wa umma. Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni viongozi wanaochaguliwa na wananchi na wanatumia muda wao kuwatumikia wananchi. Kwa maana halisi hawa ni watumishi wa umma kwa kuwanatumikia umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya uhalsia huu, viongozi hawa hawatambuliwi kisheria kama watumishi wa umma na hivyo hawa jingizwa kwenye mfumo wa utumishi wa umma. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwatambua Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kama watumishi wa umma ili waweze kupata stahili zao kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 26.4 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 29.13 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.28 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa randama ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma hadi kufikia mwezi Machi, 2015, shilingi bilioni 25.8 sawa na asilimia 88.6 za matumizi ya kawaida zilikuwa zimeshatolewa lakini fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa katika kipindi hicho zilikuwa ni shilingi bilioni 2.1 tu sawa na asilimia 30.12 ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya maendeleo katika utumishi wa umma ni pamoja na kuboresha maendeleo ya rasilimali watu ambapo yanajumuisha kugharamia mafunzo kwa watumishi ili kuongeza weledi wao.

Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni kwa namna gani imeteketeleza Sera ya Maendeleo ya Rasilimali Watu katika utumishi wa umma ikiwa asilimia 70 ya bajeti ya maendeleo haikutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya CCM imekuwa imekuwa na mazoea ya kutotekeleza bajeti ya maendeleo siyo tu kwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma bali katika Wizara zingine pia.

Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi wote kuwa endapo Upinzani utaingia madarakani bajeti ya maendeleo katika Wizara zote na taasisi za Serikali itakuwa ikitekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzania Bungeni, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kuwasilisha. (Makofii)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS –  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, MHE. VINCENT JOSEPHAT NYERERE (MB), AKIWASILISHA  
BUNGENI MAONI YA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
FEDHA KATIKA OFISI YA RAIS – MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA  
2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awalili ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza viongozi wote wa UKAWA nikianza na Mwenyekiti wa UKAWA, Mhe. Freeman Aikaeli Mbewe (Mb) ambaye pia ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Wenyeviti wenza Waheshimiwa Prof. Ibrahim Lipumba (CUF), Dr. Emmanuel Makaidi (NLD) na James Mbatia (NCCR – Mageuzi); Makatibu wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA, Waheshimiwa Maalim Seif Shariff Hamad (CUF) ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zainzibar, Dr. Wilbroad Slaa(CHADEMA) , Mosena Nyambabe (NCCR – Mageuzi) na Tozi Matwange (NLD) kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwaunganisha watanzania katika harakati za kuleta mabadilko ya kweli ya kisiasa kwa mustakabali mwema wa tafa letu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwashukuru wapiga kura wangu kwa kuendelea kuniamini; na kwa kuwa maisha ya bunge yanaelekea ukingoni, ninawaomba nitakaporudi kwao kuwaomba kura katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu, wasiniangushe maana niliwatumikia kwa uaminifu.

## 2. HALI YA UTUMISHI WA UMMA NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Kada ya Utumishi wa umma hapa nchini ina changamoto nyingi. Changamoto kubwa ni ile ya kufanya kazi kwa mazoea (business as usual) jambo ambalo limerudisha nyuma sana maendeleo ya taifa kutokana na tija ndogo katika utendaji. Kufanya kazi kwa mazoea kunaondoa ile dhana ya utendaji wa kitaalamu (professionalism) na kutokana na hali hiyo, Tanzania imeendelea kushuhudia majanga na maafa makubwa kutokana na utendaji usiozingatia utaalamu. Watanzania wameshuhudia watanzania wengi wakifariki katika hospitali za umma kutokana na kukata tamaa kwa wauguzi na madaktari, tumeona maghorofa yakiporomoka na barabara kuharibika kutokana na wakandarasi wazembe wanaopata zabuni kwa njia za kifisadi na rushwa, tumeshuhudia elimu yetu ikiporomoka kutokana na waalimu na watumishi wengine wa umma wenye dhamana ya kusimamia elimu kukata tamaa na kutozingatia kanuni za utumishi wao. Jambo hili limechangiwa sana na Serikali iliyopewa dhamana ya kusimamia masuala haya kutojali umuhimu na mazingira ya kazi kwa watumishi .

## 3. MASLAHI NA MAZINGIRA YA KAZI KWA WATUMISHI WA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiwatetea watumishi wa umma katika nyanja mbalimbali lakini cha kusikitisha ni kwamba Serikali hii ya CCM inayojiiita sikivu mara zote imekuwa ikipuuza na kubeza mapendekezo mazuri yanayotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** mionganoni mwa masuala muhimu tuliyopendekeza na serikali kuyapuuza ni kama ifuatavyo:

### 1. *Kima cha Chini cha Mshahara:*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ilipiga kelele sana kuitaka Serikali kupandisha kima cha chini cha mshahara kufikia shilingi 315, 000/= kwa mwezi lakini Serikali imeamua kuziba masikio na mpaka sasa haijatekeleza pendekezo hilo. Inashangaza sana kuona Serikali ikijigamba kuwa imepandisha kima cha chini cha mshahara kutoka shilingi 240,000/= hadi shilingi 265,000/= sawa na ongezeko la shilingi 25,000 tu.

**Mheshimiwa Spika,** hebu tuvae viatu vya hao watumishi wanaolipwa shilingi 265,000/- kwa mwezi tuone kama tunaweza kuishi kwa wiki moja tu na fedha kama hiyo. Tukumbuke watumishi hao wana familia, wanatakiwa kulipa kodi za nyumba, ada za shule kwa watoto wao na maisha mengine yanatakiwa kuendelea vilevile. Hivyo kutopandisha kima cha chini cha mshahara wa watumishi kama tunavyopendekeza ni kutokuwa na utu. Sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haishauri tena serikali bali inawaahidi watumishi wote wa umma kwamba; iwapo Upinzani utashika madaraka ya Dola kuitia UKAWA katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu wa 2015, kima cha chini cha mshahara kitapandishwa, na ngazi nyingine za mishahara kwa watumishi wa umma zitaboreshwaa sana ili watumishi waweeze kukabiliana na changamoto za maisha; hivyo watumishi wa umma wakae mkao wa kula.

### 2. *Madaraja na Mishahara ya Watumishi:*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni illitaka Serikali kushughulikia malalamiko ya watumishi wa umma ambao wanapandishwa madaraja bila mishahara yao kuboreshwa; wengine hurekebishiwa mishahara lakini mishahara mipyä hailipwi mpaka miaka miwili hadi mitatu ipite ndipo walipwe mishahara mipyä; watumishi wanaojiedeleza kielimu wanacheleweshwa kupandishwa madaraja hadi muda wa miaka mitatu na wakati mwingine hushushwa madaraji. Mpaka sasa malalamiko haya bado yapo na Serikali inaonekeana

kushindwa kuyashughulikia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahdi watumishi wote wa umma kwamba iwapo Upinzani utachukuwa mamlaka ya Dola kuititia UKAWA katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015 matatizo ya kutopandishwa madaraja na mishahara kwa wakati yatakuwa historia.

### **3. Mafao ya Watumishi wa Umma wanapostaafu.**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea malalamiko mengi ya watumishi wastaafu wanaosumbuliwa sana katika kupata mafao yao. Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani kitendo cha Serikali kuwatumikisha watumishi na wanapostaafu inawanyanyapaa. Suala la kustaafu si jambo la ghafla au la dharura; hivyo kunatakiwa kuwe na utaratibu mzuri wa mafao kwa wakati (timely pension scheme) ambapo mtumishi akistaafu apate mafao yake haraka iwezekanavyo. Kwa kuwa Serikali hii inafanya mzaha na maisha ya watumishi wake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahidi watumishi wote wa umma kwamba ikiwa Upinzani utatwaa madaraka ya Dola katika uchaguzi wa Oktoba 2015, basi Serikali ya UKAWA itaweka skimu ya mafao ya wastaafu ambapo mstaafu ataweza kupata mafao yake yote ndani ya muda mfupi iwezekanavyo.

### **4. Madai ya Walimu:**

**Mheshimiwa Spika**, walimu ni sehumu ya watumishi wa umma. Serikali hii ya CCM imekuwa ikiwatumia sana walimu katika shughuli zake mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia sensa za watu na makazi, uandikishaji wapiga kura (isipokuwa mwaka huu Serikali imewatosa walimu kuandikisha wapiga kura kwa kigezo kwamba hawana elimu ya kompyuta), lakini baada ya kazi zote hizo, Serikali huwasahau walimu kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitetea maslahi ya walimu hasa madai yao ya malimbikizo ya mishahara, posho za uhamisho na posho za mazingira magumu ya kazi lakini Serikali mara zote imekuwa ikitoa ahadi hewa za kulipa madai ya walimu. Mbaya zaidi kuna walimu wanapata ajira lakini wanafanya kazi mpaka miezi sita hawajalipwa mishahara yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahidi walimu wote nchini kuwa ikishika madaraka ya Dola katika uchaguzi wa Oktoba 2015 madai yote ya walimu yatalipwa mara moja na huo utakuwa ndio mwisho wa kulimbikiza madeni kwa walimu na watumishi wa umma wa kada nyingine. Rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa walimu ni kwamba wahakikishe wanafanya kila njia ili vyama makini vya Upinzani kuititia UKAWA vishinde uchaguzi mkuu na kutwaa Dola ili kukomesha uonevu na udhalimu uliofanywa na Serikali ya CCM dhidi ya walimu kwa miaka yote hii.

### **5. Watumishi wa Umma kushiriki katika masuala ya kisiasa:**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hii ya CCM imekuwa ikiwakataza na mara nyingine kuwatisha na kuwaadhibu watumishi wa umma wanaoshiriki katika mikutano ya kisiasa. Kambi Rasmi ya Upinzani inawajulisha watumishi wa umma kwamba, sheria ya utumishi wa umma haikatazi watumishi kuhudhuria mikutano ya siasa isipokuwa kwa muda wa saa za kazi.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu pia Serikali hii ya CCM ikatambua kwamba imeridhia Mkataba wa Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala Barani Afrika wa mwaka 2011 ambapo pamoja na mambo mengine mkataba huo unazisitiza nchi zilizoridhia mkataba huo kuwapa watumishi wake uhuru wa kuijunga na vyama vyaya siasa na kushiriki shughuli za kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali hii ya CCM imekuwa ikiridhia mikataba na itifaki mbalimbali za kimataifa na baadaye kuifungia kabatini na kutoitekeleza, Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni inawaahidi wananchi wote na Jumuiya ya Kimataifa kwamba; endapo upinzani utaingia madarakani mikataba na itifaki zote za kimataifa ambazo nchi yetu imeridhia zitatekelezwa kikamilifu.

#### **6. Maadili ya Utumishi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelipigia kelele sana suala la Ufisadi uliokithiri na matumizi mabaya ya madaraka mionganoni mwa watumishi wa umma Serikalini. Wananchi watakumbuka ufisadi mkubwa na matumizi mabaya ya madaraka ya viongozi wa umma katika masakata ya EPA, Richmond, wizi wa mabilioni ya fedha za umma katika Akaunti ya Tegeta Escrow na mengine yanayofanana na hayo. Katika matukio haya Serikali hii ya CCM imeanguka mara nne kwa kwa kuvunja baraza la mawaziri kutokana na Ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kelele zote za Kambi Rasmi ya Upinzani, na licha ya Maazimio ya Bunge katika masakata yote hayo kuelekeza hatua za kisheria na kinidhamu kuchuliwa dhidi wa waliohusika na masakata hayo, bado Serikali hii ya CCM imeendelea kuwa na shingo ngumu kutekeleza maazimio ya Bunge ya kuwachukulia hatua mafisadi na badala yake inajitahidi kuwakingia kifua mafisadi. Itakumbukwa kwamba hivi karibuni lkulu ya Rais imewasafisha baadhi ya watuhumiwa wa sakata la Escrow kuwa hawahusiki na ufisadi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda wananchi watambue kwamba maisha yao yanaendelea kuwa magumu kwa kukosa huduma mbalimbali za jamii, gherama za maisha zinazidi kupanda siku hadi siku kutokana na wizi na ufisadi mkubwa kama huu ambaa unasihamiwa na Serikali kwa kuwatetea wezi na mafisadi. Ni vema pia wananchi wakatambua kwamba, wakati Serikali inatetea wezi wa fedha za umma ambazo zingeweza kutumika kusambaza huduma za maji, afya na elimu, wakati huphuo inawakaba wananchi kuwachangisha fedha za kujenga maabaraa na fedha za matembezi ya Mwenge wa Uhuru na wananchi wanaoshindwa kutoa michango hiyo wananyang'anywa mali zao na wengine kukamatwa na polisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuuhakikishia umma wa watanzania kwamba endapo Upinzani utaingia madarakani kuititia UKAWA katika uchuguzi mkuu wa Oktoba, 2015 utakuwa ndio ukomo wa rushwa na ufisadi Serikalini.

#### **7. Kuwatambua Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kama watumishi wa umma.**

**Mheshimiwa Spika**, Madiwani na wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni viongozi wanaochaguliwa na wananchi na wanatumia muda wao kuwatumikia wananchi. Kwa maana halisi hawa ni watumishi wa umma kwa kuwanatumikia umma wa watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya uhalisia huu, viongozi hawa hawatambuliwi kisheria kama watumishi wa umma na hivyo hawajaingizwa kwenye mfumo wa utumishi wa umma. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwatambua madiwani na wenyeviti wa Serikali za Mitaa kama watumishi wa umma ili waweze kupata stahili zao kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma.

### **3. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa umma ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 26.4 ambapo kati ya fedha hizo shilingi

bilioni 29.13 zilikuwa ni matumizi ya kawaidi na shilingi bilioni 7.28 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa randama ya Ofisi ya Rais – Menejiment ya utumishi wa umma uk.3, hadi kufikia mwezi Machi, 2015 shilingi bilioni 25.8 sawa na asilimia 88.64 za matumizi ya kawaidi zilikuwa zimeshatolewa lakini fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa katika kipindi hicho zilikuwa ni shilingi bilioni 2.19 tu sawa na asilimia 30.12 ya bajeti ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika utumishi wa umma ni pamoja na kuboresha maendeleo ya rasilimali watu ambayo yanajumuisha kugharamia mafunzo kwa watumishi ili kuongeza weledi wao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni kwa namna gani imetekeleza sera ya maendeleo ya rasilimali watu katika utumishi wa umma ikiwa asilimia 70 ya bajeti ya maendeleo haikutekelezwa?

**Mheshimiwa Spika**, Serikali hii ya CCM imekuwa imekuwa na mazoea ya kutotekeleza bajeti ya maendeleo sio tu kwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma bali katika wizara zingine pia. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwaahidi wananchi wote kuwa endapo Upinzani utaingia madarakani bajeti ya maendeleo katika wizara zote na taasisi za Serikali itakuwa ikitekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Vincent Josephat Nyerere (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KATIKA  
OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

18 Mei, 2015

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Profesa Kahigi.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI PROF. KULIKOYELA  
KANALWANDA KAHIGI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016  
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA  
WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Bukombe kwa ushirikiano wao na nawahamasisha wajiandikishe katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazuoni wa masuala ya demokrasia, siasa na utawala bora wanafanua kuwa utawala bora kuwa ni ule unaojengwa katika misingi ya demokrasia kwa kuzingatia haki za binadamu, uwepo wa chaguzi huru na za haki, utaratibu unaozingatia misingi ya ushiriki wa wananchi katika maamuzi, utawala wa sharia, uwazi, huduma stahiki kwa wakati, usawa wa fursa na ujumuishi, ufanisi na ufanifu, uwajibikaji na dira ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora ni nyenzo muhimu sana katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi. Wataalamu wa utawala wamediriki kusema kuwa utawala dhaifu na ujisadi ni viini vikuu vya umaskini katika nchi nyingi na utawala bora ndiyo suluhisho la matatizo mengi yaliyozikumba nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni yetu huko nyuma tumesitiza kuwa pamoja na hatua mbalimbali ambazo Serikali imechukua, hali halisi ya utawala bora bado hairidhishi. Baadhi ya matatizo yanayokabili utekelezaji wa utawala bora tutayaeleza hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya utawala bora. Tutaanza na Mpango wa Afrika Kujitathimini Kiutawala Bora. Afrika ilibua Mpango wa Afrika Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM) mwaka 2002 na kuzindua mwaka 2003 ili kutekeleza Ubia Mpya kwa Maendeleo ya Afrika (NEPAD). Tanzania ilijunga mwaka 2004 na Bunge hili liliridhia mwaka 2005. Mpango huu ni njia muhimu ya kutathmini mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ujenzi wa utawala bora kwa lengo la kujadiliana namna bora ya kukabiliana na changamoto hizo. Utawala bora inachukuliwa kuwa nguzo muhimu katika kufanikisha maendeleo yote katika jamii ya kisasa, kijamii, kiuchumi na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya kwanza ya APRM iliyozinduliwa mwaka 2013, baadhi ya changamoto za kiutawala bora zilizobainishwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Ukiukwaji wa haki za binadamu;

(ii) Uzingatiaji usioridhisha wa utawala wa sheria;

(iii) Asasi za kidemokrasia ni chache na si huru na hufanya kazi katika mazingira magumu; na

(iv) Kiwango cha chini cha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaiuliza Serikali, imechukua hatua gani katika kushughulikia changamoto hizi na nyinginezo zilizobainishwa katika taarifa ya APRM ya mwaka 2013? Katika hotuba yetu ya mwaka jana tulipendekeza Ripoti hiyo itafsiriwe kwa Kiswahili ili isomwe na watu wengi zaidi, je, tafsiri hiyo iko tayari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa. Ingawa Tanzania ina asasi zinazoshiriki katika kupambana na rushwa au ujisadi kama vile TAKUKURU, Sekretariati ya Maadili, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Awamu ya Nne itaingia katika historia ya nchi kwa kukumbukwa kwa kashfa nyingi za rushwa kubwa, licha ya ujisadi mdogomdogo uliotopea ngazi zote za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakumbuka kashfa kubwa za ujisadi ambazo zimeitikisa Serikali hii ya CCM tangu 2005, hapa nitazitaja kwa ufupi. Kashfa ya EPA; kashfa ya Richmond mwaka 2006 na kashfa ya Akaunti ya Escrow ya Tegeta ya hivi majuzi. Kashfa hizo zimetokea katika Awamu ya Nne lakini katika Awamu ya Tatu kulitokea kashfa ya ununuzi wa Rada ambapo Kampuni ya Uingereza ya BAE Systems baadaye ilipobainika kuwa ilitoa rushwa kupata zabuni iliozwa faini ya dola milioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU ni chombo chenye mamlaka ya utekelezaji wa masuala ya kisheria na kimfumo katika kudhibiti na kupambana na vitendo vya rushwa lakini imeshindwa kuliokoa Taifa na majanga ya rushwa yanayoteketeza mabilioni ya fedha za walipa kodi na kuwanufaisha watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kuwa tangu kuanza kwa Awamu ya Nne rushwa na ubadhirifu vimeonekana kama ni mambo ya kawaida sana na katika jamii fulani mafisadi husifiwa na kujinaki kuwa ni mashujaa. Rushwa sasa inaendesha maisha ya Watanzania wengi hasa katika upatikanaji wa huduma za msingi hasa katika sekta ya afya, huduma Serikali, Polisi, Mahakama na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za binadamu. Tunashuhudia uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu ukifanywa nchini. Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa mwaka 2011, haki ya kuishi imekuwa ikikiukwa kwa kiwango kikubwa nchini na kwamba ongezeko la vifo vya raia vinavyosababishwa na vyombo vya usalama likihamo Jeshi la Polisi, vimeongezeka kwa kasi hadi kufikia vifo 193 katika kipindi cha kati ya mwaka 2005 na 2011.

Kwa muda mrefu, tumeshuhudia jinsi ambavyo Polisi wamekuwa wakitumika kuwanyanya raia badala ya kuwalinda. Aidha, baadhi ya Askari Polisi wameendelea kuvunja haki za binadamu kwa kuendelea kutumia nguvu kupita kiasi pale wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao. Kwa muda mrefu, Polisi wasio waadilifu wamekuwa wakijichukulia maamuzi mikononi mwao, ikiwemo kuwapiga watuhumiwa hata pale wanapotii sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa inatimia miaka mitatu baada ya kifo cha Mwandishi wa Habari, Ndugu David Mwangosi kilichotokea mwaka 2012 kwa kupigwa bomu na Polisi, maisha yanaendelea kama vile jambo hili lilitokea kwa bahati mbaya huku likiwa limetokea kwa kupangwa na Askari Polisi wanaofanya kazi kwa mashinikizo ya Chama cha Mapinduzi. Kama ilivyo ada ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, viongozi husika wa vyombo vya dola wamekuwa mahiri zaidi kuunda Tume kuchunguza kilichotokea, huku Tume hizi zikishindwa kuzuia kutokea tena kwa matukio ya aina hii. Tafsiri yake ni kuwa kuna kushindwa kwa hali ya juu katika kuzuia kutokea kwa matukio ya aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwashauri Polisi na Askari wote nchini kuwa ni busara kwao kufanya kazi kwa kuzingatia weledi wao badala ya kufanya kazi kwa mashinikizo ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kambi ya Upinzani inaendelea kuwahimiza Watanzania kuendelea kujandikisha kwa wingi ili tuweze kuiondoa madarakani Serikali hii iliyoshindwa kusimamia barabara tunu ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsanteni sana.  
(Makofii)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI PROF. KULIKOYELA  
KANALWANDA KAHIGI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA MAKADIRIO  
YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wafuatao: kwanza, wananchi wenzangu wote wa Bukombe kwa ushirikiano wenu, na nawahamasisha kuhakikisha kila mtu atakayekuwa

na umri wa miaka 18 Oktoba mwaka huu ajiandikishe katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Pili, naishukuru familia yangu kwa welewa na uvumilivu wao. Napenda pia kuwapongeza viongozi, wabunge, wataalamu na wadau mbalimbali ambao wanaendelea kutoa elimu kuhusu Utawala Bora, kwa sababu bila Utawala Bora hakuna amani wala maendeleo yoyote ya maana yanayoweza kutokea.

**Mheshimiwa Spika**, wanazuoni wa masuala ya demokrasia, siasa na utawala bora wanaafafanua utawala bora kuwa ni ule unaojengwa katika misingi ya demokrasia kwa kuzingatia haki za binadamu, uwepo wa chaguzi huru na za haki - utaratibu unaozingatia misingi ifuatayo: **ushiriki** wa wananchi katika maamuizi, **utawala wa sheria** (usiobagua), **uwazi**, **huduma stahiki kwa wakati**, **usawa wa fursa na ujumuishi**, **ufanisi na ufanifu** (matokeo yalenge mahitaji kwa matumizi bora ya rasilimali), **uwajibikaji** (waamuzi wote wawajibike kwa matendo yao), **dira ya kimkakati** (viongozi wafahamu nchi inakotoka, ilipo, na wanapotaka kuipeleka).

**Mheshimiwa Spika**, Utawala Bora ni nyenzo muhimu sana katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi. Wataalamu wa utawala (governance) wamediriki kusema kuwa utawala dhaifu na ufisadi ni viini vikuu vya umaskini katika nchi nyingi, na utawala bora ndio suluhisho la matatizo mengi yaliyozikumba nchi zetu.

**Mheshimiwa Spika**, katika maoni yetu huko nyuma tumesitiza kuwa, pamoja na hatua mbalimbali ambazo serikali imechukua, hali halisi ya utawala bora bado hairidhishi. Baadhi ya matatizo yanayokabili utekelezaji wa utawala bora tutayaeleza hivi punde.

#### **HALI HALISI YA UTAWALA BORA**

#### **Mpango wa Afrika Kujitathimini Kiutawala-Bora**

**Mheshimiwa Spika**, Afrika iliibua Mpango wa Afrika Kujitathmini Kiutawala-Bora (APRM) mwaka 2002, na kuuzindua mwaka 2003, ili kutekeleza Ubia Mpya kwa Maendeleo ya Afrika (NEPAD). Tanzania ilijunga mwaka 2004, na Bunge hili iliridhia tarehe 1 Februari 2005. Zipo nchi 34 kati ya 54 za Umoja wa Afrika ambazo zimeshajiungu na Mpango huu. Mpango huu ni njia muhimu ya kutathmini mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na **ujenzi wa utawala bora** kwa lengo la kujadiliana namna bora ya kukabiliana na changamoto hizo. Utawala bora inachukuliwa kuwa nguzo muhimu katika kufanikisha maendeleo yote katika jamii – ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, na mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa ya kwanza iliyozinduliwa mwaka 2013, baadhi ya changamoto za kiutawala-bora zilizobainishwa ni pamoja na:

- Ukiukwaji wa haki za binadamu;
- Uzingatiaji usioridhisha wa Utawala wa sheria;
- Asasi za kidemokrasia ni chache (Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, TAKUKURU, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, na Msajili wa Vyama vya Siasa) na si huru, na hufanya kazi katika mazingira magumu; na
- Kiwango cha chini cha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa maliasili.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inaiuliza Serikali: imechukua hatua gani katika kushughulikia changamoto hizi na nyinginezo zilizobainishwa katika taarifa ya APRM ya mwaka 2013? Katika hotuba yetu ya mwaka jana tulipendekeza Ripoti hiyo itafsiriwe kwa Kiswahili ili isomwe na watu wengi zaidi; je, tafsiri hiyo iko tayari?

### **Mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa**

Ingawa Tanzania ina asasi zinazoshiriki katika kupambana na rushwa/ufisadi (kama vile, TAKUKURU, Sekretariati ya Maadili, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma), awamu ya nne itaingia katika historia ya nchi kwa kukumbukwa kwa kashfa nyngi za rushwa kubwa, licha ya ujisadi mdogomdogo uliotopea ngazi zote za jamii.

**Mheshimiwa Spika**, sote tunakumbuka kashfa kubwa za ujisadi ambazo zimeitikisa serikali hii ya CCM tangu 2005; hapa nitazitaja kwa ufupi:

(1) Kashfa ya EPA: malipo ya ulaghai ya fedha zipatazo Dola za Kimarekani milioni 116 yaliyotolewa na Benki Kuu kwenye Akaunti ya Malipo ya Madeni ya Nje ya Tanzania mwaka 2005/2006.

(2) Kashfa ya Richmond mwaka 2006. Kashfa hii ilihu zabuni ya kuzalisha umeme; jenereta zinazofanya kazi hazikuonekana, na kashfa iliitikisa serikali hadi Mhe. Waziri Mkuu Edward Lowassa akajiuzulu. Ilihuisha Dola za Kimarekani milioni 172.

(3) Kashfa ya Akaunti ya Escrow ya Tegeta. Huu ulikuwa ni mpango kabambe wa kifisadi ambaa ulihuisha serikali hii ya CCM. Mabilioni ya fedha yalitafunwa, wakati hospitali zetu hazina dawa, madarasa yetu hayana madawati, na matatizo chungu mbovu bado yamewakandamiza wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kashfa hizo zimetokea katika awamu ya nne; lakini katika awamu ya tatu kulitokea kashfa ya ununuzi wa Rada ambapo Kampuni ya Uingereza ya BAE Systems baadaye ilipobainika kuwa ilitoa rushwa kupata zabuni ilitozwa faini ya dola milioni 12.

**Mheshimiwa Spika**, TAKUKURU ni chombo chenye mamlaka ya utekelezaji wa masuala ya kisheria na kimfumo katika kudhibiti na kupambana na vitendo vya rushwa, lakini imeshindwa kuliokoa taifa na majanga ya rushwa yanayoteketeza mabilioni ya fedha za walipa kodi na kuwanufaisha watu wachache.

**Mheshimiwa Spika**, ni bahati mbaya sana kuwa tangu kuanza kwa awamu ya nne rushwa na ubadhirifu vimeonekana kama ni mambo ya kawaida sana, na katika jamii fulani mafisadi husifiwa na kujinaki kuwa ni mashujaa. Rushwa sasa inaendesha maisha ya Watanzania wengi hasa katika upatikanaji wa huduma za msingi hasa katika sekta ya afya, huduma serikalini, polisi, n.k. Pamoja na kuwa na chombo cha kupambana na kudhibiti rushwa, wananchi wameshindwa kuripoti matukio ya rushwa kwa hofu ya kukosa huduma wanazohitaji.

**Mheshimiwa Spika**, rushwa imeonekana kukua katika vituo vya afya na hospitali mbalimbali za Serikali. Katika hospitali nyngi za umma, upatikanaji wa huduma bora na za haraka huambatana na rushwa ndogondogo na hii inachangiwa na mishahara duni katika sekta ya huduma za afya. Vilevile, baadhi ya polisi na askari wa usalama barabarani nchini wameendelea kuwa waumini wakubwa wa rushwa kwa makosa ya barabarani.

### **Uhuru wa Wananchi na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 linaleleza kuwa kila mtu ana haki ya kufanya mikutano ya amani ikiwemo maandamano na haki hii pia imetambuliwa katika Mkataba wa Nchi za Kiafrika kuhusu Haki za Binadamu wa mwaka 1981. Lakini Serikali ya CCM inawapoka wananchi haki zao kwa kuzuia mikutano, hasa ya wapinzani, na maandamano ambayo ni ya amani kunadhihirisha uvunjaji wa makusudi wa Mkataba huu muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Kambi ya Upinzani imeendelea kusisitiza umuhimu wa kutoa nafasi kwa jamii kuelezea machungu ya kero na adha wanazopata kwa kutumia haki yao ya kikatiba ikiwamo kwa kufanya maandamano ya amani nchini. Katika kipindi hiki cha miaka kumi, ni wazi kuwa uhuru wa wananchi na haki yao ya kikatiba ya kuandamana na kutoa mawazo yao umeporomoka sana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa nchi ambayo Serikali yake inajisifu kufuata utawala bora huku ikizima maandamano kwa vitisho nya jeshi la polisi na kwa kuwatumia wakuu wa wilaya na mikoa, ni dhahiri kuwa utawala wake umeshikwa ganzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakumbuka na inaendelea kulaani kitendo cha udhalilishaji alichofanyiwa Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, ambaye pia ni Mwenyekiti Mwenza wa UKAWA. Prof. Ibrahim Lipumba alipigwa na polisi kwa kutaka kufanya mikutano wa amani wa hadhara ikiwa ni kumbukizi la vifo nya Watanzania waliouawa mwaka 2001 huko Zanzibar wakiwa katika vuguvugu la kudai mabadiliko.

**Mheshimiwa Spika**, katika tukio lile la kusikitisha, wana-CUF na wanahabari walipata kipigo kutoka kwa polisi; tulishuhudia pia watoto wa shule za awali wakiwa taabani kwa kuathiriwa na mabomu ya machozi yaliyopigwa na polisi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Serikali hii ya CCM inajigamba kuwa inafuata misingi ya utawala bora na demokrasia, itakumbukwa kuwa ni Serikali hii hii ya CCM iliyopiga marufuku shughuli za kisasa kufanya katika mikoa ya Lindi na Mtwara mwaka 2013 kwa kuogopa vuguvugu la mabadiliko kutoka kwa wananchi wa mikoa hiyo waliokataa uhamishaji wa rasilimali ya gesi iliyo katika maeneo yao bila wao kushirikishwa.

**Mheshimiwa Spika**, ili kudhirihisha kuwa Serikali hii ina ubaguzi na inafanya kazi kwa upendeleo wa kisasa (double standard), wakati vyama nya siasa vinapigwa marufuku kufanya mikutano katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete alikuwa akiendelea kufanya mikutano katika mikoa hiyo bila kuulizwa na mtu au chombo chochote cha ulinzi na usalama. Upendeleo wa wazi wa namna hii ni ishara ya udhaifu mkubwa katika utawala na uendeshaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, mara nyingi kisingizio kinachotumika cha kukataza Mikutano ya vyama nya upinzani kwa kigezo kwamba taarifa za kiintelijensia ya kipolisi kwamba kutakuwa na machafuko au vurugu ikiwa mikutano hiyo itafanyika; lakini intelijensia hiyo haiwezi kung'amua vurugu na machafuko katika mikutano ya CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji; Intelijensia ya kipolisi ina "king'amuzi" kinachotambua vurugu tu kwenye mikutano ya vyama nya upinzani peke yake?

#### **Uwazi na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa msingi wa utawala bora ambao haujazingatiwa barabara ni **Uwazi** katika uendeshaji wa Serikali. Kwa miaka yote mitano ya uhai wa Bunge hili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepigia sana kelele suala la kukosekana kwa uwazi katika mikataba ya uwekezaji mkubwa katika sekta za nishati, madini na uvunaji wa mali asili nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza na kushauri kuwa mikataba yote ambayo Serikali inaingia na wawekezaji katika nchi yetu iletwe Bungeni ili ijadiliwe kwa uwazi ili kuliepusha taifa na hasara kubwa inayotokana na wizi wa hila unaofanyika kwenye mikataba inayosainiwa kwa siri.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa Serikali hajakubali kuleta mikataba ya uwekezaji Bungeni jambo linaloashiria kwamba hina mpango wa kuzuia ujisadi mkubwa unaofanyika kupitia mikataba ya uwekezaji; Kambi Rasmi ya Upinzani inawaahidi watanzania wote kwamba endapo vyama vianvyounda UKAWA vitashinda uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu 2015 na kuunda Serikali, mikataba yote ya uwekezaji itawekwa wazi na kujadiliwa Bungeni.

#### **Uwajibikaji na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili na wananchi watakuwa ni mashuhuda jinsi ambavyo awamu ya nne ya utawala wa CCM ilivyoshindwa kusimamia suala la uwajibikaji wa viongozi wa umma kama sehemu ya utawala bora. Ni katika awamu hii ya nne ambapo mawaziri 12 wamefukuzwa kazi kwa shinikizo la maazimio ya Bunge kutokana na kushindwa kuwajibika wao wenyewe kwa uzembe na makosa yaliyotokea chini ya uongozi wao.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kukosekana kwa nidhamu ya utashi wa uwajibikaji mionganini mwa mawaziri na viongozi wengine wa umma Serikali hii ya awamu ya nne imejikuta ikitia fora katika kubadili mawaziri na watendaji wakuu Serikalini mara nyingi zaidi kuliko awamu za tawala zilizotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaahidi wananchi utendaji na uwajibikaji uliotukuka na idadi ndogo ya mawaziri endapo watachagua viongozi wanaotokana na vyama vianvyounda UKAWA katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015.

#### **Ubadhirifu na Ufisadi**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 27 Machi 2015 wakati akipokea Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka unaoishia Juni 2014, Rais Kikwete akiwa ikulu, aliviagiza vyombo vyya Serikali kubaini maofisa wote wa Serikali wanaohusishwa na matumizi mabaya ya fedha za Serikali, ikiwa ni pamoja na kutoa malipo bila nyaraka zozote, kutumia fedha nje ya Bajeti na kutoa malipo bila idhini ya ofisa masuhuli, na kisha wachukuliwe hatua kali za kisheria na hatua nyingine. Mionganini mwa mambo yaliyoibuliwa na ripoti hiyo ya CAG, ni kuwepo kwa mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali kama vile malipo yasiyokuwa na nyaraka, hati za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi, fedha iliyoitumika nje ya Bajeti, matumizi yasiyokuwa na manufaa na malipo ambayo hayakuidhinishwa na maafisa masuuli.

Aidha, Rais Kikwete aliagiza kuchukuliwa kwa hatua kali za kisheria kwa maofisa wote wa Serikali ambao wanahuksika katika kulipa mishahara hewa kwa watumishi ambao wameacha kazi, wamefariki, wamestaafu lakini ambao wanaendelea kulipwa mishahara kupitia akaunti zao za benki.

**Mheshimiwa Spika**, hii siyo mara ya kwanza kwa Rais Kikwete kuagiza wabadhirifu wachukuliwe hatua. Amesema haya mwaka 2005 na hata 2010 wakati wa uchaguzi Mkuu. Ni dhahiri kuwa Serikali yake imeshindwa kusimamia utawala bora linapokuja suala la uwajibikaji na uwajibishaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na vyama vianvyounda UKAWA, imekuwa mstari wa mbele katika kuishauri Serikali ya CCM kwa takribani miaka 10, kuhusu njia mbalimbali za kukabiliana na kuziba mianya ya ubadhirifu wa mali za umma lakini ushauri wetu haukuthaminiwa. Sisi kama UKAWA, tukichaguliwa kushika serikali, ahadi yetu kwa Watanzania ni kuwa tutakabiliana na ubadhirifu kwa kufuata haki, sheria na kanuni za nchi ili kuhakikisha kuwa kodi za jasho la Watanzania zinatumika ipasavyo kwa miradi ya maendeleo na kwa manufaa yao.

### Haki za Binadamu

**Mheshimiwa Spika**, tunashuhudia uvunjwaji mkubwa wa haki za binadamu ukifanywa nchini. Kwa mujibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa mwaka 2011, haki ya kuishi, imekuwa ikikiukwa kwa kiwango kikubwa nchini na kwamba ongezeko la vifo vya raia vinavyosababishwa na vyombo vya usalama, likiwamo Jeshi la Polisi, vimeongezeka kwa kasi hadi kufikia vifo 193 katika kipindi cha kati ya mwaka 2005 na 2011. Kwa muda mrefu tumeshuhudia jinsi ambavyo polisi wamekuwa wakitumika kuwanyanyasa raia badala ya kuwalinda. Aidha, baadhi ya askari polisi wameendelea kuvunja haki za binadamu kwa kuendelea kutumia nguvu kupita kiasi pale wanapokuwa wakitekeleza majukumu yao. Kwa muda mrefu, polisi wasio waadilifu wamekuwa wakijichukulia maamuzi mikononi mwao, ikiwemo kuwapiga watuhumiwa, hata pale wanapotii sheria bila shuruti. Ushahidi wa video na picha mbalimbali unaonesha jinsi ambavyo polisi hutoa vipigo kwa raia ambaa wamekubali kujisalimisha mikononi mwao na wasio na silaha. Na mara kadha matukio kama haya imesemekana huchochewa na mashinikizo ya Viongozi wa Serikali ya CCM.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa inatimia miaka mitatu baada ya kifo cha mwandishi wa habari, David Mwangosi kilichotokea mwaka 2012 kwa kupigwa bomu na polisi, maisha yanaendelea kama vile jambo hili lilitokea kwa bahati mbaya huku likiwa limetokea kwa kupangwa na askari polisi wanaofanya kazi kwa mashinikizo ya CCM. Kama ilivyo ada ya Serikali ya CCM, viongozi husika wa vyombo vya dola wamekuwa mahiri zaidi kuunda tu Tume kuchunguza kilichotokea, huku Tume hizi zikishindwa kuzuia kutokea tena kwa matukio ya aina hii. Tafsiri yake ni kuwa kuna kushindwa kwa hali ya juu katika kuzuia kutokea kwa matukio ya aina hii. Na tafsiri ya jumla zaidi ni kuwa kila mmoja wetu, hapo alipo, hana uhakika na usalama wake. Hata wewe Mheshimiwa Spika, yumkini hauko salama – katika muktadha kama huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuwashauri polisi na askari wote nchini kuwa ni busara kwao kufanya kazi kwa kuzingatia uweledi wao badala ya kufanya kazi kwa mashinikizo ya kisiasa.

### Changamoto Nyingine Za Utawala Bora

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa za utawala bora kwenye ngazi ya kijiji na kata nchini ni watendaji kutokuwa tayari kushirikisha wananchi katika utekelezaji wa majukumu ya kimaendeleo. Katika maeneo mengi, wananchi hawashirikishwi katika kuibua miradi, miradi inapangwa na kundi dogo tu; kisha kiwango cha michango kinaamuliwa na ama mtu mmoja au kundi dogo la viongozi, badala ya mkutano wa kijiji. Kadhalika, mahali peengi mikutano ya kujadili mapato na matumizi haiitishwi; hakuna uwazi katika michango inayotolewa na wananchi kwa ajili ya miradi ya kijiji au kata. Bila kuwashirikisha wananchi, hawawezi kuiona miradi inayotekelzeza katika vijiji au kata zao kuwa ni yao, na bali ni ya serikali ambayo haikuwashirikisha katika ngazi mbalimbali za utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine kubwa ya utawala bora ni matumizi mabaya ya madaraka. Matumizi mabaya ya madaraka ni utumizi wa madaraka ambayo mtu aliyo nayo kisheria, au ambayo hujipa, kutenda jambo ambalo kisheria au kiutaratibu/kikanuni haliruhusiwi. Vitendo vya kikatili vinavyofanywa na baadhi ya polisi, vitendo vya kubambikiwa kesi vinavyotendwa na baadhi ya polisi au baadhi ya watendaji, vitendo vinavyoashiria upendeleo wa kisiasa (double standard) vya baadhi ya Wakuu wa Wilaya au Mikoa, vitendo vya kidhalimu vinavyofanywa na baadhi ya watendaji na askari wa wanyamapori kwa wananchi wanaokamatwa kwenye hifadhi, vyote hivyo ni vitendo vya matumizi mabaya ya madaraka.

**Mheshimiwa Spika**, hawa wote wanaotenda matendo hayo wanakwenda kinyume na azma ya kipaumbele namba 10 katika hotuba ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete,

alipokuwa anazindua Bunge hili la 10 tarehe 18 Novemba mwaka 2010; katika kipaumbele hicho, Mheshimiwa Rais aliahidi "... kuimarisha utawala bora, demokrasia, utawala wa sheria, haki za binaadamu na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa, dawa za kulevy, matumizi mabaya ya madaraka na ubadhirifu wa mali ya umma. Kwa ajili hiyo tutaendelea kuvijenga na kubiwezesha kirasi limali, kimuundo na kisheria vyombo vinavyoongoza mapambano hayo na vile vya kutoa na kusimamia haki nchini."

**Mheshimiwa Spika**, hali halisi ni kwamba azma hii nzuri haijatekelezwa ipasavyo; baadhi ya watu wanaoihujumu ni wateule wa Mheshimiwa Rais mwenyewe.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inaendelea kuwahimiza Watanzania kuendelea kuijandikisha kwa wingi ili tuweze kuiondoa madarakani Serikali hii iliyoshindwa kusimamia barabara tunu ya utawala bora.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA**

18 Mei, 2014

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA ESTHER N.  
MATIKO KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MAPATO  
NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS MAHUSIANO NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016  
KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. ESTHER N. MATIKO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA  
WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu, wana Mara na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuwa nami bega kwa bega. Kipekee zaidi napenda kuwashukuru wana Tarime kwa kushirikiana nami na kwa imani kubwa waliyo nayo kwangu. Nawaahidi kutowaangusha Oktoba 2015 kitaeleweka.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla ya Mahusiano na Uratibu. Jamii yoyote inayojengwa katika misingi ya kuheshimu uhuru wa watu wake katika imani yao juu ya uwepo wa Mungu na kukubali kufuata taratibu za nchi katika kuchagua imani yoyote isiyovunja sheria, ni jamii yenye uwezo mkubwa wa kushinda majaribu yoyote na misukosuko dhidi ya watu wake. Ikumbukwe kuwa, mwaka 2005 Taifa likiwa linaelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, viongozi wa dini walitamka kuwa Mheshimiwa Rais ni chaguo la Mungu. Hakuna kiongozi yeyote wa wakati ule na si Rais Kikwete mwenyewe wala Chama chake ambaa waliwataka viongozi wa dini kuacha kujihusisha na siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa imepita takribani miaka 10 toka kauli ile ya kumuidhinisha Rais Kikwete katika masuala ya dini; ambaye pia mara kwa mara ameendelea kuwatumia

viongozi wa dini kuhalalisha masuala yenyewe ukakasi kwenye jamii, hivi karibuni Rais Kikwete ambaye alitoa kauli akiwataka viongozi wa dini kutojihusisha na siasa, ni dhahiri kuwa kauli ya Maaskofu kuwahamasisha waumini wake kuikataa Katiba Pendekezwa imeiumiza Serikali na ndiyo maana Serikali imeenda mbali zaidi na kutoa hata tishio kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mathias Chikawe kuwa watazifuta taasisi za dini nchini. Kauli hizi ni kauli za hatari ambazo si tu zinalenga kuwafunga viongozi wa dini midomo bali pia zinahatarisha usalama wa taasisi za kidini na waumini wake kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Serikali hii ya CCM iliyoshindwa kudhibiti vurugu za kidini ikiwemo kuchomwa kwa makanisa na kuuawawa kwa viongozi wa dini Zanzibar, kukojolewa kwa Qurani Tukufu kule Mbegala ambapo kulisababisha vurugu, kulipuka kwa mabomu Arusha katika makanisa pamoja na migogoro wa uchinjaji nchini. Haya ni mambo ambayo kwa mara ya kwanza tumeyashuhudia katika Serikali ya Awamu ya Nne ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikitoa tuhuma za kidini na kuchochaea ugomvi wa kidini kwa kuvipaka matope Vyama vya Upinzani kuwa ni vya udini ilhali viongozi wake kwa kauli zao wamekuwa wakipasua Taifa kwa udini. Ni ishara kuwa jukumu la ulinzi na usalama kwa makundi yote nchini hasa makundi ya kidini upo mashakani, ni vema Serikali sasa ikapumzika maana imechoka kusimamia masuala muhimu kwa ajili ya utengamano wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Serikali ya CCM imekuwa ikizitumia taasisi za dini kama njia ya propaganda na kuwahadaa Watanzania. Walifanya hivyo kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2005 ikiwemo kuwaahidi waislamu kupitisha Mahakama ya Kadhi, walifanya hivyo kwenye uchaguzi wa mwaka 2010, wakafanya hivyo kwenye Bunge Maalum la Katiba na walifanya hivyo pia kwenye Muswada wa Mabadiliko wa Sheria Mbalimbali wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati nzuri sasa kuona kuwa viongozi wa dini wameamua kutokuwa sehemu ya kuwahadaa Watanzania. Viongozi walio wengi wameamua kusimamia maslahi ya Taifa kwa manufaa ya watu wote nchini. Viongozi wa Dini wengi wamekataa kutumika na Serikali ya CCM katika kuwagawa Watanzania kupitia udini. Ndiyo maana baadhi ya viongozi wa dini wameamua na kusema sasa yatosha. Viongozi wa dini sasa wameamua kusimamia maslahi mapana ya Watanzania ikiwemo kuwapa elimu ya kuikataa Katiba Pendekezwa iliyochakachuliwa na Serikali ya CCM.

Aidha, ni aibu kwa Serikali ya Rais Kikwete kuingilia faragha ya waislamu waliokuwa katika Hijra huko Makka kwa kutumia mamilioni ya Watanzania na kudai kuwafuata mahujaji hao kwa ajili ya kupigia kura kwa kile kinachoitwa Katiba Pendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitahadharisha Serikali kutozigusa taasisi za dini hasa ambazo zimeendelea kutoa elimu kwa Watanzania bila kuvunja taratibu za nchi hii. Aidha, tunawaasa viongozi wa dini zote na waumini wao kutokubali mpango huu ovu wa Serikali ya CCM unaopanga kupoka haki yao ya Kikatiba na uendeshaji bora wa taasisi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya madereva nchini. Pamoja na kuwa Serikali inajukumu la kuratibu mahusiano ya makundi mbalimbali ya kijamii, kumekuwepo na mgogoro mkubwa unaosababishwa na kukosekana kwa imani baina ya Serikali na madereva kuhusu namna ya kusimamia maslahi yao. Sote ni mashahidi jinsi ambavyo kulikuwa na usimamizi mbovu wa Serikali kuhusu madai ya madereva na adha ambayo wananchi waliipata mara mbili mfululizo kwa migomo ambapo awali madereva waligoma baada ya kutakiwa kusoma kila wanapokwenda ku-renew leseni zao kupitia chuo cha NIT. Aidha, mgomo mwingine ulisababishwa na madai ya madereva juu ya mikataba na ujira wa kazi yao dhidi ya waajiri ambaeo ni wamiliki wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli mbalimbali za viongozi na Mawaziri ambao walizitoa kwa madereva hao, ni dhahiri kuwa Serikali haijaweka mkakati wa kudumu kuhakikisha maslahi ya pande zote mbili za mgogoro yanalindwa bali mgogoro huo unatumia na Serikali kama chambo cha kujipatia kura kwenye Uchaguzi Mkuu. Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuchukua fursa hii kuwataka madereva wote kuwa wavumilivu kwa kuwa madhara ya migomo si tu inayumbisha uchumi bali pia ina athari kwa Watanzania mafukara ambao wengi ndiyo tunaotumia usafiri wa umma kwa ajili ya shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitumie rai ileile aliyotoa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbewe pamoja na Mwenyekiti Mwenza wa UKAWA kutoka CUF, Profesa Ibrahim Lipumba ambapo waliwafuata mlipokuwa na kuwasikiliza, kuwa hakuna mrefu yasiyo na ncha. Kipindi hichi ni vyema kwa madereva wote na abiria wanaotumia usafiri wa umma kutafakari ni jinsi gani wameendelea kutumika na Serikali ya CCM, ni dhahiri kuwa nguvu kubwa ya kufanya mabadiliko nchini itatokea iwapo Watanzania tutashikamana, tutajiandikisha kwa wingi katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kujitokeza kwa wingi katika zoezi zima la Uchaguzi Mkuu Oktoba na kuchagua UKAWA popote pale mlipo. (Makofisi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakayoundwa na UKAWA inaendelea kuamini kuwa kila Mtanzania ana haki ya kutoa maoni yake kwa njia ambayo anaona itapata usikivu wa watawala. Nasi kama UKAWA, tumeandaa sera na miongozo itakayohakikisha uwepo na upatikanaji wa mazingira mazuri ambayo yataleta haki kwa kila mmoja wa Madereva ambao hufanya kazi katika mazingira magumu.

Aidha, Kambi ya Upinzani Bungeni inawasihi wamiliki wa mabasi na vyombo vyaa usafirishaji ikiwemo malori kutafuta suluhu ya kumaliza mgogoro huu ambao una athari za kiuchumi si tu kwa dola bali hata kwao binafsi kama wafanyabiashara. Ni tumaini letu kuwa wamiliki wa vyombo vyaa usafiri watafanya kazi ya mazingira ya utumishi wa madereva ili kujenga uaminifu na mauhusiano bora baina yao na waajiriwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo wa wafanyabiashara. Katika utawala wa Awamu ya Nne ni dhahiri kuwa Serikali ilidhamiria kutowashirikisha wananchi kikamilifu katika maamuzi mbalimbali yanayoathiri shughuli zao za kila siku na hivyo kukosa imani kwa wananchi. Ulipaji wa kodi hauepukiki kwa Taifa lolote lile duniani. Kodi za wananchi zimeendelea kuwa chanzo kikubwa cha mapato ili zitumike katika utoaji huduma za wananchi. Kwa nchi nyingi za Kiafrika ulipaji wa kodi umekuwa hauendani na utoaji na upatikanaji wa huduma muhimu zikiwemo maji, elimu, huduma za afya, makazi, miundombinu na kadhalika. Kwa kuwa Serikali zimeendelea kuwa na matumizi makubwa na hivyo kuzua malalamiko hasa kutoka kwa walipa kodi wakiwemo wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi makubwa ya Serikali ya CCM, ubadhirifu pamoja ufisadi mkubwa, vimejenga mazingira ambayo walipa kodi hawana imani na mifumo ya Serikali ya ulipaji wa kodi. Wafanyabiashara wametafsiri mifumo ya ulipaji wa kodi kama njia mojawapo ya unyonyaji unaofanya na Serikali ya CCM. Kudhihirisha hili, Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Abdulrahman Kinana alitaja uititiri wa kodi za Tanzania kama kikwazo cha wafanyabiashara kufanikiwa. Ndugu Kinana alitoa kauli hiyo mwezi Aprili, 2015 kwenye mkutano wa hadhara katika Viwanja vya Pasua Mjini Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika mkutano huo ambao Katibu Mkuu wa CCM ambaye Mwenyekiti wake ndiye Rais Kikwete alisema kuwa wafanyabiashara wanaumizwa zaidi na kodi hizo lakini hawana mtu wa kuwasemea zaidi ya kuendelea kunyonywa. Vilevile, kama kawaida yake Katibu Mkuu huyo aliwatupia lawama Wabunge wa CCM kuwa wingi wao Bungeni hausaidii kitu kwa sababu wameshindwa kuondoa sheria zinazomkandamiza mwananchi.

Nanukuu; "Kila kona ni kodi na kila kukicha ni kodi, SUMATRA wanadai kodi, Fire wanadai kodi, taasisi zingine zinadai kodi, yaani ni kero tupu"

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Katibu Mkuu wa CCM Kinana inathibitisha madai ya muda mrefu ya wafanyabiashara nchini juu ya kunyonywa kwao na mifumo holela ya kodi. Ni katika kadha hii ambayo imesababisha mara kwa mara wafanyabiashara kuendelea kugomea mashine za kieletroniki za ulipaji wa kodi kitaalamu zinajulikana kama EFDs na iliyopelekea kukamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Ndugu Johnson Minja kwa madai ya uchochezi ya kuwataka wafanyabiashara kugomea matumizi ya EFDs.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo kumeendelea kuwepo kwa migomo baridi inayofanywa na wafanyabiashara wa maeneo mbalimbali nchini kama njia ya kushinikiza kufutiwa kesi kwa kiongozi wao huyo. Vilevile migomo hii imeendelea kuleta athari kwa walaji kwa kuwa wafanyabiashara wamekuwa wakifunga maduka mara kwa mara lakini Serikali kwa nyakati tofauti hata kwa kauli ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda imeonesha wazi kutotaka suluhu na wafanyabiashara ikiwemo kumfanya hila Ndugu Minja na kumuweka rumande wakati amba Serikali ilidai inafanya maridhiano na wawakilishi wa wafanyabiashara nchini. Kambi ya Upinzani Bungeni, inasimama pamoja na wafanyabiashara wote nchini na kuwataka kusimama imara katika kupigania maslahi yao.

Aidha, tunaendelea kutumia wataalamu wetu mbalimbali amba wanatoa elimu juu ya umuhimu wa ulipaji kodi nchini. Ni kwa misingi bora ya uwajibikaji inayotupa imani kuwa Watanzania watatupa dhamana ya kuwaongoza ili kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uwajibikaji katika matumizi na mapato ya Serikali hasa kodi za wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka wananchi kuchagua Serikali itakayotokana na UKAWA ili iweze kutoa elimu sahihi na msaada kwa wafanyabiashara na walaji itakayowawezesha kushiriki katika utoaji wa huduma bora kwa kulipa kodi kwa mfumo utakaodhibitiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Tunawaahidi Watanzania kuwa kodi zao hazitopotea bure na tutawajibika kwa kuandaa mifumo ya wazi itakayochambua mapato na matumizi ya Serikali ya UKAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa elimu ya juu nchini. Kwa muda mrefu Serikali ya CCM imeshindwa kuisimamia ipasavyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini. Hii inatokana na Serikali kuchelewesha kupeleka fedha kwa ajili ya wanafunzi na hivyo kufanya Bodi ishindwe kufanya kazi kwa ufanisi. Matokeo ya ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi imezua migogoro mingi ikiwemo migomo ya wanafunzi, kusimamishwa kwa wanafunzi ama wanafunzi kuzuiwa kufanya mitihani ama kukatishwa masomo kwa kushindwa kulipa ada mbalimbali za vyuo.

Aidha, kumekuwa na msigano ya muda mrefu baina ya wanafunzi na utawala wa vyuo mbalimbali na misigano hii huleta athari kubwa kutokana na Serikali kushindwa kuisimamia ipasavyo. Kwa mfano, migogoro na migomo ya vyuo vya UDOM, MUHAS iliyotokana na utawala wa Rais Kikwete kwa kuwa kielezo Serikali bado imeendelea kuchukua hatua dhidi ya matokeo badala ya kushughulikia vyanzo vya matatizo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa mwaka 2007, Rais Jakaya Kikwete aliahidi kutoa ufumbuzi matatizo haya alipokutana na wanafunzi wa vyuo vikuu wa CCM mwezi Februari, 2007. Alikwenda mbali zaidi kwa kuwaeleza kwamba hakuna mtoto wa maskini atayeshindwa kuendelea na masomo kutokana na masharti ya mikopo. Ikiwa ni miaka nane imepita toka ahadi hizo zitolewe migomo katika vyuo vikuu imeendelea na pia wapo watoto wa walalahoi

ambao wamefaulu kidato cha sita lakini wemeshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa mikopo na upendeleo wa wazi na upangaji wa viwango vya madaraja ya mikopo nchini usiozingatia vigezo vilivyowekwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachukua nafasi hii kuwaeleza Watanzania wote na watoto wa kitanzania kuwa, UKAWA bado inaamini kuwa ikiwa Mwalimu Nyerere aliweza kuwasomesha watoto wa wakulima mpaka elimu ya juu basi nasi tutaweza kutoa elimu bure kwa Watanzania wote bila kujali rangi, dini, kabila wala madaraja yao katika jamii. Rai yetu kubwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kukataa kutumika na kuhadaika na ahadi kemkem za CCM bali watumie fursa hiyo kujandikisha kwa wingi katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka huu popote walipo na kupiga kura Oktoba 2015. Tuwakumbushe pia vijana wote waliokosa fursa za masomo kutokukata tamaa kwa kuwa nchini Nigeria, vijana ndio waliofanikisha kuundoa utawala wa Rais Goodluck Jonathan na kufanikisha ushindi wa Rais Buhari. Hivyo hii ni fursa pekee ya kuwaepusha na maumivu makali ya miaka mitano mingine iwapo watafanya makosa kuirudisha CCM madarakani Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutishia NGOs zinazotekeleza majukumu yake. Mojawapo ya dalili ya Serikali inayoshindwa ni pamoja na kuogopa kivuli chake chenyewe. Serikali hii ambayo imetumia fedha nyingi na nguvu nyingi katika kuhalalisha maovu yake imejikuta ikishindwa na nguvu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambazo kwa kiasi kikubwa zimeweza kuonesha madhaiju ya Serikali kwa kutoa elimu kwa Watanzania wote kinyume na matarajio ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mkoani Geita Januari mwaka huu Mashirika zaidi ya 1000 yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania yalitangaziwa kufutwa kwa usajili wake kunatokana na kutotimiza matakwa ya kisheria katika utendaji wake kazi toka yaliposajiliwa. Kwa mujibu wa kikao cha bodi ya uratibu ya Mashirikia yasiyo ya Kiserikali ambacho kilieleza kuwa kufutwa kwa mashirika hayo kutokana na kushindwa kutoa taarifa za kila mwaka kama inavyosisitizwa na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2002, kifungu cha 24. Mashirika hayo pia yanadaiwa kukosa sifa ya kuendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa inaelekea ukingoni, Serikali ya CCM inakumbuka shuka kumekucha huku kwa kipindi cha miaka 10 ya utawala wake kikishindwa kukagua utendaji wa mashirika hayo. Ni matumaini yetu kuwa, Serikali hii haitoisahau Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) inayoongozwa na Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete, ambayo nayo iliukiwa masharti na kanuni za uendeshaji kwa kuwa Waziri (Mheshimiwa Sophia Simba) mwenye dhamana ya kuzisimamia taasisi zisizokuwa za Kiserikali kuwa Mjumbe wa Bodi ya WAMA. Ikiwa Serikali imeamua kusafisha mashirika hayo yasiyo ya Kiserikali yaliyokiuka sheria isisahau kuifutia WAMA usajili wake kwa kuwa nayo imekiuka sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaruka ila naomba mengine yote yaingie kwenye Hansard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011-2016). Serikali ya CCM kwa mbwembwe kubwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 iliwasilisha Bungeni Mpango wa Miaka Mitano ambao ulizinduliwa na Rais Jakaya Kikwete ambao hata hivyo katika mipango na bajeti za kila mwaka tuliveka bayana namna ambavyo Serikali imekuwa haifuati Mpango huo. Jambo hilo linadhahirika sasa ambapo mipango mingi ambayo iliyokuwa kwenye Mpango ule haijatekelezwa na hata bajeti za Serikali hazifuati vipaumbele kama ambavyo vimeainishwa kwenye mpango huo ambao tuliaminishwa kuwa ungeweza kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali yenyewe inapanga na kuwasilisha hapa Bungeni na hata baada ya kupanga inashindwa kusimamia na kutekeleza Mpango wake yenyewe, ni ishara kuwa Serikali hiyo imechoka. Kambi ya Upinzani Bungeni imojiandaa vilivyo kuhakikisha kuwa Tanzania inaweka vipaumbele vinavyotekelzeza na vitaweza kutatua matatizo ya Watanzania kupitia Serikali itakayoundwa na UKAWA ifikapo Oktoba, 2015.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na nafikiri message sent. (Makofisi)

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA ESTHER N. MATIKO KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS MAHUSIANO NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**  
**UTANGULIZI KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu, wana Mara na watanzania wote kwa ujumla kwa kuwa nami bega kwa bega. Kipekee zaidi napenda kuwashukuru wana Tarime kwa kushirikiana nami na kwa imani kubwa waliyo nayo kwangu. Nawaahidikutowaangusha Oktoba 2015, lazima kieleweke.

**Maoni ya Jumla ya Mahusiano na Uratibu**

**Mheshimiwa Spika,** jamii yoyote inayojengwa katika misingi ya kuheshimu uhuru wa watu wake katika imani yao juu ya uwepo wa Mungu na kukubai kufuata taratibu za nchi katika kuchagua imani yoyote isiyovunja Sheria, ni jamii yenye uwezo mkubwa wa kushinda majaribu yoyote na misukosuko dhidi ya watu wake. Ikumbukwe kuwa, mwaka 2005 Taifa likiwa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani, viongozi wa dini walitamka kuwa Mheshimiwa Rais ni Chaguo la Mungu. Hakuna kiongozi yeyote wa wakati ule, na si Rais Kikwete mwenyewe wala Chama chake amba waliwataka Vongozi wa dini kuacha kujihusisha na siasa.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa imepita takribani miaka 10 toka kauli ile ya kumuidhinisha Rais Kikwete katika masuala ya dini ; ambaye pia mara kwa mara ameendelea kuwatumia viongozi wa dini kuhalalisha masuala yenye ukakasi kwenye Jamii, hivi karibuni Rais Kikwete ambaye alitoa kauli akiwataka viongozi wa dini kutojihusisha na siasa. Ni dhahiri kuwa kauli ya Maaskofu kuwahamasisha waumini wake kuikataa Katiba pendekewa imeiumiza Serikali na ndio maana Serikali imeenda mbali zaidi na kutoa hata tishio kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Mathias Chikawe kuwa watazfuta taasisi za dini nchini. Kauli hizi ni kauli za hatari ambazo si tu zinalenga kuwafunga viongozi wa dini midomo bali pia zinahatarisha usalama wa taasisi za kidini na waumini wake kuelekea uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015.

**Mheshimiwa Spika,** ni Serikali hii ya CCM iliyoshindwa kudhibiti vurugu za kidini ikiwemo kuchomwa kwa makanisa na kuuawawa kwa viongozi wa dini Zanzibar, kukoolewa kwa Quran Tukufu kule Mbagala ambapo kulisababisha vurugu, kulipuka kwa mabomu Arusha katika

makanisa pamoja na mgogoro wa uchinjaji nchini. Ni mambo ambayo kwa mara ya kwanza tumeyashuhudia katika Serikali ya awamu ya nne ambayo kwa muda mrefu imekua ikitoa tuhuma za kidini na kuchochea ugomvi wa kidini kwa kuvipaka matope vyama vya Upinzani kuwa ni vya udini ilhali viongozi wake kwa kauli zao wamekua wakipasua taifa kwa udini. Ni ishara kuwa jukumu la ulinzi na usalama kwa makundi yote nchini hasa makundi ya kidini upo mashakani. Ni vema Serikali sasa ikapumzika maana imechoka kusimamia masuala muhimu kwa ajili ya Utengamano wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikizitumia taasisi za dini kama njia ya propaganda na kuwahadaa watanzania. Walifanya hivyo kwenye uchaguzi Mkuu wa 2005 ikiwemo kuwaahidi Waisalmu kupidisha mahakama ya Kadhi, walifanya hivyo kwenye uchaguzi wa mwaka 2010, walifanya hivyo kwenye Bunge Maalumu la Katiba, Walifanya hivyo kwenye Muswada wa Mabadiliko wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2015 ambapo tulishuhudia kwenye baadhi ya vyombo vya habari jinsi ambavyo wabunge wa Bunge lako wakigawanyika wakiwemo wabunge wa CCM wao kwa wao.

**Mheshimiwa Spika**, ni bahati nzuri sasa kuona kuwa viongozi wa dini wameamua kutokuwa sehemu ya kuwahadaa watanzania. Viongozi walio wengi wameamua kusimamia maslahi ya taifa kwa manufaa ya watu wote nchini. Viongozi wa dini wengi wamekataa kutumika na Serikali ya CCM katika kuwagawa Watanzania kupiditia udini. Ndio maana baadhi ya Viongozi wa dini sasa wameamua na kusema, sasa yatosha. Viongozi wa dini sasa wameamua kusimamia maslahi mapana ya Watanzania ikiwemo kuwapa elimu ya kuikataa Katiba Pendekezwa iliyochochakachuliwa na Serikali ya CCM.

Aidha, ni aibu kwa Serikali ya Rais Kikwete kuingilia faragha ya waislamu waliokua katika Hijja, Makka kwa kutumia mamilioni ya Watanzania na kudai kuwafata mahujaji hao kwa ajili ya kupigia kura kwa kile kinachoitwa Katiba Pendekezwa. Pengine Serikali hii inayotaka kutenganisha masuala ya dini na siasa leo pia imesahau kuwa walioshiriki katika Mchakato huu wa Katiba waliapa kwa kutumia dini zao. Ni katika mchakato huu ambaeo Matokeo yalichakachuliwa ikiwemo suala la Makamu Mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi Mheshimiwa Hajji Khamis Ambari alihesabiwa kupiga kura huku akiwa hajapiga kura.

**Mheshimiwa Spika**, kambi ya Upinzani Bungeni inahitahadharisha Serikali kutozigusa taasisi za dini hasa ambazo zimeendelea kutoa elimu kwa watanzania bila kuvunja taratibu za nchi hii. Aidha, tunawahasa viongozi wa dini zote na waumini wao kutokubali mpango huu ovu wa Serikali ya CCM unaopanga kupoka haki yao ya kikatiba na uendeshaji bora wa taasisi zao.

### **Mgogoro wa Madereva Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa Serikali inajukumu la kuratibu mahusiano ya makundi mbalimbali ya kijamii, kumekuwepo mgogoro mkubwa unaosababishwa na kukosekana kwa imani baina ya Serikali na Madereva kuhusu namna ya kusimamia maslahi yao. Kimsingi ni kweli kuwa Serikali haiqiri madereva kwa magari ya watu binafsi hasa wale wa magari ya abiria na magari ya mizigo. Lakin sote ni mashahidi jinsi ambavyo kulikuwa na usimamizi mbovu wa Serikali kuhusu madai ya madereva na adha ambayo wananchi waliipata mara mbili mfululizo kwa migomo ambapo awali madereva waligoma baada ya kutakiwa kusoma kila wanapoomba leseni upya katia Chuo cha Usafirishaji (NIT). Aidha, mgomo mwengine ulisababishwa na madai ya madereva juu ya mikataba na ujira wa kazi yao dhidi ya waajiri ambaeo ni wamiliki wa magari.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kauli mbalimbali za viongozi na mawaziri ambaeo walizitoa kwa madereva hao, ni dhahiri kuwa Serikali haijaweka mkakati wa kudumu kuhakikisha maslahi ya pande zote mbili za mgogoro yanalindwa bali mgogoro huo unatumwiwa na Seriali kama

chambo cha kujipatia kura kwenye Uchaguzi Mkoo ujao. Na ikumbukwe kuwa, ujanja unaofanywa na Serikali ndio uliopelekeea kutaka kupigwa kwa Mkoo wa Wilaya ya Kinondoni ambaye ilibidi afichwe na kulindwa na askari polisi kwa usalama wake Kituo cha Mabasi yaendayo Mikoani cha Ubungo .

Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuchukua fursa hii kuwataka madereva wote kuwa wavumilivu kwa kuwa, madhara ya migomo si tu inayumbisha uchumi bali pia ina athari kwa watanzania mafukara amba wengi ndio tunaotumia usafiri wa umma kwa ajili ya shughuli zetu za kila siku. Aidha, natumia rai ile ile aliyotoa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbewe pamoja na Mwenyekiti Mwenza wa UKAWA kutoka CUF Prof. Ibrahim Lipumba amba waliwafuata mlipokua na kuwasikiliza, kuwa hakuna marefu yasiyo na ncha. Kipindi hichi ni vyema kwa madereva wote na abiria wanaotumia usafiri wa umma kutafakari ni jinsi gani wameendelea kutumika na Serikali ya CCM. Ni dhahiri kuwa nguvu kubwa ya kufanya mabadiliko nchini itatokea iwapo watanzania tutashikamana, tutajiandikisha kwa wingi katika daftari la kudumu la wapiga kura na kujitokeza kwa wingi katika zoezi zima la Uchaguzi Mkoo Oktoba na kuchagua UKAWA popote pale mlipo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali itakayoundwa na Umoja wa Vyama vya Upinzani (UKAWA) inaendelea kuamini kuwa kila mtanzania ana haki ya kutoa maoni yake kwa njia ambayo anaona itapata usikivu wa watawala. Nasi kama UKAWA, tumeandaa Sera na miongozo itakayohakikisha uwepo na upatikanaji wa mazingira mazuri ambayo yataleta haki kwa kila mmoja wa madereva amba hufanya kazi katika mazingira magumu. Ni dhahiri kuwa Serikali imelilea tatizo hili kwa muda mrefu na pia imeendelea kutoa ahadi za uwongo kwa madereva kupitia kwa Waziri wa Kazi jambo ambalo liliisababisha mgomo kwa mara ya pili na kuleta adha kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Kambi ya Upinzani Bungeni inawasihi wamiliki wa mabasi na vyombo vya usafirishaji ikiwemo malori kutafuta suluhu ya kumaliza mgogoro huu amba una athari za kiuchumi si tu kwa dola bali hata kwao binafsi kama wafanyabiashara. Ni tumaini letu kuwa wamiliki wa vyombo vya usafiri watafanya kazi mazingira ya utumishi wa madereva ili kujenga uaminifu na mauhusiano bora baina yao na waajiriwa wao.

#### **Mgomu wa Wafanyabiashara**

**Mheshimiwa Spika,** katika utawala wa awamu ya nne ni dhahiri kuwa Serikali ilidhamiria kutowashirikisha wananchi kikamilifu katika maamuzi mbalimbali yanayoathiri shughuli zao za kila siku na hivyo kukosa imani kwa wananchi. Ulipaji wa kodi hauepukiki kwa Taifa lolote lile duniani. Kodi za wananchi zimeendelea kuwa chanzo kikubwa cha mapato ili zitumike katika utoaji huduma za wananchi. Kwa nchi nyingi za kiafrika, ulipaji wa kodi umekua hauendani na utoaji na upatikanaji wa huduma muhimu zikiwemo maji, elimu, huduma za afya, makazi, miundombinu na kadhalika, kwa kuwa Serikali zimeendelea kuwa na matumizi makubwa na hivyo kuzua malalamiko hasa kutoka kwa walipa kodi wakiwemo wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi makubwa ya Serikali ya CCM, ubadhirifu pamoja ufisadi mkubwa, vimejenga mazingira ambayo walipa kodi hawana imani na mifumo ya Serikali ya ulipaji wa kodi. Wafanyabiashara wametafsiri mifumo ya ulipaji wa kodi kama njia mojawapo ya unyonyaji unaofanywa na Serikali ya CCM. Kudhihirisha hili, Katibu Mkoo wa CCM abdulrahman Kinana alitaja utitiri wa kodi za Tanzania kama kikwazo cha wafanyabiashara kufanikiwa. Ndugu Kinana alitoa kauli hiyo mwezi April 2015 kwenye mikutano wa hadhara katika Viwanja vya Pasua mjini Moshi.

**Mheshimiwa Spika**, ni katika mukutano huo ambao Katibu Mkuu wa CCM ambaye Mwenyekiti wake ndiye Raisi alisema kuwa wafanyabiashara wanaumizwa zaidi na kodi hizo lakini hawana mtu wa kuwasemea zaidi ya kuendelea kunyonywa. Vilevile, kama kawaida yake Katibu Mkuu huyo aliwatupia lawama wabunge wa CCM kuwa wingi wao bungeni hausaidii kitu kwa sababu wameshindwa kuondoa sheria zinazomkandamiza mwananchi.

**"Kila kona ni kodi na kila kukicha ni kodi, Sumatra anadai kodi, Fire wanadai kodi, taasisi zingine zinadai kodi, yaani ni kero tupu"**

**Mheshimiwa Spika**, kauli ya Katibu Mkuu wa CCM Kinana inathibitisha madai ya muda mrefu ya wafanyabiashara nchini juu ya kunyonywa kwao na mifumo holela ya kodi. Ni katika kadhaa hii ambayo imesababisha mara kwa mara wafanyabiashara kuendelea kugomea mashine za kieletroniki za ulipaji wa kodi kitaalamu zinajulikana kama EFDs. Mashine hizi zinazotolewa na TRA zinatolewa kwa gharama kubwa na pia kiwango cha asilimia 18 kimeonekana kuwa kikubwa kwa wafanyabiashara. Ni katika kadhaa hii hii ndiyo iliyopelekea kukamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa Mwenyekiti wa Jumuia ya Wafanyabiashara Tanzania, Johnson Minja (34) kwa madai ya uchochezi wa kuwataka wafanyabiashara kugomea matumizi ya EFDs Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka leo kumeendelea kuwepo kwa migomo baridi inayofanywa na wafanyabiashara maeneo mbalimbali nchini, kama njia ya kushinikiza kufutiwa kesi kwa kiongozi wao huyo. Vile vile, migomo hii imeendelea kuleta athari kwa walaji kwa kuwa wafanyabiashara wamekuwa wakifunga maduka mara kwa mara. Lakini Serikali kwa nyakati tofauti hata kwa kauli ya Waziri Mkuu Mizengo Pinda imeonesha wazi kutotaka suluhi na wafanyabiashara ikiwemo kumfanya hila Ndugu Ninja na kumuweka rumande wakati ambao Serikali imedai inafanya maridhiano na wawakilishi wa wafanyabiashara nchini.

Kambi ya Upinzani Bungeni, inasimama pamoja na wafanyabiashara wote nchini na kuwataka kusimama imara katika kupigania maslahi yao. Aidha, tunaendelea kutumia wataalamu wetu mbalimbali ambao wanatoa elimu juu ya umuhimu wa ulipaji kodi nchini. Ni kwa misingi bora ya uwajibikaji inayotupa imani kuwa watanzania watatupa dhamana ya kuwaongoza ili kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uwajibikaji katika matumizi na mapato ya Serikali hasa kodi za wananchi wa Tanzania.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka wananchi kuchagua Serikali itakayotokana na Umoja wa Vyama vya Upinzani "UKAWA" ili iweze kutoa elimu sahihi na msaada kwa wafanyabiashara na walaji, itakayowawezesha kushiriki katika utoaji wa huduma bora kwa kulipa kodi kwa mfumo utakaodhibitiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Tunawaahidi watanzania kuwa, kodi zao hazitopotea bure na tutawajibikiwa kwa kuanda mifumo ya wazi itakayochambua mapato na matumizi ya Serikali ya UKAWA.

### **Wanafunzi wa Elimu ya Juu Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Serikali ya CCM imeshindwa kuisimamia ipasavyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini (HESLB). Hii inatokana na Serikali kuchelewesha kupeleka fedha wa ajili ya wanafunzi na hivyo kufanya Bodi ishindwe kufanya kazi kwa ufanisi. Matokeo ya ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi imezua migogoro mingi ikiwemo migomo ya wanafunzi, kusimamishwa kwa wanafunzi ama wanafunzi kuzuiwa kufanya mitihani ama kukatishwa masomo kwa kushindwa kulipa ada mbalimbali za vyuo. Aidha, kumekuwa na misigano ya muda mrefu baina ya Wanafunzi na utawala wa vyuo mbalimbali na misigano hii huleta athari kubwa kutohana na Serikali kushindwa kuisimamia ipasavyo. Kwa mfano migogoro na migomo ya vyuo vya UDOM, UDSM, MUHAS iliyopata kutokea katika utawala wa Rais Kikwete ni kielezo kuwa Serikali bado imeendelea kuchukua hatua dhidi ya matokeo badala ya kushughulikia vyanzo vya matatizo hivyo kuacha madai ya msingi ya wanafunzi wa vyuo hivyo yakipuuzwa. Ni wanavyuo wengi ambaa wamesimamishwa vyuo, kuna waliosababishiwa

ulemavu, wengine wakashindwa kurudishwa vyuoni na wengine wakiwa hawajui hatma ya masomo yao kutokana na matatizo ama madai yao kutopatiwa ufumbuzi wa kudumu.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa mwaka 2007 Rais Jakaya Kikwete aliahidi kuyapatia ufumbuzi matatizo ya wanafunzi wa elimu juu nchini ili kupunguza migomo na migogoro. Katika Mkutano wake na wanafunzi wa vyuo vikuu wa CCM mwezi Februari 2007 alikwenda mbali zaidi kwa kuwaeleza kwamba hakuna mtoto wa maskini atayeshindwa kuendelea na masomo kutokana na masharti ya mikopo. Ikiwa ni miaka 8 imepita toka ahadi hizo zitolewe migomo katika vyuo vikuu imeendelea na pia wapo watoto wa walalahoi ambao wamefaulu kidato cha sita lakini wemeshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa mikopo na upendeleo wa wazi katika upangaji wa viwango vya madaraja ya mikopo nchini usiozingatia vigezo vilivywewekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachukua nafasi hii kuwaeleza watanzania wote na watoto wa kitanzania kuwa, Umoja wa Vyama vya Upinzani "UKAWA" bado inaamini kuwa ikiwa Mwalimu Nyerere aliweza kuwasomesha watoto wa wakulima mpaka elimu ya juu basi nasi tutaweza kutoa elimu bure kwa watanzania wote bila kujali rangi, dini, kabilia wala madaraja yao katika jamii. Ni rai yetu kubwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kukataa kutumika pamoja na kuhadaika na ahadi kemkem za CCM bali watumie fursa hiyo kujandikisha kwa wingi katika daftari la kudumu la wapiga kura mwaka huu popote walipo na kupiga kura Oktoba 2015. Tuwakumbushe pia vijana wote waliofanikisha kuundoa utawala wa Rais Goodluck Jonathan na kufanikisha ushindi wa Rais Buhari. Hivyo hii ni fursa pekee ya kuwaepusha na maumivu makali ya miaka mitano mingine iwapo watafanya makosa kuirudisha CCM madarakani Oktoba 2015.

#### **Migogoro Kati ya Wakulima na Wafugaji**

**Mheshimiwa Spika**, katika miaka 10 ya mateso ya awamu ya nne kumeibuka migogoro kati ya wakulima na wafugaji hasa katika sehemu za Morogoro, Rufiji, Kongwa, Babati, Arusha n.k. Kwa muda mrefu tumekuwa tukipendekeza mara kadhaa njia za kuchukua kuondokana na jambo hili kwa serikali kuchukua hatua mahsus za kupima ardhi nchi nzima na kuyatambua maeneo kwa ajili ya matumizi kwa makundi haya lakini bado tumeendelea kushuhudia migogoro hiyo kuendelea kugharimu maisha ya watanzania masikini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kusema kuwa, sasa imetosha na ni wazi kuwa Serikali imeshindwa kutatua tatizo hilo.

#### **Serikali kutishia NGO Zinazotekeleza Majukumu Yake**

**Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya dalili za Serikali inayoshindwa ni pamoja na kuogopa Kivuli chake chenyewe. Serikali hii ambayo imetumia fedha nyngi na nguvu nyngi katika kuhalalisha maovu yake imejikuta ikishindwa na nguvu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ambazo kwa kiasi kikubwa zimeweza kuonesha madhaifu ya Serikali kwa kutoa elimu kwa watanzania wote kinyume na matarajio ya Serikali. Ni hivi karibuni mkoani Geita Januari mwaka huu Mashirika zaidi ya 1000 yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania yalitangaziwa kufutwa kwa usajili wake kunatokana na kutotimiza matakwa ya kisheria katika utendaji wake kazi toka yaliposajiliwa. Ni kwa mujibu wa kikao cha bodi ya uratibu ya mashirikia yasiyo ya kiserikali ambacho kilieleza kuwa kufutwa kwa mashirika hayo kutokana na kushindwa kutoa taarifa za kila mwaka kama inavyosisitizwa na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na 24, 2002. Mashirika hayo pia yanadaiwa kukosa sifa ya kuendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa inaelekea ukingoni, Serikali ya CCM inakumbuka shuka kumekucha huku kwa kipindi cha miaka 10 ya utawala wake kikishindwa kukagua utendaji wa

mashirika hayo. Ni matumaini yetu kuwa, Serikali hii haitoisahau Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) inayoongozwa na Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete, ambayo nayo ilikiuka masharti na kanuni za uendeshwaji kwa kuwa Waziri (Mhe. Sophia Simba) mwenye dhamana ya kuzisimamia taasisi zisizokuwa za kiserikali kuwa Mjumbe wa Bodi ya WAMA. Ikiwa Serikali imeamua kusafisha mashirika hayo yasiyo ya Kiserikali isisahau kuifutia WAMA usajili wake kwa kukiuka Sheria za nchi.

### **Hali ya Usalama Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, hali ya Usalama nchini sio nzuri na hivyo ni dhima ya Serikali mpya ijayo itakayoundwa na upinzani kuboresha kitengo cha usalama wa Taifa kuliko hali ilivyo sasa. Hii ni kutokana na ujisadi mwingu kuendelea kujitokeza nchini na kushindwa kuziliwa na kitengo hiki kwa maslahi ya taifa zima. AIDHA, mauaji na ukatili dhidi ya watu wenyewe ulemavu wa ngozi yameendelea kulitikisa taifa. Ni jambo la kushangaza kuwa Usalama wa Taifa unashindwa kutoa taarifa za kiinteljensia kuhusu ukatili kwa kundi hili la watu wasiozidi 200,000 nchi nzima. Jambo la kusikitisha zaidi, yakiwa yamepita si chini ya masaa 48 tangu Waziri Mkuu Pinda asome hotuba yake ya kukabiliana na mauaji ya watu wenyewe ulemavu wa ngozi tarehe 12 Mei 2015, tukio la kusikitisha la kukatwa kwa mkono kwa mwanamama Remi Luchoma (30) limetokea kwenye mkoa wa Katavi, tarehe 14 Mei 2015 anapotoka Waziri Mkuu mwenyewe. Hii ni aibu kubwa kwa utawala wa CCM na Rais Kikwete.

### **Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, Kitendo cha Chama Cha Mapinduzi kushindwa kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kiwango kikubwa kuliko matarajio yake na kulazimisha kuapishwa kwa viongozi wake ambao wananchi hawakuwachagua kulipelekea pia kwa baadhi ya viongozi wa Serikali za Mitaa na wakazi wake kuchukua jukumu la kuwaapisha viongozi wao wenyewe. Jambo hili liliababisha vurugu na tataruki kubwa miongoni mwa wananchi ambao walikuwa wanapinga kuchakachuliwa matokeo na Serikali ya CCM. Jambo hilo linatoa picha juu ya kitakachotokea katika uchaguzi wa mwaka huu ambapo kwa uhalsia ni kuwa Chama cha Mapinduzi hakiko tayari kuachia ngazi hata pale ambapo wananchi wamekikataa. Kwa vyovypote vile Jambo hili litahatarisha amani na utulivu katika nchi. Tunapenda kuwakumbusha CCM na vibaraka wake kuwa, haki haiporwi bali hucheleshwa na watananzia sasa wameamka.

### **Mahusiano ya Vyama vya Siasa**

**Mheshimiwa Spika**, katika awamu hii ya nne ya miaka kumi ya uchungu na maumivu makali tumeshuhudia kuwepo kwa mahusiano yasiyordhisha kati ya vyama vya siasa hasa uhasama na kushambuliana kwa silaha na vitisho wakati wa chaguzi kuu na chaguzi ndogo. Tumeshuhudia kuchomwa kwa ofisi za Chama cha Wananchi CUF huko Zanzibar, kuumizwa kwa viongozi wa vyama vya upinzani katika maeneo mbalimbali nchini na hata baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani kubambikiwa kesi zinazotokana na uchaguzi. Jambo la kushangaza na kustaajabisha, ni kuwa hakuna mwanaCCM ye yote ambaye amekumbwa na kesi za kudhuru zinazohusiana na chaguzi ambazo zimefunguliwa na Jamhuri bali ni wanasiwa wengi wa upinzani ambao mpaka sasa wana kesi zinazotokana na chaguzi za mwaka 2005 na 2010. Kwa vyovypote vile kukithiri kwa vitendo hivi ndiko kunakolazimu vyama vya siasa kuwa na utaratibu wa kulinda mali na viongozi wao kwa gharama zao wenyewe. Na ni kwa kushindwa huko kwa Serikali kulinda vyama kunapotupa sababu ya kujilinda wenyewe kwa mifumo yetu kama ambavyo CCM inafanya kwa kuratibu na kuendesha kikosi chake cha Ulinzi cha Kijani (Green Guard) kwa kuwa nao CCM hawana imani na mfumo wa ulinzi na usalama wa Serikali yake yenyewe.

### **Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011-2016)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya CCM kwa mbwembwe kubwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 iliwasilisha Bungeni Mpango wa Miaka mitano ambao ulizinduliwa na Rais Jakaya

Kikwete ambao hata hivyo katika mipango na bajeti za kila mwaka tuliweka bayana namna ambavyo Serikali imekuwa haifuati mpango huo. Jambo hilo linadhihirika sasa ambapo mipango mingi ambayo ilikuwa kwenye mpango ule haijatekelezwa na hata bajeti za Serikali hazifluati vipaumbele kama ambavyo vimeainishwa kwenye mpango huo ambao tuliaminishwa kuwa ungeweza kuleta maisha bora kwa kila mtanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kama Serikali yenewe inapanga na kuwasilisha hapa Bungeni, na hata baada ya kupanga inashindwa kusimamia na kutekeleza mpango wake yenewe; ni ishara kuwa Serikali hiyo imechoka. Kambi ya Upinzani Bungeni imejiandaa vilivyo kuhakikisha kuwa Tanzania inaweka vipaumbele ambavyo vinatekelezeka na vitawenza kutatua matatizo ya watanzania kupitia Serikali itakayoundwa na UKAWA ifikapo Oktoba 2015.

#### HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie kwa kuyakumbuka maneno ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliywahi kusema; "Na hakutakuwa na watu wa kizazi hiki na karne hii ambao watatakiwa kujitoa muhanga kwa ajili ya maisha bora katika siku zijazo wakakubali, wakati wanawaona watu wachache wakiendelea kuneemeka machoni pao bila kujali wakati ujao, wakati wao (wananchi) na watoto wao wakiendelea kuishi katika maisha duni na dhalili."<sup>1</sup>

Hizi ni salamu kwa CCM ambao wanaendelea kusema kuwa 'kelele za mpangaji hazimnyimi mwenye nyumba usingizi'. Chagua UKAWA kwa mustakabali wa Taifa kwa kuwa, mwenye nyumba amejenga nyumba kwenye kiwanja cha mkopo, marejesho Oktoba 2015!

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Esther N. Matiko (MB),

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI  
OFISI YA RAIS – MAHUSIANO NA URATIBU**

18.05.2015

**MWENYEKITI:** Sasa namwita mchangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Kapteni Mstaafu John Chiligati, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye hoja ya bajeti, nitoe angalizo dogo tu kwamba pengine hatuwatendei haki wananchi wanaotusikiliza kwa kugeuza

<sup>1</sup> 'Reflections On Leadership in Africa' VUB University Press, 2000.

Bunge hili kuwa ni uwanja wa kampeni. Kipindi cha kampeni bado, tuwe na subira kitafika, kila chama kitapata fursa ya kumwaga sera zao kwenye kampeni. (Makof)

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawachanganya wananchi tunaposema kwamba sisi mkituchagua mshahara kima cha chini milioni moja, barabara za lami kila mahali na kadhalika bila kuwaambia hizo pesa za kufanya mambo hayo mtatoa wapi wakati ndiyo bajeti hii sasa tunatakiwa tuchambue, tuishauri Serikali pesa zipatikane ili tufanye mambo hayo, ndiyo kazi ambayo imetuleta hapa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuwatendee haki wananchi kwa kuishauri Serikali jinsi gani ya kutatua matatizo yao kupitia bajeti hii. Ndiyo mambo wananchi wanataka kusikiliza siyo mambo ya kampeni rahisirahisi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niingie kwenye shughuli za bajeti. Nataka nianzie na hotuba ya Waziri Kombani ule ukurasa wake wa 17, ameeleza habari za urasimishaji wa mali za wanyonge, mpango wa MKURABITA. Kwanza nitangaze maslahi kwa mujibu wa kanuni zetu kwamba mimi ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya MKURABITA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa ule zimeelezwa kazi ambazo MKURABITA wamezfanya, nataka niwapongeze MKURABITA kwa kazi ambazo zimeorodheshwa kwenye kitabu chetu cha bajeti, urasimishaji ardhi katika Wilaya mbalimbali na kutoa hati miliki za kimila na vilevile kurasiusha biashara za wafanyabiashara wadogo wadogo, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili niungane na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwamba pamoja na kazi ya urasimishaji ambayo imefanywa na MKURABITA lakini urasimishaji wenyewe unakwenda taratibu mno, kasi ni ndogo. Jinsi tunavyochelewa kurasiusha rasilimali za wanyonge ndivyo tunavyochelewa kuondoa umaskini. Watu hawa wanaoitwa wanyonge wana rasilimali zao, wana ardhi hawa, wana biashara ndogondogo hawa, lakini haziwasaidii kujiondoa kwenye umaskini kwa sababu hazijarasiushwa. Ile ardhi ya mwananchi wa Manyoni inamsaidia tu kulima muhogo, kisamu, mahindi na karanga lakini kama haijarasiushwa haimsaidii kuwa mtaji ambao utamsaidia afanye mambo makubwa zaidi. Kwa hiyo, urasimishaji ni suala ambalo litaondoa umaskini harakaharaka lakini unakwenda pole pole. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini unakwenda polepole? Wamesema wenzetu wa Kamati, kwanza, bajeti zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za urasimishaji ni ndogo sana. Kuanzia MKURABITA wenyewe bajeti ni ndogo sana, karibu shilingi bilioni tatu tu. Halmashauri ambazo ndivyo hasa vyombo vya kurasiusha, maana MKURABITA yeye anawezesha na kuratibu, anayetakiwa kurasiusha ni Halmashauri zetu za Wilaya mbalimbali lakini bajeti ni ndogo sana. Wizara ya Ardhi ambaye ndiye msimamizi mkuu wa sera nzima ya ardhi naye bajeti vilevile ni ndogo sana, tatizo linaanzia hapo.

Nataka niishauri Serikali, maana kazi yetu sisi Wabunge ni kushauri, hili ni eneo ambalo linakwenda kuondoa umaskini moja kwa moja yaani kama ni sindano unapiga palepale penye ugonjwa. Ni eneo ambalo lazima kweli tuliongezee bajeti. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa kwamba MKURABITA hata mwaka huu unoishia mwezi Juni wamepangiwa shilingi bilioni tatu, lakini wiki mbili zilizopita tulivyokutana kwenye Bodi yetu zile pesa zilikuwa hazijatoka. Sasa katika eneo ambalo linaondoa umaskini kama hili halafu senti hata moja haipo, hapana! Serikali hapa hamuwatendei haki wakulima wadogo wadogo, hamuwatendei haki wanyonge na Waziri ukija hebu tueleze ni lini hasa MKURABITA watapata fedha katika miezi hii iliyobaki. Wananchi vijijini sasa wanadai, wafugaji na wakulima wanadai warasiushiwe ardhi yao wapate hati miliki wazitumie kama dhamana ya kupata mikopo benki. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwa nini urasimishaji unakwenda polepole, chombo chenyewe hiki MKURABITA ni kidogo sana, kina watu kama 27 tu, ndiyo wasimamie urasimishaji nchi nzima. Halafu chombo chenyewe hakina nguvu ya kisheria. Hata wanapokwenda kuwezesha hizi Halmashauri wanakwenda kuwapa elimu, wanawapa vifaa vya kupimia, wanawapa hata hela za kuanzia, wakishaondoka wakirudi wanakuta vile vifaa vimepotea, zile hela hawajarasiusha, hata nguvu ya kuwahoji hawana kisheria. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza Serikali itazame mfumo wa kuongezea nguvu hiki chombo cha kurasimisha. Sasa hivi MKURABITA ni programu tu, hebu tuwe na chombo hasa cha kisheria, kitaitwa jina gani sijui, kama ni Tume kama ni nini lakini kiwe kina nguvu ya kusimamia urasimishaji, kina nguvu ya kuhoji, kina nguvu ya uwezeshaji. Ili hiki chombo tunachoshauri Serikali kifanye kazi vizuri kiundiwe Mfuko Maalum wa Urasimishaji ili hata hizi Halmashauri ambazo kupitia bajeti za kawaida ni tabu kupata pesa za kutosha ziende zikakope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, chombo hiki kiwe na mfuko, tena ukae benki na ufanye kazi kibenki. Kwa sababu sasa hivi pale kwenye Wizara ya Ardhi kuna Mfuko wa kukopesha Halmashauri lakini ni mdogo na kwa sababu unasihamiwa Kiserikali, kirasi, wanakopa hawarudishi, ule mzunguko haupo. Huu tunaopendekeza ambaa utakuwa chini ya hii Tume ya Urasimishaji ukae benki na ufanye kazi kwa utaratibu wa benki, uwe ni dhamana tu kwamba Halmashauri inapokwenda, Serikali imeshaweka dhamana wakope kwa taratibu za benki, warudishe kwa taratibu za benki na uzungu. Tukifanya mambo haya mawili tunaamini kabisa kwamba urasimishaji utakwenda kwa kasi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, muda ni mdogo sana, niende kwenye Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi. Kama Kamati ilivyo sema, ni kweli tuna mmomonyoko mkubwa sana wa maadili ya viongozi na hiki ndicho chombo cha kusimamia hayo maadili, sasa lazima tuishauri Serikali jinsi gani chombo hiki kiweze kusaidia. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hili la viongozi kutumia ofisi za umma kwa maslahi binafsi, ni tatizo kubwa na linaathiri sana maadili ya kazi na uongozi katika nchi yetu. Badala ya kiongozi atumie nafasi ya ofisi ya umma kwa maslahi ya umma ambavyo ndivyo inavyotakiwa sasa viongozi wanatumia ofisi za umma kwa maslahi biafsi. Jambo hili tulianza kwenda kukaa pemberi ya barabara tuliporuhusu kiongozi wakati huo huo kiongozi wa umma, wakati huohuo ni mfanyabiashara na kadhalika, hapo ndipo tulipoanza kwenda pemberi. Sasa ulishatolewa ushauri huko nyuma kwamba hebu tuweke sheria itakayotenganisha, mtu achague, ukitaka kuwa mfanyabiashara fanya biashara, tumikia nchi hii kwa kufanya biashara. Kama unataka uongozi wa umma basi uwe kiongozi wa umma, tumikia watu. Ile sheria tunataka wakati mna-wind up mtueleze imefikia wapi? Nchi nyingine sheria hii wanayo na inawasaidia kuondoa huu mgongano wa kimaslahi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa rushwa vilevile ni tatizo kubwa sana. Kuna rushwa ya sirisiri haionekani, kuna rushwa nyingine mtu tu Chiligati mnamjua na mshahara wake na kuku anaofuga lakini hizo malii alizonazo, hayo majumba, magari ni lundo kabisa kabisa. Hata hamhoji kwamba wewe bwana hebu tueleze, hakuna anayehojojiwa, kwa hiyo watu wanaona ni sawasawa tu. Nadhani hapa Serikali vilevile mtueleze ni kwa nini hamuwezi mkatuhoji kupitia Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Nyangwine.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nianze kuchangia hoja hii lakini kabla ya hapo naomba niweke mambo sawa kwa kumwambia Mheshimiwa mwenzangu Esther Matiko kwamba kule Tarime afanye utafiti wa kutosha na kamili baada ya hapo ndipo aje aseme hayo aliyo sema, namshauri labda aende Musoma au sehemu nyingine. (Kicheko/Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, mimi nimwambie kwamba hii hotuba nina wasiwasi kama ameifanya utafiti wa kutosha. Anasema kwamba viongozi wa dini hawaiamini CCM, mimi nafikiri kwamba yeye amefanya utafiti kwa Manabii wa Uongo. Unajua kuna viongozi wa

dini na Manabii wa Uongo. Sasa kama ni Manabii Uwongo ndiyo hawaiamini CCM basi afanye utafiti wa kutosha. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza Mawaziri katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Waziri wa Kazi Maalum, Utumishi, Mahusiano na Uratibu pamoja na Utawala Bora. Tumekaa nao, mimi ni Mjumbe wa Kamati, tumejadili masuala mengi sana yanayohusiana na Ofisi ya Rais na nikiri moja kwa moja kwamba naunga mkono maoni ya Kamati na mengine ambayo nichangia kuongezea nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Mojawapo ya kazi kubwa ambayo Chama cha Mapinduzi kimefanya ni kushughulika na umaskini wa kaya binafsi ambazo ni maskini sana na TASAF ndiyo imefanya kazi hiyo. Wale ambaa hawaajafanya utafiti wa kutosha wafike na waangalie TASAF inavyofanya kazi. Kaya nyingi maskini zinakiri, tumekwenda kama Kamati wanasema kabisa walikuwa hawawezi kula hata mlo mmoja kwa siku lakini sasa hivi wanakula milo miwili au mitatu kwa siku, watoto wao wanasoma. Jamani tufanye nini ili muone kwamba watu wanafanya kazi? Wengine wao tumesafiri nao wamefika mpaka hata Mexico wameona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mpango huu wa TASAF uwezeshwe kwa kupewa fedha za kutosha ili uweze kusaidia familia maskini maana najua kabisa kwa kufanya hivyo tutaweza kupunguza pengo lililopo kati ya maskini na matajiri. Mimi napendekeza kwamba TASAF ipewe hela za kutosha ili kufanikisha suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mimi napendekeza kwamba elimu itolewe kwa zile familia zinazosaidiwa ili angalau kila baada ya miaka mitatu au mitano waweze ku-graduate watokane na hili lindi la umaskini. Njia mojawapo ya kufanya ni kuwapatia elimu ya ujasiriamali. Naomba hilo Waheshimiwa Wabunge tushirikiane na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ili kuhakikisha tunasaidia maskini kuondokana na lindi la umaskini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea Tume ya Mipango. Tume ya Mipango ni dira ya kusaidia ...

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Nyambari kaa chini..

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Huyo taarifa anataka kudanganya, Mwenyekiti hajampa ruhusu kwa hiyo naendelea mimi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mwenyekiti nilikuwa ...

**MWENYEKITI:** Hatuna muda naomba tuendelee, endelea Mheshimiwa Nyangwine.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni muhimu ili mjadala uende vizuri.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu anafahamu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa ambazo ni muhimu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae sijakuruhusu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Sasa hauniruhusu kwa kutumia kifungu gani?

**MWENYEKITI:** Nimesema naomba ukae.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde dakika zangu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kifungu chochote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali naomba ukae kwanza.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha taarifa hujakifuta kwenye Kanuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali kaa kwanza, Mheshimiwa Nyangwine endelea. (Makofii)

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde dakika zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango imesaidia sana na inabuni mipango ya maendeleo. Katika nchi yoyote ile, Tume ya Mipango ndiyo dira.

Napendekeza kwamba Tume ya Mipango ifanye utafiti wa kutosha kuweza kubaini kwa nini uchumi wa Tanzania unakuwa kwa kasi sana lakini raia wa Tanzania ni maskini, raia wa Tanzania hawana hela za kutosha.

Vilevile ifanye utafiti wa kutosha kuhakikisha kwamba rasilimali tulizojaliwa kama wanyama, mito, bahari, maziwa, misitu, gesi, mafuta, madini na hata geographical location ya nchi yetu inawanufaishaje watu maskini. Tutumie nafasi hiyo ili kuweza kuikomboa nchi yetu kutoka katika lindi la umaskini.

Naishauri sana Tume ya Mipango ifanye tafiti za kutosha na hili litawezekana endapo Tume ya Mipango itawezeshwa na ifanye kazi kwa umakini wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika Tume ya Mipango naishauri iangalie namna gani rasilimali zinavyoibowiwa na wawekezaji uchwara, wawekezaji ambaa ni wezi na siyo waaminifu ili kuwafanya raia wa Tanzania waweze kuwa ndiyo wawekezaji wanaoweza kumiliki uchumi wa nchi yetu. Hili litawezekana endapo Tume ya Mipango itafanya tafiti za kutosha. Namshukuru sana mama yangu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwenye Kamati alisitiza na alieleza namna Tume ya Mipango itakavyoweza kufanya tafiti katika kipindi hiki.

Mimi naomba Bunge lako lisaidie sana Tume ya Mipango ipewe fedha za kutosha ifanye utafiti wa kutosha ili kuwawezesha wananchi wetu, Watanzania wenzetu ndiyo wawe wawekezaji katika nchi yetu na ndiyo waweze kumiliki uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Kamati na hasa taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti kuhusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Mengi yamesemwa lakini tunapendekeza kwamba taasisi hii iongezewe uwezo. Tunashukuru kabisa kwamba mwaka jana waliweza kuajiri wafanyakazi zaidi ya 400 na ofisi sasa hivi zinajengwa katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati imependekeza na mimi naomba kurudia kwamba ishirikiane na vyombo vya dola kama vile Polisi, Mahakama hata Usalama wa Taifa kuwachunguza, kuwabaini, kuwakamata, kuwashtaki, kuwahukumu, kuwafunga, kuwafilisi na hata ikiwezekana tutunge sheria ya kuwanyonga au kuwapiga risasi wala rushwa, wala rushwa ni tafizo katika nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Naishauri Serikali iiwezeshe Sekretarieti hii ifanye kazi kwa uadilifu, iwjengjee ofisi na hali kadhalika iwave meno ya kuchunguza sio tu kuhakiki madeni na rasilimali au mali za viongozi tu, iweze hata yenyewe kushtaki na iweze kutoa hukumu na mwisho kabisa ipanue wigo viongozi wote wa umma kuanzia ngazi ya Kata, Tarafa, Wilaya, Mkoa na Taifa, viongozi wote wachunguzwe wakiwemo Madiwani ili kubaini hizo mali wanazozipata kwa haraka haraka, kijana anamaliza chuo kikuu baada ya miezi miwili, miaka miwili unakuta amejenga majumba makubwa, anaendesha magari ya kifahari, heshima haipo, dharau kubwa, hawa watu naomba nao wachunguzwe kwa kuiwezesha hii taasisi iwezeshw.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Taasisi ya Uongozi (*Uongozi Institute*) iwezeshw kifedha na hali kadhalika ifanye utafiti na iingize mtaala wa maadili katika mafunzo yao ili kuwafunza viongozi kuwa na maadili mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea kuhusu Bodi ya Mishahara. Tulishauri kwamba ufanyike utafiti na Mtaalam Mwelekezi awepo ili kubaini kwa nini kunakuwepo na tofauti kubwa sana kati ya Mkurugenzi na mtumishi wa chini. Unakuta Mkurugenzi anapata shilingi milioni 12 lakini mtumishi wa chini anapata shilingi 350,000/= na wanafanya kazi katika ofisi moja hiyo hiyo na maslahi mengine pia yanatofautiana, nashauri kuwepo na uwiano wa kutosha. Namshukuru Waziri alieleza Kamati kwamba amejitahidi kufanya hivyo lakini hiyo taarifa naomba ikamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi ya Tanzania, kwa kuwa MKURABITA imeshindwa, mimi nashauri ardhi iingizwe katika *Big Results Now* ili ardhi ya Tanzania ipimwe na hii itasaidia kila Mtanzania kujivunia kwamba ana kitu cha thamani kinachoweza kumsaidia.

Kwa hiyo, naomba Serikali isikie, isaidie na ifanye kila linalowezekana ardhi ya Tanzania ipimwe. Watanzania najua kwamba wanawenza kuchangia kadri watakavyoweza ili ardhi yao ipimwe ili wawe na kitu cha kujivunia katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea nashauri uwezeshw na naamini kabisa kwamba Rais ajaye atatoka ndani ya CCM achangie Mfuko huu ili uweze kufanya kazi kuwasaidia maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Mary Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Clara Mwatuka na Mheshimiwa Philipa Mturano ajiandae.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kuchangia naomba nianze kwa kusema kwamba hotuba ya wenzetu upande wa Upinzani inasema kwamba wao watakaposhika nchi hii watahakikisha kwamba wafanyakazi wanapata mishahara minono na kuondokewa na kero zote ambazo zinawakabili. Napenda kuwaambia wafanyakazi kwamba kheri ya malaika unayemjua kuliko shetani usiyemjua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia suala la utawala bora. Suala hili lingeanzia kwenye vyama vyetu. Tukiangalia humu ndani katika huo utawala bora kwenye Viti Maalum kuna kaka, dada, shemeji na nyumba ndogo. Nafikiri wanapozungumzia suala la utawala bora kwamba Chama cha Mapinduzi hakina utawala bora basi tungearanza kwenye vyama vyetu kuonyesha suala la utawala bora ndani ya vyama vyetu. (Makof/ Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Na watoto wamo humo humo!

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana aliyezungumza na Mheshimiwa Esther kazungumzia suala la Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kwamba katika ziara zake amekemea sana suala la kodi yaani utozwaji wa kodi ambazo hazina ulazima kwa wananchi. Napenda kumpongeza kwa sababu Katibu Mkuu wa CCM ndiye mwenye llani, ndiye anayeisimamia Serikali yake kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri. Nashukuru amelitambua hilo kwamba Katibu Mkuu amefanya kazi nzuri ya kusimamia na kukemea mambo ambayo hayaendi vizuri kwa Serikali yetu. (Makof)

**MBUNGE FULANI:** Swadakta.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake alioitoa siku ya Mei Mosi paleMwanza. Alitoa hotuba ambayo iliwapa matumaini mapya wafanyakazi juu ya maslahi yao.

Naiomba Serikali kwa mwenendo uleule wa Mheshimiwa Rais alioutoa wa kuwapa matumaini mapya wafanyakazi juu ya maslahi yao basi ihakikishe kwamba inatekeleza kwa kuwaongeza mishahara watumishi hasa wa kima cha chini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa mishahara ya kima cha chini wanapata taabu kutokana na hali ya maisha inavyopanda kila wakati. Wafanyakazi hawa wana watoto wanawasomesha na pia wanahitaji kujenga nyumba bora, lakini kutokana na kipato kidogo wanachokipata wanashindwa kukidhi haja ya kuwapeleka watoto wao wakasome mahali pazuri, wanashindwa kuwa na nyumba bora na kulipa hata kulipa kodi tu katika nyumba ambazo wamepanga.

Kwa hiyo, naomba sana, matumaini mapya aliyowapa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania basi Serikali ione umuhimu wa kuyafanyia kazi na hatimaye kuongeza mishahara kwa kima cha chini ili waweze kujikumu kimaisha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la madeni. Tumekuwa tukizungumza sana kuhusu suala la madeni kwa wafanyakazi. Serikali imekuwa ikitoa ahadi kwamba inaratibu madeni hususani ya walimu, wauguzi, madaktari na askari. Naiomba Serikali na hasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu ihakikishe kwamba inayaratibu madeni hayo na kuwalipa wafanyakazi ambao wanadai madai yao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwalipa wafanyakazi madeni yao unarejesha mioyo ya kufanya kazi vizuri zaidi. Wafanyakazi hawa wanapokuwa wanapata mishahara midogo halafu wanakuwa na madai ya malimbikizo ya likizo wanakufa moyo wa kufanya kazi. Kwa hiyo, naitaka Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ihakikishe kwamba tunawatendea haki wafanyakazi ambao wanadai madai yao ili walipwe na hatimaye wafanye kazi vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la upungufu wa wafanyakazi. Naishukuru Serikali, ni kweli kabisa imejitahidi kuhakikisha inaongeza idadi ya wafanyakazi lakini bado idadi hiyo haitoshi kwa sababu bado kuna upungufu wa wafanyakazi katika sekta mbalimbali kama vile ya wauguzi na madaktari. Nazungumzia Madaktari na Wauguzi kwa sababu tumeamua tunajenga hospitali kwa maana ya zahanati na vituo vya afya katika Kata na Vijiji lakini kuna upungufu wa wauguzi na madaktari. Kwa hiyo, naiomba Serikali, kwa kuwa wananchi wamefanya jitihada kubwa ya kujenga vituo vya afya na kujenga zahanati basi tuhakikishe kwamba wanapatikana watumishi ambao watafanya kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwa walimu, naishukuru Serikali juzi katika sherehe za Maadhimisho ya Elimu niliona Naibu Waziri akitoa idadi ya walimu ambao wameajiriwa safari hii. Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na kwamba kumekuwa na ongezeko la walimu hasa wa sayansi lakini bado hawatoshi, naomba ongezeko la walimu liendelee ili kusudi kazi ya kuwafundisha watoto wetu ifanyike kwa uangalifu na ustadi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la wenzetu Wagani. Huko vijiji tunahitaji kuwepo na wagani kwani waliopo ni wachache. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kada ya wagani, ni vizuri nao wakapata ajira ili kusudi wafanye kazi zinazopaswa kufanya huko vijiji. Wakati Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie ni mkakati gani ambao wameuweka ili kupata watumishi hawa kama ambavyo nimezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache niliyokuwa nayo, naomba nishukuru kwa kunipatia nafasi na niendelee kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo inatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Clara Mwatuka.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kunijalia kuwepo mpaka tarehe ya leo ukilinganisha na afya yangu ilivyokuwa na mtihani toka nyuma. Kwa kweli nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nikishukuru chama changu ambacho kilinileta hapa Bungeni baada ya kuniona kwamba ni mtu muhimu katika chama, nimegombea awamu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ilikuwa chama changu kichanga, lakini awamu mbili hizo ni kutokana na siasa za nchi yetu sikuweza kupata nafasi na chama kikaona upo umuhimu wa kunipatia nafasi ya kujumuika katika jengo hili. Kwa hiyo, nakishukuru sana chama changu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee tena napenda niishukuru familia yangu nikianza na mume wangu mpenzi Ndugu George Mwatuka ambaye amenivumilia kuwa mbali naye akakaa kama mseja wakati ana mke. (Makof/Kicheko)

Pia nawashukuru watoto wangu ambao walikuwa wanahitaji mapenzi yangu, wamenikosa kwa muda mrefu lakini wamevumilia, nawashukuru sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna nyingine tena napenda kuushukuru uongozi wa Bunge, kwa kweli kulingana afya yangu jinsi ilivyokuwa inasumbua, ofisi ilinihadumia mpaka hivi sasa namshukuru Mungu kwani kidogo inanipa matumaini kwamba bado ni mzima. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nawashukuru Wabunge wenzangu ambao naamini wengi walikuwa karibu na mimi kwa sababu kila mtu utasikia unaendeleaje siku hizi, hii ni kuonyesha kwamba tulikuwa pamoja na walikuwa wananipenda na wanaendelea kunipenda. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema mambo machache kutokana na bajeti ambayo kwa kweli ni muhimu lakini naomba sasa viongozi maana hapa kuna kipengele cha utawala bora. Maana ya utawala bora ni kufuatana na viongozi wake kuwa bora, wakiwa viongozi bora basi na mambo yote yatakuwa bora na siyo bora viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunachangia bajeti, tunaomba pesa kwa ajili ya kuendeleza Wizara na kwamba hizo fedha zinazoombwa, nina imani mwanzo umekuwa mzuri, waswahili wanasema safari njema huonekana asubuhi, nimeona Ofisi ya Waziri Mkuu imeshughulikiwa vizuri na hakuna aliyeinga na watu walikuwa wanakubali kutoa pesa ambazo zinahitajika. Hivyo basi, nina imani kwamba hata bajeti za Wizara nyingine zinazoendelea hakuna atakayeona kwamba tunakwenda kinyume, tutaunga mkono na kwamba hata hii mimi naiunga mkono kwamba hayo yaliyosemwa ni mazuri tu, cha kuomba ni utekelezaji tu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hali iliyopo katika nchi hii nakuwa na mashaka sana jinsi inavyokwenda kwa sababu kila kukicha utakuta mambo yanakwenda songombingo. Ulilolitegemea kwamba litakuwa hivi linageuka linakwenda vile na hata ulilolitegemea hili litakuwa hivi linapotoshwa. Labda tumuombe Mwenyezi Mungu aliyemuweza wa yote na mpangaji wa mema yote aingilie kati ili kufanikisha azma zilizopo juu ya utawala uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifadhaishwa sana kwenye Bunge la Katiba ambalo tulitegemea kwamba mambo yanekwenda vizuri, lakini nasikitika Rais alitamka wazi kwamba Rasimu ilioletwa ni nzuri na nitamshangaa yule atakayeikejeli lakini bahati mbaya kwa mara ya kwanza kabisa yeye mwenyewe akasimama kuanza kukejeli na kadhalika. Kwa kuwa yeye ni Kiongozi Mkuu, tulio chini sasa tunalazimishwa kufanya kama anavyotaka yeye, kama alivyoongoza kwa kusema yeye msimamo wake ni huu. Kama Kiongozi Mkuu wa nchi hakupaswa kusimama hadharani, ilibidi yale ayasemee kwenye chama, lakini alisimama hadharani, pale ndiyo alipokosea na haya ndiyo yanayozaa mpaka sasa hivi watu ndani humu hatuelewani, tunakwenda tu na utaratibu wa vyama badala ya kusema kwamba tunatetea na tunatunga sheria kwa ajili ya nchi. Sasa akisimama wa CUF anatetea chama chake, akisimama wa CHADEMA chama chake, akisimama wa CCM naye anakwenda kwenye chama chake matokeo yake mambo yanakuwa hovyo. Kwa hiyo, nawaomba wenzangu hiivi sasa tuache mambo ya vyama tuangalie mustakabali wa nchi kwa manufaa ya wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ni wakati mzuri ambao watu tunategemea kwamba tunakwenda kugombea tutafute nafasi za kurudi tena hapa Bungeni. Sasa tusishughulike sana na kutafuta jinsi gani ya kurudi hapa Bungeni kwa hivi sasa, muda wa kampeni upo, tuusubiri tu, sasa tuendelee na shughuli iliyotuleta hivi sasa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali huwa inasema mengi kwamba wamejitahidi, mimi nakubali kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmejitahidi kwani mmeefanya haya ambayo yapo, lakini wajue kwamba ni jukumu lao kufanya hivyo kwa manufaa ya nchi. Hizi kelele za wapinzani ni kwa sababu hawajapata nafasi, wanalililia nafasi na kazi ya vyama vya

upinzani ukishapita uchaguzi ni kuikosoa Serikali iliyopo madarakani ili wanapokwenda kinyume wajirekebishe. (Makofi)

Kwa hiyo, mnarekebishiwa pookeni marekebishiyo hayo ili mjisahihishe. Mkikubali hivyo, hakuna haja ya kugombana humu ndani, tutakwenda sawa tu. Mtambue kwamba hawa wanawasukuma ninyi ili mlete maendeleo, ataleta nani, hawana mafungu hawa? Mafungu yapo kwenye CCM kwani ndiyo chama tawala. Sasa ukiuliza ninyi mmefanya nini, Serikali hii imefanya hivi na vile, ni jukumu lenu CCM, kwa hiyo mtuvumilie. Wanaposema hawa msiseme wanajisumbua tu sisi ndiyo tunakwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mume na mke wanapogombana ndani ya nyumba kwa kawaida mume ndiye anayekuwa na matatizo. Mama akitulia kimya bila kujibu yule bwana anahakikisha kwamba ugomvi hauendelei. Sasa na ninyi CCM mnapoona wapinzani wanapiga kelele msiwajibu, muwaache tu waseme wakiona namna gani hawataendelea. Wanaotusikiliza wanatuona kama mwendawazimu ambaye amemkuta mtu anaoga bafuni au msala wa nje akachukua nguo yake akakimbia nayo, ukaacha kuoga ukamkimbiza mwendawazimu, wanaokuona nje watasema nini wendawazimu! Kwa hiyo, ndiyo tunavyoonekana sisi kule nje. (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana ndugu zangu CCM, mnapotenda mazuri hakika nawaunga mkono nasema hapa mmefanya vizuri na mnapokwenda vibaya nasema mmekwenda vibaya na ndivyo navyosema kwamba Rais alikwenda vibaya, alikosea mwanzo, haya yote yanazaliwa ye ye msababishaji. Kwa hiyo, sisi tusipende kuunga tu kuunga mkono hata lile bovu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza au pili?

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Ya kwanza bado moja. (Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Ya pili.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Habari hiyo ni ya kweli? Niambieni.

**MWENYEKITI:** Ya pili.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Eeh, haya! (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Mheshimiwa Philipa Mturano, atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

**MHE. PHILIP A. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kunifikisha salama siku ya leo kwa sababu afya ilikuwa siyo nzuri lakini nashukuru kwamba naweza kusimama na kuongea machache niliyonayo kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita zaidi katika kipengele cha mahusiano. Siku za hivi karibuni tumeshuhudia kuwepo kwa vurugu za aina mbalimbali; migomo ya wafanyabiashara, madereva na matatizo ya mauaji mbalimbali ya ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi. Ni vitu ambavyo katika hali halisi haviashirii kuwepo kwa amani katika nchi yetu. Hili suala kwa kweli halina itikadi ya vyama. Tunatakiwa tuweke mbali itikadi zetu, tuangalie haya masuala ambayo yanaendelea kutumaliza sisi Watanzania na kutufanya turudi nyuma kwa kukosa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza naiomba sana Serikali pamoja na ahadi nyingi ambazo imezitoa kuhusu migomo ya madereva, itekeleze kwa sababu ni mamilioni ya Watanzania ambao tumewapoteza, nguvu kazi ya Taifa imepotea, wengi wamekuwa vilema, watoto wamebaki yatima, wajane wamekuwa wengi, lakini zaidi ya yote idadi ya watu inazidi kupungua. Sisi tunataka tupigiwe kura ili tuweze kuendelea kuwepo lakini tutapigiwa kura na nani ikiwa watu wenyewe ndiyo hao wanakwisha?

Naiomba Serikali isikilize yale wanayoyazungumza kwa sababu kusikiliza ni bure na kutekeleza ni kitu kingine, tusiyadharau, tuyasikilize. Inawezekana kweli kuna mengine ambayo wanayasababisha wao lakini mengine zaidi inawezekana ni Serikali. Kwa hiyo, naomba tuwasikilize ili tuweze kukaa katika hali ya amani; wao wafanye kazi kwa amani na sisi tunapopanda magari hayo tuwe na amani na uhakika kwamba tunafika salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili lingine ambalo limeashiria ukosefu wa amani hapa nchini, mauaji ya ndugu zetu albino. Pamoja na kazi inayofanywa na Serikali kudhibiti mauaji hayo lakini binafsi nimeona bado kwa sababu hawa watu, wateja wao hawajulikana, wangejulikana pengine haya mambo yangeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho kuna mkubwa mmoja alimaliza kuhutubia lakini anaondoka tu huku nyuma mtu akakatwa kiganja cha mkono. Tungewajua hawa watu ambao wanapelekewa hivi viungo ni akina nani, wakatajwa hadharani angalau mmoja, akapata adhabu inayostahiki pengine ingeweza kuleta hofu mionganoni mwa jamii na hata wale wengine ambao wanafanya vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hili kwa uchungu sana kwa sababu siyo siri tumebebesha lawama sisi wanasiasa kwamba tunatumia vitu hivi ili tuendelee kuwepo, kitu ambacho inawezekana siyo kweli. Kama kuna mwanasiasa ambaye anafahamika kwamba anatumia kitu hiki basi wangeweza kumtaja, lakini wote tumebebesha lawama hizi kwamba sisi ndiyo tunaofanya hivyo ili tuweze kuendelea kuwepo kwenye nafasi. Kwa sababu wale ambao wanaua tunaoonesha kwenye televisheni wanaonekana ni watu wanyonge, maskini, hawana chocote, kama hivi vitu vina thamani inakuwaje hawa watu wako hivyo? Ni lazima kuna mahali wanavipeleka, sasa huko vinakopelekwa, hao wanaovichukua, hao watu wa mwisho ndiyo tunaowataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusu hii migomo ya wafanyabiashara. Kumekuwepo na minong'ono mingi sana lakini ifike mahali tukubali kwamba hata upande wa Serikali kunakuwa kuna matatizo, kwa sababu hawa watu wanatozwa kodi kubwa na zile kodi zinazotozwa hazilingani na huduma ambazo Serikali inaitoa. Kwa hiyo, ni lazima tujipime hapo kwamba ni wapi tulipoteleza badala ya kusema kwamba pengine ni itikadi za vyama, ooh sijui UKAWA wanafanya hivi, hapana! Sisi UKAWA hatuzui Serikali kutoa huduma, ninyi kama mnafanya vizuri sisi tunawaondoaje? Ni wajibu wetu sisi kuwaambia kwa sababu sisi ndiyo jicho la pili, kwa hiyo, ni lazima haya myasikilize na myakubali. Msipoyasikiliza na kuyakubali

mtajirekebishaje? Sisi ni kioo chenu, ninyi wenyewe hamuwezi kujiona. Kwa hiyo, haya ni lazima myasikilize, myashughulikie, myatature ili kuendelea kujenga imani kwa wananchi pengine wataendelea kuwachagua, hakuna anayejua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia migomo hii ya wanafunzi kuhusu mikopo, tunaomba sana hili suala lisijirudie tena. Sasa hivi vyuo vikuu vimekuwa vingi, wanafunzi wanaoingia vyuo vikuu ni wengi, tumechoka kuona vijana wanaoingia barabarani kudai mikopo. Kama haiwezekani, naomba kitu kimoja, tudahili wale ambao tuna uhakika wa kuweza kuwapatia mikopo. Kama tunaona uwezo wetu ni kulipia mikopo watu 100, basi tuwaweke hao hao watu 100 lakini tusiweke watu 2000 wakati hatuna uwezo huo, inaonekana ni ubaguzi, ndiyo maana migomo inaendelea.

Kwa hiyo, naomba tufanye vitu ambavyo tuna uwezo wa kuvifanya ili kuondoa matatizo katika jamii na ili wanafunzi wetu waweze kusoma waache kukaa barabarani wanarandaranda kila siku kwa sababu ni haki yao, tumewaaahidi kwamba unapoingia kama una vigezo hivi na hivi ni lazima upate mkopo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumetokea migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo sasa limeikumba nchi nzima. Kila eneo utakalokwenda ukipita pori moja, la pili kama kilomita 10 tu utakutana na watu wanaswaga ng'ombe, ni ugomvi kila siku na wafugaji.

Mimi naomba Wizara ya Ardhi, wapime maeneo ambayo yatafaa kwa ajili ya ufugaji na maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya wakulima, mipaka yetu iwe mizuri, hii itasaidia kuondoa migogoro, otherwise kila mtu anajihesabia haki. Kwa hiyo, Serikali ni lazima mlione hili, mlifikubali, mlisughulikie mpunguze migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nataka kukizungumzia ni masuala ya dini. Dini tunaziheshimu sana, sisi sote ni zao lao, kwa wale wasioingia misikitini basi wanaoingia kanisani, ni wachache ambao wanaabudu Miungu yao mingine. Hawa viongozi wetu wa dini tunawaheshimu sana na tutaendelea kuwaheshimu kwa sababu wanatupatia miongozo mizuri na tuseme wanaongoza kundi kubwa la watu ambao ndiyo sisi wenyewe. Pia wakati mwengine waangalie wasije wakasababisha baadhi ya kauli zao zikawagawa Watanzania. Amani ya nchi hii itakapovurugika haitachagua mpentekoste, mu-RC, muislamu, muangilikana, wala mpagani, wote tutakwenda na maji. Kwa hiyo, tuwaombe viongozi wetu wa dini waendelee kutuhubiri habari njema ambayo nadhani ndiyo hiyo waliyotiwa na Mwenyezi Mungu kwamba wahakikishe amani inatawala. Pale ambapo wanaona kwamba amani inavurigika basi kile ambacho wenzetu wale wamepewa zaidi yetu, pengine hekima, weledi kutoka kwa Mwenyezi Mungu wavitumie kutusaidia lakini isije ikaonekana kwamba wao wamekuwa ni sehemu ya kuvuruga amani. Hatupendi na tunaamini na wao hawapendi lakini kama Watanzania wenzetu tunaomba hili walijue. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa nchi hii hususan walimu wamekuwa ni watu ambao muda mrefu wamelalamikia mafao yao na wameyafanya kazi na wengine ni ya miaka sita iliyopita. Huyu mtu mnapotmuajiri si mnajua kabisa kwamba ameanza tarehe 05 Juni mwaka fulani, anastahili kupanda cheo baada ya muda fulani. Sasa inakuwaje wakati wa kuanza kulipa yale malimbikizo wengine wanapewa, wengine wanakosa? Ni nani tumlaumu? Sijui ni Serikali au ni Mkurugenzi whatever lakini wote ni Serikali. Tuambwiwe tu kwamba labda Wakurugenzi huwa wanapeleka taarifa ambazo si sahihi Serikalini labda kwa Mawaziri huko na wao wanaleta fedha kulingana na ile idadi waliyopelekewa. Tumeanza kazi siku moja, mwenzangu anapanda cheo, mimi sijapata barua ya onyo, wala karipio wala tatizo lolote kazini, kwa nini nisipande daraja au nisipate mafao yangu?

Naomba hili nalo Serikali iliangalie kwa sababu linazidisha migogoro, amani inakosekana makazini, watoto wetu wanakosa kufundishwa vizuri kwa sababu walimu hawana morali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Blandes, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka niseme mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpatieni. Nilitaka nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Celina Kombani pamoja na Mheshimiwa George Mkuchika. Sisi ambao tuko kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tunajua kazi nzuri wanayoifanya viongozi wetu hawa. Nawaombea wachaguliwe tena warudi hapo hapo ili wachape kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Katibu Mkuu Ikulu, Bwana Peter Ilomo kwa kazi nzuri. Nawapongeza watendaji wote ambao wako chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Rais, lakini pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Watendaji wote Wakuu ambao wako chini ya ofisi hii wakiwemo TASAF, TAKUKURU na zinginezo. Kwa kweli kazi inafanyika sana, japo wakati mwininge bajeti inabana lakini wanajitahidi, hongereni sana. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na mawili au matatu. Kwanza naomba nianze na TAKUKURU ambayo iko chini ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo mimi ni Makamu Mwenyekiti wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ambayo imefanywa na TAKUKURU ni nzuri sana ingawa rushwa haijaisha lakini tunaona matunda mazuri. Hata haya mambo yanayoibuka humu ni kwa sababu ya TAKUKURU, wanajitahidi. Nimpongeze sana Mkurugenzi wa TAKUKURU amekuwa karibu sana na Wabunge, anatushirikisha, tunatoa maoni yetu kwenye Kamati yetu. Namshukuru sana Ndugu yetu Hosea. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo sidhani kama TAKUKURU imewezeshwa vizuri ili iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi. Kwa mfano, kwangu Karagwe ninakotoka TAKUKURU hawana hata ofisi, wanajibanza mahali tu wanapanga kwa mtu, sasa wanakosa uhuru wa kufanya kazi zao. Inapotokea pengine hapo walipopanga huyo mtu naye anatuhumiwa kwa rushwa watafanyaje? Kwa hiyo, nilitaka nisema kwamba tuwape TAKUKURU bajeti ya kutosha ili watufanyie kazi nzuri na nia wanayo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kumekuwepo na malumbano ambayo nasema hayana tija kwenye nchi yetu. TAKUKURU kama tulivyoona katika nchi zingine kwa mfano, Malawi na Uingereza tulienda tukaona, TAKUKURU zao wamepewa meno ya kutosha, hapa kwetu TAKUKURU haina meno hata kidogo. Ni sawa sawa na kufuga mbwa kisha ukamng'oa meno halafu utegemee kwamba atafanya kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuwaambia TAKUKURU wanapotaka kupeleka mtu mahakamani mpaka wapate consent ya DDP siyo kizuri. Hivi tunaogopa nini? Kwa nini hawa watu tuisiwa madaraka ya moja kwa moja, wakakamata, wakachunguza, wakashtaki, mahakama ikaamua? Maana kuna kesi nydingi zimekaa kwa DDP kwa muda mrefu lakini hatoi kibali, sheria haimbani, haimpi ni siku ngapi anatakiwa atoe kibali, tungekuwa na sheria ya kusema basi awe consulted lakini ndani ya wiki mbili arudishe majibu ili vijana wetu wa TAKUKURU waendelee na kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejifunza Malawi, wenzetu hawana cha kupindapinda hata kidogo. TAKUKURU wakishachunguza wakakamata ni moja kwa moja mahakamani. Malawi ni nchi ya kawaida, ipo Afrika hapa wala haipo Ulaya. Nilikuwa napendekeza, pamoja na kwamba kwenye Katiba Inayopendekezwa tumeweka hayo mambo, lakini ni nani anajua Katiba itapita lini? Kuna kupita na kutopita, kwa nini msilete sheria nzuri hapa tukawapa TAKUKURU meno? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ndani ya TAKUKURU kuna watendaji ambao ni watumishi wetu hivyo ni lazima tuwazungumzie. Mishahara yao ni midogo sana pamoja na kwamba tunawapa kazi kubwa ya kufanya, kukamata fedha nyangi. Hebu tuwaboreshee maslahi yao. Kule kwangu Karagwe TAKUKURU wamepanga huko uchochoroni, watafanyaje kazi zao wakati hawana hata nyumba? Tuwape nyumba na mafao mazuri lakini pia waendelee kupata elimu ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sijaelewa kazi za TAKUKURU mpaka nilipofika Uingereza. Nilijiona mambo makubwa sana ambayo na wenzetu wanatakiwa waende huko wakajifunze ili waweze kufanya kazi nzuri. Watumishi wa TAKUKURU Karagwe hawana hata gari. Wanapigwa simu kwamba kuna mtu anatoa rushwa mahali fulani, kutoka Karagwe Mjini kwenda labda mpaka huko Bushangara Nyakaiga, anaondoka na taxi anakuta tayari biashara imeshamalizika anabaki kubabaika tu. Wapeni nyenzo ili wafanye kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigosie kidogo TASAF. Sisi Wabunge tulipata fursa ya kutembelea Malawi, wengine wakaenda Mexico na sehemu zingine. Kwa sisi ambao tumeona wenzetu wanachokifanya huko, TASAF yetu ya hapa iko mbele na imepiga hatua nzuri sana. Kuna mahali tumekwenda tumekuta bado wako kwenye TASAF II, sisi tumeimaliza hiyo tunakwenda TASAF ya III. Hii TASAF ya III ni ya uhamilishaji wa fedha, yaani kuzisaidia kaya maskini, watu wanyonge ambao hawawezi kupata hata mlo wa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongoza kikosi kwenda Mkoa wa Mara, Wilaya ya Bunda. Nilishuhudia siku hiyo wananchi wenyewe kipato cha chini wanapewa ruzuku ya fedha. Walitoa ushuhuda kwamba fedha hizo zimewasaidia kujenga nyumba, wamepeleka watoto shule, fedha hizo zinawawezesha kutibiwa lakini pia walitoa ushuhuda kwamba wameweza kununua mifugo kwa ajili ya kuboresha maisha yao. Pengine anayesema kwamba TASAF haijafanya kitu ni kwa sababu hajafika kule kwenye ground. Pengine tu ningeomba Waheshimiwa Wabunge wengine watembelee huko wakaone, kwa kweli wananchi wanasifu sana kwamba TASAF mmefanya jambo nzuri. Kwa hiyo, nawapongeza sana watendaji wa TASAF pamoja na changamoto walizonazo lakini wanajitahidi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu ambalo nilitaka niseme kwa upande wa TASAF, tulipitisha fedha hapa nadhani ilikuwa kitu kama shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kuwawezesha wenzetu wa TASAF wawafikie wananchi mpaka kwangu kule Ihembe II, Karagwe. Kwa masikitiko makubwa, napenda yasijirudie tena, badala ya kuwapa TASAF hizi shilingi bilioni 18.5 wafanye kazi, Serikali imewapelekea shilingi bilioni tatu tu. Ni fedha ndogo sana na tutawalaamu kwamba hawafanyi kazi lakini ni kwa sababu ya kutopata fedha. Nataka niishauri Serikali hii kwamba kwa kuwa mwaka wa fedha haujaisha, ningeomba wakati tunaendelea na kikao hiki cha bajeti hebu ipeleke hizi fedha za TASAF zilizobaki karibu shilingi bilioni 15 ili hawa watu wetu waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA. Naipongeza sana Serikali kule kwangu Karagwe wameshaingia na wameanza kupima vijiji vya Nyakayanja na Chonyonyo lakini naomba waongezewe uwezo wa fedha ili wasonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka nizungumzie Chuo cha Viongozi wa Umma. Kile chuo ni kizuri sana na kingeweza kutusaidia kwa sababu hata sisi Wabunge hatujapata mahali pa kupitia wakatu-shape. Sisi pia tungependa kwenda kujifunza huko lakini chuo hiki kwa kweli kimeshindwa kusonga kwa sababu ya uhaba wa bajeti, fedha tumepitisha lakini hawajapewa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia habari ya ajira ya walimu. Naipongeza sana Serikali, vijana walishaanza kulalamika lakini Mheshimiwa Celina Kombani mmetoa ajira nzuri kwa walimu. Kuna changamoto ndogo tu mbili; moja ni kwamba kuna watu wametenganishwa mke na mume, mume yuko Kagera, mke yuko Mtwara. Katika mazingira ya sasa hivi hiyo ndoa ni lazima ife. Kwa hiyo, ningeomba muweke utaratibu wa namna ya kuangalia, mwenye ndoa yake aje na cheti muwasaidie waweze kuungana na familia zao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naishukuru Ofisi ya Mheshimiwa Rais ilitupatia trekta la kulimia kule kwa ma-sister, Nyakaiga Karagwe. Tulipewa trekta jipya na majembe lakini tulipungukiwa kifaa kimoja ambacho ni harrow. Juzi nilisema na hapa naomba niseme kwamba naomba mnikabidhi niende nacho niwapelekee hawa ma-sister ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hii Sekretarieti tumeitembelea mara nyingi kwa kweli wana kilio kikubwa sana. Kwanza, hawana jengo au mahali pa kukaa. Ukiona wanapokaa yaani unaweza kuijuliza hata hayo maadili yenyewe watayasmamia vipi. Ni jengo bovu na la zamani. Nataka Serikali iwekeze vizuri ili jengo hili liweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili kuna idara nyingi ambazo zimekuwa na matatizo na mfano ni Tume ya Mipango. Tume ya Mipango wamejitalidi kuongeza staff lakini bado nchi hii ni kubwa. Tungependekeza kwamba fedha ziongezwe kwenye Tume ya Mipango, hakuna chombo muhimu cha kuinua uchumi wa nchi hii kama Tume ya Mipango. Nataka niwaombe wenzetu wa Serikalini tunapopitisha bajeti hapa hebu acheni kuipeleka sehemu zingine au kupeleka kidogo, wapeni watu wafanye kazi na najua mnapenda hivyo tujitahidi kadri ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kusema kupitia Bunge lako hili Tukufu, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwanza alichagua viongozi mahli akina Mheshimiwa George Mkuchika, Mheshimiwa Celina Kombani na Mheshimiwa Mary Nagu. Nawapongeza sana kuna watu humu ndani watawaponda ni kwa sababu hawajui kazi mnazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kusema kwamba hoja hii naiunga mkono kwa 100%, niwaombe wenzetu tuijishe kwa kishindo ili Mheshimiwa Rais na Ofisi yake wakafanye kazi, ahsante sana.

**MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nitamuita Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Shibuda.**

MHE. LOLEIA J. M. BUKWIMBA: **Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kuwapogezza Mawaziri kwa kazi nzuri kabisa ambayo wanaendelea kuifanya katika Taifa letu. (Makof)**

**Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona jinsi ambavyo Serikali imeweza kutoa ajira nyingi sana hasa za walimu, watumishi kwa upande wa sekta ya afya pamoja na sekta mbalimbali. Ninachotaka kusema ni kwamba tunaishukuru Serikali kwa ajili ya ajira hizo**

**Iakini bado kuna upungufu mkubwa sana hasa katika sekta nyingine kama sekta ya afya hasa vijijini, unakuta kwamba kituo cha afya au zahanati watumishi ni wachache sana. Kwa hiyo, niendelee kuiomba Serikali katika mwaka ujao wa fedha kipaumbele kiwe ni sekta ya afya ili kuweza kusaidia hasa wananchi walioko vijijini waweze kupata huduma safi na iliyo bora kwa ajili ya maisha yao.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu asilimia kubwa ya Watanzania wanajishughulisha na shughuli za kilimo, niombe pia katika sekta ya kilimo wale Maafisa Ugani waongezwe. Nilipokuwa nikiangalia katika ukurasa wa 82 katika kitabu cha bajeti inaonyesha jinsi ambavyo Serikali imejipanga kuajiri Maafisa Ugani 1,791, ni wachache sana hawa, nchi yetu ni kubwa na kila mahali tunahitaji Mafisa Ugani ili waweze kusaidiana na wananchi katika kuhakikisha kwamba tunabadilisha kilimo chetu ambacho ni kilimo cha mkono kiwe kilimo bora ili wananchi pia waweze kujifunza na kuweza kupata uwezo wa kupunguza umaskini. Kwa sababu wananchi wengi wanategemea kilimo kama hatutaweza kubadilisha mtindo wa kilimo chetu kupitia wataalam wetu ambaa tunawapata, niombe Serikali iweze kuboresha zaidi kwa kuongeza ajira hasa katika sekta ya kilimo tupate watumishi wa kutosha ili waweze kufanya kazi zao kuwasaidia wananchi katika masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niongelee watumishi wa kada nyingine mfano Maafisa Watendaji wa Vijiji ni kada muhimu sana. Nikitoa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, sehemu nyingi vijijini Maafisa Watendaji wa Vijiji hawajaajiriwa, wanakaimu. Pia napenda kushukuru Serikali mwaka jana ililetu Muswada tukaupitisha hapa Bungeni ili hizo kada ndogo ndogo wawe wanaajiriwa kwenye Serikali za Mitaa huko huko katika Halmashauri. Pamoja na kwamba tumeshapitisha hiyo azma kwamba watu waajiriwe kutoka maeneo husika lakini napenda kusema kwamba bado vijiji vingi vina Watendaji wa Vijiji ambaa wamekaimu, hawajaajiriwa rasmi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa wito kwamba wanapoajiri waangalie wale walokaimu na wana sifa waweze kupewa kipaumbele katika ajira hizo. Isiwe wakati wa ajira wanachukuliwa watu kutoka mbali hata hawaijui kazi hiyo, wanaachwa ambaa tayari wameshafanya kazi hizo kwa muda mrefu, wengine wamekaimu kwa miaka mitano, wengine mitatu, kwa hiyo tuwape vipaumbele hao ambaa tayari wako kazini wenye sifa za kuajiriwa. Hilo nalizungumzia kwa sababu limejitokeza kule Geita katika Halmashauri yangu. Niombe Serikali iingilie kati ili tuangalie wale ambaa wanakaimu wapewe kipaumbele kupewa ajira katika nafasi za Serikali za Vijiji pamoja na Kata. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nzungumzie upande wa Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Napenda kutoa masikitiko yangu kwamba katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuna baadhi ya maeneo kulitokea vurugu, hakukuwa na amani katika upigaji kura hasa kwa upande wa wanawake na wazee pamoja na watu wenye ulemavu, kulikuwa na vurugu za hapa na pale. Kwa hiyo, niombe katika uchaguzi ujao wa Oktoba, 2015, Serikali iweke mkakati mzuri, kwanza, iongeze vituo vya kupigia kura lakini vilevile ihakikishe kuna usalama ili watu waweze kwenda kupiga kura kwa uhuru kabisa kwa sababu inatokea watu wenye ulemavu, akina mama na wazee wanazuiliwa kupiga kura. Ilifika mahali mimi nina ushahidi kuna akina mama walinifuata wakaniambia wanataka kufanya maandamano kipinga vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali katika uchaguzi huu ujao tuhakikishe unakuwa wa uhuru na amani. Wakati mwininge watu wanakoka moto siku ya kuamkia uchaguzi usiku mzima wamekoka moto katika kituo cha kupigia kura, je, huo ni utaratibu unaotakiwa?

Niombe Serikali iweze kuingilia kati na wananchi wamenituma hasa wale wa Katoro ambapo kulikuwa na vurugu za hapa na pale Serikali iweze kuweka mkakati wa kutosha kuhakikisha wananchi wanaweza kushiriki haki ya Kikatiba ya kupiga kura zao kwa uhuru, haki na amani. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni madai ya watumishi. Watumishi wengi wanayo madai mbalimbali hasa walimu wanaidai Serikali. Pamoja na kwamba katika kitabu cha bajeti kimeonyesha kwamba tayari kuna kiasi fulani cha fedha ambapo baadhi wameshalipwa. Niombe Serikali iangalie uwezekano wa kukamilisha madai ya hawa watumishi wengine ambao hawajawahi kulipwa malimbikizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu watumishi wengi wanapokuwa hawajalipwa malimbikizo au wanaposhindwa kulipwa madai yao, wengi wanakuwa wamekata tama, hawafanyi kazi kwa moyo.

Kwa hiyo, niombe Serikali iweze kuhakikisha kwamba inaangalia mahitaji ya watumishi mbalimbali mfano Walimu, watumishi katika sekta ya afya na watumishi mbalimbali na kuhakikisha kwamba wanalipwa madai yao. Mimi nilikaa na Walimu na baadhi ya watumishi wakaonyesha kwamba kweli wanazo changamoto nyingi. Hasa kwa upande wa madai, niombe Serikali iweze kutilia mkazo suala hili kwa sababu watu wengine wana madai hata ya miaka sita huko nyuma lakini hawajaweza kulipwa, kwa kweli waangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali pia iweke utaratibu mzuri kuna walimu wengine wanalamika kwamba walimu wanapewa hela za likizo nusu. Niombe Serikali hebu iweke utaratibu mzuri, kama mwaka huu anatakiwa kwenda likizo apewe fedha zake kamili siyo kupewa hela nusu. Katika Halmashauri yangu ya Geita hiyo ni changamoto. Kwa hiyo, niombe Serikali ijipange sasa kuhakikisha kuwa walimu wanapokwenda likizo au watumishi wengine wa Serikali wahakikishe wanapewa mafao yao vizuri ili hatimaye waweze kufanya kazi zao kwa amani na furaha na kuweza kulitumikia Taifa letu vizuri kwa sababu kila afanyaye kazi lazima alipwe kwa haki. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana juu ya hilo kwa sababu walimu walio wengi na watumishi wengine bado wana madai yao mengi. Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake aliwapa moyo watumishi wa Serikali, niombe Serikali itilie mkazo katika utekelezaji ili kuweza kukamilisha na kumaliza changamoto za muda mrefu za watumishi wa Serikali hasa kutokulipwa haki zao za msingi kwa wakati. Niombe sana Serikali izingatie hayo kwa ajili ya kuwawezesha hawa watumishi kuweza kufanya kazi zao kwa amani. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wapo watumishi ambao wanafanya kazi katika sehemu za migodi, niombe pia Ofisi yetu ya Serikali hasa Utumishi wa Umma tuangalie hata watumishi hawa walio katika sekta binafsi je, wanatumikishwa inavyopaswa na wanalipwa kwa haki? Kwa hiyo, kwa kuwa Serikali kazi yake ni kusimamia isimamia pia hata hawa wanaofanya kazi migodini kwa sababu sehemu zenye migodi pia tunapata malalamiko mbalimbali ya watumishi hao. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke mkono wake iangalie utaratibu wa kuweza kusaidia watumishi hawa ili waweze kuishi kwa amani na kwa moyo wakijua kwamba Serikali ipo ambayo inasimamia mahitaji na maslahi yao. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na napenda kuunga mkono hoja, nikiamini kwamba Serikali inakwenda kuyafanya kazi yale yote ambayo watumishi wanahitaji. Ahsante sana. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Shibuda, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Innocent Sebba.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** **Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kuweza kupata fursa hii na mimi niweze kuchangia maombi ya pesa na kuhusu mipango ya bajeti ya matumizi kwa ajili ya Ofisi ya Rais na Utumishi wa Menejimenti ya Umma pamoja na Tume ya Mipango kwa mwaka 2015/2016.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kutoa maanganizo muhimu na kudodosa uwajibikaji wa Serikali ili iweze kujitambua pale palipo na uwezo wa kujikosoa basi ijisahihishe. Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utawala Bora), majukumu ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na majukumu ya Tume ya Mipango huthaminisha sana utumishi wa utawala bora wa Serikali na husadikisha vilevile utumishi wa Chama Tawala kuthaminika na wananchi wanoongozwa na hicho chama.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika mserereko wa kuelekea katika kipindi cha uchaguzi wa mwaka 2015. Utumishi bora wa Serikali na utumishi wa Menejimenti wa Umma utahitajika sana kuonekana kwamba unathaminisha na kusadikisha Serikali pamoja na Chama Tawala. Hivyo hivyo, Utumishi wa Menejimenti ya Umma huongeza thamani ya Chama Tawala lakini vilevile utumishi wa kudhulamu na kupora maslahi tua umma huponza siasa za chama tawala na vilevile hukaribisha chuki za wananchi dhidi ya Chama Tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utumishi wa utawala bora wa dola hujenga na kuthaminika kwa kauli za viongozi wanaoongoza nchi. Nasikitika kusema kwamba patokeapo mtusuano kati ya umma na chama tawala na patokeapo mtifiano kati ya dola na wananchi wa makundi mbalimbali ya kijamii kwa mfano wakulima na wafugaji, wavuvi, wachimbaji wadogo wadogo au wafanyabiashara basi hapo hutoke shutuma ambazo hujenga utengano kati ya umma na Serikali na Chama Tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi na mipango ya bajeti hii, je, itanufaisha vipi usalama wa wafugaji ambao wanaathirika na utumishi mbovu wa utawala wa uchumi unaosimamiwa na Wizara ya Maliasili?

Wizara ya Maliasili ambayo inasababisha vifo vya wafugaji pamoja na mifugo ambayo hiyo siyo dhana ya utawala bora wa kiuchumi. Sasa naomba Wizara hii itambue kwamba wafugaji wako njia panda kuhusu utawala bora wa uchumi unaotekelizwa na Serikali. Sababu ni kwamba wafugaji wananyimwa haki za malisho, wanaathirika na matatizo mbalimbali yanayosababishwa na utawala ambao kwa kweli unasimamiwa na Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapotokea kuna matatizo wafugaji wanaauawa na mifugo pia inapigwa risasi, hii kwa kweli ni tabia ambayo naikumbuka mimi kama kijana mkongwe kwamba matukio ya kuuawawa Afrika na kuitwa nguruwe mwitu ilikuwa ni ubeberu ambao ulitekelezwa wakati wa kipindi cha kudai uhuru wa Afrika hususani huko Afrika ya Kusini. Sasa leo matendo hayo kwa nini yanatokeo hapa Tanzania na pana ukimya? Kwa nini pana ukimya wa utawala bora? Nimeona hilo nilisisitize. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti ni fursa ya kuotesha na kunufaisha ustawi na maendeleo ya jamii na kuwa ni fursa ya uwezeshwaji wa familia kuweza kujipatia manufaa ya mipangilio mbalimbali ya Tume ya Mipango, je, kwa nini TASAF wasiwe na mpango mkakati wa

kuwanunulia majembe kaya ambazo zinahitaji ili waweze kujinasua badala ya kuwapelekea pesa?

Nasema hivyo kwa sababu kuna wananchi ambao kazi zao huwa inalazimika wakawe vibarua kwa matajiri kwa sababu hawana majembe. Sasa namuomba Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu atusaidie, je, TASAF wanaweza wakatambua Wilaya kama Maswa zinazohitaji majembe, wakanunuliwa wananchi ili waweze kunufaika na huu mpango mikakati wa TASAF? Nitashukuru sana kama hili atanisadia kulijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya hitilafu na kasoro ambazo husababisha ajenda za kisiasa ni masuala ya menejimenti ya utumishi wa umma na vilevile kasoro za utawala bora.

Kwa hiyo, ningeomba uwajibikaji ambao una kasoro, kwa mfano, utawala bora wa uchumi, Tume ya Mipango nina uhakika kabisa ina majukumu muhimu, lakini hadi leo tuna matatizo ya masoko ya pamba, tuna matatizo ya viwanda, hivi ikiwa Obama alitumia fedha za Serikali za nchi yake kufufua uchumi wake kwa nini sisi tumeamua kutelekeza wananchi zaidi ya milioni 15 ambao wanahitaji viwanda vya kuthaminisha mazao yao hadi leo hii wanangojea kwa kusema waje wawekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipodai uhuru wa Tanganyika tulisema wananchi watashika hatamu za uchumi, patatokea uvezeshwaji, ni kwa nini hili jambo tumelitelekeza na je, dhamira hasa ya siasa na mwendelezo wa siasa ya uchumi na utawala bora ina mantiki gani kwa kasoro hizi za wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya bajeti hizi ni sehemu mojawapo ambayo inategemea kuwa mbegu ya kunufaisha na kukuza mipango mikakati ya kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunashuhudia Katibu Mkoo wa Chama cha Mapinduzi aliwahi kuhimiza pawepo suluhu na ahueni kwa wafugaji. Vilevile Katibu Mkoo

amekuwa akisemea sana juu ya mipango ya utawala bora na kuhusiana na operesheni za waathirika mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba Utawala Bora, Tume ya Mipango mtuambie waathirika wa Operesheni Tokomeza, Operesheni ya Ihefu na Operesheni ya Wahamiaji Haramu wa Rukwa, ni lini waathirika hawa ambao wamefukarishwa watapata fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiit, ikiwa leo wahimili wa Wizara hizi wameshasafishwa, sasa walioangamia, waliofukarishwa, waliokuwa maskini Serikali inatoa tamko gani la kuwalipa fidia kwa makosa ya utumishi uliotendeka wa menejimenti mbovu ya umma na vilevile utawala mbovu wa uchumi uliotekelzeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya suala hili tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuzungumzia Tume ya Mipango kuhusu wafugaji asilia wa Tanzania. Utawala bora wa kutoa malisho, kuna wanyama kaya na wanyama pori. Utawala wa uchumi wa mifugo na thamani wa mazao ya mifugo italindwa na kukuzwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa tusadikishwe kwamba thamani ya mifugo inaheshimika katika utawala bora wa uchumi na vilevile katika Tume ya Mipango ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini Tume ya Mipango italeta suluhu ya kurejesha fahari ya Victoria Federation kwa masuala ya ushirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile jamii ya makundi ya wafugaji na wakulima wa pamba wana mchoko wa fikra. Kwa hiyo, wanaomba kufahamu ni lini mnyororo wa thamani ya mazao yao utaibuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadhirifu wa Operesheni mbalimbali zinazojirudiarudia dhidi ya wafugaji, zinaangamiza na ni madhila ambayo yanafanya sasa Wananchi na hususan Wafugaji, wawe na michoko ya mawazo ya kuthamini na kuamini siasa za Uongozi Bora wa Chama cha Mapinduzi.

Naomba sasa zitolewe kauli za kuwakaribisha Wafugaji wawe na imani na wawe na misingi ya kwamba, suluhu zitapatikana dhidi ya matatizo ambayo wamekuwa wakidanganywa na Wizara ya Maliasili. Wizara ya Maliasili iliwaambia italeta suluhu, lakini hadi leo sioni suluhu yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Utawala Bora utambulisse kasoro zinazosababishwa na Wizara ya Maliasili zitatataliwa vipi, za kuhujumu wafugaji, rushwa na ubadhirifu wa kila aina kwa wafugaji. Hivi sasa Wafugaji hawajui wataponea wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kumtakia heri Mheshimiwa Celina Kombani. Namtakia kura nyangi kwa wapiga kura wake. Wafugaji nawaomba Mama Celina Kombani hana matatizo na hata Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu. Maeneo ambayo madhila yametokea naomba Wafugaji na Wakulima mkae mjiulize nani mnampigia kura; kwa sababu kuna baadhi ya watumishi wao hawapendi wafugaji na ninyi sasa kipindi kimefika cha kuwaadhibu watu amba wanang'ang'ania supu ya nyuki, lakini mimi najua hakuna supu ya nyuki ila kuna mishikaki ya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usipoziba ufa utajenga ukuta. Kilio cha Wafugaji waathirika wa Operesheni mbalimbali naomba kipatiwe majibu ya kusadikisha utulivu wa fikra dhidi ya migutuko inayoandalila katika kurasa mbalimbali, amba wanajenga utengano wa utulivu wa mawazo ya Wafugaji dhidi ya umuhimu wa kuwa na Siasa Bora na Uongozi Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema niyaseme haya kwa sababu kuna wanasiada uchwara, ambao wanaendelea kuhimiza maneno ambayo hayana maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba, wale ambao wanapitapita Kanda ya Ziwa kutafuta kura, ninaomba kuwaambia Kanda ya Ziwa ina wenywewe. Ninaomba

kuwaonya ambao mnakuja kuhujumu fikra za Wananchi wa Kanda la Ziwa kwa kuwapa ahadi mbalimbali. Sisi siyo bendera fuata upemo, Mwenyezi Mungu atatunusuru, mtaona 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Rais, ambaye ndiye Mkuu wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maswali kadhaa ambayo ni muhimu tujiulize. Kwanza, kwa nini Taasisi mbalimbali ziwe Ofisi ya Rais? Kwa nini MKURABITA iwe Ofisi ya Rais? Kwa nini TAKUKURU iwe Ofisi ya Rais na isiwe chini ya Waziri Mkuu? Kwa nini TASAF iwe Ofisi ya Rais na isiwe TAMISEMI? Tumeenda Malawi kuna TASAF wanaita MASAF ipo kwenye Wizara nyine. Kwa nini sisi tuiweke Ofisi ya Rais? Tunaiweka tu ili Ofisi ya Rais yenyewe iwe na Taasisi au ili kitokee kitu gani? Kwa nini Utumishi wa Umma; Walimu na wengine wawe Ofisi ya Rais? Sasa utashangaa hizi Taasisi za Ofisi ya Rais ndiyo zina njaa kweli kweli, njaa imeanzia ikulu, yaani njaa ipo ikulu.

Kwa ufahamu wangu, tunaweka TAKUKURU ikulu tukimaanisha Rais atakuwa na *political will*, atawea kupambana na rushwa kwenye maeneo mbalimbali ya Serikali. Ukiona TAKUKURU ina-fail maana yake Rais hana *political will*, hana utashi wa kisiasa wa kupambana na rushwa. Ndiyo maana utashangaa tunazungumza kila siku TAKUKURU ipewe meno na Wabunge wengine wa CCM tunawashangaa, wamekuja kwenye Bunge la Katiba, tunashangaa tunakuja huku Bungeni anazungumza *the same business!*

Tunapokuja katika mambo serious, sasa tunatunga Katiba, tuibadilishe hii TAKUKURU tunaipitishia karibu bilioni 60, inatuhumu kesi kubwa zote. Mwaka huu wamefutiwa kesi, katika kesi 40 wameachiwa kesi kumi na mbili. Kesi zote zile muhimu Mwendesha Mashitaka amezifuta kwa Serikali!

Sasa unashangaa watu wanakuja tena hapa kupitisha bajeti wakijua kabisa hawa watu watakapotuhumu rushwa kubwa kubwa kesi zao zitafutwa! Linakuja Bunge la Katiba mnaendelea! Sijui nini! You guys, ni shida sana kuendeshwa na Serikali ya namna hii.

Kwa hiyo, kwa TAKUKURU *ku-fail* maana yake Serikali nzima *ime-fail*. Miaka yao kumi hii hawakuwa na nia ya kupambana na rushwa. Hamkuwa na nia! Rais hakuwa na nia ya kupambana na rushwa, ndiyo maana TAKUKURU *ime-fail*; kesi zake mmeona mambo hayaeleweki. Mmekuja kwenye Katiba mmeshindwa kuwapa meno. Kwa hiyo, Awamu hii ya Nne imeshindwa kupambana na rushwa.

Upatikanaji wa fedha; hawa TASAF hata mkiwaliza Mawaziri, tuliwaambia kwenye Kamati, hii Kamati tu hapa walipitishwa Wabunge watatu, Blandes, Sharia na mwengine. Sisi tukawaambia hawa TASAF, mmeomba bilioni kumi na nane mwaka jana, mpaka sasa hivi mmewapa bilioni tatu, sasa mnatuletea hapa, mnaomba tena mabilioni ya shilingi, fedha tulizowapitishia mwaka jana hamjapeleka! Hivi ninyi mnataka hao Wakurugenzi wa TASAF na Wafanyakazi wawachukulieje?

Hiki Chuo cha Uongozi wameomba pesa hamjapeleka hata shilingi! Hivi mnataka wawaeleweje ninyi Mawaziri na CCM yenu? Hawa watu wa *Presidential Trust Fund* ndiyo wamechakaa, wana kaofisi hapo Mikocheni, wana miaka kadhaa hawajapewa hata shilingi, mnaleta tena hapa tupitishe fedha! Hivi ninyi Mawaziri wa hizi Wizara na Rais ambaye Taasisi

hizo zipo chini yake ninyi ni Watanzania? Mnaomba vitu wakati fedha tunapitisha kila mwaka hampitishi fedha? Wala ninyi hamuwezi kujibu hizi hoja.

Hoja za Taasisi za Rais kutopata pesa, ilitakiwa aje ajibu Waziri wa Fedha au Waziri Mkuu, ninyi Mawaziri hamuwezi kujibu mtajibu nini? Hata nikiwaptishia hizi za mwaka jana mme-fail, mwaka huu mta-fail, mwaka juzi mme-fail! Sasa njaa imeanzia Ikulu; hivi ninyi Watanzania mnaotusikiliza fikirieni, Taasisi zilizoko Ikulu ndiyo zina njaa; hivi ninyi huko kwenye Halmashauri si mtakufa? Mtakufa na mtakwisha! Kama Rais mwenyewe ameshindwa kuhudumia Taasisi zipo hapo anashinda nazo, huko Kibondo huko mtakwisha. Hii Serikali imefika mwisho. Hii Serikali imegota, imechoka na imechakaa.

Haiwezekani, unaweka Taasisi ziko chini ya Rais, ndiyo zinakuwa na njaa. Watu wanazungumza TASAF hapa, Benki ya Dunia ndiyo inatoa pesa, ninyi CCM hamuwezi kuchangia. Mmetoa bilioni tatu kwenye bajeti ya mwaka jana, kati ya bilioni kumi nane, simameni mseme tunawashukuru Benki ya Dunia. Ninyi mnakusanya kodi hamna uwezo wa kutekeleza vitu hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika Waziri!

**MBUNGE FULANI:** Kwani unaendelea si alikunyima taarifa kabisa?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mimi ulininyima taarifa, hakuna kuongea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiendeshe Bunge kwa upendeleo. Mimi niliomba taarifa mbona hukunipa; huyu ni nani? Ni Mbunge kama mimi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, huyu siyo Mbunge kama wewe ni Waziri, kaa chini!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Uwaziri si wa kupewa zawadi.

**MWENYEKITI:** Nasema kaa chini!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Wewe nisikilize, mimi ulininyima taarifa; huyu taarifa ya nini?

**MWENYEKITI:** Nasema kaa chini Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Hakuna kumpa taarifa. Mheshimiwa Mwenyekiti, sema kwanza Kanuni ya kumpa huyu na Kanuni ya kuninyima mimi unayotumia? Usiendeshe...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali usibishane na Kiti, kaa chini!

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni, Kifungu Namba 64(d) ambacho kinasema, katika majadiliano hatatumia Jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. (Makofii)

Ndugu yangu Mkosamali, Mheshimiwa, wakati anachangia ameeleza kwamba, Rais hana utashi wa kisiasa wa kupambana na rushwa, Rais hana nia ya kupambana na rushwa. Nimesimama hapa kumtaka afute kauli hiyo kwa maana ya kwamba, amekwenda kinyume na Kanuni zetu za majadiliano tulizokubaliana hapa. Mchana nitakavyomjibu, tutaeleza namna gani Rais huyu amefanya katika kupambana na rushwa. (Makofii)

Mimi naomba tu, Mheshimiwa Mkosamali ni mtu mwelewa, amekwenda shule, Kanuni ambayo nimelieleza kiustaaraku tu, afute hiyo kauli kwamba, Rais hana nia ya kupambana na rushwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali futa hiyo kauli!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafutaje wakati ndiyo hali halisi? Hali halisi ipo hivyo. Jambo lipo hivyo! Ofisi yake tumemsikia juzi Katibu Mkuu Kiongozi, anasafisha watu na maeneo mengine, rushwa zote zimeanzia Bungeni. Hakuna mambo ambayo ni executive.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Rushwa nimesema hapa, kesi zote zikichunguzwa, DPP anazifuta. Mmekuja kwenye Bunge la Katiba na Rais akaja hapa, akawaambia mbadilishe mambo ya Warioba. Hamna dhamira ya kupambana na rushwa, mbona yapo wazi na ushahidi mwaka 2011/12, TAKUKURU imetuhumu zaidi ya kesi 4,000 imeshinda kesi 41 tu. Dhamira inaonekana nchi hii, unataka ushahidi gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, Kanuni inasema usitumie Jina la Rais. Mheshimiwa Mkosamali, heshimu Kiti Mwenyekiti ninazungumza. Kaa chini! Umeombwa kufuatana na Kanuni tuliyojiwekea sisi wenyewe, ufute huo usemi. Siyo maelezo marefu, futa usemi halafu uendelee na hoja yako.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema kesi wanazotuhumu TAKUKURU, wakituhumu kesi elfu nne, wakishinda wanashinda kesi 40 au 50; sasa huo ni uongo? Kuna nia kweli ya kupambana na rushwa hapo? TAKUKURU imetuhumu kesi kubwa arobaini na ngapi mwaka jana tu za rushwa kubwa wamezifuta zote hawazipeleki Mahakamani. (Makof)

Sasa Rais angekuwa na nia angeleta sheria hapa, mngebadilisha huu utaratibu. Hii si Wizara yake? TAKUKURU labda tuseme tusichangie kuhusu Rais, TAKUKURU ipo katika Ofisi ya Rais. Sasa kama Ofisi ya Rais haipambani na rushwa ni ya nini?

**MWENYEKITI:** Muda umeisha.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha wakati umeniingilia na wenzako.

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha kaa chini, kwa sababu ulikuwa unaratibiwa huku, naomba ukae. Naomba ukae muda wako umeisha. Namwita sasa msemaji wa mwisho Mheshimiwa Innocent Sebba.

**MHE. INNOCENT R. SEBBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, nawashukuru Mawaziri wanaohusika na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Ninapenda nichukue nafasi hii kwanza, kuwapongeza pamoja na kelele zinazopigwa, hawa wenzetu tunawaita ni wapiga debe siyo wasafiri. Siku zote mpiga debe huwa siyo msafiri. Wale wanaosafiri wanajua wanapoelekeea. Kwa hiyo, nawapongeza, Watanzania wanajua kazi nzuri mnayoifanya, msikate tamaa kwa ajili ya hawa wapiga debe na wala wasiwatishe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais na Ofisi yake pamoja na Taasisi mbalimbali ambazo zipo chini ya Ofisi yake. Kazi nzuri imefanyika tunaiona. Nichukue nafasi hii kupongeza Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Hapa tulipo ni kwa sababu ya hivi Vyombo kwa kazi nzuri wanayoifanya. Amani tunayoiona Tanzania ni kwa sababu ya kazi nzuri inayofanywa na Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashangaa mtu anasimama anasema nchi hii haina amani, Vyombo vya Usalama vimepooza, mimi nafikiri huyo mtu ndiyo amepooza. Hivi tungekuwa tumeppooza majirani zetu wangekuwa wanakimbilia Tanzania? Vyombo vyetu vya Usalama vingekuwa havifanyi kazi vizuri wangekuwa wanakimbilia Tanzania? Lazima tujiulize. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanaona yanayofanyika na wanawaona hao wapiga debe kuwa siyo wasafiri na mwisho wa siku watawapeni majibu yaliyo sahihi Oktoba. Haiwezekani Waheshimiwa Wabunge ambaa mmeaminiwa na Watanzania, mnakuja hapa kupiga kelele! Watanzania wanataka mwongelee juu ya matatizo yao, siyo kuja hapa kuanza kupiga kelele. Mnawatukana watu wazima kama Waziri Mkuu mnasema hana akili, hawez! Hivi ni kweli tulipofikia hapa Tanzania Chama cha Mapinduzi hakijafanya kazi yoyote? Hivi hao Watanzania mnaowaambia hakuna kilichofanyika ni kweli hawaoni? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Nichukue nafasi hii kukipongeza chombo kinachozua rushwa, TAKUKURU. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa pamoja na mazingira waliyonayo. Nampongeza Mkurugenzi wa TAKUKURU, Dkt. Edward Hosea, amejitahidi sana na amefanya kazi nzuri. Ninaamini walivyoanza sivyo walivyo sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hoja hii nitajikita sana kwenye Ofisi ya TAKUKURU. Wameweza kufungua ofisi maeneo mengi, lakini kuna maeneo mengine ambayo bado hayajafikiwa ikiwemo kule kwetu Kyerwa. Kwa kuwa hakuna Ofisi ya TAKUKURU, hali ya Kyerwa kwa rushwa ni mbaya sana. Imekithiri kiasi kwamba, maskini hawezu kupata haki. Katika hili ninaiomba Serikali jitihada zake za kuendelea kupanua Ofisi za TAKUKURU watukumbuke na sisi Wilaya ya Kyerwa. (Makofi)

Ninajua kazi hii ni ngumu na inahitaji pesa nyingi ndiyo maana hawakuweza kufungua ofisi kila Wilaya ya Tanzania. Ninaamini hata kule kwetu watatukumbuka. WanaKyerwa hawana haki, polisi hawatoi haki, Mahakamani hakuna haki, kila unapoenda lazima uwe na pesa, lakini tungekuwa na chombo hiki kizuri, ninaamini hawa watu wangeweza kupatiwa haki yao. Naiomba Serikali wakati inahitimisha, iwaeleze WanaKyerwa ni lini watafungua Ofisi za TAKUKURU kule ili hawa watu waweze kupatiwa huduma na waweze kujitambua kuwa ni sehemu ya Watanzania na waweze kupewa elimu ya kutosha juu ya kutotoa na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili naomba Serikali iliagalie kwa umakini na ilipe kipaumbele, kwa sababu sisi tupo Mpakani na nchi jirani na hao watu wamekuwa wakitumia mianya hii kwa sababu wanajua hakuna anayedhibiti rushwa. Majirani zetu wametumia nafasi hii kuingia na kuwatumia baadhi ya Watendaji ambaa siyo waaminifu; Watendaji ambaa wengine ni waaminifu, lakini kuna wengine siyo waaminifu wanaihujumu nchi yetu. Kwa hiyo, mnapokuja kutupa majibu, hebu tupeni majibu kulingana na hali halisi na mazingira tulianayo. Majirani zetu wametumia nafasi hii kuijimarisha na kuiingiza mambo ya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakaporudi mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhwani Kikwete na Mheshimiwa Selemani Jafu.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 2.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa asubuhi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Selemani Jafo cijiandae.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru sana mchana huu kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau nianze na kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Nagu katika Hotuba yake, kwenye kitabu ukurasa wa tano, Hotuba inasema kwamba, Tume ya Mipango ilifanya ufuatiliaji wa Miradi mbalimbali na utekelezaji wake katika Mikoa mbalimbali na ilifuatilia Miradi mingi. Mkoa mmojawapo uliofuatiliwa ni Mkoa wa Rukwa na Miradi iliyofuatiliwa ilikuwepo na Miradi ya Kilimo, Elimu na Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakiwa Mkoa wa Rukwa walipambana na changamoto nydingi sana na kwamba, Halmashauri za Mkoa wa Rukwa zinategemea ukusanyaji au zinategemea ushuru wa mauzo ya mahindi kama kipato chake kikubwa cha mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua kuanzia mwaka wa mauzo 2013/14, lakini mwaka 2014/15 NFRA haijawahi kulipa deni na inadaiwa deni la bilioni 2.5. Ukichukua hizi bilioni 2.5, ndio chanzo kikuu cha kuziwezesha Halmashauri hizi za Mkoa wa Pwani kuweza kutekeleza Miradi yake, ukitilia maanani pesa zinazotoka Hazina huwa zinachelewa sana kufika Mkoa wa Rukwa na kwenye Halmashauri zingine na wakati mwingine kiasi kilichoombwa siyo kinachokwenda. Wakati mwingine kule Rukwa wame-experience baadhi ya robo kutokupata kabisa pesa. Naomba kuelekeza ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri au kwa Serikali, ishinikize NFRA walipe hili deni ili Halmashauri za Mkoa wa Rukwa ziendelee kutekeleza majukumu ya wananchi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na Hotuba ya Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri, kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo sasa imeendelea kutoa ajira kwa Watumishi na imeendelea kulipa baadhi ya madeni ambayo Watumishi wanadai. Nataka kuishauri Serikali, wanapokuwa wanatoa ajira ni vizuri wale waajiriwa wakapewa na job descriptions ili wanapokwenda maeneo yao ya kazi, wajue exactly ni kitu gani cha kufanya ili siku ya siku hata hizo OPRAS zinazosemwa, ziweze kujazwa accordingly.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ajira ni vizuri waajiriwa wakapewa semina elekezi na hasa wale Viongozi ambao wanakuwa wamepata madaraka, ni vizuri wakapewa semina elekezi. Hizi semina elekezi zisiwe zinaishia tu kwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Sina uhakika kama Wakurugenzi huwa wanapewa semina elekezi. Vilevile zisiishie ngazi

hizo, ziende hata kwa Maafisa Watendaji wa Kata na Maafisa Watendaji wa Vijiji. Kwa sababu hawa wanapokuwa wanaajiriwa mara nyingi hawapewi semina elekezi, kiasi ambacho walio wengi hawajui nani atoe uamuzi huu na nani asitoe amuzi. Kwa hiyo, ni vizuri wakapewa semina elekezi ambayo ni kama capacity building kwa Watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya upandishwaji wa vyeo kwa Watumishi; nakumbuka katika Kitabu cha Mheshimiwa Kombani, ukurasa wa 41, amesema wamefundisha Watumishi 110 kwa ajili ya OPRAS. Sasa sielewi kama hawa 110 ni TOTS au ni Watumishi 110 tu walipata mafunzo ya OPRAS?

Ninavyoilewa mimi, sasa hivi Mtumishi hawezi kupandishwa cheo bila kujaza fomu ya OPRAS na fomu ya OPRAS Mheshimiwa Waziri anajua jinsi ilivyo na utata, siyo Watumishi wote wanaoilewa ile fomu; kwa sababu inabidi Mtumishi ajaze malengo, ajaze activities, pengine na indicators ya kazi anayotakiwa kufanya ili baadaye watakafomfanyia tathmini, ionekane ameshatekeleza yale yote aliyokuwa anatakiwa kwa mwaka ule na ndipo apandishwe cheo. Kwa hivyo, ninaomba Serikali pamoja na hao Watumishi 110, lakini iongeze bidii ili angalau kila mwajiriwa aweze kuifahamu OPRAS ni nini na namna ya kujaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishwaji wa vyeo au madaraka; Watumishi wanapopandishwa vyeo, ninaikumbusha Serikali kwamba, upandishwaji huo uendane pamoja na uongezaji wa mishahara. Mtumishi anaweza akapandishwa cheo, lakini akaendelea kuwa na mshahara wake ule ule wa miaka nenda rudi hata kwa miaka minne, mitano, sita inayofuata mshahara haubadiliki. Ninajua kabisa kwamba, kila mwaka PE, makadirio ya mishahara, yanawekwa na wanajua ni watumishi wangapi baada ya muda gani watakuwa wamepandishwa vyeo. Kwa hiyo, wakati wa bajeti waongeze na mishahara ya watumishi ambao watapandishwa vyeo ili wasikae na mshahara ule ule wakati wamepandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Watumishi kukaimu nafasi mbalimbali katika maofisi imekuwa kama ugonjwa; Watumishi wanakaimu kwa muda mrefu sana. Tunajua madhara ya kukaimu, huyu anayekaimu siku zote hawezi kutoa maamuzi yote, atakuwa *limited* na baadhi ya maamuzi, kwa sababu anakaimu. Sasa mtu anapokaimu na asipotoa maamuzi yote, hii inakwamisha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Muda umeisha. Sasa ninamwita Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete!

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi nipate kutoa maoni yangu na mawazo yangu juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais katika Idara zake zote kama ilivytambulishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, niseme ninaunga mkono hoja iliyotolewa na Mawaziri wote watatu. Pamoja na hilo, nianze kwa kuwashukuru sana Wananchi wa Kitongoji cha Mtambani katika Jimbo la Chalinze, ambao jana wameonesha kwamba, bado wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi, pale walipomchagua Bwana Kajole kuwa Mwenyekiti wao wa Kitongoji, ikiwa ni ishara kwamba, wameridhika na shughuli ambazo tunaendelea kuzifanya za kusukuma maendeleo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa nataka njikite katika maeneo ya Utawala Bora. Tukianza kuzungumzia la msingi zaidi ni kwamba, kwenye Utawala Bora yapo mambo ya msingi ambayo lazima tuyazingatie. Kwanza, la muhimu sana ni upatikanaji wa haki za watu, maana hili eneo ni muhimu sana. Kwa kipindi kirefu na humu Bungeni kwako tumekuwa

tunajadiliana juu ya jinsi gani tunaweza tukajihakikishia haki za watu zinapatikana. Inaonekana may be kuna wenzetu wachache hawaelewi nini maana ya haki kupatikana, pale wanapotaka kuchanganya kazi za Mwendesha Mashtaka na watu wa TAKUKURU; lakini siyo kosa lao, kwa sababu kuna mmoja ametuambia shughuli yao ni kulalamika na wanaitekeleza kwa juhudui kubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaelekeze tu kwamba, katika masuala ya Utawala Bora, TAKUKURU shughuli yao ni kuchunguza makosa ya rushwa, lakini siyo wao wanaopeleka mahakamani. Shughuli ya kupeleka mahakamani ni shughuli ya DPP. Kwa hiyo, kama wao wanaona jambo hili halijakaa vizuri, basi utaratibu wetu wa kisheria kama ulivyoelekeza katika Bunge letu ni kuleta hapa vifungu vya sheria ili tuweze kuviangalia na kuona tunafanyaje. Ndani ya dhana ya Utawala Bora, hili ni jambo ambalo inabidi liangaliwe kwa macho mawili makubwa, kwa sababu tunaweza kugonganisha Mihimili miwili ya Dola ikawa tabu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nataka kuchangia katika eneo la TASAF. Kule kwangu Chalinze kumetokea tatizo moja ndani ya TASAF na Mheshimiwa Waziri naomba ulisikilize vizuri hili jambo. Kuna watu waliletwa wakaja kufanya tathmini ya majina ya watu wanaostahili kulipwa zile hela za TASAF. Yale majina yakapelekwa katika ofisi inayostahili kulipwa, lakini baadaye yalipoletwa sasa kwa maana ya kuletwa malipo kwa watu wanaostahili, lilitokea tatizo majina yaliyokuja yalikuwa machache sana ukilinganisha na majina ambayo yalifanyiwa assessment mwanzo.

Sasa kumetokea sintofahamu, mimi binafsi kwa kuwa ninafahamu na tulipata nafasi ndani ya Halmashauri yetu tukakutana na Mtendaji Mkuu wa TASAF alituelewesha. Ningependa nitoe angalizo kwa Wizara kwamba, siku nydingine unapofanyika upembuzi namna hii, basi ni vyema mkawa na hakika na takwimu zenu ili tusije kupata malalamiko mengine kama watu wetu wanavyolalamika. Tumeambiwa kwamba, wapo watu ambaio wanastahili kupewa na wengine hawastahili kupewa. Binafsi naipongeza sana Ofisi ya TASAF, maana sasa kwa kweli hata wale wazee wetu ambaio milo ilikuwa ni tabu kidogo na maisha yao yalikuwa siyo mazuri sana, mambo sasa yameimarika na kwa kweli ninakupongezeni sana ninyi Watendaji Wakuu wa Ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo lipo jambo la Mipango. Idara yetu ya Mipango inafanya kazi nzuri sana katika kuainisha vipaumbele vyetu, lakini pili kupanga mambo gani yafanyike mwanzo na yepi yafuatie. Yapo mambo makubwa ambayo mimi leo ninataka niyazungumzie, ambayo yametokea juzi hasa katika Mji wa Dar es Salaam kutokana na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango haiwezi kuwa Mipango tu ya Maendeleo bila kuangalia makazi ya watu na pia bila kuangalia uchumi unavyoendelea kukua. Tatizo kubwa sana limetokea kwamba leo hii shilingi yetu imeendelea kushuka, lakini kushuka kwa shilingi wakati mwingine hakuendani na hali halisi ya maisha ya watu. Watu wameendelea kulalamika na sisi kama Idara ya Mipango ni lazima tuone ni jinsi gani sasa Mipango yetu tunayopanga inaweza ikafanana na kuainisha kama siyo kuwezesha watu wetu hawa wakakaa sawa. Miundombini yetu ya nyumba imekuwa mibovu sana, sasa Mipango gani ambayo inapangwa bila kuangalia ukuaji wa population zetu kwa maana ya idadi ya watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nataka pia nichangie katika eneo la utumishi. Katika Halmashauri yetu ya Bagamoyo tunao Watumishi wengi sana ambaio wanakaimu nafasi zile. Tunatambua kwamba, upo utaratibu wa kipindi cha uangalizi, lakini wapo watumishi ambaio sasa yapata mwaka wa pili kama siyo wa tatu, bado wapo katika kipindi cha uangalizi. Siyo jambo jema sana, kwa sababu watu hawa wanafanya kazi na sisi wengine tunawaona wanavyofanya kazi na tunaridhika na ufanyaji kazi wao, lakini tunachokiogopa hapa isifike

kipindi kile cha kwamba sasa wanatafutwa watu wa kuja kushika nafasi zile basi hawa wakaonekana hawana maana. Haitapendeza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo kwa wenzetu hawa wanaosimamia Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kujaribu kuona ni jinsi gani wanaweza kuwapatia nafasi za kudumu hawa wenzetu ili wawe huru zaidi, wasiwe watu ambao wanaishi katika wasiwasi wa kuogopa kesho wanaweza wakaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, lilielezwa jambo hapa kuhusiana na msimamo wa Rais juu ya Katiba. Mimi nataka niwakumbushe wenzetu hawa kwamba, Rais pia ni sehemu ya Bunge hili, tunapoamua jambo Rais naye tumeamua nae kwa sababu wajibu wake kutia saini ni lazima kutia saini. Kama kuna mtu ana tatizo na hilo, tulete utaratibu wetu kama ilivyo kawaida wa kufanya mabadiliko ya sheria zetu ili tumpe nafasi yeye acae huko na kuamua vinginevyo. Kwa sababu haya siyo kwa mara ya kwanza, lakini ndiyo utaratibu katika Mabunge yote ya Jumuiya za Madola ambayo Marais wamepewa nafasi za kukubali documents zinazotoka Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nizungumzie jambo kubwa la upotevu wa amani katika baadhi ya maeneo yetu. Ninatambua kwamba, Ofisi ya Rais moja ya jitihada zake kubwa ni kuhakikisha amani inatulia katika maeneo tunayoishi. Kumekuwa kunatokea migogoro ya Wakulima na Wafugaji, lakini yapo maeneo ambayo yamechukuliwa hatua kubwa na tumeona mambo yametulia, lakini yapo maeneo ambayo bado hali si nzuri sana; watu wameendelea kupoteza mali zao na hata wengine mali zao zinakamatwa na baada ya kukamatwa hata utaratibu wa kuhakikisha haki ya mtu inapatikana nao haujafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu kule ninayo malalamiko juu ya watu wanaoishi katika eneo la Chamakweza na Mbala, ambao mifugo yao ilikamatwa na watu wa Ranchi ya NARCO pale Vigwaza. Cha kushangaza zaidi, wale watu wanaoishi kwenye Mbunga mle ndani wanajichukulia utaratibu wao, hakuna suala la kuitana pande zote mbili, hakuna suala ambalo linafanana na utaratibu wa Kimahakama ili kuwezesha haki kupatikana na matokeo yake sasa, watu wetu wameendelea kupoteza ng'ombe na wameendelea kupoteza haki zao. Wapo watu ambao wamepigwa na wakaumizwa, wapo watu hatuna uhakika sana lakini tunaambiwa wamevunjwa hata viungo vyao na hata utaratibu wa kukamata wale mifugo, kwa maana ya ng'ombe wanasema tu bwana asilimia ishirini ya ng'ombe, asilimia 15 ya ng'ombe. Kwa kweli nitafurahi sana kama Ofisi ya Rais itatuambia juu ya utaratibu unaofaa, kwa sababu kama hatutafuata utawala wa kisheria ambao ndiyo moja ya msingi wa Utawala Bora, tunaweza kujikuta tunaiingiza jamii yetu katika mgogoro mkubwa sana siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ninamwita Mheshimiwa Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa Athumanzi Mfutakamba!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, amenipa fursa japo na mimi nichangie machache katika jioni hii ya leo katika Wizara nyeti, ninaamini inawagusa watu wengi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu tunapozungumza Utawala Bora katika nchi yetu na tukilinganisha na nchi zingine, sisi tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, angalau tupo mahali salama; maana wenzetu wengine sasa hivi wanakimbia, wengine wanataharuki. Mimi nina imani kwamba, misingi bora

iliyowekwa katika nchi yetu ndiyo inatuwezesha leo hii kila mtu yupo katika amani kufanya jambo lake. Jambo hili ndugu zangu ninawaomba, kila mtu achukue nafasi yake kuhakikisha tunalinda amani na utulivu wa nchi yetu, ndiyo jambo la msingi kuliko kitu kingine chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi katika suala zima la Watumishi. Wenzetu wamezungumza na wenzangu wa kwanza wamezungumza, katika nchi yetu hii Watumishi wanafanya kazi kubwa sana. Nami ninaishukuru Serikali imeweza kufanya mapitio kila muda, katika kuboresha masilahi ya Wafanyakazi, lakini kuboresha hali za kazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wengine ndiyo tupo katika *field*, kuna mambo lazima yarekebishiwe. Jambo la kwanza, katika suala zima la ajira, leo hii ninashukuru katika kada ya ualimu wengi wanaajiriwa katika ualimu angalau ile *incidental allowance* wanaipata. Kuna changamoto katika kada ya afya, ninaiomba Serikali katika Idara ya Afya tuangalie kama tunawa-post wafanyakazi hasa Manesi na Madaktari, lazima tuhakikishe zile *incidental* zao zinaenda mapema ili wanapofika katika *site* ya kazi, waweze kufanya kazi kwa kujiona wana amani ya kutosha katika mazingira ya kazi. Kwa hiyo, ninaona hili ni jambo la msingi sana kuweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu hapa amesimama amezungumza, changamoto kubwa ya wafanyakazi ni madai mbalimbali. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri akija hapa kuhitimisha, atueleze kwamba sasa tatizo hilo linafika mwisho. Hili tatizo wakati mwingine linasababisha hata morali ya wafanyakazi inashuka, watu wakati mwingine wakiwa mahali pa kazi hawafanyi kazi vizuri kwa sababu kuna malimbikizo yao ya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine naomba nizungumze wazi, inawezekana hata Wakuu wa Idara ambao tumewaweka katika vitengo wanafanya kazi pengine hawafanyi kazi zao sawa sawa. Kwa hiyo, ninyi huku juu mnaweza mkasema mambo yako vizuri kumbe huko chini hali siyo shwari. Kwa hiyo, ninaiomba Ofisi ya Utumishi iangalie itafanya vipi kuhakikisha kila Wilaya na kila Idara, watu waliopewa majukumu wanahakikisha wanasimamia haki za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakumbuka siku zilizopita hapa kulikuwa na suala zima la mserereko. Kuna baadhi ya watu wameajiriwa Serikalini, wameajiriwa toka miaka hiyo iliyopita, lakini kwa bahati mbaya walishindwa kupanda vyeo. Leo hii kuna wengine wanaajiriwa juzi, mtu aliyeajiriwa mwaka 2002 anafanana na aliyeajiriwa mwezi wa jana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linaleta usumbu mkubwa sana kwa watu ambaa muda mrefu sana wako kazini. Wanajiona wametumikia muda wote, lakini leo hii anafanana na mtu juzi amemaliza chuo juzi amekuja kuanza kazi. Hili hata ukienda katika elimu ya juu kwa ma-lecturer utoalikuta hilo. Katika kila Idara tatizo hilo limekuwa kubwa; bahati mbaya tumefuta utaratibu wa mserereko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-declare *interest* hapa kabisa, mimi nitashika shilingi katika mshahara wa Waziri, hasa kuhakikisha utaratibu wa mserereko unarudi. Wapo wafanyakazi ambaa hawajapandishwa siyo kwa hiyari yao, kuna watu wamesababisha wasipande grade. Wamewasimamisha kwa makusudi, leo hii kumpa *punishment* huyu mfanyakazi asipande kwa mserereko ni jambo ambalo haliwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, ahakikishe tunatengeneza mfumo, wale watu ambaa wameachwa kwa makusudi, ambaa leo haki zao zinafanana na watu wa mwanzo, utoke utaratibu katika mwaka huu wa fedha, watu wale wapande kwa mserereko waweze kupata haki zao stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala zima la research katika nchi yetu, kuna wakati mwingine tunalaumu; kuna baadhi ya sehemu zingine kwa mfano, kama Idara ya Kilimo, tunatazamia nchi hii kwamba, tuate takwimu nzuri sana kutoka katika Idara ya Kilimo, tuate takwimu nzuri sana kutoka katika Idara mbalimbali za Serikali; lakini naomba niseme kwamba, katika baadhi ya Mawizara kuna watu wamepewa madaraka hasa kusimamia Wakuu wa Vitengo, hawana utaalamu wa maeneo hayo, hasa katika sehemu ya TEHAMA (ICT). Hilo ni tatizo kubwa, kwa sababu kama sasa hivi tunaenda katika suala zima la sayansi na teknolojia, tunategemea kama Watanzania, katika Idara ambayo tunajua Dunia sasa hivi inabadilika, lazima katika Vitengo vyta Serikali wapewe watu hawa ambaa wana uwezo, siyo mtu tu kwa sababu yupo siku nyngi anapewa Idara ambayo yeye hana taaluma nayo! Nazungumza hapa specific katika suala zima la ICT. Katika Idara zetu Serikali tunaweza tukafanya research yakutosha; je, kila Wizara Wakuu wa Idara wana competence ya hilo eneo?

Tusiwasahau vijana ambaa tunasema wameanza kazi juzi tunawadharau; hapana, hawa watu wana uwezo wao mkubwa na nina imani tukiwapa madaraka watafanya mabadiliko makubwa sana katika nchi hii. Mimi ninajua, kama tutaiheshimi ICT katika nchi yetu, tutafanya mabadiliko makubwa sana na kila mtu ataona anapata fursa ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo kuna suala zima ukienda sehemu nyngine kutakuwa na madai ya wafanyakazi hasa wanapopata ajali kazini; hapa bado kuna upungufu kidogo, najua Serikali inayafanyia kazi vizuri sana. Naomba tuboreshe sana, Wafanyakazi wa Serikali ambaa muda mwingine wanapata ajali kazini, tuangalie jinsi gani tutahakikisha wanapata malipo yao stahiki. Kuna wafanyakazi wengine walipata ajali za magari, kwa mfano, Jimboni kwangu kule, muda mrefu hawajalipwa, ni tatizo kubwa sana. Wakati mwingine tunapata msukumo mkubwa, wafanyakazi hata morali inashuka, kumbe tatizo kubwa ni jinsi gani kurekebisha suala zima la madai yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja katika suala zima la mishahara ya wafanyakazi. Nina imani nikifuatilia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, alizungumza wazi kwamba, mwaka huu inawezekana mishahara ikapanda. Mimi napongeza katika hilo, ni suala kubwa kama Rais wetu wa Nchi amezungumza katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sichoki kupendekezo mapendeleko yangu ya kila siku; siku zote ninasema tukipandisha mishahara, tuweke utaratibu kwamba, wale wenyeh mishahara yta chini, watu wa kada ya chini, tuwapandishe kwa asilimia kubwa na wale Wakuu wa Idara na Wakurugenzi tuwapandishe kwa asilimia ndogo. Tukiweka flat rate kwa mfano tukipandisha kwa 10%, mtu anayelipwa mshahara wa 3,000,000/= asilimia 10 yake ni 300,000/= na mtu anayelipwa 300,000/= asilimia 10 yake ni 30,000/=. Ina maana hatujamsaidia huyu mtu wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri, mwaka huu kabla haijaletwa bajeti hapa ya Wizara ya Fedha, tuangalie jinsi gani utaratibu wa mishahara mwaka huu uende katika suala zima tofauti. Watumishi wa kada ya chini, ambaa purchasing power yao ni ndogo, tuhakikishe jinsi gani tunawaihau angalau na wao wawe katika hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kupanda madaraja wenzangu wamezungumza sana na hili ni tatizo kubwa sana; kuna watu wako makazini kwa muda mrefu hawapandi madaraka. Mwanzo nimelizungumza, inawezekana wakati mwingine ni roho mbaya tu ya Wakuu wa Idara. Ofisi ya Utumishi naomba mliangalie hili, inawezekana Wizara inapata lawama kumbe huko Wakuu wa Idara ndio wenyeh tatizo lenyewe. Lazima mlisimamie, haiwezekani kila Mbunge anakuja analalamikia hilo, lazima huko kwenye Idara kuna matatizo. Inawezekana huko kuna mambo ya rushwa, huwezi ukajua Mheshimiwa Waziri. Vilevile inawezekana Mkuu wa Idara

mwagine hataki kumpandisha mtu mpaka apewe rushwa na inawezekana rushwa nyingine zikawa mbaya, rushwa za ngono, ikawa ni hatari katika Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo; aunde Timu Maalum ifuatilie kila Wilaya ni nani alishahiki kupanda na kwa nini hajapanda. Hapo utagundua kumbe Waziri unapewa lawama, inawezekana kuna watu ambao ni chanzo cha hiyo lawama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tume ya Mipango, tunavyozungumza haya yote lazima tuju gani pesa itapatikana. Mimi naishauri Tume ya Mipango, najua inafanya kazi kubwa sana, lakini tuongeze juhudhi. Ninsema hivyo kwa sababu lazima Tume ya Mipango iilekeze Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, jinsi gani itawekeza katika sehemu ambazo zitaleta tija katika Taifa letu hili. Mimi nina imani kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiweka katika uwekezaji wa reli, ikiweka katika uwekezaji wa kilimo, vijana wengi wataweza katika suala zima la ajira, nchi yetu itaweza kubadilika na uchumi utakuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Tume ya Mipango katika hilo, ihakikishe inafuatilia kwa karibu zaidi. Kwa mfano; tulikuwa na Bandari Kavu ya Kisarawe, ambayo imewekwa katika Kitabu cha Mpango tokea mwaka 2010, mpaka leo hii hiyo kazi hajatekeleze. Wakati Bandari Kavu ile kama Tume ya Mipango mkiwa mnasimamia, lengo kubwa ni kuondoa mizigo inayojaa Dar es Salaam. Leo hii Dar es Salaam ime-stuck haitembe! Haitembe kwa sababu mizigo yote inatoka Dar es Salaam katikati ya mji! Kama mngejenga Bandari Kavu ya Kisarawe kama mlivyokusudia, maana yake mizigo yote mikubwa baada ya kutoka bandarini ingekuja huku Kisarawe katika Bandari Kavu, ingeondoka na Reli ya TAZARA na Reli ya Kati na magari mengine. Tungepiga marufuku malori makubwa kufika katikati ya mji. Hata mkakati mwagine wa kuondoa foleni, foleni hizi nyingine inaonekana kumbe Mipango yetu tunavyopanga hatuwezi kuietekeleza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naombwa sana, Mheshimiwa Waziri wa Uwezesaji na Tume ya Mipango mmenisikia, tunahitaji Bandari Kavu ya Kisarawe mujenge kwa ajili ya uchumi wa nchi hii yetu ya Tanzania. Tusipofanya hivyo ndugu zangu, nchi ita-stuck. Kama nilivyosema, leo hii ukitoka Maili Moja mpaka unafika Dar es Salaam magari hayatembe, malori yote yamejaa kwenda Dar es Salaam, kwa nini yafike katikati ya mji? Wakati Mpango wetu kumbe tulikuwa tumelenga katika strategic area, eneo linapita reli mbili, eneo zuri la Bandari Kavu, mizigo yote ingekuwa inapofika bandarini, ingekuja Kisarawe kule, hakuna gari kubwa linaingia katikati ya mji! Kila siku tunapoteza pesa nyingi sana kwa ajili congestion ya Mji wa Dar es Salaam!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya haya, nina imani tutakuza uchumi wetu. Hata hii mishahara tunayoipigia kelele hapa, maana yake mishahara haitapatikana kama Mipango haitakuwa mizuri ya kukusanya pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya niliyozungumza inatosha. Naiomba sana Serikali, hasa katika suala zima la kupanda grade za wafanyakazi kwa mserereko, mwaka huu lirudi kuwaokoa wale wafanyakazi ambao waliachwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Eng. Mfutakamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ole Medeye!

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niseme kabisa kwamba, naunga mkono bajeti zote hizi mbili, Taarifa hizi mbili, pamoja na ile ya tatu ya Mheshimiwa Mkuchika. Nianze na Taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja kwenye suala ambalo amelizungumza vizuri ndugu yangu mchangiaji aliyejita, Mheshimiwa Jafo. Kwa kweli, Tabora ina nafasi nzuri sana kwenye suala la Bandari Kavu, kwa hiyo, tuweze ku-link Bandari Kavu ya Kisarawe na Bandari Kavu ya Tabora. Tabora tuna barabara tano sasa hivi za lami, kuna reli, kuna uwanja wa ndege wa lami na ninaamini hizi nchi jirani zinaweza kuja kuchukua mizigo yao ya kontena pamoja na mingine ili kusukuma uchumi wetu haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la Tume ya Mipango. Nimeipitia Taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha hapa na leo asubhi nilipata bahati kuuliza swali la Malengo ya Milenia na pia Malengo Endelevu (*SDGs*). Nimeangalia Taarifa ya Mheshimiwa Waziri na nimegundua kwenye ukurasa wa 13, ziko Wizara ambazo zimefuatiliwa; Kilimo, Viwanda, Usafirishaji, Ujenzi, Nishati, Maji, Afya na Fedha. Mimi ningependeka za Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia hasa TEHAMA nayo pia ifuatiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivi kufuatana na kiasi ambacho Serikali yetu imewekeza. Mkongo wa Taifa ni kiashirio kwamba, tunaweza kuwa na fursa nydingi za ajira kwa maana ya kuunganisha na mikongo ile ya kimataifa, tunao ESCOM na ule mkongo mwingine unakuja mpaka Dar es Salaam. Mkongo wa Taifa sasa hivi unafika kila Wilaya, kwa hiyo, kutaweza kuwa na ICT Hubs kwenye ngazi za Halmashauri, ili watu waweze kupata ajira. Sasa mimi ninajua suala la kibajeti unafanyaje; Venture Capital Fund, kama tunaweza kutengeneza *proposal* zikavutia wawekezaji wa nje, tukafanya hata kwa utaratibu wa PPP, sisi tukatoa ardhi, inaweza kusaidia sana kuvutia watu kama akina Microsoft, IBM, HP, hata hawa Google, Facebook na kadhalika, wanaweza kusaidia sana na hasa kama tutaangalia kwenye programu zetu za hivi Vyuo Vikuu na hasa Vyuo vya Ufundii. Kama tunaweza kuandaa mitaala, ambayo inaweza kuwatayarisha vijana wetu wakaweza kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani sasa hivi 75% ya wanafunzi wanaofaulu kwenye Vyuo Vikuu wenye taaluma za sayansi, teknolojia na TEHAMA, 75% wanajijiri wenye, hawaendi kutafuta ajira yoyote. Ndiyo tunaona hii Google, tunaona Microsoft, tunaona Hewlett Packard, tunaona Apple, hawa ni watu ambao walitoka kwenye Vyuo vya IV League wakaanza kufanya shughuli zao wenye, hawakutegemea ajira Serikalini. Sisi tunao Mkongo wa Taifa, ndiyo mwanzo wa kiashiria ambacho COSTECH inaweza kutoa ushirikiano na kukaribisha makampuni mbalimbali haya wakaja kuwekeza huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, tumeona maeneo mengi wanapozungumza matumizi ya ardhi hakuna *value addition*. Wanataka ardhi ipimwe wauze viwanja, lakini hizi ardhi zinaweza kuleta *value activities*, shughuli ambazo zinaweza kuleta thamani sana kwenye ardhi yetu hii kwa kuleta makampuni mbalimbali na pia watu wakawekeza kwenye shughuli mbalimbali badala ya kuuza viwanja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia Europe yenye 50% ya vijana wanaofaulu kutoka Vyuo Vikuu pia wanajijiri. Hii ni kwa sababu mazingira yamejengeka, kiasi ambacho kuwapa fikra na fursa kwamba, siyo lazima uende Serikalini tu. Nimpongeze Mheshimiwa Celina Kombani, kwa sababu tumepeata Walimu kama 250 Uyui, lakini pia tumepewa vibali vya kuajiri Madaktari na Wauguzi wengine kwenye Sekta ya Afya; nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la AGOA, naomba niliseme tena hapa kwa sababu Mipango wanaweza kutusaidia. Huu ni Mpango ambao umeanza tangu mwaka 2000, lakini kwa bahati mbaya, sasa sijui kama Mipango siyo mizuri, sisi tumekuwa katika uzalishaji kwa kutumia fursa ya soko la Marekani. Maana yake sisi tunatoa bidhaa, wao wanunua ile bidhaa, kwa hiyo, kuna supply side na demand side. Sisi tumekuwa tunatoka 18% mwaka 2000, mwaka huu 2015 ni 4%! Tume ya Mipango itazame tatizo liko wapi, kwa sababu tunaweza kupata fursa za ajira zikaongezeka na pia Pato la Taifa. Tulifanyie kazi hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye SDG, Mpango wa Maendeleo wa Kimataifa, ambao utekelezaji wake utaanza Septemba 2015 kwenye suala la ajira, umaskini na afya. Naomba teknolojia za *remote sensing*, jinsi ya kupata taarifa na pia kutumia hizi simu za mkononi, kwa sababu iko Taasisi moja New York inasimamia suala hili, Ofisi ya Mipango jjitahidi kutumia Wataalamu hawa, inaitwa *The Sustainable Developement Solution Network (SDSN)*, a frame work of post 2015 indicators, wanaweza kutusaidia pia Mipango yetu ikawa mizuri, lakini suala zima hii Mipango inalipiwa na nini, fedha zitatoka wapi. Kwa hiyo, hili tuliangalie tunapokwenda katika utaratibu huu wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ni mambo aliyozungumza *Health Economist* mmoja, yaani Mchumi wa Afya, Profesa Jefrey Sites; yeye alisema, alipokuwa anafanya utafiti wa chandarua kimoja kwa kila Mtanzania, yeye ametoka Chuo Kikuu cha Harvard alisema, katika Wilaya zilizo maskini hapa Tanzania, Wilaya yenye umaskini wa kukithiri ni Uyui. Sasa nimeona hapa maeneo mengi wanakwenda kuangalia maendeleo yamekwendaje katika vipimo vya viashiria, wamekwenda Bunda, Nyasa, Sengerema, Bukoba na Ikungi, sikatai huko ni Tanzania pia, lakini waje Uyui watusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kuwapongeza tu Tume ya Mipango, kwa suala la *Risk Management* lilitopo ukurasa wa 15, yaani tahadhari ya vile viashiria. Wamelieleza vizuri na mimi ninaamini kabisa tukiongeza bidii haya Malengo ya kutoka 2015 mpaka 2030 na sisi tunaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ole-Medeye!

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda nitumie fursa hii kutoa pole sana kwa Wananchi wa Kitongoji cha Madebe, Kijiji cha Engutukoiti, Kata ya Oldonyosambu, ambao mwezi uliopita tarehe 21 walivamiwa na nyumba zao kubomolewa na hivyo, kuacha zaidi ya watu takribani 100 bila kuwa na makazi. Hawana makazi, hawana chakula, wala vyombo vya usafiri, kwa sababu walivyokuanavyo vimeharibowi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko makubwa sana kwamba, hadi leo hii waliohusika kufanya uharibifu huo, ingawa wanajulikana kwa sababu wananchi walitoa taarifa Polisi, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi yao. Kwa maana hiyo, ningependa kupitia Mkutano huu niseme kwamba, ukweli Idara ya Polisi katika Wilaya ya Arumeru haitendi haki kwa Wananchi wa Jimbo langu, wanawaonea. Tarehe 21 nilipigiwa simu kwamba, kuna wananchi wamekamatwa wamebekwa ndani na wamechukuliwa kilometra 60 kutoka kwenye makazi yao wakapelekwa mpaka Makao Makuu ya Wilaya kule Usa wakawekwa ndani, wanawake, watoto wadogo pamoja na wanaume. Wanawake kosa lao, kwa nini mmepiga ukunga kuomba msaada! Walitaka wafanyeje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ichukue hatua kali dhidi ya Uongozi wa Polisi Wilaya ya Arumeru pamoja wale Polisi wanaohusika ambao wanashirikiana na wahalifu kwenda kuwanyanya Wananchi wa Kitongoji cha Madebe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo siyo dogo ni kubwa na limekiuka haki za binadamu. Kwa sababu kwa mfano, nimekwenda mpaka pale ninachoambiwa ni kwamba, wananchi hawa ardhi wanayoishi siyo ya Wilaya yao ni ya Wilaya nyingine. Wanatakiwa waondoke ili ardhi ile watumie watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hii ni moja. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamruhusu Mwananchi wa Tanzania kwenda kuishi popote ilimradi asivunje Sheria. Hawa wametolewa wanataka kuwahamisha! Ni nani huyo tunayetaka kumleta pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba vyombo vinavyohusika kusimamia haki za binadamu hususan Utawala Bora, watazame suala hili. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu baada ya kumfikishia suala hili ameniahidi kwamba, atachukua hatua. Nami nina imani nae kwa sababu mara zote ambapo nimempelekea tatizo linalotoka katika Jimbo langu, alilishughulikia kwa dharti. Namwomba sana na hili aliye kipaumbele kama ambavyo amekuwa akifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ambayo tunaijadili leo hii; naomba niwapongeze Mawaziri wote wa Nchi, Ofisi ya Rais. Niwapongeze Makatibu Wakuu na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango pamoja na Watendaji wote, kwa kazi njema ambayo wamekuwa wanaifanya. Ningeomba tuzidishe bidii, ili basi pale ambapo kuna mapengo, tuweze kuyaziba mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ningeanza suala la Sekretarieti ya Maadili. Sekretarieti ya Maadili imekuwa ikifanya kazi nzuri, tunatambua mazingira waliyopo siyo mazuri sana ya kufanya kazi, lakini kazi yao inaonekana. Ombi langu kwao ni kwamba, badala ya kusubiri taarifa iletwe juu ya Viongozi, ni vizuri tukawa tunafutilia. Sheria ni pana na inaweka miiko mingi kwa Viongozi ambayo Sekretarieti hii ndiyo inapaswa kufutilia na kuchukua hatua pale ambapo maadili yamekiukwa.

Kuhusu TASAF, naishukuru Serikali imesaidia sana kaya maskini kama ambavyo ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani alikuwa ametamka hapo awali. Ukweli ni kwamba, imewasaidia sana zile kaya maskani. Tatizo moja tu ambalo nimeliona, zipo baadhi ya kaya ambazo kwa bahati mbaya katika utambuzi, wako watu ambao wameachwa. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, wako watu wanaostahili wameachwa na hivyo ningeomba sana Serikali ikatazame upya suala hilo ili kuhakikisha wale wote wanaohusika wanapewa huduma inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utumishi wa umma, ni kwa bahati mbaya Mawaziri huwa hawawezi kujisemea, lakini ukweli ni kwamba, masilahi ya Mawaziri ni madogo sana ukilinganisha na kazi wanazofanya. Mawaziri wana Majimbo yao, Mawaziri wana Wizara ambazo zinahudumia Taifa nzima, lakini mshahara anaupokea ni ule wa Ubunge ukiongoza na posho kidogo anayopewa kama Mwenyekiti unavyopewa posho kidogo kwa ajili ya kazi yako ya Uenyekiti. Sasa ni vizuri Serikali ikaangalia namna ya kuboresha masilahi ya Mawaziri, kwa sababu ukweli mzigo wanaoubeba ni mkubwa sana. Wakati wa mjadala wa Katiba mpya nilisema, Mbunge wa Jimbo abaki Mbunge, Waziri awe ni Waziri kwa sababu ya kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi sana, Mawaziri ukiwa Waziri Mkuu kwa miezi sita ukastaafu, unaendelea kutunzwa na Serikali mpaka kufa kwao, lakini Waziri ukiwepo katika

nafasi hiyo kwa miaka 20 ukastaafu, unaenda kufia shambani, hakuna anayekutunza, hakuna anayejua kwamba utaishije. Sana sana unaambiwa utakuwa na passport wewe na mwenzio hadi kufa kwako, lakini passport kama hujasafiri ina faida gani kwako?

Ningesauri utaratibu ufanyike ili sheria inayohusika irekebishwe, Mawaziri wapewe angalau pensheni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ajira, bado vinachelewa kutoka, havitoki kwa wakati, ningeomba sana Serikali, Menejimenti ya Utumishi wa Umma wafanye hima. Mimi nilikuwa najiuliza inachukua siku ngapi baada ya kupokea ombi la kuajiri, kufanya uchambuzi wa ombi lile na hatimaye kutoa majibu. Kama Wizara ina charter kwa nini haifuatwi mpaka ufuatilie na kwenda kukumbusha mara ngapi ndipo uweze kuambiwa ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mipango, napenda kuipongeza Tume ya Mipango, wanafanya kazi nzuri ya kuchambua na kupanga Mipango ingawa nao tatizo kubwa ambalo unalikuta, nilikuwa naangalia bajeti, fedha walizopata ni kidogo sana. Nadhani ni vizuri tukaangalia chombo hicho kama ndiyo kinachosimamia Mipango yote nchini, kikawezesha kwa dhati ili kiweze kutimiza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa kulizungumzia chini ya Tume ya Mipango ni kuhusu utaratibu ulioanzishwa na Serikali, ni kweli tumegatua madaraka kwenda kwenye Halmashauri; kwa mfano, tumewapa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, lakini hatuwawezeshi kwa fedha. Ningeomba fedha za Mipango ya Maendeleo ziende kwenye Wilaya. Jambo kubwa ambalo nimeliona katika muundo wa bajeti ya mwaka unaokuja, fedha nyangi sana zimewekwa Wizarani. Wizarani wanafanya nini na fedha hizo?

Miradi ya Maendeleo inatekelezwa kwenye Halmashauri, kazi ya Wizara ni kupanga na kufanya ukaguzi; kwa nini wanabakia na fedha hizo zote? Sisi nadhani hatuhitaji charity kwamba, Waziri kwa furaha yake anasema leo nakupa shilingi milioni 100, hatuhitaji hilo, fedha ziende kwenye Halmashauri ambao ndiyo wanaotekeliza Miradi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea; kwanza, tungetaka kujua una mtaji gani, halafu hautangazwi, ndiyo sababu vijana wengi ambaa wangestahili kupata mikopo kuititia Mfuko huu hawaiipati, kwa sababu hawaijui. Ningeomba Serikali iutangaze Mfuko huu kuititia vyombo vinavyohusika, TBC na vyombo vingine, ili vijana wapate kujua na kuchukua mikopo.

Serikali mtando; ningeshauri Serikali Idara zote zitumie fursa inayotolewa na Serikali mtando na hususan kwa sababu naona bado kuna Idara za Serikali zina anwani pepe inayoishia na dot com. Ningeomba hili wapewe muda ndani ya miezi mitatu wawe wamehama kutoka dot com waje dot Tz. Kwa sababu siri nyangi za Serikali zinavuja kwa kutumia anwani zinazotokea nje ya nchi. Ni vizuri tukatumia anwani ambazo tunayo mamlaka nayo, tunazihifadhi hapa hapa ili siri za Serikali zisiweze kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono hoja. (Makofij)

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika suala la utawala bora hasa katika sehemu ya upambanaji na kuzuia rushwa, ili kuweza kupunguza tatizo la rushwa na kuweza kujenga jamii yenyehaki sawa ni vyema sasa Serikali iangalie haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie namna ambavyo inaweza kuboresha maslahi ya wafanyakazi (watumishi wa Serikali) yaani watumishi wa Umma. Hii itasaidia katika kupunguza ama kutokomeza rushwa.

Pili, ni Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Utaratibu wa kutayarisha na kutoa Hati za Haki Miliki za Kimila naishauri Serikali ifanye zoezi hilo na itoe hati hizo kwa Halmashauri zote nchini na sio tu kwa baadhi ya Halmashauri ambazo ni chache, Serikali itoe hati kwa wananchi wote katika Halmashauri zote ili wananchi waweze kutumia hati hizo ili waweze kujikwamua kutoka katika wimbi la umasikini na kuwa na maendeleo zaidi.

Tatu, ni vyema Serikali ikaangalia upya Tume ya Mipango katika kuboresha maslahi na kuleta ufanisi wa kazi. Pia ni vyema sasa Chuo cha Mipango Dodoma (IRDP) kirudishwe katika Ofisi ya Tume ya Mipango, yaani kitoke Ofisi ya Hazina ili kiweze kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa tano wa hotuba hii ya Utawala Bora inazungumzia ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015, Tume ya Mipango ilifuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mikoa mbalimbali ukiwemo wa Rukwa. Miradi mbalimbali ilikaguliwa ikiwemo ya Kilimo, Elimu na Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kikuu cha mapato kwa Halmashauri za Mkoa wa Rukwa kinatokana na ushuru wa mauzo ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri hizo zinakabiliwa na changamoto kadhaa na changamoto namba moja ni ama kutopelekewa fedha, fedha kucheleweshwa au kupelekewa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo, pia NFRA inadaiwa Sh. 2,588,389,586/= na Halmashauri za Mkoa wa Rukwa. Hivyo basi, naiomba Serikali ishinikize NFRA kutoa fedha hizo ili kulipa deni hilo ili Miradi ya Maendeleo Rukwa iweze kutekelezwa kwa ufanisi wa viwango vya juu ili kilimo, elimu na afya vihudumiwe inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana utekelezaji wa majukumu yanayotekeliza na Ofisi ya Rais. Naunga mkono na ninaomba mipango yote iliyopangwa kwenye Bajeti ya mwaka unaoanza Julai, 2015 ifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaitarifu Serikali kuitia swali Bungeni ya kuwa majengo ya nyumba za watumishi zilizopo katika Kijiji cha Chamwino zimetelekezwa kwa muda mrefu na

kupelekea uchakavu mkubwa. Nimeona katika hotuba ukurasa wa 68 kuwa kuna mpango wa kuzikarabati nyumba hizo. Naomba mipango ya ukarabati huo uanze mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuchakaa kwa majengo hayo kunatokana na kutokaliwa kwa muda mrefu, na hii inawapa mashaka wananchi wa Kijiji cha Chamwino kama azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma bado ipo. Aidha, ukarabati wa majengo ya Ikulu ya Chamwino unaendelea hivi sasa ungepewa msukumo ili ukarabati huo ukamilike haraka kuwezesha Ikulu hiyo ya Chamwino ianze kutumika. Hali ya sasa ambayo haitoi fursa ya kutumika kwa Ikulu Ndogo ya Chamwino inawapa wananchi mashaka kama azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma bado ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Serikali iweke maelezo wazi juu ya kazi za ukarabati wa majengo ya Ikulu Ndogo Chamwino ili kuwaondolea wananchi mashaka waliyonayo juu ya mpango mzima wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatachia heri katika utekelezaji wa majukumu yote.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote waliowasilisha Hotuba za Bajeti ili tuweze kuzijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo nilikuwa napenda kupatiwa ufanuzi. Kwanza ni Ajira za Watendaji wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufanuzi kuhusu utaratibu uliopangwa na Serikali hasa kutokana na ucheleweshaji mkubwa sana katika Halmashauri zetu wa kuwapata Watendaji wa Vijiji na Mitaa na kuleta athari kubwa za kiutendaji katika Halmashauri za Miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bado kuna changamoto kubwa sana ya Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa, hawana Ofisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao. Hili jambo liko kwa muda mrefu sana, naomba kujua kama katika bajeti hii Serikali imejipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bado Wenyeviti wanapatiwa posho kidogo sana kulingana na majukumu waliyonayo. Je, katika bajeti hii ni ongezeko kiasi gani wamewekewa hawa viongozi wetu ili wafanye kazi kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo huwa tunakutana nayo wakati tukifanya ziara za Kamati katika Idara za Serikali ni pamoja na Watumishi wa Umma kukaimu nafasi kwa muda mrefu. Napenda kujua tatizo ni nini? Je, hakuna Sheria inayotoa mwongozo muda maalumu wa kukaimu nafasi zilizo wazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kumekuwa kunakosekana uwajibikaji wa moja kwa moja. Ni vyema kama kuna chombo kinachodhibiti mwenendo mzima wa watumishi pamoja na kudhibiti mali ya Umma, ni vyema watumishi wanaofuja mali za Umma na kutokuwajibika, adhabu kubwa ingetolewa ili kutoa funzo kwa wengine na kusaidia kutojirudiarudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kuwa watumishi hawa hawa wanapewa adhabu ya kuhamishwa kituo. Hilo siyo jambo jema. Naomba kupata mkakati wa Serikali ili kukomesha. Hii ni pamoja na wanaofanya ufisadi katika mali za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami naomba uniruhusu nichukue nafasi hii, kuwapongeza Mawaziri wote wanenewa waliokuwa chini ya Ofisi ya Rais, kwa kazi nzuri waliyafanya na kwa Hotuba nzuri iliyogusa maeneo yote; hongereni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Hotuba yake leo amegusia mambo ambayo nisingependa yapite bila kuyazungumzia. Nilimtegemea sana angeyasema haya wakati wa Wizara yangu, kwa sababu NGO zina-fall katika Wizara yangu, lakini naona amepitiwa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja alilolisema limeniudhi zaidi ambalo analisema kwamba, Serikali imejikuta ikishindwa nguvu na mashirika yasiyo ya kiserikali; huo ni uwongo, kama hajui mashirika yasiyo kiserikali yanapewa nguvu na Serikali. Serikali ndiyo imetunga Sheria ya kuwepo mashirika haya. Mashirika yanaongozwa na Sheria ya NGO, Sheria Na. 24 lakini pia mashirika haya mengine yanaanzishwa kwa kutumia BRELA, mengine yameanzishwa kwa kutumia vyama mbalimbali ambapo na vyama vya siasa viko upo. Mashirika yasiyo ya Kiserikali mengine yanakuwa registered chini ya RITA, Sheria ya Wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wote wakishaji-register huko kwingine lazima wanakuja kwenye Bodi ya NGO na kupata certificate ya compliance, yaani ukabilifu na chini ya Sheria ya NGO kuna mambo yake lazima yatekelezwe. Kwa hiyo, siyo kweli, sisi tuna-coordinate shughuli zao. Nguvu zaidi wanapata NGOs kutokana na fedha ambazo zinatoka kwa wafadhili. Wafadhili hawa wasidhani zile pesa zinafika kwao Serikali hatujui, hizi fedha zinatokana na Mikataba ambayo Serikali imeingia na nchi mbalimbali na tumekubaliana pesa nyiningine zifike kwenye NGOs.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzi-register hizi NGOs ndiyo maana tuna sheria mbalimbali za ku-control NGOs ambazo kama zikiukiwa, basi NGOs hizo zitafungwa au zinajifunga zenyewe. Kwa mfano, lazima kila mwaka NGO itoe taarifa ya kazi. Ya pili, itoe taarifa ya fedha iliyokaguliwa na wakaguzi wanaotambulika kisheria, lakini pia walipe ada. La muhimu zaidi, wasifanye kazi kinyume na madhumuni ya kuandikisha NGOs hizo. Kwa hiyo, hizo NGOs ziko chini ya Serikali na haziwezi kabisa sisi kutushinda na ndiyo maana tunafuatilia haya. (Makofii)

Lingine alilosema ambalo limenitisha sana, amesema kule Geita, ameandika hivi; ni hivi karibuni Mkoani Geita, Januari mwaka huu, mashirika zaidi ya 1000 yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania, yalitangaziwa kufutwa; hiyo siyo kweli, kwanza Geita hakuna mashirika 1000, hayafiki hata 100. Kwa hiyo, namshauri asije Bungeni na takwimu ambazo hazina uhakika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa tumepitisha sheria inahusu masuala ya takwimu, a-verify hizo sources za information yake, kwa sababu kule Geita wamepata wasiwasi sana, wanatupigia simu na mkumbuke NGO ambayo imekiuka hizi taratibu nne nilizotaja, inajifuta zenyewe automatically baada ya miaka miwili kama hakufanya hivyo. Kwa hiyo, hatuna hata haja ya kufuta hizo NGOs, ukweli ni kwamba, Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imefuta mashirika 24 na mashirika hayo 24 ni ya kimataifa tu ambayo yalikiuka masharti ya uendeshaji wa NGO. Aidha, ninavyojua mimi na Wizara yangu tunavyojua, tumefuta shirika la humu ndani moja tu na shirika hilo tulilifuta kwa sababu linalohusiana na masuala ya ushoga. Sasa nimwulize Mheshimiwa Mbunge alitaka hata hili la ushoga tusilifute? Jamani, shirika hilo lilikuja kwetu likaji-register kama sisi kwa sisi foundation, biashara ni ushoga tumelifuta. (Makofii)

Kwa hiyo, asije hapa Bungeni akaanza kusema mashirika 1000 ni shirika hili moja ndiyo limefutwa, tunafanya kazi sisi na hizo nyingine ambazo hazifuati utaratibu zitajifuta zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye WAMA, naona hii WAMA inawapa tabu sana. Kwanza, wajue kabisa WAMA ni Shirika lisilo la Kiserikali na lisilolenga kutafuta faida, Non-Governmental Non Profit Company, lilirosajiliwa na BRELA kama Wanawake na Maendeleo Foundation Limited. Limekuwa likifanya kazi zake vizuri, taarifa zake zote tunazo na linaendeshwa kwa kufuata kanuni, taratibu na katiba yake. Cha kufurahisha zaidi ni kwamba, WAMA ni NGO ya kuigwa, kwa sababu tunapokea pongezi nyingi sana. Mimi nikiwa Mjumbe wa Bodi, tumekuwa tukipokea barua nyingi sana, kwa sababu WAMA imesomesha mpaka sasa hivi zaidi ya watoto 1000 kutoka nchi nzima bila kubagua kona zote. Watoto 1000 wanaotoka kwenye familia zisizokuwa na uwezo au yatima. WAMA imesa idia vikundi nya wanawake 60,000 wamefaidika kujikwamua kiuchumi, hiyo ndiyo NGO inafanya kazi. Kubwa zaidi, kwenye upande wa afya, imekuwa ikitoa vifaa nya afya kwa vituo nya afya zaidi ya 80 nchi nzima, bila kubagua wapi au wapi. Hivi karibuni wametoa vifaa nya dola 400,000 kule Rukwa, ambayo ni takribani milioni 800. (Makof)

Sasa jamani, WAMA ni sehemu mojawapo ya mfano mzuri sana wa kuigwa na inafanya kazi yake inavyopaswa kama ilivyoandikwa katika Katiba yake. Nami nikiwa Mjumbe wa Bodi, sikatazwi. Waheshimiwa Wabunge, hapa wote mnaruhusiwa kuanzisha NGO zenu, mnaruhusiwa pia kuwa Wajumbe kwenye Bodi. Sheria ya NGOs haimkatazi Waziri kuwa kwenye NGO, kwa sababu ni kazi ya kujitolea na kwa WAMA hata tukikaa kwenye vikao hatulipani posho, sisi tunafanya kazi moja tu ya kusaidia jamii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na mimi naendelea kuifagilia WAMA kwa kazi nzuri inayofanya kuwaendeleza wanawake. Sasa namwita Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sauti yangu ni mbovu kidogo, lakini nafikiri wataniskia. Naomba na mimi niungane na wenzangu kuwapongeza sana Mheshimiwa Celina na Mawaziri wote kutoka Ofisi ya Rais, ambao wametuwasilishia bajeti yao hapa, ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami sidhani kama ningechangia kwenye hii Hotuba, lakini nimeamua baada ya kusoma Kitabu hiki cha wenzetu hasa kuhusiana na suala hili la mgomo wa madereva. Nimesoma, wenzetu wanasema, Serikali hajijajiwekea mkakati wa kudumu kuhakikisha masilahi ya pande zote mbili, lakini hasa hili, mgogoro huo unatumwa na Serikali kama chombo cha kujipatia kura kwenye Uchaguzi Mkuu ujao. Nimeendelea kusoma jinsi wanavyojifagilia kuhusiana na huu mgogoro wa madereva wanasema, nasi kama UKAWA tumeandaa Sera na Miongozo itakayohakikisha uwepo wa upatikanaji wa mazingira mazuri, ambayo yataleta haki kwa kila mmoja wa madereva ambao hufanya kazi katika mazingira magumu na mengine na mengine ambayo wameandika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nitumie nafasi hii kueleza hali halisi ya huu mgomo. Mgomo ultanguliwa na tarehe 9, maana mgomo ulikuwa tarehe 10. Tarehe 9 nilipata barua ya tarehe 8 ya Viongozi wa Madreva kwamba, wangependa wakutane na Mawaziri; Waziri wa Kazi na Ajira, Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Uchukuzi na Waziri mwengine.

Sasa mimi ni kama mwenye dhamana ya wafanyakazi hasa katika Sekta Binafsi, nikaona nikutane nao kwa sababu ilikuwa ni siku baada tu ya ile likizo ndefu ya pasaka. Kwa hiyo, nikawaita Viongozi wao ambao walitokana na uongozi katika malori, mabasi, taxi na daladala. Nikakaa nao pale Wizarani, kutaka kujua tatizo la kutuita ni nini. Walikuwa na madai, madai yao yalikuwa mikataba ambayo hili linanihusu katika Wizara yangu na nillilzungumza tukaongea nao. Walikuwa na madai mengine kama haya ya kusoma. Walikuwa wana madai yanahu sumberu wa traffic na ratiba ya SUMATRA inavyokinanza na ratiba ya traffic. Tuliongelea pia suala la chama chao, kuwa na chama kimoja kikubwa kwa madereva wote. Baada ya hapo tuliajana tukakubaliana tuwe na kikao kingine tarehe 18, ambacho kitahusu sasa wale Mawaziri ambao walikuwa wanatakiwa kusudi waweze kutoa sasa taarifa zao. (Makof)

Tarehe 10, saa kumi na mbili, mgomo huo ukatokea na si kama alivyo sema Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika suala hili kwamba, waligoma kutokana na uwongo wa Serikali. Kilichosababisha ule mgomo wa tarehe 10, kuna baadhi ya madereva waliwekwa ndani baada ya kuonekana kuna tatizo. Kwa hiyo, waligoma kushinikiza madereva wenzao waachiwe, ndiyo ilikuwa sababu. Nilikuwa nimeahidi tarehe 10 hiyo ningeenda kuzungumza na wenzao sasa, kuwaeleza tulichoongea ofisini na kitakachofanyika tarehe 18 ili waweze kukutana na Mawaziri. Kwa hiyo, tarehe 10 kwenye ule mgomo tulikutana mimi, alikuwepo Mkuu wa Mkoa Bwana Sadiki, alikuwepo Bwana Kova, alikuwepo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Bwana Makonda maana ni eneo lake na tulikuwa pia na Katibu Mkuu wa Uchukuzi.

Katika mkutano ule tulizungumza tukatoa ufanuzi ambao tulielewana na kuendelea kupanga kikao cha tarehe 18 kama tulivyo elewana. Tarehe 18 Mkutano uliitishwa pale Wizarani kwangu, wadau wote walihuduria ikiwemo SUMATRA na Traffic Police, Wizara zote zinazohusika; Mambo ya Ndani na Uchukuzi. Kikao kile tuliona kiwe cha Watendaji; Makatibu Wakuu na Watendaji wao ili likitorea lolote ambalo halitakubalika, basi Kikao cha Mawaziri sasa kikutane. Wenzetu wale walitaka kile Kikao kingekuwa cha Mawaziri na naona hilo halikuwapendeza na baada ya kuona pia yale madai ambayo walikuwa wameyazungumza hayachukui nafasi haraka kama walivyotarajia, basi wakaona waitishe mgomo tena tarehe 4 na ndiyo ilikuwa sababu ya mgomo wa tarehe 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza na kilichonishangaza hata kabla ya mgomo wa tarehe 4, wenzetu upande wa pili wameichukua hii kama turufu, sasa wanatugeuzia kibao. Kwa sababu Viongozi wale wamekuwa wakinipigia simu wanasema, kuna Mbunge mmoja anatoka Mkoa wa Dar es Salaam wa Upinzani na mmoja hatoki Mkoa wa Dar es Salaam, wamekuwa wakiwasumbua sana, kuwaambia njooni tuwaeleze la kufanya, kwa maana ya kutaka kuchochea ule mgomo kwa masilahi ya Upinzani, kwa masilahi ya kushinikiza mgomo usiishe, kwa masilahi yao mengine ya kisiasa. Kwa kweli ilinisikitisha na mpaka sasa bado wanawapigia simu wale Viongozi wa Madereva. Leo hii imejidhihirisha kwamba, Kambi ya Upinzani inasema inawasihi wamiliki wa mabasi na vyombo vyaa usafirishaji ikiwemo malori, kutafuta suluhi ya kumaliza mgogoro. Mnawaeleza haya kama nani kwa sababu hamna vyombo vyaa kusuluhisha mgogoro wala hamna sheria ambazo mnazisimamia? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunda Kamati, Kamati hii imeundwa ni Kamati ya Kudumu. Mimi naomba nimpongeze sana kijana wetu DC Makonda, ambaye sasa hivi mnasema alitaka kupigwa na madereva. Hivi mtu aliyetaka kupigwa na madereva wangemsikiliza baadaye na kumfanya sasa ndiye mlezi wao wa kitaifa?

Makonda alifanya kazi kubwa kwa niaba ya Serikali, kuhakikisha yale tuliyoyazungumza tarehe 10, yanaundiwa Kamati ambayo iliundwa na Mheshimiwa Waziri MKuu. Katika Kamati ile kuna wahusika wote Makatibu Wakuu wale, Wizara yangu ya Kazi na Ajira, Wizara ya Uchukuzi, lakini wamo watu wa Polisi, Wizara wa Mambo ya Ndani, SUMATRA wapo, kama vile haitoshi ile

Kamati tuna waajiri kwa maana ya watu wenye mabasi, TATOA, TABOA na madereva watano. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii imeshakaa tarehe 12 na kesho tarehe 19 itakaa tena na itakuwa Kamati ya Kudumu, itakuwa inazungumzia masuala yao yote yanayohitaji masuala ya haki zao kama madereva. Kubwa, tumewaomba waunde chama. Jana kama vile nilijua hili itatolewa hapa, nikamwuliza Kiongozi wao, Katibu Mkuu wa Madereva wa Malori wamefikia wapi akasema, Mheshimiwa sasa hivi tunamalizia tu Katiba kusudi tupeleke kwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi, tuweze sasa kuona taratibu za kuunda hicho chama. Hicho chama sasa ndiyo kitakuwa cha kudumu kuwasemea katika hii Kamati na pia kuwa na majadiliano na Serikali.

Kitu ambacho walikuwa wanakosa hawa madereva ni umoja, utakuta watu wa taksi wako peke yao, wa daladala peke yao, wanajikusanya kwa chama ambacho hakijaandikishwa Serikalini kama Chama cha Wafanyakazi. Kwa hiyo, sasa watakuwa na Chama chao Wafanyakazi, lakini pia kuna chama ambacho walitaka wakiunde wale madereva wa mabasi, tumewakubalia kwa sababu chama ndiyo mahali pa kusemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kuzungumza haya ili kutoa hali halisi ya huu mgomo wa madereva, haukushinikizwa na Serikali badala yake mgomo huu unatumwi na wenzetu wa upande wa Upinzani kwa ajili ya faida yao; ikiwemo Mwenyekiti wa Chama unaenda pale kwenye mgomo kuwaambia nini? Unawaeleza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba niseme, hands-off katika hii migomo, naomba muiachie Serikali ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa naomba nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana inayogusa ofisi ya juu kabisa nchini mwetu. Ninaanza kwa kusema nami ninaunga mkono hoja. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitzungumza mengi na labda mengine ni yale ambayo yanahitaji msisitizo tu.

La kwanza, ni kuwapongeza Mawaziri wenzangu waliota hoja za leo kwa ufanisi na kwa ufasaha mkubwa; nawapa hongera sana. (Makofii)

La pili, ni kuhusiana na kitu ambacho Mheshimiwa Mkuchika atakielezea zaidi, nacho ni kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi kinatambua na kimerithi Ahadi za Mwanachama kutoka TANU, kutoka Afro-Shirazi na hiyo ahadi haitakuja kubadilika ninavyoona mimi hata siku moja. Kwamba, rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea rushwa. Sasa hilo tu ndilo linalotuongoza sisi kama Serikali ya Chama cha Mapinduzi na tunajitahidi katika ofisi hii chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais, lakini chini wa utekelezaji wa siku hadi siku wa Kisera wa Mheshimiwa Mkuchika na vilevile TAKUKURU, kuhakikisha tunatekeleza hiyo ahadi ya

mwanachama ambayo unaweza kusema ni ahadi ya mwananchi. Kwa sababu hamna mwananchi atakayepingana na hiyo ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kusema tu, lilzungumzwa kama vile tulipokuwa tunaandaa Katiba Inayopendekezwa, hili suala tuliliweka kando, hapana, ni kwa vile tu baadhi yenu hamkuwemo. Mkisoma Sura ya 15, Sehemu ya Nne, Ibara ya 249, kwa mara ya kwanza tangu Uhuru, Chombo cha Kuzuia na Kupambana na Rushwa kinaundwa Kikatiba. Hiyo ni hatua kubwa sana. Nimewahi kusema kwamba, kuiweka katika Katiba ni jambo la msingi sana, kwa sababu hakuna Kiongozi ye yule ukiacha katika sheria, ambaye atakuja kusema tubadilishe sheria mazingira yamebadilika, basi tufute Chombo cha Kuzia na Kupambana na Rushwa. Ndiyo maana tukasema hii tunaiweka katika Katiba kwa sababu huwezi ukabadili.

Kukiweka Chombo hiki katika Katiba kina maana kubwa sana, mengine ni ya utekelezaji tu. Sasa sijui nani anampeleka Mahakamani nani; hili linazungumzika. Hili wastaarabu wote wanakaa chini, wanaangalia mifano mbalimbali duniani na lazima tutakuja tutakuwa na mwafaka ili kuweza kuwa na chombo au azma ambayo inatekelezeka ya kuzuia na kupambana na rushwa. Mimi sioni kama hili ni jambo ambalo linaweza likatupa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la pili. Hoja ya leo inazungumzia ofisi ya juu kabisa katika nchi, unaweza kusema inamzungumzia *citizen number one* na usimamizi wake na vyombo vyake. Huyu mwananchi namba moja ndiyo Rais. Sasa tunazidi kuwaomba wenzetu kutambua kwamba, unapokizungumzia chombo hiki, kipe heshima inayohitajika. Huwezi ukamzungumzia Rais kama vile unamzungumzia Mbunge wa Rungwe Mashariki. Hapana, mimi utanisema, unaweza kunisema kwa lolote lile, hata ukinitusi aah siyo hoja, lakini heshima ya Rais lazima tuitetee wakati wowote ule. Duniani kote ndivyo ilivyo. Sisi tumeiga masuala haya ya Vyama Vingi mfumo wetu ni wa Kiingereza. (Makof)

Waingereza wao wanasema Upinzani ule ni Upinzani wa Mtukufu Malkia siyo Upinzani wa UKAWA, Upinzani wa CHADEMA, Upinzani wa nini, hapana wanasema ni Upinzani wa Mtukufu Malkia, *Her Majesty's Opposition*. Ukitisema tu *Her Majesty's Opposition*, unatambua *citizen number one* wa Uingereza, ambaye ni Malkia, huwezi ukazungumza kama vile unamzungumza mtu ye yole yule wa kawaida. Hii ni heshima, lazima tuilinde heshima hiyo. Sasa nadhani hili tuelewane na tuliendeleze na tujenge jadi ambayo hata watoto wetu na wajukuu zetu watakuja kutuheshimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nizungumzie kuhusu uzalendo. Mimi niseme, nimesikitika sana kwamba, anaweza akatoka Mtanzania, akaenda nchi za nje akaisema nchi yake vibaya, yaani ni kitu kibaya sana. Watakushangilia lakini watakushangaa, hakuna Mmarekani ye yole ambaye atakuja huku ataizungumzia nchi yake vibaya nje ya Marekani hata siku moja. Siasa zao zitakuwa mle mle ndani, lakini unapoenda nje ya nchi unasema oooh sijui tunateswa, sujui sheria hizi ziko hivi na hivi, wanakupigia makof iakini moyoni wanakushangaa wanasema wewe ni mtu wa ajabu. Huo siyo uzalendo. (Makof)

Hata katika familia ya kawaida, mambo yenu ni ya ndani, mtoka nje yale siyo mambo ya kuzungumzwa ndani ya mipaka ya wewe, mke wako na watoto wako. Kiongozi mmoja maarufu alikwenda Marekani huko akatusema, akasema haki za binadamu, akasema tutawapeleka *The Hague*, wale walimshangilia lakini walimshangaa. Wanavyotudharau sasa, wanasema tutawaletea vilevile na Wanasheria wawasaki. Hee jamani, yaani hatujasoma hata sheria! Hata upande huo kweli Wataalam hampo; hee kitu cha ajabu sana!

Kwa hiyo, nilitaka kusema uzalendo ni kitu muhimu sana. Mambo ya nchini tuyazungumzie nchini, tukienda nje sisi ni Watanzania. Tutoke Upinzani, tutoke Chama Tawala au tutoke kusipokuwa na chama chochote, ndiyo maana ya uzalendo. Sasa hilo liliniumba sana

nilipokuwa nasikiliza, nikasema hee jamani hata Waingereza hawafanyi hivyo, Wajerumani hawafanyi hivyo. Wakinika nje, Mjerumani ni Mjerumani, Mwingereza ni Mwingereza basi. Kwa hiyo, Tanzania akitoka nje ni Tanzania, humu ndani ndiyo kama hivi sasa tunazungumza, tunabishana, tunatukanana lakini yaishie humu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye staha ndani ya Bunge. Hili tumezungumza sana, lakini tuendelee kukumbushana. Naona ndugu yangu, kijana wangu ananiangalia sana, mwanafunzi wangu, nitaendelea kulizungumza, kwa sababu staha ni kitu muhimu sana. Unapomwangalia mtu haiba yake, anavyozungumza ulimi wake ndiyo heshima yake na lazima ailinde na kuilinda anakilinda chama chake, anailinda familia yake na anajilinda yeye mwenyewe. Sasa Bunge sisi tuko huru sana humu, hamna sanasana labda iwe vurugu sana ndiyo tunaweza tukamchukua mtu tukambeba, Spika akasema mtoeni nje lakini inatokea kwa nadra sana, lakini tumejiwekea Kanuni zetu. Kwa hiyo, uhuru una mipaka na mipaka yake ni rahisi tulitengeneza sisi wenyewe, mipaka hiyo ni Kanuni. (Makof)

Sasa kama kanuni inasema Mwenyekiti au Spika au Naibu Spika akisimama wewe kaa, unajitakia umaarufu; kweli ni umaarufu huo? Hapana! Unaendelea kusimama unabishana naye ili iweje?

**MWENYEKITI:** Wanataka nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Ili iweje? Huko sasa, basi hili nadhani limefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, siku moja nilijaribu kuelezea hivi vyombo, sijui ilikuwa ni wakati wa Bunge au Bunge Maalum la Katiba. Nilieleza kwamba, fizikia ya hii kitu ndiyo maana inaitwa Microphone na Speaker. Sasa tunatofautiana sauti, lakini mara nyingi tunaweza kukusikia tu huna haja ya kupiga kelele, tutakusikia. Inauumiza sana masikio kwa sababu sasa tunashindwa kujua lipi la muhimu na lipi ni kelele.

Sasa nimeacha fizikia niende ya mwalimu. Wanasema ukisahau kila kitu nenda kwenye misingi ya mwalimu. Mwalimu amesema, *don't argue, don't shout* basi. Kumbukeni hilo. Jenga hoja usipayuke au jenga hoja usipige kelele. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana. Naendelea kuwashukuru Wananchi wa Busokelo, Wananchi wa Rungwe Mashariki na nitaendelea kushirikiana nao. Pamoja na kwamba, tayari nimeshawaeleza kwamba, miaka kumi na tano ya kupita bila kipingwa kila wakati ni heshima kubwa na ni wakati mzuri wa kusema mwingine achukue kijiti, lakini huo ndiyo mwanzo wa kulitumikia Taifa katika ngazi nyingine bila shaka. Sasa kuna rafiki yangu atanisaidia hii Oktoba kwa jinsi vijana hasa vijana wangu wa Upinzani, kambi hiyo wanafunzi wangu wanasema wananchi watasema kuni ya masika usimtume motto. Kwa hiyo, wananchi hawatawatuma kuchukua kuni ya masika, kwa sababu tupo na tutaendelea kuwepo. Ahsanteni sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa George Mkuchika!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Napenda pia kabla sijasahau, niwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Newala, kwa kuniweka humu ndani kwa miaka

kumi. Nawapongeza sana jinsi walivyochangua CCM wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwamba, mlivyofanya kule Newala kupata asilimia 84, hata Mikoa mingine na Wilaya nyingine walifanya hivyo, ndio maana CCM kijumla nchi nzima mijini tu kwa asilimia 79, mijini tu kwa asilimia 80. Kwa hiyo, msisikilize porojo zinazotolewa kwamba, mtu mwingine anachukua nchi, hakuna anayechukua nchi hii kwa kugawana asilimia 20 iliyobaki. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ilikuwa kiashiria tosha kwamba, CCM itaendelea kuongoza nchi hii, yale tuliyofanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa tunayakamilisha Oktoba. (Makofi)

Napenda kuchukua nafasi hii kuweka wazi jambo moja ambalo limepotoshwa sana. Katika vyombo vya habari na hata humu ndani imezungumzwa habari kwamba lkulu imewasafisha watu. Nataka kusema hivi, Katibu Mkuu Kiongozi alipokutana na Waandishi wa Habari, alimsimamisha Katibu Mkuu wa Nishati na Madini kupisha uchunguzi. Aliwaita kuwaambia kwamba, baada ya uchunguzi kufanyika, ameonekana hana hatia. Ndiyo nchi hii inavyoendeshwa, *rule of law, you don't condemn somebody unheard.* (Makofi)

Tungekuwa sisi tunafanya maamuzi ya paparapapara, pengine wengine mnaoitwa Wabunge hivi sasa hapa mko jela, mko wapi, lakini hatufanyi hivyo. Unasikiliza jambo, unapeleleza, unasikiliza huku na kule halafu unaamua. (Makofi)

Sasa, pale ameeleza kwamba amekutwa hana hatia. Akaulizwa swal je, Mawaziri hawa kwenye Tokomeza, akasema na wao hakuna ushahidi wa kuonyesha kwamba na wao wameshiriki. Sasa nini cha ajabu! Nchi hii tuna uzoefu, Mzee Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili, alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, maana inawezekana wengine mlikuwa hamjazaliwa, sasa nataka niwapeni historia mimi mzee wenu. Akajiuzulu kwa sababu ya matatizo yaliyofanywa na watu waliokuwa chini yake na Waziri aliyekuwa anahuksika na usalama naye akajiuzulu na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga na Mwanza wakajiuzulu. Bara ya Mzee Mwinyi aliyomwandikia Rais, Baba wa Taifa aliagiza iandikwe magazetini tuisome na akaagiza Mawaziri na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote waisome barua ile. Mimi nimeisoma kwa DC Mbulu nikiwa Mkuu wa Wilaya.

Barua inasema; Baba wa Taifa, yametokea mauaji na matatizo haya haya katika maeneo haya haya. Mimi Waziri wa Mambo ya Ndani, sikushauriwa, sikushiriki, sikuagiza, sikufahamishwa, lakini alimradi mimi ni mkubwa wao na nilipaswa kufahamu, Mwalimu nakuomba uniruhusu jambo moja tu, nijiuzulu. (Makofi)

Mwalimu akamruhusu Mzee Mwinyi akajiuzulu. Hakuna ushahidi wa Mwalimu kuitisha Mkutano wa Waandishi wa Habari, leo namsafisa Mwinyi, leo namsafisha Mzee Mwinyi, haikutokea. Alimpa kazi nyingine, akafanya vizuri, baadaye akawa Rais Serikali ya Muda ya Mapinduzi Zanzibar, akawa Rais waZanzibar, akawa Makamu wa Rais, akawa Rais wa nchi hii.

Kwa hiyo, mimi naomba sana, nakanusha, hakuna mkutano ulioitishwa na lkulu kumsafisha mtu yeoyote. Walieleza nini kimetokea kwenye Tokomeza, mlitaka kujua wale Mawaziri, hawakutia mkono wao, lakini pia yule Katibu Mkuu alifuata taratibu kabla hajafanya malipo na nini na nini, aliomba ushauri wa kisheria akapewa.

Nilidhani jambo hili niliweke wazi. Kwa hiyo, mtu kuwajibika kisiasa siyo kwamba ulifanya lile jambo, hapana. Kumbukeni babu yenu Mzee Mwinyi alivyosema, sikushiriki, sikushauri, sikushauriwa, sikufahamishwa, lakini kwa sababu waliofanya hivyo wako chini yangu, mimi ndio nawasimamia, Mwalimu naomba kitu kimoja tu, uniruhusu nijiuzulu. Kwa hiyo, nilitaka kulieleza, hii lugha ya kusafishwa safishwa, hakuna, sijui hata imetoka wapi!

Sasa jambo la pili, leo msemaji mmoja hapa, bahati mbaya hayupo, lakini nafikiri huko atapata salamu, kathubutu kusema kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, Rais hana utashi wa kisiasa wa kupambana na rushwa, hana nia ya kupambana na rushwa. Sasa mimi nataka niwaeleze ukweli wa mambo kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Nne, ina utashi na nia ya kupambana na rushwa na nataka nikupeni mifano dhahiri. Moja, imejenga Makao Makuu ya Jengo la TAKUKURU, limejengwa katika Awamu hii. Imefungua ofisi saba za Kanda, Awamu hii. Tumeweka Ofisi za Mikoa na Wilaya zote, Awamu hii, bado zile chache tu zile mpya. Tumewapa zana za kufanya kazi Watendaji wa TAKUKURU. Tumewaongeza Rasilimali watu, mwaka juzi tumeajiri watu 394, TAKUKURU ina Wanasheria waliobobe 130, kuna Wataalamu wa Ph.D katika Information Technology. Tunawasomesha ndani na nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, Rais Kikwete muda alipoingia madarakani, ndiye aliyeagiza Bunge tupanue wigo wa sheria za kupambana na rushwa. Yalikuwepo makosa manne tu, tumeongeza sasa yamefika mpaka 24. Sheria ile ya mwanzo haikuwepo na makosa, rushwa sijui ya ngono, hamna, kila kitu cha rushwa sasa tumepanua tumeweka ni katika Serikali hi ya Awamu ya Nne.

Lingine, ni Rais Kikwete wa Awamu ya Nne ndiye aliyeagiza kwamba, kuanzia sasa ninataka Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ijadiliwe Bungeni. (Makofi)

Huko nyuma ilikuwa hajadili Bungeni na ninyi wenyewe mnajua yanayotokea. Sasa Rais Kikwete amekubali Makao Makuu ya Bodi ya Ushauri ya Mambo ya Rushwa katika Bara la Afrika iwe Arusha Tanzania. Tulishindana na Nigeria, Tanzania tukashinda, tumetenga fedha mwaka huu bilioni 2.5 kuanza kujenga hilo jengo, lakini ni Serikali hii ya Rais Kikwete akiwa madarakani. Leo Viongozi Waandamizi wa nchi hii wako Mahakamani, Mawaziri wako Mahakamani, Makatibu Wakuu wako Mahakamani. Leo unakuja hapa bila aibu unasema Serikali hii haina dhamira ya kupambana na rushwa! Rais anao utashi wa kupambana na rushwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, niseme hapa, ile Mo Ibrahim Award, sisi tumo mle tumeshindana, hatukufika huko kuwa wa mwanzo, lakini Mo Ibrahim Award Tanzania ni nchi ya 10 katika kupambana na rushwa katika nchi 53 za Bara la Afrika. Mo Ibrahim na jopo lake wanakubali kwamba, Tanzania tuko mstari wa mbele kupambana na rushwa. Mwaka 2013 katika Mkuutano wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalopambana na madawa na pamoja na rushwa, Tanzania ilitambuliwa kuwa nchi ya mfano wa kuigwa katika mapambano dhidi ya rushwa. Kwa hiyo, mimi nataka niwaeleze ndugu zanguni kwamba, nchi hii Serikali, Rais wake, Chama Tawala, tena Chama Tawala kimeweka ndani ya Ilani ya Uchaguzi kwamba, tutaendeleza mapambano dhidi ya rushwa. (Makofi)

Sasa ndugu yangu mmoja hapa nadhani Msemaji Kambi ya Upinzani, alikuwa anazungumzia Idara ya Usalama wa Taifa ufisadi mwingu kuendelea kujitokeza nchini, chombo kinashindwa kuzuia, kutoa taarifa, mauaji ya albino na dhidi ya wenyewe ulemavu na kadhalika na kadhalila. Mimi naomba ndugu zanguni tusichanganye mambo, someni Sheria ya Mwaka 1999 ya Usalama wa Taifa. Sheria ile inataka chombo hiki kifanye kazi kimya kimya na hakuna nchi ambayo Idara ya Usalama wa Taifa inafanya kazi hadharani kama mnavyotaka ninyi. Siyo kazi ya Usalama wa Taifa kumkamata mwizi, lakini ni kazi ya Usalama wa Taifa kusema pale kuna dalili ya mwizi na ninyi mnajua, tumewaokoeni katika mzingira magumu, walitaka kuwadhulu, chombo hiki ndiyo kimesema jamani hebu ondokeni hapa. (Makofi)

Sasa, Idara ya Usalama wa Taifa inatekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa. Kazi yeke ni kukusanya taarifa na kutoa ushauri Serikalini au kwa Kiongozi wa Serikali ili hatua zichukuliwe. Kazi ni kukusanya taarifa na kumpelekeea mhusika ili

achukue hatua, ndiyo maana hujakamatwa hata siku moja na Afisa Usalama wa Taifa, siyo kazi yao.

Mimi naomba sana kwa siku zijazo hapa ndani, ili chombo hiki tuwe tunakizungumza vizuri, ni vizuri ukasoma sheria. Sheria ile tumeipitisha ndani ya Bunge hapa, iliyoanzisha Chombo cha Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Chiligati, mimi nakushukuru sana, umezungumzia mmomonyoko wa maadili kwa Viongozi wa Umma kupitia Ofisi ya Umma, kutumia Ofisi ya Umma kwa masilahi yako binafsi, Viongozi kufanya biashara, Sheria ya kutenganisha biashara na Uongozi imefikia wapi? Suala hili lipo katika Sheria inayopendekezwa ya Kudhibiti Mgongano wa Masilahi. Mapendeleko yameandalowi na kujadiliwa na wadau na wakawasilisha katika mamlaka inayohusika kwa hatua zaidi.

Jambo lingine ambalo ningelipenda kulizungumzia ni kuhusu TAKUKURU. Kusema kweli upande wa TAKUKURU, mimi nataka kushukuru tu kwamba, wako Waheshimiwa Wabunge wanaotambua umuhimu wa chombo hiki, wako Wabunge mmekipongeza chombo hiki, lakini pia mmeona mazingira magumu tunayofanya nayo kazi. Yale yanayohusu kuimarisha chombo, nadhani kama alivyosema mwenzngu hapa, Waziri mwenzangu Mwandosya, Bunge Maalumu la Katiba, kwa mara ya kwanza, 1977 TAKUKURU ilikuwa haijazaliwa, kwa hiyo, ilipotengenezwa Sheria ya 1977, hapakuwepo kifungu cha TAKUKURU; lakini katika Katiba Inayopendekezwa, ambayo Watanzania wanaingoja kwa hamu, tumeweka kifungu kinachosema patakuwepo Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Bunge kwa maana na ninyi na mimi nawaombeeni mrudi tena Bungeni kama tunavyotaka kurudi wa CCM wengi tu, tutapata fursa ya kukaa na kutunga sheria kwamba chombo hicho tunataka kiwe na nguvu kiasi gani.

Sasa hoja nyingi zilizotolewa kuhusu TAKUKURU, muda pengine unaweza ukawa mdogo, tutatoa kwa maandishi.

TAKUKURU ishirikiane na Vyombo vingine nya Usalama, tunashirikiana nao. Elimu itolewe ya rushwa hasa wakati wa uchaguzi, tumekubali tutafanya hivyo na jana tu APNAC, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU ametoa semina kuhusu mambo ya rushwa. Kuimarisha TAKUKURU, kama nilivyosema Katiba Inayopendekezwa. Kufungua ofisi mpya tumesikia, mtuwezeshe tu mafungu ya fedha kwenye bajeti. Wapewe mafunzo, kama nilivyosema tunawapa mafunzo nje na ndani ya nchi.

Moja ninalotaka kusema; mara nyingi sana utakuta watu wanasma, Chama Tawala kimeshindwa kupambana na rushwa. Mimi nataka kutoa taarifa kwa Watanzania wenzangu wote, vita dhidi ya rushwa siyo ya mtu mmoja. Rushwa inaliwa katika Jimbo la Mkosamali Kigoma, TAKUKURU Hosea yuko Dar es Salam, Mkosamali Diwani kule Kigoma, watu wanakula rushwa ndani ya Halmashauri, nani mtu wa mwanzo kushughulika aliyeko pale, Mkosamali au Dkt. Hosea! Kwa hiyo, mimi nasema, naomba tushirikiane wote, akina Mkosamali, Machali, wote akina Mkuchika, kila mmoja apambane na rushwa eneo analoongoza ili Tanzania yetu iwe mahala pazuri pa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa nitapigiwa kengele ya mwisho, nataka kushukuru tena kwa kunipa nafasi. Kabla sijakaa, mimi ni Mwanachama wa Club ya Yanga, nataka nichukue nafasi hii kupongeza Yanga wenzangu kwa kuchukua ubingwa wa nchi hii. Nawatakia kila la heri, wakawakilishe vizuri nchi ya Tanzania ili wajue kwamba hawa Yanga ndiyo miamba ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkuchika ahsante sana na mimi ni Yanga mwenzio. (Makofii)

Sasa naomba niwaite watoa hoja, ninaanza na Waziri wa Uwezesha, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, utatumia nusu saa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru sana na kukupongeza kwa kuendesha Bunge letu kwa umahili mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunifikisha hapa tena kwa mara nyingine na kuwa hapa Bungeni kwa miaka 20, nyote nisaidieni kumwomba na kumshukuru Mwenyezi Mungu. (Makofii)

Vilevile napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyonionyesha kwa kunitua tena kwenye ofisi yake. Namwomba Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu sana, kwa sababu ya kutuona sisi na nimpongeze sana kwa kuendesha nchi hii kwa umahiri mkubwa. Aidha, ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyofanya asubuhi, pamoja na Makamu wa Rais, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais na vilevile kwa kutuongoza na kutupa maelekezo mazuri ya kutuwezesha sisi kufanya kazi yetu vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kukushukuru wewe, lakini kuitia kwako kumshukuru sana Mheshimiwa Anne Makinda, Spika wa Bunge letu, kwa uongozi makini katika kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Umahiri wenu na Wenyeviti wengine na Naibu Spika, umetusaidia sisi kutekeleza wajibu wetu kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninyi wanawake ambaa mmekalia Kiti hicho, mmeuonyesha Umma wa Watanzania na Dunia nzima kwamba, wanawake wana uwezo na hata pale ambapo hawawezeshwi wanajiwezesha wenyewe. Ahsanteni sana kwa kutupa mfano mzuri. (Makofii)

Naomba pia nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, akisaidiwa na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kwa michango yao mizuri sana. Wametuelekeza vizuri wakati tukiwasilisha majibu ya maoni yao wakati wa Kamati na hapa Bungeni wametoa mawazo mazuri ambayo sasa hivi yanatufanya tuweze kutoa ufanuzi wa mambo ambayo pengine tulikuwa hatujayasema.

Nitakuwa mchoyo sana wa fadhila kama sitawashukuru Wabunge wote, kwa michango yao mizuri na kwa ushirikiano wao. Sisi Mawaziri tumefanya kazi yetu vizuri kutokana na ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana, tuendelee kushirikiana kwa leo kuitisha Mafungu haya ya Ofisi ya Rais, lakini vilevile kwa muda uliobaki. Niwapongeze Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, kwa kushirikiana na sisi katika kutengeneza Hotuba zetu na leo mchana huu kujibu hoja mbalimbali za Wabunge. Nawashukuru sana Wakuu wa Taasisi ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais, kwa sababu kwa kiasi kikubwa ndiyo wanaotekeliza na leo wametoa ufanuzi kwa hoja ambazo zimetolewa.

Vilevile, naomba niwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Wilaya ya Hanang, kwa ushirikiano, upendo na kusaidiana na mimi kuleta maendeleo kwenye Wilaya yetu. Wananchi wa Jimbo la Hanang wamekuwa wakijitolea na kutoa michango yao katika kuleta maendeleo, ambayo yameniwezesha mimi kuongoza utekelezaji wa llani ya Chama changu. Ninawashukuru sana, nataka niwaahidi kwamba, hii ni awamu ya pili, awamu ya kwanza ilikuwa mwaka 2005 mpaka 2010, awamu ya pili mwaka 2010 mpaka 2015, nina hakika, nikipewa muda

mwingine na mimi nitachukua fomu kwa vyovyote nigombee, nitafanya kazi kubwa zaidi ya yale ambayo tumeyafanya pamoja na nitashirikiana nao. (Makofii)

Mwisho kabisa, familia yangu imekuwa na upendo mkubwa sana na ushirikiano wa karibu sana na mimi, ambao umeniwezesha kutekeleza wajibu wangu kama Mbunge na kama Waziri. Nampongeza na namshukuru sana mpenzi wangu, Profesa Joseph Nagu, kwa ushirikiano ambao naamini usingekuwepo, kazi yangu ingekuwa ngumu sana. Namshukuru, namwomba Mwenyezi Mungu ampe maisha mengi zaidi ili na mimi niweze kutekeleza wajibu wangu vizuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze tutoa ufanuzi kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge, zinazohusiana na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hoja za Kamati kama alivyowasilsha Mheshimiwa Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Amesema kwamba, Tume ya Mipango ijengewe uwezo kwa kutengewa fedha na rasilimali watu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Tume ya Mipango, ndio ambayo inatusaidia sisi kufanya tafiti mbalimbali, kuwa na fikira nyingi za kuja na Mipango mbalimbali, ambayo hatimaye tukiitekeleza kwa umakini na umahiri, ndio italeta maendeleo na kuleta mabadiliko ndani ya nchi.

Serikali imekuwa ikitenga na itaendelea kutenga fedha kwa kugharimia shughuli za Tume ya Mipango kulingana na upatikanaji wa mapato ya Serikali. Kama nilivyosema katika Hotuba yangu, ukurasa wa 11, Tume ya Mipango iliajiri watumishi wapya 26 na watumishi wengine saba walihamia Tume ya Mipango kwa utaratibu wa kawaada wa Utumishi wa Umma. Lengo letu kuu ni kuwa na rasilimali watu ya kutosha katika kutekeleza majukumu ya Tume. Kamati vilevile kupitia Mheshimiwa Mwenyekiti, iliitaka Serikali itilie maanani kujenga uwezo wa Wataalam wa Tume ya Mipango kielimu ili wawe na weledi stahiki katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea ushauri huo, Tume ya Mipango imekuwa na itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kugharimia mafunzo kwa watumishi wake wa kada zote. Kwa mfano, mwaka 2014/15, Tume ya Mipango imeweza watumishi wanane kushiriki katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi wawili waliwezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na bado Tume itaendelea kufanya hivyo.

Tatu, Kamati iliitaka fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 3.8, zitolewe zote kabla ya Mwaka wa Fedha 2014/15 kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesikia hilo, Naibu Waziri wa Fedha alituahidi kwenye Kamati, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika kutoa fedha za maendeleo za Fungu 66 - Tume ya Mipango ili iweze kutekeleza Mpango Kazi wa Miradi ya Maendeleo katika muda mfupi uliobaki na upatikanaji wa fedha na shughuli zinazoweza kutekelezwa katika kipindi kilichosalia.

Nne, Serikali ifanye tathmini ya Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano. Kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu, Serikali imefanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/12 hadi 2012/15, 2015/16 kwa kipindi cha kuanzia Julai 2011 hadi Disemba 2013. Kazi ya kuboresha mapitio haya inaendelea ili kujumuisha kipindi chote cha Mpango na taarifa kamili itawasilishwa kwa wadau Novemba mwaka huu, sambamba na mapendeleko ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 mapa 2020 na 2021).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati imetaka Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 mpaka 2020/21, uzingatie katika kukuza uchumi wa wananchi wa kawaida ili kuhakikisha kuwa, wananaufaika ipasavyo na rasilimali za nchi yao. Ushauri ni mzuri na utazingatiwa kwa kuangalia zile sekta ambazo zinahusu watu walio wengi hasa Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye hoja ya Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Esther Matiko. Hoja yake iliyotolewa ya mwanzo kabisa ni kwamba, Kambi ya Upinzani Bungeni kuititia kwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mara kwa Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu juu ya katazo la Serikali kwa Taasisi za Dini kushiriki masuala ya siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa jibu la hoja yake, namwomba Mheshimiwa Matiko na Wapinzani wengine waone kwamba, wao ni kama kioo chetu na kwa hivyo wakitumia muda wao kutuonesha upungufu, tutatumia maelezo yao kuimarisha nchi hii na maendeleo kuwa makubwa zaidi kuliko wakitukana, kuliko wakizua na kuliko wakitusema vibaya. Lazima nikiri, Mheshimiwa Matiko hajawahi kunitukana, lakini nasema kwa ujumla, kwa kweli ninaomba mchukue majukumu yenu, kama alivyoeleza Profesa Mwandosya Mheshimiwa wetu kwamba, uzuri, ustaarabu na staha ya mtu inatokana na mdomo wake na maneno yanayotoka mdomoni. (Makofii)

Lazima niseme kwamba, mimi nitayaangalia yale yanayojenga, yale ya kutusemasema na kututukana siwezi kuyagusa, kwa sababu na mimi nitakuwa nimekiuka ushauri wa Mwatuka nafikiri, kusema kwamba, ukimkimbiza mtu ambaye amechukua nguo zako ambaye labda akili yake siyo nzuri, basi na wewe utakuwa kama wale wale. Kwa hiyo, mimi sitatukana na sijawahi kutukana na Chama changu cha Mapinduzi hakiamini kwenye kusema maneno mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajulikana wazi kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulingana na Katiba ya Mwaka 1977, haiendeshwi kwa misingi ya dini, lakini wananchi wake wana dini. Waamini wema ndiyo raia wema wa nchi. Ingawa Serikali haigemei upande wa dini yoyote, lakini inathamini dini. Vilevile ijulikane wazi kwamba, Serikali inatambua mchango mkubwa wa madhehebu ya dini katika kudumisha amani, utulivu, umoja na mshikamano katika Taifa letu. (Makofii)

Katazo la Serikali kwa madhehebu ya dini kutoshiriki katika masuala ya siasa lina lengo la kuleta umoja ndani ya madhehebu yetu. Lina lengo la kuondoa mgawanyiko ambaao unaweza kuleta machafuko ndani ya Taifa letu. Katika madhehebu ya dini kuna wa aina nydingi, kuna watu wenye vyama mbalimbali, kwa hiyo, unapoongelea jambo ambalo pengine linapendeza chama kimoja, wale wengine kwa vyovyothe vile wataathirika. Kwa hiyo, tunachoomba ni kwamba, ndani ya madhehebu yetu na kwenye makanisa na misikiti, tujaribu kuona tunawatengeneza waumini wema, ambaao hatimaye watakuwa raia wema na watapunguza kazi ya Serikali hasa na kupunguza watakaokwenda jela walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kwamba, Serikali inathamini dini na itaheshimu dini mbalimbali, lakini yenye wema haina dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther Matiko vilevile aliongelea kuwa, katika Mwaka 2011/2012, Serikali iliwasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Hata hivyo, yeye anaona Serikali imekuwa haifuatilii Mpango huo kwa kuwa Miradi mingi ambayo ilikuwa kwenye Mpango huo haijatekelezwa na hata bajeti haifuati vipaumbele vya Mpango. Vilevile anasema, Serikali inapanga na kuwasilisha Mpango Bungeni, lakini inashindwa kusimamia na kutekeleza Mpango wake wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifirii kwamba hiyo hoja ni sahihi. Sura ya Pili ya Kitabu cha Mpango wa Maendeleo Mwaka 2012/13, 2013/14 na 2014/15 zimekuwa zikieleza mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa ujumla na hususan vipaumbele vyake kupitia Mpango wa kila mwaka na mafanikio ya kuridhisha yamepatikana hususan katika utulivu wa uchumi jumla. Miundombinu ya barabara imejengwa, tumeongeza nishati ya umeme kwenda vijiji, katika elimu tumepiga hatua, hata katika nyanja ya afya tumepiga hatua na ndio maana nasema hoja hiyo siyo sahihi. Inawezekana kutokana na ufinyu wa bajeti na pale ambapo wabia wa maendeleo wakati mwingine hawatekelezi kama wanavyoahidi, basi kuna mambo ambayo pengine hatukuyafikia, lakini kwa ujumla wake na kwa kiasi kikubwa Mpango umetekelozwa.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa Daraja la Jakaya Kikwete Malagalasi, huduma ya Treni za Deluxe kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, Barabara ya Iringa - Dodoma, Bomba la Gesi Mtwara - Dar es Salaam na mengine ambayo pengine yatanichukua muda kuyataja. Huu ni ushahidi tosha kwamba, Serikali haijashindwa kusimamia utekelezaji wa Mpango wake na imepata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwa wachangiaji wengine kama Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Ole-Medeye, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Shibuda na wengine nitawataja kadiri nitakavyokuwa nawakuta.

Hoja ya kwanza ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, ni vyema Tume ya Mipango ikapewa fedha za kutosha ikiwa ni pamoja na kuwezesha kuendesha utafiti hususan kwa nini uchumi unakua lakini raia wengi bado ni maskini. Rasilimali zetu zinanufaishaje watu maskini na je, rasilimali zinazoibiwa na wawekezaji uchwara tunazizua namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge juu ya umuhimu wa kuiwezesha Tume ya Mipango kuendesha tafiti muhimu. Kimsingi, Tume ya Mipango kama kitovu cha fikra na ushauri kwa Serikali, utafiti ni moja ya majukumu yake ya msingi kabisa. Mipango na Sera za Nchi zinapaswa kuongozwa na utafiti na uchambuzi wa kina na kwa kweli hatupaswi kuongea bila kufanya utafiti. Kwa kadiri inavyowezekana, Serikali itaendelea kuipatia Tume ya Mipango rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa tafiti zitakazosaidia kuboresha Sera na Mipango ya Maendeleo ya nchi yetu ya uhakika.

Vilevile Waheshimiwa Wabunge wanasema kuwa, tuna matatizo ya masoko ya pamba kwa kukosa viwanda, kwa nini Serikali isitumie fedha zake kuanzisha viwanda na badala yake tunaendelea kusubiri wawekezaji. Hili limesisitizwa na kusemwa na Mheshimiwa Shibuda Magalle, Mbunge wa Maswa Magharibi. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano utajielekeza kukuza ujenzi wa viwanda, ikiwa ni pamoja na viwanda vinavyotumia pamba na thamani ya mlolongo wa thamani ili tuweze sasa kutumia pamba ya Wasukuma na wengine wote wanaolima pamba.

Kwenye viwanda vya nguo ndiko ambako kuna ajira kubwa, viwanda vya nguo vinatumia malighafi ya wakulima, kwa hiyo ni soko kubwa la wakulima. Tutaendelea kuboresha soko la pamba na bei kwa wakulima ili hali iwe nzuri zaidi na kama ilivyokuwa wakati wa Victoria Federation.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ridhiwani amesema Mipango iangalie makazi ya watu na ongezeko la idadi ya watu. Serikali inakubali kabisa hoja hii. Maendeleo kimsingi yanapaswa yawe maendeleo ya watu na kama ni maendeleo ya watu; idadi yao, jinsi watu wanavyoongezeka na makazi yao ni vigezo muhimu katika kupanga utoaji wa huduma za jamii

kama afya, elimu, maji na miundombinu kama umeme, barabara na kadhalika. Serikali itaendeleza juhudzi zaidi kupanga makazi kwa kupima viwanja na kutoa hati na huduma nyingine ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Jafo ameongelea kwamba, Tume ifuatilie ujenzi wa Bandari Kavu ya Kisarawe. Serikali imezingatia ushauri uliotolewa, hata hivyo, Mradi huu umekutana na changamoto ya upatikanaji wa ardhi. Serikali inaendelea na jitihada za kutatua tatizo hili na tunamwomba Mheshimiwa Mbunge naye atusaidie kupata eneo la kujenga Bandari Kavu.

Mheshimiwa Mfutakamba amsema Serikali ijenge Bandari Kavu Tabora. Tunachukua ushauri huo, lakini kwa sasa tutaanza na Kisarawe na Kibaha na Tabora baadaye itafuata, kwa sababu Tabora ni eneo muhimu sana hasa kwa biashara ya nchi nyingine baada ya Ziwa Tanganyika.

Hoja nyingine ya Mheshimiwa Mfutakamba ni Tume ifuatilie TEHAMA na Mkongo wa Taifa. Tunakubaliana na ushauri na Serikali imeanza kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kuanza Mradi wa ICT Park unaoratibiwa na COSTECH.

Ushauri wa Mheshimiwa Mfutakamba kuhusu AGOA nao tumeuzingatia. AGOA ni soko la nchi zinazoendelea Marekani na kwa kweli una masharti yake. Kwa hiyo, tutajaribu kuwaelimisha Watanzania kujua masharti yanayotakiwa na wakati huo huo kuboresha uzalishaji na viwango wa bidhaa ambazo tutazisafirisha kwenda Marekani. Ukweli ni kwamba, kama tunataka kuongeza biashara ya Tanzania na Marekani, lazima uwekezaji wa wawekezaji kutoka Marekani waje hapa wanaojua soko lao, watatusaidia sana kuongeza biashara na Marekani. Vilevile Mheshimiwa Mfutakamba ametupa pongezi kwa utafiti wa ukuaji wa uchumi na hali ya umaskini na mwaliko kwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, kufanya utafiti kama huu uliofanyika kwa Wilaya zilizotajwa. Tutaendelea na utafiti, kwa sababu bila utafiti hatuwezi kufika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nihamie kwenye TASAF. TASAF ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, ametoa maoni yake ambayo na mimi nitayagusia, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa John Shibuda Magalle.

Waheshimiwa Wabunge wamesema TASAF imefanya kazi nzuri katika kusaidia kaya maskini. Ombi lao ni kutaka tusaidie Mpango huu wa TASAF ili uweze kuendelea kusaidia zaidi hizi kaya maskini, pia wapewe fedha za kutosha zaidi. Tumepokea pongezi na ushauri. Tunapokea ushauri wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa walengwa. Mpango huu una Idara mahususi inayoshughulikia na kuhamasisha na kujenga uwezo wa kaya kuweka akiba na kuijunga na vikundi vyta kuweka akiba na kuwekeza ili kujenga uwezo wa kaya kutekeleza Miradi ya Kiuchumi. Vilevile Waheshimiwa Wabunge wamesema TASAF ipo mbele na inafanya vizuri sana. TASAF III inasaidia watu maskini. Kule Mkoa wa Mara, walengwa wametoa ushuhuda jinsi walivyofaidika na mpango.

Waheshimiwa Wabunge pia walisema tulipitisha bajeti mwaka wa jana kupitisha bilioni kumi na nane, lakini zilizotoka ni bilioni tatu tu na wakatoa ushauri. Tumepokea pongezi na ushauri, Serikali itaendelea kutoa mchango wa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2014/15, ikiwemo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, kadiri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa John Shibuda Magalle, ameuliza kwa nini TASAF haiwapi majembe walengwa badala ya kuwapa fedha. Je, TASAF inaweza kutambua Wilaya kama Maswa na kuwapa majembe? Kaya zinazotambuliwa na kuandikishwa katika Mpango wa Kunusuru Kaya

Maskini, wanapata ruzuku ya kujikimu ili kupata mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi na kuwezesha watoto wadogo kuhudhuria kliniki na wale wenye umri wa kwenda shule waweze kwenda shule. Aidha, kaya hizo zinapewa fursa za kufanya kazi za muda ili kuongeza kipato katika kaya ili wafanye maamuzi mbalimbali ya matumizi ya fedha zinazopatikana, ikiwemo ununuzi wa pembejeo za kilimo kama majembe. Sehemu kuu mojawapo ya Mpango pia ni kuwajengea uwezo wa kuweka akiba na kuwekeza ili Mpango kuwa endelevu na vilevile waweze kufanya wenyewe maamuzi ya matumizi ya fedha na kuhusisha familia.

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete amesema Chalinze majina yaliyofanyiwa utambuzi na kuandikishwa mengine hayakurudi. Ni kweli inawezekana wakati wa utambuzi kaya maskini zilishirikishwa, ambapo wananchi wote katika kijiji husika hushiriki kuweka vigezo vya umaskini, chini ya Uongozi wa Serikali ya Kijiji na Wataalam Wawezeshaji kutoka Halmashauri. Baada ya kukubaliana kwa vigezo vya umaskini, huchagua Kamati ya watu 14, ambao watafanya kazi ya kwenda kaya hadi kaya. Orodha hiyo huletwa kwenye Mkutano wa Kijiji. Ikitokea kuna kaya ambazo hazijatambuliwa, TASAF itarudi tena kwenda kufanya utambuzi na kuona ni kitu gani kifanyike. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ridhiwani, kuna namna ya kuwasiliana na TASAF kwenye mfumo wa computer na baadaye kukokotoa na kutoa orodha ya kaya maskini sana, maskini kidogo na ambayo siyo maskini sana. Kwa hiyo, kaya zile ambazo ni maskini sana, ndiyo huletwa tena kwenye Mkutano wa Kijiji na kuridhia. Sasa kama kuna kaya ambazo zimesahauliwa, ninaomba tuiarifu TASAF ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Ole-Medeye amesema TASAF imesaidia sana kaya maskini. Zipo kaya ambazo zimeachwa kama alivyosema Mheshimiwa Ridhiwani, naomba sana Mheshimiwa Ole-Medeye na wengine wote ambao wanafikiria kuna kaya maskini ambazo zimesahauliwa, tujaribu kuieleza TASAF ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa David Ernest Silinde, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, aliongea juu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wakati wa Kamati. Naomba hawa niwajibu kwa maandishi baadaye kwa sababu muda pengine unaweza usitoshe. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, majibu haya ambayo ninayatoa kwa ufupi, nitayatoa kwa kirefu kwa maandishi kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, imetoa maoni mbalimbali na moja ya maoni ambayo yametolewa ni kutozingatia ushauri kuhusu kuujengea uwezo Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, kwa kuutengea fedha za kutosha ili uweze kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi katika Wilaya zote nchini hususan za mipakani. Maelezo ya mtoa hoja hayajaonesha jinsi Serikali ilivyozingatia ipasavyo, zaidi ya kutambua umuhimu wa MKURABITA. Serikali inatambua umuhimu wa kupima ardhi ya Wilaya zote zilizoko pembezoni na hata zile ambazo zipo katikati ya nchi ili kuimarisha usalama wa wananchi walioko katika Wilaya za pembezoni.

MKURABITA imeandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano, ambapo upimaji wa ardhi ya Wilaya za pembezoni umepewaa kipaumbele. Hata hivyo, MKURABITA imeendelea kuujengea uwezo Halmashauri za Wilaya zilizopo mipakani ili ziweze kurasimisha rasilimali ardhi za wananchi wao. Hadi sasa Halmashauri za Wilaya za mipakani zilizojengewa uwezo ni Ngara, Karagwe, Tunduma, Moshi, Kasulu, Ludewa, Missenyi, Kigoma, Masasi na Mtwara na tutaendeleo kufanya hivyo.

Vilevile Kamati imesema kuna benki nyingi nchini zinasita kupokea hati za kimila kama dhamana ya mikopo. Ni vyema Serikali ikachukua hatua madhubuti ya kuelimisha taasisi za kibenki nchini kuhusu uhalali wa hati za kimila kutumika katika dhamana ya mikopo. MKURABITA

inaendelea kufanya mazungumzo na mabenki kuhusu uhalali wa hati za haki miliki za kimila kutumika na wananchi kama dhamana. Kwa sasa hati miliki za kimila zinakubalika na Benki ya CRDB, nawapongeza sana; benki zote za jamii au Community Banks; Benki ya Ushirika na Benki za Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba benki wanaosikiliza waone umuhimu kwa sababu hawa ndiyo wateja ambao wakiwa na uwezo wataongeza amana kwenye benki zao. Lakini nafikiri tutaangalia na sheria ili kuona kwamba mabenki yanalindwa kwa kiasi gani na watu wanaweza wakatumia hati za kimila bila kuleta matatizo kwenye benki.

Aidha, MKURABITA imeendelea kuwaelimisha wananchi ili wajenge tabia ya kuandaa na kutunza mipango ya shughuli zao na kumbukumbu za mapato na matumizi ili kuziwezesha benki kufanya tathmini ya uwezo wao wa kulipa mikopo.

Vilevile Kamati imeitaka Serikali ihakikishe kuwa mpango huu unawezeshwa kikamilifu kifedha kwa kutengewa bajeti ya kutosha ili kutekekeza jukumu lilokusudiwa katika uanzishwaji wake na kuwanufaisha wananchi wa Tanzania. Serikali imeendelea kutenga fedha za utekelezaji wa MKURABITA katika bajeti ya kila mwaka. Katika mpango wa pili tutasisitiza umuhimu na kipaumbele cha MKURABITA kwa sababu mimi naamini kwa kweli MKURABITA ndiyo utakaowakomboa masikini na wanyonge wa Tanzania, kwa sababu MKURABITA utawezesha mitaji iliyo mfu iwe hai na itumike kama dhamana katika mabenki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu vilevile imetaka Serikali iongeze kasi ya upimaji wa ardhi katika maeneo mbalimbali. Utekelezaji wa shughuli za MKURABITA utaendelea kutumia mfumo wa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kufanya urasimishaji kumilikiwa na Serikali za Mitaa na hivyo kuwa endelevu, rahisi na wa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha azma hii, Serikali inaendelea kuratibu na kuandaa mfuko wa urasimishaji ardhi katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii ni kwa ajili ya kuongeza kasi ya urasimishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Chiligati ambaye nampongeza sana, ni Mwenyekiti wa MKURABITA, anauliza lini MKURABITA itapata fedha za utekelezaji wa urasimishaji wa urasimishaji?

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutatoa majibu haya kwa maandishi. Naomba mtupitishie bajeti yetu ili kusudi muda uliobaki utumike katika kutekeleza mambo ambayo ni muhimu kwa sababu kwa kweli Ofisi ya Rais sehemu ninayoongoza mimi ni muhimu sana katika kuondoa unyonge wa masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofii)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Naomba nifanye masahihisho. Wakati namtaja Waziri, nilisema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwezeshaji. Ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu.

Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Celina Kombani, utatumia nusu saa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo mmetufikisha, nasi tumeichukua, mingine tutaijibu na mingine tunaifanya kazi na mingine siyo ya kuitolea majibu ya moja kwa moja bali tunaifanya kazi ili tuone tunaitekeleza kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki kwa kuniamini kwa muda wa miaka kumi, nawashukuru sana kwa kushirikiana na mimi. Naomba wachukue ushauri wa Mheshimiwa Shibuda kwamba hata mwaka huu wembe ni ule ule wanichague kuwa Mbunge wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuishukuru familia yangu, kwa kweli palipo na mafanikio ya mwanamke yupo mwanaume na palipo na mafanikio kwa mwanaume mwanamke yupo. Kwa hiyo, naishukuru sana familia yangu, watoto pamoja na wajukuu kwa kushirikiana nami kwa kipindi chote cha miaka hiyo ambayo nalitumikia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Ndugu yangu Clara Mwatuka, waswahili wanasema utu uzima dawa. Kweli ushauri wake tumeuchukua, lakini pia nachukua na ushauri wa Mheshimiwa Mwандосya kwamba hili siyo Bunge la vijembe, bali wote tushikamane na tushirikiane, tuwe wazalendo, tuhakikishe kwamba tunajenga Taifa letu na siyo kupigana vijembe.

Mheshimiwa Mwenyeiti, mahali ambapo mwenzako amefanya vizuri unasema kweli amefanya vizuri na ambapo amefanya vibaya, unasema kwamba amefanya vibaya. Kila siku ukisema vibaya, vibaya, sasa haieleweki ni wakati gani amefanya vizuri na wakati gani amefanya vibaya. Kwa hiyo, ni ku-appreciate mahali ambapo mnaona tunafanya vizuri na kutukosoa ambapo mnaona kwamba hatukufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Clara Mwatuka, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Innocent Sebba, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa George Mkuchika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa upinzani, jambo kubwa ambalo nimeliona, wamesema kuhusu watumishi wa umma kutozingatia utendaji wa kitaalamu, yaani

professionalism hivyo nchi kushuhudia majanga na maafa, kwa mfano, kuporomoka kwa maghorofa, barabara kuharibika kutokana na uzembe wa makandarasi.

Ndugu zangu, watumishi wa umma wanapotekeleza majukumu yao huzingatia utendaji wa kitaalamu yaani professionalism. Iwapo atabainika mtumishi mmoja amekosea, anachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Siyo vyema, siyo busara wala siyo uungwana kusema kwamba watumishi wote wa umma ni wabovu. Wangekuwa wabovu hata jengo la Bunge nafikiri tusingekaa. Kwa hiyo, wapo wanaofanya vizuri na wapo wanaofanya vibaya. Wale ambao wanafanya vizuri, ni vizuri ku-appreciate kwamba wanafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawafanyi vizuri, kwa hiyo, hakuna anayenyooshea vidole, bali baada ya miaka mitano wanakupiga chini. Kwa hiyo, kila mtu azingatie taaluma ya mwenzake kwamba ni muhimu; tuiseme tu majanga yametokea nchi hii kwa sababu watumishi wa umma ni wazembe. Wapo wazembe wanachukuliwa hatua za kisheria na wale ambao sio wazembe ni vizuri tukawapongeza kwa sababu wanatumia profession zao vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi ya Upinzani wanasema kwamba ongezeko la shilingi 25,000/= la kima cha chini dogo. Mimi nasema kwamba katika awamu ya nne tumetoka kwenye mshahara wa shilingi 65,000/=, sasa hivi tupo kwenye kima cha chini cha shilingi 265,000/>. Jamani hilo ongezeko siyo dogo. Kwa hiyo, Serikali ya awamu ya nne imewajali watumishi na itaendelea kuwajali watumishi na tutaendelea kupandisha kima cha chini cha mshahara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mary Chatanda, kwa bahati nzuri aliiangalia hotuba ya Rais, akasema kabisa kwamba Rais aliagiza moja, mbili, tatu na Waheshimiwa Wabunge ni vyema tukaangalia hotuba za viongozi wetu. Ni kweli ametoa angalizo na ametuagiza mambo mbalimbali ya kushughulikia kuhusu watumishi wa umma. Kwa hiyo, nasi tunashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba siku ya Mei Mosi Mheshimiwa Rais amesema tutaongeza kima cha chini cha mshahara; nasi tunasema tumeongeza na tutaongeza. Mheshimiwa Chatanda napenda kukuarifu kwamba kwa mwaka huu wa Fedha tutaongeza kima cha chini kwa asilimia 13.5. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, agenda ya kusema kwamba Upinzani ndiyo walioomba kima cha chini kiwe ni shilingi 315,000/=, napenda kusema kwamba siyo busara kupoka agenda za Vyama vya Wafanyakazi. Vyama vya Wafanyakazi ndivyo vilivyoomba kwamba kima cha chini cha mshahara wa wafanyakazi kiwe ni shilingi 315,000/= na siyo Vyama vya Upinzani. Kwa hiyo, sisi pamoja na TUCTA kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ndiyo tunakaa pamoja. Msipokonye agenda. Ninyi siyo Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Siasa, tufanye kazi za siasa na Vyama vya Wafanyakazi tuache wafanye majadiliano na Serikali. Tumefanya vizuri, tumejadiliana na TUCTA, tumekaa nao; hicho kima cha chini, kwa pamoja tumekubaliana kwamba kitaongezeka kwa asilimia 13.5 na siyo ninyi. Msipoke agenda za watu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafo hapo hapo, pia naye alizungumzia kuhusu kima cha chini. Ni kweli kima cha chini tunapandisha mwaka hadi mwaka. Alitoa ushauri kwamba mnapopandisha kima cha chini, kima cha juu msiongeze kwa asilimia ile ile. Mheshimiwa Selemani Jafo, ndivyo tunavyofanya. Tukipandisha kima cha chini

kwa 13.5%, kima cha juu ujue kinapandishwa kwa 3% hakiwezi kupandishwa kwa 15% kama ilivyo kima cha chini.

Pia tunaposhusha Pay as You Earn, tunashusha kwa kima cha chini; kima cha juu hata ninyi mkiaangalia kwenye salary slips zenu bado mnakatwa 30%, lakini kima cha chini wanakatwa 12%. Kwa hiyo, mwangalie hata salary slips zenu mtaona kwamba kima cha chini kinakatwa kidogo Pay as You Earn, lakini kima cha juu ni 30%. Kwa hiyo, mishahara ya kima cha juu inakatwa sana Pay as You Earn ukilinganisha na mishahara ya chini.

Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Selemani Jafo na Kambi ya Upinzani walisema kuhusu suala la kutopandishwa madaraja ya watumishi mbalimbali. Napenda kuwaeleza kwamba watumishi mbalimbali wanapandishwa vyeo na vigezo vya kupandishwa vyeo viro, lakini kikubwa ni kuangalia kwamba je, bajeti yetu inaruhusu kwa kiasi gani? Je, huyo mtu ameeajiriwa lini? Je, anastahili pia kujaza fomu za OPRAS na kadhalika.

Aidha, napenda kuwafahamisha kwamba kwa sasa hivi mtumishi akipandishwa cheo tuna-feed moja kwa moja kwenye mfumo wa *Human Capital Management Information System*, kwa hiyo, hakuna malimbikizo ambayo yanatokea kwa upande wa mishahara.

Nakubaliana na Mheshimiwa Jafo kwamba pengine kuna baadhi ya waajiri wanachelewesha kuleta barua pale Utumishi. Kwa hiyo, nawaagiza waajiri wote walete barua za upandishwaji wa vyeo kwa wakati ili tuweze ku-feed mishahara yao ili wapate kwa wakati na kupunguza malimbikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi ya Upinzani wamesema kwamba wastaifu wanacheleweshewa mafao. Nakataa kabisa kwamba jamani, hali ya zamani na sasa ni tofauti kabisa. Mifuko yote ya Pensheni sasa hivi inafanya vizuri sana. Baadhi ya watumishi wastaifu wanapata mafao yao miezi mitatu kabla hawajastaifu. Nina mfano wa LAPF na PSPF wanafanya hivyo. Kwa hiyo, Mifuko yote ya Pensheni kwa ujumla sasa hivi wanafanya vizuri sana kwa sababu pamoja na mwajiriwa kutakiwa kutoa taarifa miezi sita kabla, sisi wenye pale Utumishi kutokana na mfumo mzuri tulionao, tunajua kabisa kwamba mwezi huu nani anastaifu, tunakata mshahara moja kwa moja. (Makof)

Kwa hiyo, hii inaonyesha kwamba sasa hivi tatizo hili ni dogo sana kwa upande wa mafao ya watumishi. Bali kuna watumishi wachache ambao walikuwa wamehama kutoka sehemu moja kwenda nyngine kwa sababu ya data zao kutoonekana, ndiyo maana wakati mwingine inachelewa.

Mheshimiwa Vincent Nyerere na Mheshimiwa Mary Chatanda walisemea kuhusu madai ya walimu. Nisingependa sana kuongea madai ya walimu tu, bali naomba njibui kuhusu madai ya walimu pamoja na ya watumishi wote wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kuanzia mwezi Julai, 2015 jumla ya watumishi wa umma 48,698 wamelipwa malimbikizo ya mishahara ya shilingi bilioni 49.5. Kati ya hao, jumla ya walimu 27,451 wamelipwa stahili zao za shilingi bilioni 13. Hapa nina jedwali la malipo ya watumishi mbalimbali kwa mwaka huu wa fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 24.5; watumishi wa afya wamelipwa shilingi bilioni 6.8; watumishi wa Magereza, Polisi na Uhamiaji, wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 1.3 na aatumishi wengine wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 16.4. Kwa hiyo, hizou shilingi bilioni 49.5 breakdown hii hapa ninayo. Kwa hiyo, tunaendelea kulipa malimbikizo ya Watumishi kwa kadri yanavyowasilishwa katika Ofisi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba wale ambao walikuwepo kuanzia mwaka 2006 waliona madeni yalikuwa mengi sana, lakini kwa sasa madeni hayo yamepungua na sasa hivi ninavyozungumza kuna madeni ambayo yamerudishwa kwa waajiri, lakini ukiangalia madeni ambayo tunadaiwa ambayo yapo kwenye mfumo ni kama shilingi bilioni 3.5 ambazo tunazilipa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo alieleza pia concern yake ya kwamba tumefuta promotions za mserereko. Mheshimiwa Jafo, hatujafuta promotions za mserereko kwani sheria hiyo haijafutwa, ipo pale pale kama kuna watumishi ambao wamekwama muda mrefu, naomba utuletee ili tuone tunawashughulikia kwa namna gani. Kama ni kwa mserereko au tunawapandisha vyeo kwa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hasa Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, amesema kutokana na utafiti uliofanyika, umebaini kwamba kuna tofauti kubwa sana kati ya mishahara ya kima cha chini na kima cha juu. Ni kweli anavyosema, utafiti umefanyika na Bodi ya Mishahara na baada ya kufanya utafiti imeona kwamba kuna tofauti kubwa sana. Tofauti hizo za mishahara zitafanyiwa kazi na tuneshaanza. Kama nilivyosema ni kwamba tunapopunguza Pay as You Earn tunapunguza kwenye kima cha chini lakini kwenye kima cha juu hatupunguzi. Yote hii ni kwa ajili ya kuangalia kwamba hiyo tofauti haiwi kubwa sana na huo utafiti unafanyiwa kazi na Bodi ya Mishahara, matokeo yake pengine tutatunga sheria ya kuwianisha na kuoanisha mishahara ndiyo jukumu kubwa la Bodi ya Mishahara ambayo wamepewa. Kwa hiyo, naomba uwe na subira, jambo hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Jasson Rweikiza amesema Wakala wa Maafunzo kwa Njia ya Mtando, yaani TaGLA itengewe bajeti ya kutosha ili kujenga uwezo wa kutekeleza jukumu lake la kuwajengea uwezo watumishi wa umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano.

Nakushukuru Mheshimiwa Rweikiza kwamba Wakala wa Maafunzo kwa Njia ya Mtando utatengewa bajeti ili kutekeleza majukumu yake na kweli bajeti yao inatakiwa kuongezeka ili ofisi nydingi zaidi ziwasiliane nao kwa njia ya video conference na kwa njia ya mtando. Ushauri wako tumeuchukua, tunaufanya kazi na bajeti ikiruhusu watawezeshe zaidi ili kuwasaidia watumishi wengi wa umma na wasio wa umma.

Mheshimiwa Ritta Kabati wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu aliongelea sana suala la watumishi kukaimu muda mrefu na pia Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete aliliongelea.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, kukaimu kuko kwa aina mbili; kuna wale wanaokaimu mtu akienda likizo, kwa hiyo, anakaimu kwa muda mfupi. Lakini kuna wale wanaokaimu nafasi wazi ambazo ziko katika taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wake kwa kweli ni mrefu kidogo. Kwa mfano, kwa upande wa Halmashauri, wanatakiwa kwanza wakae kwenye Baraza la Madiwani kupitisha wale ambao wana uwezo wa kukaimu sehemu husika. Akiishakaimu wanahakikisha kwamba wanaleta Utumishi. Kwa hiyo, inategemeana kwamba Mkurugenzi ameleta kwa wakati au hakuleta kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakishaleta Utumishi tunaendelea na ile process ya vetting na tukishafanya hivyo basi tunarudisha kwenye Halmashauri husika na Halmashauri hizo zinafanya uteuzi. Naomba kama kuna hoja maalum katika Halmashauri au taasisi yoyote

ambapo kuna watumishi wamekaimu muda mrefu, ni vyema tukakumbushana ili tuweze kumaliza zoezi la vetting ili wasikae katika nafasi hizo kwa muda mrefu. Kwa sababu wakikaa kwenye nafasi hizo kwa muda mrefu kule kujiamini kunakuwa ni kudogo sana.

Kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi na tutahakikisha kwamba wale watumishi wa umma wenye sifa tunawafanyia upekuzi haraka ili waweze kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Lollesia Bukwimba, alielezea Watendaji wa Vijiji wanaojitolea kwa muda mrefu na kwamba kibali kinapotoka, wapewe kipaumbele. Mimi nakubaliana naye lakini *the bottom line* wawe na sifa husika na siyo wale ambao hawana sifa. Wale ambao hawana sifa kwa sasa kwa kweli hatutawachukua. Naomba wakaimishwe wale mnaoona wana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sehemu wanaangalia mambo ya uzawa katika nafasi hizo za vijiji. Niziagize Halmashauri mbalimbali kwamba tume-delegate nafasi hizo lakini hatukuangalia mambo ya uzawa, tunachoangalia ni sifa husika. Kwa hiyo katika sehemu fulani kama wazawa wana sifa, wana haki ya kuajiriwa, lakini kama hawana sifa, Tanzania yetu wenye sifa wako wengi, wapewe wale wenye sifa na si kuangalia mambo ya uzawa wa sehemu husika.

Mheshimiwa Mary Chatanda alielezea kuhusu suala la upungufu wa wauguzi na madaktari, pia na Mheshimiwa Lollesia Bukwimba naye ameliongelea sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwafahamisha kwamba kipaumbele chetu kilikuwa upande wa walimu. Kwa sasa upande wa elimu kwa kweli tumeweza kufanya vizuri sana, walimu ni wengi na hata ukiangalia kwenye hotuba yangu mwaka ujao walimu ambao tutawaajiri ni 21,000 tu ukilinganisha na miaka mingine tulikuwa tunaajiri 38,000 au 31,000 na kadhalika. Hii inaonesha kwamba tumeanza kujitosheleza kwa upande wa walimu. Tatizo kubwa tulilonalo ni upande wa walimu wa sayansi. Kwa hiyo, tutaendelea kuajiri hao walimu wengi wa sayansi ili wafundishe watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa afya bado tunalo tatizo, lakini tunaendelea kuipa Wizara ya Afya kipaumbele kuajiri watumishi wengi zaidi ili watosheleze katika zahanati na vituo vya afya.

kwa upande wa Kilimo na Mifugo, kadhalika tumeipa kipaumbele. Kwa hiyo, zile nafasi ambazo tulikuwa tunaajiri walimu sasa tunahamishia kada nyingine ili tuplicate wataalam wengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chatanda, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Lollesia ni kwamba tutaendelea kuajiri watumishi wa umma katika kada hizo muhimu.

Mheshimiwa Kasikila na Mheshimiwa Philipa Mturano, walikuwa na concern yao ya upandishwaji wa vyeo vya walimu kwamba walimu wanaweza wakaajiriwa kwa pamoja lakini wanapanda vyeo katika miaka tofauti. Vigezo ambavyo vinatumika katika kuzingatia upandishaji vyeo ni pamoja bajeti, tange, miundo ya utumishi na ujazaji wa fomu ya OPRAS kwa mtumishi husika. Kwa hiyo, hivi ni vigezo ambavyo vinaangaliwa pia na utendaji wake wa kazi. Kwa hiyo, tutaendelea kupandisha vyeo kulingana na vigezo ambavyo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na lingine kuhusu Tume ya Utumishi wa Umma kwamba iendelee kutoa elimu kwa Watumishi wa Umma kuhusu mambo ya maadili. Hilo lilitolewa na Kamati ya Bunge. Napenda kusema kwamba Tume imetoa elimu kwa Watumishi wa Umma kuhusu uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu na kama mlivyoona kwenye hotuba yangu tulitoa na takwimu kwamba ni watumishi wangapi ambao wamefundishwa kuhusu maadili na kufuata sheria na nidhamu katika sehemu zetu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kasikila alisema semina elekezi isiishie tu juu, bali ishuke na kwa watumishi wengine. Napenda kukubaliana na Mheshimiwa Kasikila kwamba mtumishi anapoajiriwa anatakiwa kupata ABCs za kufanya kazi, apewe job description, aelewe kwamba anaenda kufanya nini, kwa sababu darasani alitoka na nadharia, sasa kwenda kwene practical ni kazi ngumu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa watumishi wote wa umma na wale wanaowaongoza. Kwanza wale ambao ni senior staff, ni vyema watumishi wa umma wanaokuja kuripoti katika sehemu zenu za kazi, mwafundishe kazi. Baadhi ya waajiri au Wakuu wa kazi ni wachoyo, hawataki kuwafundisha wale vijana kazi katika sehemu za kazi. Kwa hiyo, kijana anapoenda pale, anaambiwa tu wewe si umesoma! Kwa hiyo, nitoe wito kwamba hao wapatiwe mafunzo kazini. Hiyo ni njia mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine ni *induction course*. *Induction course* kwa watumishi wa Mahakama, zinatolewa na Chuo cha Utumishi wa Mahakama Lushoto. Watumishi wa umma *induction course* inatolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, naagiza waajiri wahakikishe kwamba watumishi wanaoajiriwa wapya hasa wale ambao wanaoajiriwa wengi kwa pamoja ni vyema wakawapeleka kwenye *induction course* katika vyuo ambavyo nimevitaja hapo juu. Suala la upandishaji vyeo nimeishamjibu Mheshimiwa Kasikila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, yeye ameongelesa kuhusu suala la kukaimu kwa muda mrefu. Nachukua lile la Bagamoyo na tutangalia kwamba ni watumishi wangapi ambao wanakaimu pale ili tuweze kuona ni nini kinakwamisha suala la vetting ili tukupe majibu ambayo yatawaridhisha hao wenzetu ambao wanakaimu na tuone kama kuna tatizo gani.

Mheshimiwa Jafo kwa ujumla nimeshamjibu. Suala la ajira nimesema kwamba kuna vipaumbele ambavyo tumejiwekea wenyewe, promotions za mserereko ziko pale pale, waajiri tu watuletee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole-Medeye aliongelea vibali vya ajira. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwani ni kweli vibali vya ajira baadhi yao vinachelewa kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, wakati wa kuandaa bajeti kama wakati huu, inatakiwa Halmashauri au Taasisi husika kuweka waajiriwa wapya kwenye mfumo. Kama hawakuwaweka kwenye mfumo ina maana kwamba ajira mpya haitapatikana. Kwa hiyo, niwaagize tu Maafisa Utumishi wote ambao wanashughulikia mfumo wa *Human Capital Management Information System* waweze kuingiza ajira mpya kwenye mfumo ili wasipate taabu ya vibali wakati unapofika.

Kwa hiyo, kama kuna specific case kwa upande wa Arumeru tuko tayari kuhakikisha kwamba kibali hiki kinatolewa kwa wakati. Kwa hiyo, ndugu yangu kama hamjapata kibali mpaka sasa hivi, naomba mlete ili tuweze kushughulikia kibali hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaotaka kuangalia kwamba vibali vimetolewa, tuna jedwali ambalo tunaangalia Wilaya na vibali ambavyo tayari vimeshatolewa. Kwa hiyo, kwa nafasi zile ambazo tume-delegate kwa Halmashauri, Halmashauri wenyewe waendelee na mchakato wa ajira. Kwa zile nafasi ambazo sisi Utumishi tunazishughulikia na Sekretarieti ya Ajira tutazichukua na kuzitangaza mara moja ili Watumishi waweze kuwekwa katika taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Nyambari Nyangwine aliongelea Kituo cha Kuwaenzi Wazee au Waasisi wa Taifa ambao ni Baba wa Taifa, Mwalimu Julius

Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Yeye amependekeza kwamba kituo hiki badala ya kujengwa Bagamoyo, kijengwe Dar es Salaam pale Mnazi Mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Nyambari kwamba tumechagua kupeleka hicho Kituo cha Bagamoyo kwa sababu za msingi kabisa. Pale Mnazi Mmoja nafasi ni ndogo, Dar es Salaam hakuna nafasi. Kwa hiyo, tulihitaji nafasi kubwa na kwa sababu za msingi kabisa kwamba kwanza tunataka kuwe na sehemu au vyumba nya kutunza nyaraka za waasisi. Pili, tuwe na sehemu ya ukumbusho wa kuhifadhi vitu vyao, zawadi zao na mali zao. Kwa hiyo, hiyo sehemu inatakiwa pia iwe kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kunatakiwa kuwe na kumbi za midahalo ya mikutano ambazo zitatumika katika makongamano na midahalo inayohusu fikra zao; nne, kuwe na viwanja nya kutosha nya michezo na matamasha mbalimbali yatafanywa kulingana na falsafa zao na mwisho, watu binafsi wanakaribishwa kuchangia ujenzi wa kituo hiki kwa kuzingatia utaratibu wa PPP.

Kwa hiyo, tumekipeleka Bagamoyo kwa sababu ya ukubwa wa sehemu ambayo tumepewa na tumeona hicho Kituo cha Kuwaenzi Wazee ni vyema tukakiweka huko Bagamoyo ambako tumpata nafasi kubwa.

Baada ya kusema hayo, niendelee kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa nasaha na busara zenu. Mambo mengi ambayo hatukujibu hapa, tutajibu kwa maandishi na kusambaza kabla bajeti hii haijaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kutuwezesha kuendesha kipindi hiki cha mchana na pia kwa busara zako na pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imeungwa mkono! Katibu!

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

### **Fungu 4 – Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kif. 1001 - Administration and HR Mgt... ...Tsh. 1,236,324,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 6 – Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi**

Kif. 1001 - Admin and HR Mgt ... ... ... Tsh. 3,605,963,506/=

Kif. 1002 - Comm. and Advocacy Div ... ...Tsh. 928,674,432/=

Kif. 1003 - Internal Audit Unit ... ... ... ...Tsh. 78,401,706/=

Kif. 1004 - Procurement Mgt Unit... ... ... Tsh. 85,310,664/=  
Kif. 2001 - Planning, Research and Dev. ...Tsh. 224,546,950/=  
Kif. 2002 - Infrastr. Division ... ... ... ...Tsh. 194,139,563/=  
Kif. 2003 - Resource Mob. & Econ Sect... ...Tsh. 237,237,334/=  
Kif. 2004 - Social Sector Div.... ... ... ...Tsh. 196,377,178/=  
Kif. 2005 - Agric. Productivity Div. ... ... ... Tsh. 107,360,923/=  
Kif. 2006 - Agric. Marketing Div. Syst ... ... ...Tsh. 103,614,566/=  
Kif. 2007 - Agric. Partnership & Coord... ...Tsh. 196,377,178/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**Fungu 9 – Ofisi ya Rais, Bodii ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - Admin and HR Mgt... ... ... Tsh. 1,393,396,000/=  
Kif. 1002 - Finance and Acc. Unit ... ... ... Tsh. 158,984,000/=  
Kif. 1003 - Planning Unit ... ... ... ... Tsh. 48,016,000/=  
Kif. 1004 - Internal Audit Unit ... ... ... ... Tsh. 12,800,000/=  
Kif. 1005 - Legal Services ... ... ... ... ...Tsh. 188,626,000/=  
Kif. 1006 - Information Comm. Techn ... ....Tsh. 35,284,000/=  
Kif. 2001 - Prod. and Research Unity ... ... ...Tsh. 101,512,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Remuneration Unit ... ... ... Tsh. 1,323,834,000/=

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza pale kwenye Subvote 229900 - Other Operating Expenses.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia trend ya ongezeko la fedha kutoka mwaka mmoja kwenda mwingine, mwaka 2013 ilikuwa shilingi milioni 28 tu, mwaka 2014 ikaongezeka kwa kiasi kikubwa, shilingi 401,600,000/=, mwaka huu imekwenda kwenye shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate ufanuzi wa kina, ni sababu gani ambazo zinapelekea kuongezeka kwa kiwango hiki cha fedha ilhalii hata tukiangalia pale juu, kiwango cha mishahara siyo kikubwa sana namna hiyo, lakini hizi fedha kwenye matumizi mengine, other operating expenses kiwango kiko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatukupata kauli ya kuridhisha, nakusudia kuondoa Shilingi. Naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, hapo ni ufanuzi, kwa hiyo, huwezi kuondoa shilingi! Hapo umeomba ufanuzi tu. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Machali anafahamu hata kwenye Kamati tulieleza hilo jambo kwamba hizo ni fedha za Mtaalam Mwelekezi ambaye atafanya job evaluation kwa ajili ya kada zote nchi nzima ili kuhakikisha kwamba lile suala la uwiano wa mishahara na kazi linafanyika na pia kuangalia gap ya mishahara kati ya taasisi moja na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni kwa ajili Mtaalam Mwelekezi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu

Kif.1001- Admin and HR Mgt ... .... Tsh. 20,575,672,000/=

### Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

Kif.1001- Admin and HR Mgt ... .... Tsh. 316,467,965,00/=  
Kif.1002 - Finance and Accounts ... .... Tsh 493,443,000/=  
Kif.1003 - Policy and Planning ... .... Tsh. 603,078,000/=  
Kif. 1004 - Internal Audit Unit ... .... Tsh. 310,542,00/=  
Kif.1005 - Inform and Comm. Techn. .... Tsh. 449,272,000/=  
Kif. 1006 - Procurement Mgt Unit ... .... Tsh. 314,000,000/=  
Kif. 2001- Cabinet Secretariat ... .... Tsh. 2,023,165,000/=  
Kif. 2002 - Government Comm.... .... Tsh. 455,270,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 - Good Governance.... .... Tsh. 606,011,000/=

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ilifanya kazi nzuri sana katika uchaguzi, kwa sababu ilianza kazi mapema. Mwaka huu tunaelekeea Uchaguzi Mkuu tayari...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Medeye eleza kipengele gani hapo unachozungumzia? Unazungumzia nini?

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kasma 210100; kwamba hivi sasa wako watu ambao wameanza Kampeni ya Uchaguzi Mkuu 2015, wanapita kwenye Majimbo wakigawa zawadi mbalimbali na wakiwaahidi wananchi kuwapa mambo mbalimbali. Kwenye Jimbo langu kwa mfano yuko Bwana mmoja ni Diwani, ameshindwa kuiendesha Kata yake, amekwenda kwenye Kata ya mwenzake akakuta wananchi wakichimba kisima, akaleta tanki la maji, akawaambia mimi nawaletea hili. (Makofii/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamelikataa, lakini liko bado pale kwa sababu amelitelekeza. Naomba kujua mikakati ya Serikali kwa ajili ya kudhibiti watu kama hawa ambao wanaanza kampeni kabla ya wakati? (Makofii/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI TA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kulikuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge wanachama wa APNAC, walieleza matatizo kama anayoyaeleza Mheshimiwa Ole-Medeye, bahati nzuri Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU alikuwa ndio mtoa mada pale. Niliagiza tangu jana na nikasema tunakuja leo kuomba fedha hapa; na mwaka huu tumeomba apewe nyingi kidogo kwa kujua kwamba kuna shughuli za uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Ole-Medeye tutawasiliana naye na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU yuko hapa, hilo jambo litafanyiwa kazi. Lakini nasema kwamba ni haramu kipindi hiki watu wako hapa wanafanya kazi za nchi, watu wanajipitishapitisha kinyume cha utaratibu. Watashughulikiwa! (Makofii)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 - Public Service Appeal .... ....Tsh. 450,980,000/=  
Kif. 2004 - Public Sec Reform Coord.... ....Tsh. 420,002,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

### **Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - Admin and HR Mgt .... .... Tsh. 19,551,956,000/=

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Esther Matiko. Tunaanza na Mheshimiwa Assumpter Mshama. Haya majina yote yameletwa na vyama, kama wewe hujaleta, usisimame.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza. Ni muda mrefu ambao tumekuwa na matatizo ya mishahara ya walimu, tumekuwa na matatizo ya madaraja ya walimu kupanda lakini hawapewi mishahara stahiki, walimu wanahamishwa wanakwenda kwenye vituo vingine miaka mitatu hajalipwa pesa zake. Napenda kujua ni lini au Mheshimiwa atutamkie leo ni lini tatizo la walimu litakwisha ama sivyo naondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri Mheshimiwa Majaliwa majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madaraja ya walimu na malipo yao ni suala ambalo Serikali ilishafanya utaratibu wa kuhakiki madeni yote ya walimu na juzi nilipokuwa natoa mchango wangu kwenye Wizara yetu, nilitoa takwimu kati ya shilingi bilioni 54 ambazo ziliikuwa zimehakikiwa na kukubalika, sasa mpaka mwezi Aprili, 2015 tumeshalipa jumla ya shilingi bilioni 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimehakikiwa na fedha inayokuja kulipwa na ambayo Hazina wameahidi kwamba mpaka Juni watakuwa wamelipa, ni jumla ya shilingi bilioni tatu tu kwa walimu wote. Utaratibu wa upandishwaji umeboreshwa na maboresho hayo, mwalimu au mtumishi atakapokuwa anapandishwa na mtiririko wa kifedha utakuwa unalipwa moja kwa moja. Kwa hiyo, tumeweka mkakati pia wa kudhibiti kuwepo kwa madeni baada ya walimu wote nchini kupandishwa madaraja yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mshama!

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kwingine sijui kinachoendelea sana, lakini nimekuwa nikisikia hili tatizo mara nyingi

labda nitolee mfano kwenye Wilaya ya Misenyi. Tuna zaidi ya walimu 200 amba nina mafaili yao ofisini kwangu yaliyo tofauti tofauti. Wengine ni wa vidato na wengine ni wa kuhamishwa bila kulipwa, wengine wanazaidi ya miaka mitatu wamepanda vyeo lakini hawajapata mishahara yao. Wengine tangu wameajiriwa sasa ni miaka miwili hajapata mshahara hata mara moja.

Kwa hiyo, napenda kujua hilo litatatuliwa lini? Especially kwa wale amba nina evidence ofisini kwangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mshama kwamba matatizo ya walimu tumeyatatuwa kwa kiasi kikubwa sana. Kwa mwaka 2014 tumekaa na Vyama vya Walimu vikao saba kuangalia matatizo ya walimu tu. Kwa hiyo, tatizo la kuhuisha muundo wao, tayari; tatizo la malimbikizo kama alivyojibu Mheshimiwa Majaliwa na pia chombo kimoja cha walimu ambacho kitaendelea kuboresha hali za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kuna specific case katika Wilaya fulani, ninaomba hiyo kesi ije. Sisi katika mfumo wetu mpaka sasa hivi, hata hao walimu waliaojiriwa juzi tu, tayari wameshaingizwa kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo walimu wenyе matatizo na matatizo; na matatizo haya yanatokana na nini? Mwalimu amepangiwa kwenda Ludewa, yeye anaripoti Ludewa halafu anaondoka anaenda kupangiwa sehemu nyingine. Kwa kuwa check number yake tunai-control pale Utumishi, mtumishi wa Serikali hana ujanja sasa hivi.

Kwa hiyo, matokeo yake kama ana check number na sisi tunamwona na watu huko kwenye ajira akiajiriwa upya, sisi tunaiona ile check number tunaanza ku-query, kwa nini? Kwa hiyo, tukim-trace tunakuta alikuwa ame-abscond sehemu fulani. Kwa hiyo, mchakato wa kumrudisha tena kwenye system, inaweza ikachukua hata miaka miwili kwa sababu ni lazima umwombee kibali maalumu kwa Katibu Mkuu Kiongozi tuone ni kwa sababu gani alikuwa ana payroll number?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuta baadhi ya watumishi, pengine alikuwa Magereza, ametorosha mfungwa, ameenda kusomea ualimu, sasa amekuwa ni mwalimu. Lakini check number tunai-note.

Kwa hiyo, watumishi sasa hivi, ile kucheza kwamba naweza kuacha hapa nikaajiriwa kwenye Taasisi nyingine ya umma ambayo iko kwenye payroll yetu, hawezi akacheza. Kwa hiyo, kuna specific cases kama hizo, sisi tunazishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Mshama pamoja na Mkurugenzi wa Misenyi, watuletee tuone kwamba kuna tatizo gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Jafo!

**MHE. SULEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, concern yangu kubwa vilevile ilikuwa ni suala zima la watu waliosahaulika amba kwa kipindi kirefu wamefanya kazi lakini sasa hawajapanda madaraja. Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba hapa utaratibu wa kupanda kwa mserereko kwa watu amba wanaweza kupeleka maombi yao kule rasmi, lakini

tatizo ni kubwa kweli, siyo kwa Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kisarawe, ni kubwa kwa nchi nzima.

Hivi sasa malalamiko yamekuwa makubwa; kuna watu wengine wameajiriwa toka mwaka 2002 na wengine 2001, lakini kwa sababu hawajapanda kwa muda mrefu sana na anaambiwa kwa sasa hivi utaratibu ni mpaka baada ya miaka mitatu ndiyo aweze kupanda, kule, utaratibu ni kwamba mshahara wake umefutwa. Halikadhalika katika Vyuo Vikuu, kuna ma-lecturer ambaao sasa hivi wanafundisha, aliajiriwa kipindi cha nyuma lakini sasa kuna mtu kaajiriwa leo hii, wanakutana na kulipwa mshahara mmoja. Hiyo linaleta *disharmony* katika mazingira ya kazi.

Sasa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hayo akiyapata ofisini kwake atayafanya kazi, lakini nikwambie, huko katika mazingira ya kazi, japokuwa ninyi Mawaziri mnajua hivyo, lakini huku kuna matatizo makubwa. Sasa naomba kauli ya Serikali hapa; je huo utaratibu wa mserereko kwa wale watumishi ambaao *special* hawakupanda lakini walikuwa wanastahili kupanda, utawezekana? *Alternatively*, je, kama utaratibu hauruhusu, lakini hata ikiwezekana watu wale wawe wanapanda kwa kila mwaka kwa madaraja ilimradi waweze kufikia ile rank ambayo inastahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo lakini naomba ufanuzi wa kina; la sivo, nitatoa shilingi katika mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kama kuna hoja mahsus, hoja hiyo tutazishughulikia lakini *case by case* ni kwamba watumishi ambaao wamekaa muda mrefu katika cheo kimoja tunawapandisha kwa msesereko na hiyo siyo kesi ya kwanza. Kama mnakumbuka wakati tunaanza *Decentralization By Devolution* yaani *D By D* watumishi wa kilimo walikaa kwa muda mrefu katika kada moja, tumewapandisha vyeo.

Upande wa elimu pia, walivyo-delegate kwenye Halmashauri, kulikuwa na walimu ambaao wamekaa muda mrefu ambaao walikuwa *Central Government* tumewapandisha kwa mserereko. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo, kama una hoja mahsus, kama una sehemu mahsus kama vyuo vikuu tunaomba utuletee hizo kesi, tutazishughulikia na inawezekana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SULEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni mahsus, lakini siyo kwa vyuo vikuu, maana yake ni kwa Tanzania nzima. Kwa kauli hiyo, sasa naomba Maafisa Utumishi wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha wale watumishi wote ambaao kwa muda mrefu hawajapanda, wapelekwe Wizarani ili mradi waweze kupata haki yao stahili. Ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ole-Medeye!

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nazungumza chini ya Kasma 2101000. Mwaka jana nilipochangia Bajeti ya Ofisi ya Rais nilzungumzia juu ya suala la maslahi ya viongozi wastaifu, na leo narudia kulizungumzia suala hilo, lakini Mheshimiwa Waziri hakulijibu suala hilo, amekwepa.

Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini na nasema iwe ni kabla Bunge hili kumalizika wataleta mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Maslahi ya Viongozi wastaifu ili Mawaziri ambaao wako nje sasa hivi wanatembea barabarani kwa miguu, angalau waweze

kupata maslahi kama ambavyo viongozi wengine waliostaafu, waliotumikia Serikali wanapata maslahi yao? (Makofij)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli jibu la papo kwa papo halitakuwa rahisi kiasi hicho, sipendi kudanganya. Ni kweli Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mawaziri, concern yao kubwa ni kwamba wapewe pensheni wakati wa kustaafu na pia kuangalia mafao yao.

Kwa hiyo, hilo tunalingalia kama Serikali na siwezi kulijibu leo hii au kipindi hiki cha Bunge, lakini nasema wazo lake ni zuri na siyo Mawaziri peke yao, bali wapo watumishi mbalimbali ambaao wametumikia Taifa muda mrefu na wana title kubwa, lakini wanatembea barabarani wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, hilo tutaliangalia kwa ujumla wake na siyo kwa Mawaziri peke yake, bali tutaangalia na kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakamata mshahara wa Mheshimiwa Waziri wa Uhusiano na Uratibu, siyo wa Waziri wa Utumishi.

**MWENYEKITI:** Unakamata mshahara wa nani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mary Nagu!

**MWENYEKITI:** Eh! Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nakamata mishahara miwili, naanza na huu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hapa nchini wana malalamiko mbalimbali likiwemo pia suala la kujunga na kujitoa kwenye vyama vya wafanyakazi na takribani miaka kama sita iliyopita kilitokea movement hapa nchini, baadhi ya walimu wakitaka kuanzisha Chama chao cha Wafanyakazi. Hii ni kutokana na kuona kwamba Chama cha Walimu ambapo wapo, hawardhishwi na utendaji kazi wao.

Sasa naomba niulize Serikali, Waziri wa Utumishi ambaye anahuksika na watumishi wa kada ya ualimu; kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 20(1) kinatoa right ya watu kuamua wa-associate na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ndogo ya (4) au fasili ya (4) ya Kifungu hicho cha 20 kinaleza bayana kwamba; "itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujunga na chama chochote." Sasa mfumo wa sasa wa Trade Union hapa nchini unadhihirisha kabisa kwamba baadhi ya watu wameingizwa huko pasipo wao kuomba ili kusudi wawe wanachama.

Sasa naomba kauli ya Serikali, imefika mahali walimu ambaao walitaka kuunda chama chao cha wafanyakazi wanazungushwa. Serikali inazungumza nini kuhusu kuwasaidia walimu hawa ambaao waliamua ku-associate ili kusudi kuweza kuunda chama chao wanazungushwa na Wizara ya Kazi kwa muda mrefu, naomba kauli ya Serikali. Kama sikuridhika, nakusudia kutoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Kazi na Ajira!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala analozungumza Mheshimiwa Machali ni kweli kwamba kuna walimu wametaka kuunda chama chao tofauti na chama

kilichopo cha CWT. Taratibu za kuunda chama kipywa kwa aina hiyo hiyo ya kada ya wafanyakazi, ina masharti kadhaa; mojawapo, chama kipywa hicho kisiwe na madhumuni sawa na chama kilichopo; chama hicho hicho hicho kisije kikawa na wanachama wa aina hiyo hiyo, kwa mfano, kama ni walimu wa sekondari wanatoka CWT wanaunda chama kingine cha walimu wa sekondari na wa msingi na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, kuna hivyo vigezo ambavyo tusipoviangalia, kwanza tutakuwa na *conflict of interest* katika makundi haya, tutaweka utitiri wa vyama ambavyo vina madhumuni sawa, vina malengo sawa na wafanyakazi wale wale kwa sababu ambayo siyo za lazima. Vyama hivi kweli ni vya hiari; na chama anachokisemea Mheshimiwa Machali, naye akiwa ni mwalimu na chama hicho kisiwe cha eneo moja, kiwe cha Kitaifa, kama vilivyo vyama vya siasa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chama kile kilitaka kuundwa na walimu zaidi kutoka Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, hakiku-satisfy. Pia madhumuni yake ukiangalia, pamoja na kwamba walikiita jina tofauti, madhumuni yake ni yale yale; kutetea haki za walimu, kuhakikisha masuala na maslahi ya walimu na vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, wameendelea kushauriana na Msajili ya Vyama vya Wafanyakazi kwamba ninyi bado mna *affiliation* na CWT na mnapokuwa na chama kimoja mnakuwa na nguvu zaidi ya kujadiliana na Serikali. Kwa nini mwendelee kujibagua bagua?

Kwa hiyo, hatuna nia mbaya ya kutosajili hiki chama isipokuwa waendelee tu kukubaliana. Mara ya mwisho nimeona barua yao, wanaulizwa kwanini hamtaki kusajili chama chetu? Wameendelea kuelezwaa kwamba unless mnataka kuunda chama tofauti, madhumuni tofauti na watu tofauti na kiwe cha Kitaifa, chama hicho kitaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo tatizo peke yake. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tunasema kwamba Katiba ya nchi ndiyo sheria mama; na sheria yoyote ambayo itatungwa kinyume cha Katiba, hiyo sheria inakuwa dissolved automatically, hatuwezi tukaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 20(4); "Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kuijunga na chama au shirika lolote." Ni Katiba inazungumza hivyo. Leo kuna walimu kibao na hata ukienda kwenye kada nyingine za watumishi sijasikia wengine wakilalamika; wanakatwa pesa zao mojawapo ikiwemo ni agency fee, pasipo hiari yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, huwezi ukamlazimisha mtu kwamba unakuwa ni agent wake. Haiwezekani! It is like mimi leo nijifanye kwamba nataka niwe agent labda wa group fulani, wakati sijakaa na kuzungumza nao. Haikubaliki!, inakuwa ni jambo ambalo lipo kinyume cha Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huu utaratibu wa kusema kwamba hicho chama kimekuwa na malengo yanayofanana, leo hata tukiangalia kwamba vyama vya siasa vimeudwa, baadhi ya malengo yanafanana; kukamata dola na kuiendesha nchi. Haiwezekani kwamba tuje tuseme labda wafanyakazi wana seek freedom yao ya kushirikiana kwa mambo yao msingi, tuseme kwamba hawa wana malengo yanayofanana na chama fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili aeleze, ametumia kigezo gani? Ni sheria gani ambayo inakataza kwamba chama kikiwa na malengo yanayofanana kikataliwe kusajiliwa? Ni sheria gani mnatumia? *This is unconstitutional!* Haiwezekani kufanya namna hii, mnawakatilia watu jambo ambalo linakiuka misingi ya Kikatiba.

Mheshimiwa Waziri, nafikiri mwende mkae muangalie. Haya mambo ya kuzuia watu kuweza ku-associate, Katiba imewapa *right* hiyo. Unawapa *right* kwa mkono wa kulia mnawanyanganya kwa mkono wa kushoto, *this is unfair*. Mheshimiwa Waziri analifahamu hili suala kwa muda mrefu. Tumefanya *consultation* nje, lakini leo nashangaa, kidogo anajaribu kutoa vitu ambavyo huwa hazungumzi hivi. Kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba suala hili, hebu Serikali itoe kauli ya kuwapatia watu hawa. Walimu wao watapata haki yao lini kwa mujibu wa Katiba kama inavyoainishwa katika Ibara ya 20? Naomba kauli ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachoongelea ana-quote Katiba, lakini tujuje kwamba Katiba ni sheria mama na baada ya hapo sheria zinatungwa kwa ajili ya utekelezaji wa hiyo Katiba, baadaye kanuni pia zinatungwa. Halafu tukumbuke pia hivi vyama vina Katiba zao.

Hili suala la *agency fees* ni la kisheria; Sheria ya Taasisi za Kazi. Lakini chama cha CWT kina kanuni, na actually tunazungumza na CWT kuhusiana na hii *agency fee* ambayo najua inawasumbua walimu, hata mimi inanisumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaambia wajaribu kubadilisha Katiba yao kusudi mwalimu kabla hajakatwa *agency fee* aridhie kwa kujaza fomu, kwa sababu ile *agency fee* inakatwa kwa chama ambacho kina zaidi ya asilimia 50 ya wafanyakazi wa aina hiyo ambao wapo kwenye chama chao. Ile agency, maana yake, watakapokuwa wanasaidia kulinda na kutetea haki za wafanyakazi wengine katika chama hicho, yule ambaye hayupo kwenye kile chama naye atatetewa. Lakini tunachosema, asikatwe bila ridhaa yake. Kwa hiyo, hii tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la chama kingine najua wengi wanataka kuijunga na chama kingine kwa ajili ya kukwepa hii *agency fee*. Sasa lazima tuangalia kanuni na taratibu za kuunda hivi vyama; hatuwanyimi haki. *Actually* wengine kati ya hao ambao wanataka kuunda chama hiki, wanatoka CWT. Kwa hiyo, tunabomoa chama kimoja, tunajenga chama kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri walimu wale waendelee kukubali. Tuangalia kwanza hili suala la CWT, *agency fee*, kuhusu Katiba yao, lakini waendelee kuangalia kwamba hamna sababu ya kuunda chama kingine kama CWT ipo pale na inatetea maslahi ya walimu kama kawaida.

**MWENYEKITI:** Kifungu hiki kinaafikiwa? Mheshimiwa Machali, hukutoa hoja ya kutoa shilingi. Hukutoa shilingi! Ulisema unakusudia kutoa shilingi na ulipotoa maelezo yako, hukutoa shilingi. Kifungu hicho kinaafikiwa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Sawa, nyongeni walimu!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif.1002 - Finance and Accounts Unit ... ... Tsh. 324,929,000/=

Kif.1003 - Government Comm. Unit ... ... Tsh. 262,412,000/=

Kif.1004 - Procurement Mgt Unit ... ... Tsh. 314, 249,000/=

Kif.1005 - Internal Audit Unit ... ... Tsh. 184,403,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 - Panning Division ... ... ... ... Tsh. 618,204,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naenda kwenye subvote 210500 - Personal Allowance In Kind.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tu hapo, nahoji tu kwamba fedha zinaongezeka kwa kiasi kikubwa. Mwaka wa 2013 ilikuwa ni shilingi 20,470,000/=; mwaka uliofuta ambaa utaishia tarehe 31 Juni, 2015 ni shilingi 13,860,000/=. Tunaenda mbele, unakuta shilingi 94,260,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahoji kwamba nyongeza yote hii ni ya nini, wakati ukiangalia mwaka juzi kidogo ilikuwa imepungua. Kutoka shilingi milioni 20, ikaja shilingi milioni 13, leo inakwenda shilingi milioni 94. Naomba sababu za Serikali za kuongeza matumizi haya ya posho ambazo pengine tunafikiri bado tunasema kwamba nchi ipo kwenye hali ngumu; maeneo mengine miradi ya maendeleo watu wamepunguziwa kwa mfano kwenye reli, hali siyo nzuri na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kauli ya Serikali, ni sababu gani zinazopelekea hizi posho ama Personal Allowances - In Kind? Hapa kuna nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuelewe, Personal Allowance - In Kind maana yake ni nini? Maana yake ni stahili za wafanyakazi ambaa ni entitled kwa ajili ya ununuzi wa samani, maji na umeme; yaani utilities in person. Kuna utilities, umeme kwa ajili ya jengo hili, lakini kuna umeme haki ya mfanyakazi. Kwa hiyo, wale entitled wanapewa allowance kama hizi.

Sasa kwa kuwa allowances hizi kwa mwaka huu zinaongezeka, ina maana lazima kutakuwa na ongezeko la aina fulani. Kwa hiyo, hizi ni kwa ajili ya wale watumishi wanaostahili allowance kama hizo. Umeme, maji, rental, simu na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Kifungu hiko kinaafikiwa!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1007 - Inform and Comm. Tech Unit... Tsh. 126,090,000/=

Kif. 2001 - Policy Dev. Division... ... ... ... Tsh. 822,814,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Mgt Services Division ... ... ... ... Tsh. 848,312,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Subvote 2002, kifungu kidogo 210500 - Personal Allowances In Kind.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunahitaji maelezo ya kina, tufafanulie ni wafanyakazi wameongezeka? Maana ukiangalia hiyo trend hapo, utaona kwamba 2013/2014 ilikuwa ni shilingi milioni 33, mwaka 2014/2015 shilingi milioni 59, lakini mwaka huu 2015/2016 ni shilingi milioni 252. Sasa kama hizo utilities Mheshimiwa Waziri alizotaja hapa kwamba ni umeme, maji; sidhani kama zinaweza zikafika hiyo amount. Kwa hiyo, ni bora utuelezea kwa kina, kama hazina maelezo stahili ziweze kupelekwa hata kwenye mashule zikajenge choo watoto wetu wasome.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aelewé kwamba kila mwaka tunatoa promotion. Sasa ukitoa promotion, mtu anayekuwa entitled huwezi ukamwacha nyuma. Kwa hiyo, suala la kuongezeka kwa watumishi ambao ni entitled ni lazima, huwezi ukalikwepa! (Makofii)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2003 - Establishment Div ... .... .... Tsh. 809,184,000/=

Kif. 2004 - Ethic Promotion Div ... .... .... Tsh. 220,356,000/=

Kif. 2005 - Human Capital Mgt Div... ....Tsh. 1,179,117,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - Human Resources Dev. Div.... ....Tsh. 8,473,392,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, halafu wajiandae Mheshimiwa Dkt. Mbassa na Mheshimiwa Mtutura!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Najielekeza kwenye subvote 220700 - Rental Expenses. Mwaka wa juzi ilikuwa ni sifuri kabisa, mwaka uliofuta wa 2014/2015 ni shilingi 28,870,000/= na mwaka 2015/2016 inaonekana wanaomba kiasi cha shilingi 2,034,750,000/=.

Naomba tu Mheshimiwa Waziri atusaidie kujua, wanategemea kupanga au kukodi majengo gani au ni kitu gani ambacho kinakuja ku-cost shilingi 2,034,000,000/=? Kwa nini pengine msifikirie kujenga majengo yenu? Huu utaratibu wa kupanga majengo, ni wazi wakati mwininge unakuta ndiyo mianya ya kuja kuweza kupiga pesa! Kwa nini msijenge? Shilingi bilioni mbili kutoka shilingi milioni 28, ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ije kutupa maelezo. Kama ingekuwa inaruhusiwa kutoa shilingi, tunaomba ufanuzi wa kina watoe maelezo ya kina, ni kitu gani? Kwa nini msijenge mnaenda kupanga

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, angeona *tittle* hii ya Civil Service Training and Development, hicho ni Chuo cha Utumishi wa Umma; na tunafanya expansion katika mikoa mbalimbali. Sasa hivi tumeanzisha Tawi la Mbeya. Kule tunapanga majengo, Tawi la Singida tunapanga majengo na pia Tawi la Dar es Salaam tumepanga majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alilosema kwamba, je, tuna mpango gani wa kujenga majengo yetu? Mpango huu tunao wa kujenga majengo yetu na majengo haya tutayajenga katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo linalekeza hapa kwa upande wa Serikali ya awamu ya tano, pia nako kutakuwa na *rental expenses* ambazo zinahitajika kwa viongozi mbalimbali ambao wataingia katika awamu ya tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Gervas Mbassa! Bado Mheshimiwa Machali? Ni mara moja tu, hii siyo mara mbili. Hairudiwi mara mbili. Ulikuwa unataka ufanuzi. Namwita Dkt. Gervas Mbassa!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na hiyo ilikuwa ni hoja mojawapo lakini najielekeza kwenye kasma ndogo 221100 - *Travel out of country*. Kifungu hiki kwa mwaka wa pesa uliopita, kilipewa shilingi 21,533,000/=, lakini zamu hii kimepangiwa shilingi 11,654,000/= ilhali kifungu cha usafiri ndani ya nchi kina pesa kidogo. Hizo fedha ni kwa ajili ya nini? Tunaomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, maelezo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kama kinavyojieza kwamba ni usafiri nje ya nchi; sasa mara nyingi *development partners* wetu wanatusaidia kwa mambo ya malazi na kadhalika, lakini kwenye *travelling expenses* wanataka tujigharamie wenyewe. Kwa hiyo, hatuwezi kuachie hizo fursa kwa kusema kwamba hatuwezi kugharamia gharama za usafiri. Kwa hiyo, hilo ni gharama za usafiri nje ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Mtutura!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu, kifungu ambacho nilitaka kuuliza, kimeshaulizwa na Mheshimiwa Machali.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

Kif. 3004 - Diversity Mgt Unit ... .... .... Tsh. 260,185,000/=  
Kif. 4002 - Mgt Information System Div ... Tsh. 3,722,017,000/=  
Kif. 4003 - Records and Archives Div. .... .... .... Tsh. 0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote*)

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya  
Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kif. 1001 - Admin. and HR Mgt... .... .... Tsh. 1,954,273,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mshahara wa Waziri bado!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mshahara wa Waziri, Mheshimiwa Mkuchika, bado?

**MWENYEKITI:** Ni mmoja tu. Mheshimiwa Machali aliyetoa hoja ni Mheshimiwa Waziri wa Utumishi. Kwa hiyo, ndiyo mwenye mshahara tu. Ndiyo huo unaoushika. Kama hukuushika huo, basi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - Finance and Accounts ... ... ...Tsh. 305,797,000/=  
Kif. 1003 - Plann, Monitoring and Eval ... ...Tsh. 180,724,000/=  
Kif. 1004 - Government Comm. Unit ... ...Tsh. 142,696,000/=  
Kif. 1005 - Procurement and Mgt Unit... ...Tsh. 147,218,000/=  
Kif. 1006 - Internal Audit... ... ... ... ...Tsh. 121,557,000/=  
Kif. 1007 - Inform. and Comm. Tech Unit ... Tsh. 88,784,000/=  
Kif. 1008 - Legal Services Unit... ... ... ...Tsh. 322,389,000/=  
Kif. 2001 - Public Service Leaders Div.... ... Tsh. 554,338,000/=  
Kif. 2002 - Political Leaders Div. .... ... ... Tsh. 407,765,000/=  
Kif. 2003 - Zonal Offices ... ... ... ... ... Tsh. 1,991,150,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

#### Fungu 66 – Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango

Kif. 1001 - Admn. And HR Mgt ... ... ... ....Tsh. 1,854,667,435/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, tumeshahoji tayari.

Kif. 1002 - Finance and Accounts... ... ... ...Tsh. 422,736,400/=

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao umetupatia tunaleta majina hapo na utatusoma na majina yameandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haiwezekani mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mary Nagu upite na wakati majina tayari yapo hapo mezani. Ndiyo siku zote utaratibu ambao tumekuwa tunafanya.

**MWENYEKITI:** Mshahara ni wa yule aliyetoa hoja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zipo mbili. Mheshimiwa Mary Nagu ana hoja yake, Mheshimiwa Mkuchika, sawa alimezwa na Mheshimiwa Celina Kombani na kuna hoja ya Mheshimiwa Mary Nagu.

**MWENYEKITI:** Hapa Planning Commission hamna mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Machali hapa tupo Tume ya Mipango, hakuna mshahara wa Waziri hapo. Msome hiyo ni Tume ya Mipango. Kuna mshahara wa Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango, siyo mshahara wa Waziri.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - Planning and Monitoring Div ... Tsh. 405,354,000/=  
Kif. 1004 - Government Comm. .... .... ....Tsh. 305,211,000/=  
Kif. 1005 - Internal Audit Unit .... .... .... .... Tsh. 255,030,000/=  
Kif. 1006 - Procurement Mgt Unit .... .... ....Tsh. 221,446,000/=  
Kif. 1007 - Library and Doc. Unit .... .... ....Tsh. 149,793,000/=  
Kif. 1008 - Mgt Information System .... .... ....Tsh. 189,481,000/=  
Kif. 2001 - Macro Economy Cluster .... ....Tsh.1,065,856,600/=  
Kif. 2002 - Productive Sector Cluster.... .... Tsh. 897,760,000/=  
Kif. 2003 - Infrastr. and Services Cluster.... .... Tsh. 738,314,900/=  
Kif. 2004 - Social Serv. & Demogr. Cluster... Tsh. 920,058,000/=  
Kif. 2005 - International Trade &Econ. Relat..Tsh. 446,187,665/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

### **Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - Admn. And HR Mgt .... .... ....Tsh. 1,862,220,000/=  
Kif. 1002 - Finance and Accounts... .... .... ....Tsh. 237,808,000/=  
Kif. 1003 - Plann, Monitoring & Evaluation ...Tsh.157,627,000/=  
Kif. 1004 - Government Comm. Unit .... .... ....Tsh. 251,866,000/=  
Kif. 1005 - Legal Service .... .... .... ....Tsh. 34,416,000/=  
Kif. 1006 - Procurement Management ... ....Tsh. 174,949,000/=  
Kif. 1007 - Management Inf. Systems... .... ....Tsh. 509,355,000/=  
Kif. 1008 - Internal Audit .... .... .... .... Tsh. 211,531,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - Recruitment Mgt Division ... ...Tsh. 1,365,570,000/=

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitajielekeza kwenye subvote 210100 kwenye basic salaries, pensionable posts.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashuhudia trend ya fedha ikiongezeka kutoka mwaka mmoja kwenda mwaka mwingine. Ni jambo jema kuweza ku-motivate rasilimali watu tuliyonayo ili kusudi waweze kufanya kazi kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa tangu mimi nimekuwa Mbunge, tumeshuhudia na tukimsikia Dkt. Edward Hosea akizungumzia kukosa meno na kuomba rungu ili kusudi aweze kuwa anapeleka kesi za Watuhumiwa wa Rushwa Mahakamani moja kwa moja; na ameshuhudiwa akizungumza kwamba tatizo ni Ofisi ya DPP. Sasa kwa kuwa tunatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na rasilimali watu ambayo inalipwa mshahara ili kusudi iweze kufanyakazi vizuri. Nataka Serikali itueleze; sikilizeni swali, mbona mna wasiwasi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaajiri kwa kutumia mishahara ambayo mmekuwa mnaongeza mwaka hadi mwaka, aina ya rasilimali watu ambayo itaweza kusikiliza kilio cha Dkt. Edward Hosea ili kumruhusu kumpa meno ya kupeleka hizi kesi moja kwa moja Mahakamani ili kuondokana na vikwazo vya Ofisi ya DPP. Ni lini, kwa sababu mishahara hii hapa inaongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, sasa hicho kifungu kina uhusiano gani na hilo swali? Hebu nitafsirie hapo, kina uhusiano gani na hilo swali. (Kicheko)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nahusianisha kazi ya mshahara kwa sababu mtu hawesi kwenda kufanya kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, hizi pesa ambazo zinaongezeka, ni kwa namna gani Serikali itahakikisha wanaajiriwa watu wenyewe weledi watakaojali kilio muhimu cha Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU? Kwa sababu ni mishahara hii inaongezeka na inawezekana kuna watu wengine wataajiriwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, unatakiwa uulize, hizo fedha zilizoongezeka ni za nini?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo suala hilo tu, kwa sababu ni lazima tuhusianishe vitu hivi.

**MWENYEKITI:** Ndiyo ultakiwa upatiwe jibu hilo. Sasa unauliza hizo fedha zimeongezeka ni za nini?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni hiyo, Serikali watueleze ni lini watafanya hiki ambacho nauliza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa havioani na hiyo hoja!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Quality Control... .... .... .... .... Tsh. 622,497,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**Fungu 94- Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - Admn. and HR Mgt ... ....Tsh. 9,615,923,000/=  
Kif. 1002 - Finance and Accounts Unit ....Tsh. 145,825,000/=  
Kif. 1003 - Plann, Monitoring & Evaluation...Tsh. 676,242,000/=  
Kif. 1004 - Internal Audit Unit ... ....Tsh. 119,327,000/=  
Kif. 1005 - Procurement Mgt Unit ....Tsh. 78,176,000/=  
Kif. 2001 - Civil Service ....Tsh. 1,024,238,000/=  
Kif. 2002 - Local Governt Service ....Tsh. 607,204,000/=  
Kif. 2003 - Teachers' Service ....Tsh. 1,489,960,000/=  
Kif. 2004 - Fire and Immigration Services... ....Tsh. 0  
Kif. 2005 - Health Service....Tsh. 313,360,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 4 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kif. 1001 - Admn. And HR Mgt ... ....Tsh. 250,000,000/=

**Fungu 6- Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi**

Kif. 1001 - Admn. And HR Mgt ... ....Tsh. 7,681,848,000/=  
Kif. 1002 - Comm. & Advocacy Div ....Tsh. 435,859,000/=  
Kif. 1003 - Internal Audit Unit... ....Tsh.130,758,000/=  
Kif. 1004 - Procurement Mgt Unit ... ....Tshs190,838,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001- Plann, Research and Dev. Div ...Tshs1,861,544,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo!

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kifungu namba 2001, 6294 nilitaka kujua tu kwa sababu hapa naona pesa nydingi zote ni za kigeni. Sasa nikiangalia jambo hili, sehemu ya Planning, Research and Development kwa kitengo hiki ni very sensitive. Je, hatuna commitment yetu ya local funds? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwenye development fedha nydingi ni kutoka nje na fedha za kwetu tume-commit katika other charges kitabu kilichopita.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - Infrastructure Division ... .... Tsh. 427,276,000/=  
Kif. 2003 - Resources Mob. & Econ. Sect... Tsh. 1,280,520,000/=  
Kif. 2004 - Social Sectors Division ... .... Tsh. 631,089,000/=  
Kif. 2005 - Agricultural Productivity Div ... Tsh. 549,187,000/=  
Kif. 2006 - Agriculture Marketing Div. Syst... Tsh. 870,427,000/=  
Kif. 2007 - Agric. Partnership and Coord.... Tsh. 217,588,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya  
Baraza la Mawaziri**

Kif. 1003 - Policy and Planning ... .... Tsh. 145,503,265,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

Kif. 1001 - Admn. And HR Mgt ... .... Tsh. 2,700,000,000/=  
Kif. 1002 - Finance and Accounts Units.... .... .... Tsh. 0  
Kif. 1003 - Government Comm. Unit... .... Tsh. 50,000,000/=  
Kif. 1004 - Procurement Mgt Unit ... .... .... ..Tsh. 0/=  
Kif. 1006 - Planning Division ... .... .... Tsh. 50,000,000/=  
Kif. 1007 - Inform. and Comm. Tech Unit ... Tsh. 50,000,000/=  
Kif. 2001 - Policy Dev. Division.... .... .... .... Tsh. 0  
Kif. 2002 - Management Services Div. .... Tshs 100,000,000/=  
Kif. 2003 - Establishment Division .... .... .... .... Tshs 0  
Kif. 2004 - Ethic Promotion Division ... .... Tsh. 200,000,000/=  
Kif. 2005 - Human Capital Mgt Div ... .... Tsh. 140,772,000/=  
Kif. 3001 - Human Resources Dev. Div .... Tsh. 200,000,000/=  
Kif. 3004 - Diversity Mgt Unit.... .... .... Tsh.100,000,000/=  
Kif. 4002 - Mgt Information System Div ... Tsh. 5,369,172,000/=  
Kif. 4003 - Records and Achieves Div.... .... .... Tsh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

**Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya  
Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kif. 1001 - Admn. And HR Mgt ... .... Tsh. 1,000,000,000/=  
Kif. 1003 - Plann. Monitoring and Eval. ... .... Tsh.150,000,000/=  
Kif. 1004 - Government Comm. Unit ... .... Tsh. 53,667,000/=  
Kif. 1007 - Information and Comm. Tech Unit ... .... Tsh. 0  
Kif. 1008 - Legal Services Unit ... .... .... .... ..Tsh. 0  
Kif. 2001 - Public Service Leaders Div ... .... Tsh. 151,200,000/=  
Kif. 2002 - Political Leaders Division... .... Tsh. 131,000,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

### Fungu 66 - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango

Kif. 2001 - Macro Economy Cluster ... .... Tsh. 307,480,000/=

Kif. 2002 - Productive Sector Cluster ... .... Tsh. 413,660,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 - Social Serv. Demogr. Cluster... Tsh. 2,995,016,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Subvote 6526 - Population Planning Project, kuna fedha pale ambazo zimetengwa za ndani pamoja na nje. Nilikuwa naomba ufanuzi wa huu Mradi wa Population Planning Project ni kitu gani, just in brief Serikali itusaidie kuweza kueleza ni nini? Subvote 6526.

**MWENYEKITI:** Nimekiona, Population Planning Project. Haya tueleze Mheshimiwa Waziri, idadi ya watu. Mheshimiwa Machali haelewi, mweleze vizuri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru sana Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Esther Matiko kwa kutokuendelea sana na walichokuwa wanat aka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hili ni kwamba katika mipango tunapanga maendeleo na kwa vile nilieleza wakati nikitoa maelezo yangu ni kwamba haya ni maendeleo ya watu. Kwa hiyo, ni lazima tujue na lazima tujifunze parten ya population ili baadaye mipango yetu iende vizuri; watoto wengi, vijana wengi au wazee wengi, kwa hiyo, mambo gani ya maendeleo tuyaelekeze wapi. Kwa hiyo, suala la kujua masuala ya idadi ya watu na structure yao kwa kweli ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

### TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati yako imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais na Taasisi zake; Fungu 20 na 30 – Ikulu, Fungu 32 – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu 67 – Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 94 – Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu Namba 9 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma, Fungu Namba 6 – Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Miradi na Fungu 4 –

Idara ya Kumbukumbu za Nyaraka za Taifa na Fungu 66 – Tume ya Mipango kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 kifungu kwa kifungu bila mabadiliko yoyote. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makof)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 – Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma yalipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Waliokubali wameshinda, kwa hiyo, matumizi ya Wizara hii yamepita. Nawapongeza sana Mawaziri wote kwa kazi nzuri mliyofanya.

Pia nawapongeza watendaji wote na ninaamini kwamba fedha zitakazotengwa zitatolewa kama zilivyoombwa, siyo tunazipitisha hapa, halafu baadaye hazitolewi! Zitatolewa kama zilivyoombwa ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Sasa, namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Jenista!

#### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kutoa hoja kama ifuatavyo:-

KWA KUWA katika Mkutano huu wa Ishirini wa Bunge unaoendelea Bunge letu linategemea kupokea ugeni wa Rais wa Msumbiji ambaye atalihutubia Bunge;

NA KWA KUWA katika Kikao cha Kamati ya Uongozi ya Bunge kilichofanyika tarehe 15/05/2015, Wajumbe wote wa Kamati hiyo waliohuduria walikubaliana na kupanga kuwa Rais huyo alihutubie Bunge kesho tarehe 19/05/2015;

NA KWA KUWA kwa kutambua kuwa, ili Mheshimiwa Rais wa Msumbiji aweze kulihutubia Bunge ni lazima Kanuni zitenguliwe ili aruhusiwe kuingia na kukaa ndani ya Ukumbi wa Bunge, sehemu itakayoandalialiwa kwa ajili ya kutoa hotuba;

NA KWA KUWA kwa kutambua kwamba katika Mkutano huu wa Ishirini muda uliopo ni mchache sana, inabidi kuliomba Bunge likubali kutengua baadhi ya Kanuni kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa muda wa kutosha kufanya kazi ya majadiliano ya bajeti na wakati huo huo kupata muda wa kusikiliza hotuba ya Rais wa Msumbiji;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Ishirini, Kanuni ya 139(1), 143(f), 99(8), 99(9), 99(12) na 99(13) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 139(1) na 143(f) ambazo kwa ujumla wake zinaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni wataketi maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao zitenguliwe na badala yake Mheshimiwa Rais wa Msumbiji aruhusiwe kuingia na kukaa sehemu atakayopangiwa ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa ajili ya kutoa hotuba. (Makof)

Mheshimiwa Kanuni ya 99(8) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa Waziri anayewasilisha hotuba utakuwa ni dakika zisizozidi 60, itenguliwe na badala yake muda wa dakika 45 utumike kuwasilisha hotuba za Waziri siku hiyo ya tarehe 19/05/2015. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(9) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa kuwasilisha maoni ya Kamati na ya Msemaji wa Upinzani utakuwa ni dakika zisizozidi 30, itenguliwe na badala yake muda wa dakika 20 utumike kuwasilisha Maoni ya Kamati na Maoni ya Msemaji wa Upinzani kwa siku hiyo ya tarehe 19/05/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(12) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Mbunge anayejadili Makadirio ya Wizara atasema kwa muda usiozidi dakika 10 itenguliwe na badala yake muda wa dakika saba utumike kwa Mbunge atakayejadili Makadirio ya Wizara iliyopangwa siku hiyo ya tarehe 19/05/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(13) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Waziri Mto Hoja atajibu ndani ya muda wa dakika 60, itenguliwe na badala yake muda wa dakika 40 utumike kwa Waziri Mto Hoja kujibu kwa Wizara iliyopangwa siku hiyo ya tarehe 19/05/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda kwa hiyo, hoja imekubaliwa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna Tangazo kutoka kwa Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, ameomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kutohana na ugeni wa Mheshimiwa Rais wa Msumbiji Bungeni kesho, wageni wa kawaida wanaotembelea Bunge kwa sababu mbalimbali hawatapokelewa wala kuruhusiwa kuingia Bungeni kipindi cha asubuhi, isipokuwa wageni wenye mialiko rasmi kwa ajili ya ujio wa Rais.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kutokuja na wageni hao muda wa asubuhi, badala yake wageni hao wanaweza kupokelewa wakati wa mchana Bunge litakaporejea.

Sasa baada ya hayo, shughuli zote zilizopangwa zimekwisha, naliahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.51 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 19 Mei, 2015 Saa Tatu Asubuhi)